

BUNGE LA TANZANIA

MAJADILIANO YA BUNGE

MKUTANO WA KUMI NA TISA

Kikao cha Pili – Tarehe 1 Aprili, 2020

(Bunge Lilianza Saa Nane Mchana)

Spika (Mhe. Job Y. Ndugai) Alikalia Kiti

D U A

Spika (Mhe. Job Y. Ndugai) Alisoma Dua

SPIKA: Waheshimiwa Wabunge, tukae.

Waheshimiwa Wabunge, tunaanza Mkutano wetu wa Kumi na Tisa kikiwa ni Kikao cha Pili katika utaratibu mpya kama nilivyokuwa nimeelekeza jana. Kama nilivyoahidi kwamba tutakuwa tunaendelea kuboresha hapa na pale kwa kadri ambavyo tunaendelea kupata ushauri kutoka kwenu Waheshimiwa Wabunge wa mahali gani na namna gani tuendelee kuboresha. Katibu.

NDG. STEPHEN KAGAIGAI - KATIBU WA BUNGE:

HATI ZA KWASILISHA MEZANI

SPIKA: Hati za Kuwasilisha Mezani, Waheshimiwa Mawaziri mtaziwasilisha hapo hapo kwenye *microphone* zenu. Tuanze na Ofisi ya Mheshimiwa Waziri Mkuu, Waziri wa Nchi, Mheshimiwa Jenista Mhagama.

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU, SERA, BUNGE,
KAZI, VIJANA, AJIRA NA WENYE ULEMAVU:**

Hotuba ya Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mheshimiwa Kassim Majaliwa Majaliwa ya Makadirio ya Bajeti ya mwaka 2020/2021 na Mapitio ya Mpango wa Bajeti ya mwaka 2019/2020.

SPIKA: Nakushukuru sana Mheshimiwa Waziri wa Nchi. Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Katiba na Sheria, hapo hapo ulipo.

**MHE. MOHAMED O. MCHENGERWA - MWENYEKITI WA
KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA KATIBA NA SHERIA:**

Taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Katiba na Sheria kuhusu utekelezaji wa Bajeti ya Ofisi ya Waziri Mkuu kwa Mwaka wa Fedha 2019/2020 pamoja na Maoni ya Kamati kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Ofisi hiyo kwa Mwaka wa Fedha 2020/2021

SPIKA: Ahsante sana. Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Bajeti.

**MHE. MASHIMBA M. NDAKI - MAKAMU MWENYEKITI WA
KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA BAJETI:**

Taarifa ya Kamati ya Bunge ya Bajeti kuhusu utekelezaji wa bajeti ya Mfuko wa Bunge kwa mwaka wa fedha wa 2019/2020 pamoja na Makadirio ya Mapato na Matumizi kwa mwaka wa fedha 2020/2021.

**MHE. OSCAR R. MUKASA - MWENYEKITI WA KAMATI YA
KUDUMU YA BUNGE YA MASUALA YA UKIMWI:**

Taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Masuala ya UKIMWI kuhusu Utekelezaji wa Bajeti ya Ofisi ya Waziri Mkuu (Tume ya Uratibu na Udhhibit wa UKIMWI) kwa Mwaka wa Fedha 2019/2020 pamoja na Maoni ya Kamati kuhusu

NAKALA MTANDAO(ONLINE DOCUMENT)

Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Ofisi hiyo kwa Mwaka wa Fedha 2020/2021.

SPIKA: Nakushukuru sana Mheshimiwa Mukasa. Sasa namuita Msemaji Mkuu wa Kambi Rasmi ya Upinzani kuhusu Ofisi ya Waziri Mkuu.

MHE. HALIMA J. MDEE - K.n.y. MSEMADI MKUU WA KAMBI RASMI YA UPINZANI BUNGENI KWA OFISI YA WAZIRI MKUU:

Taarifa ya Msemaji Mkuu wa Kambi Rasmi ya Upinzani kuhusu Ofisi ya Waziri Mkuu juu ya Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Ofisi hiyo kwa Mwaka wa Fedha 2020/2021.

SPIKA: Ahsante. Katibu.

NDG. STEPHEN KAGAIGAI – KATIBU WA BUNGE:

MASWALI NA MAJIBU

(Maswali yafuatayo yaliulizwa na kujibiwa kwa njia ya mtandao)

Na. 10

Barabara ya Msambazi- Lutindi-Kwabuluu

MHE. TIMOTHEO P. MNZAVA aliuliza:-

Barabara ya Msambazi - Lutindi – Kwabuluu ni muhimu kwa uchumi na maisha ya watu wa Korogwe hususan Kata za Tarafa ya Bungu, lakini barabara hii ni mbovu na korofisana.

(a) Je, ni lini Serikali itajenga barabara hii kwa kiwango cha lami?

(b) Je, ni lini barabara hii itapandishwa kuwa ya mkoa hasa ikizingatiwa kuwa inakwenda kuunganisha Bumbuli na Lushoto?

**WAZIRI WA NCHI, OFISI WA RAIS, TAWALA ZA MIKOA
NA SERIKALI ZA MITAA alijibu:-**

Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Timotheo Paul Mnzava, Mbunge wa Korogwe Vijijini, lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Spika, barabara ya Msambiazi - Lutindi - Kwabuluu ni barabara ya Mkusanyo (*Collector road*) yenye urefu wa kilometra 17.5. Kuanzia Mwaka wa Fedha 2017/2018 hadi 2019/2020 Serikali imeifanyia matengenezo kwa gharama ya shilingi milioni 43. Katika Mwaka wa fedha 2020/2021 Wakala wa Barabara za Mijini na Vijijini (*TARURA*) Wilaya ya Korogwe umeomba kutengewa shilingi milioni 50 kwa ajili ya matengenezo ya barabara hii. *TARURA* Wilaya ya Korogwe inaendelea kufanya upembizi wa kina wa mtandao wa barabara zake utakaobaini vipaumbele vya ujenzi wa mtandao wa barabara Wilayani Korogwe kwa viwango vya lami, changarawe na vumbi.

(b) Mheshimiwa Spika, kabla ya kuanzishwa kwa *TARURA*, barabara hii iliombewa kuingizwa kwenye orodha ya barabara zinazohudumiwa na *TANROADS* kupitia Baraza la Madiwani ambapo baada ya kuanzishwa kwa *TARURA* imepewa jukumu la kuendelea kuihudumia barabara hiyo. Aidha, Serikali imeshatoa maelekezo kwa Makatibu Tawala wa Mikoa yote nchini kuhusu utaratibu wa Bodi za Barabara za Mikoa, Wabunge au Kikundi cha watu kutuma maombi ya kupandishwa hadhi barabara. Utaratibu huu umetolewa na Kamati ya Kitaifa ya Kupanga Barabara katika Hadhi Stahiki (*National Roads Classification Committee- NRCC*).

Na. 11

Hitaji la Gari la Wagonjwa – Manyoni

MHE. AISHAROSE N. MATEMBE aliuliza:-

Ukosefu wa gari la kubeba wagonjwa Wilaya ya Manyoni umekuwa na madhara makubwa ikiwemo

NAKALA MTANDAO(ONLINE DOCUMENT)

kusababisha vifo vya akinamama na watoto pindi wanapotakiwa kukimbizwa kwenye hospitali za Rufani.

Je, Serikali ina mpango gani wa kuipatia Manyoni gari la Wagonjwa?

WAZIRI WA NCHI, OFISI WA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA alijibu:-

Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swalii la Mheshimiwa Aisharose Ndogholi Matembe, Mbunge wa Viti Maalum kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Halmashauri ya Wilaya ya Manyoni ina magari mawili ya wagonjwa, gari moja lipo kwenye Kituo cha Afya cha Nkonko na jingine katika Kituo cha Afya cha Kintinku. Hospitali ya Wilaya inatumia *pickup* na gari aina ya *land cruiser hardtop*. Serikali itatoa kipaumbele kwa Halmashauri ya Wilaya ya Manyoni pindi itakapopata magari ya wagonjwa kwa ajili ya vituo vya kutolea huduma za afya nchini.

Na. 12

Barabara Inayoelekea *Kalambo Falls*

MHE. SILAFU J. MAUFI aliuliza

Serikali inatambua vivutio kadhaa vya utalii ikiwemo *Kalambo Falls* Mkoani Rukwa. Hata hivyo, barabara ya kuelekeea maporomoko hayo kutokea Kijiji cha Kawala hairidhishi.

(i) Je, Serikali ina mpango gani wa kuiboresha barabara hiyo itakayokuwa ikitumika na watalii?

(ii) Je, kwa nini kipande hiki chenye urefu wa kilometra 12 kuanzia barabara ya Kijiji cha Kawala kisiwekewe lami?

**WAZIRI WA NCHI, OFISI WA RAIS, TAWALA ZA MIKOA
NA SERIKALI alijibu:-**

Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swalı la Mheshimiwa Silafu Jumbe Maufi, Mbunge Viti Maalum, lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Spika, Serikali imefanya matengenezo ya kilometa 6.5 za barabara ya *Kalambo Falls* kwa kiwango cha changarawe na kujenga makalvati kwa gharama ya shilingi milioni 160.8 ili kuhakikisha barabara hiyo inapitika katika kipindi chote cha mwaka.

(b) Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa fedha 2020/2021 Wakala wa Barabara za Vijiji na Mijini (*TARURA*) umepanga kufanya usanifu wa kina wa kipande cha barabara ya kutoka Kijiji cha Kawala hadi *Kalambo Falls* chenye urefu wa kilometa 12 ili kubaini gharama halisi zinazohitajika kwa ajili ya kujenga kipande hicho cha barabara kwa kiwango cha lami.

Na. 13

Mamlaka ya Uhamisho Kubaki kwa Katibu Mkuu Kiongozi

MHE. MUSSA B. MBAROUK aliuliza:

Tarehe 12 Septemba, 2019 katika Mkutano wa Kumi na Sita wa Bunge yamepitishwa Marekebisho ya Sheria ya Utumishi wa Umma ili kumpa Katibu Mkuu Kiongozi Mamlaka ya mwisho ya uhamisho wa watumishi wa umma.

Je, kwa kumpa Mamlaka ya Mwisho Katibu Mkuu Kiongozi hakutasababisha ukiritimba katika uhamisho wa Watumishi wa Umma?

WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, MENEJIMENTI YA UTUMISHI WA UMMA NA UTAWALA BORA alijibu:-

NAKALA MTANDAO(ONLINE DOCUMENT)

Mheshimiwa Spika, ninapenda kujibu swalii la Mheshimiwa Mussa Bakari Mbarouk, Mbunge wa Tanga Mjini kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Sheria ya Utumishi wa Umma Sura 298, imefanyiwa marekebisho katika Kifungu cha 4(3) kuptitia Kifungu cha 69 cha Sheria ya Marekebisho ya Sheria Mbalimbali Na. 13 ya Mwaka 2019 kwa kumpa Katibu Mkuu Kiongozi Mamlaka ya Mwisho ya Uhamisho wa Watumishi wa Umma kwa kuzingatia Mamlaka yake kama Mkuu wa Utumishi wa Umma kwa mujibu wa Kifungu cha 4(2) cha Sheria hii.

Mheshimiwa Spika, pamoja na Mamlaka hayo, Kifungu cha 8(2) cha Sheria hiyo kinampa Katibu Mkuu (Utumishi) Mamlaka ya kuwa Msaidizi Mkuu wa Katibu Mkuu Kiongozi. Hivyo, katika kutekeleza majukumu ya Katibu Mkuu Kiongozi, Kifungu cha 8(3)(h) cha Sheria husika kinampa Katibu Mkuu (Utumishi) Mamlaka ya kuhamisha Watumishi wa Umma kutoka Taasisi moja kwenda nyingine Tanzania Bara.

Mheshimiwa Spika, hata hivyo, ili kuboresha utoaji wa huduma kwa wananchi, Katibu Mkuu (Utumishi) amekasimu Mamlaka yake kwa Katibu Mkuu (TAMISEMI) ili aweze kuhamisha Watumishi wa Umma katika Mamlaka za Serikali za Mitaa. Vilevile, Katibu Mkuu (Utumishi) amekasimu Mamlaka yake kwa Makatibu Tawala wa Mikoa ili waweze kuhamisha Watumishi wa Mamlaka za Serikali za Mitaa katika Mikoa yao. Pamoja na kukasimisha Mamlaka yake, Katibu Mkuu (Utumishi) anaweza kuhamisha Watumishi katika Mamlaka za Serikali za Mitaa yeye mwenyewe pale inapobidi.

Mheshimiwa Spika, Ninapenda kuliarifu Bunge lako Tukufu kuwa marekebisho yaliyofanyika katika Sheria ya Utumishi wa Umma Sura 298, yamempa Katibu Mkuu Kiongozi Mamlaka ya mwisho ya uhamisho wa Watumishi wa Umma ili kuwezesha uhamisho unaofanywa naye kutopingwa au kutotenguliwa na Mamlaka nyingine. Hata hivyo, Mamlaka hayo yatatumika kwa kuzingatia masilahi mapana katika

NAKALA MTANDAO(ONLINE DOCUMENT)

Utumishi wa Umma au pale ambapo Katibu Mkuu Kiongozi hakuridhika na uhamisho uliofanywa na Mamlaka nyingine zilizopewa au zilizokasimiwa madaraka hayo kama ilivyoelezwa.

Na. 14

Mpango wa Kunusuru Kaya Masikini Nchini

MHE. JORAM I. HONGOLI aliuliza:-

Mpango wa Kunusuru Kaya Maskini umesaidia kuboresha hali za maisha ya Watanzania, hata hivyo baadhi ya Kaya Maskini hazikuingizwa kwenye Mpango huo:-

Je, ni lini Serikali itaingiza Kaya zote katika Mpango huo?

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, OFISI YA RAIS,
MENEJIMENTI YA UTUMISHI WA UMMA NA UTAWALA BORA
alijibu:-**

Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swalii la Mheshimiwa Joram Ismael Hongoli, Mbunge wa Lupembe kama ifuatavyo;

Mheshimiwa Spika, Kipindi cha Kwanza cha Mpango wa Kunusuru Kaya Masikini kilitekelezwa kwa miaka sita (6) kuanzia mwaka 2013 hadi 2019. Rasilimali zilizokuwepo zilitosheleza kufikia vijiji/mitaa/shehia 9,960 sawa na asilimia 70. Katika Kipindi hiki jumla ya Vijiji/Mitaa na Shehia 5,590 nchini kote hazikufikiwa.

Mheshimiwa Spika, Ninapenda kulijulisha Bunge lako Tukufu kuwa Kipindi cha Pili cha Mpango huu kimezinduliwa rasmi tarehe 17 Februari, 2020 na Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mheshimiwa Dkt. John Pombe Joseph Magufuli. Wakati wa uzinduzi wa Kipindi cha Pili, Mheshimiwa Rais aliagiza kufanyika kwa uhakiki wa walengwa wenye sifa za kuwemo kwenye Mpango huo,

kuhakikisha kaya zote zenye watu wenyewe uwezo wa kufanya kazi wanafanya kazi na kulipwa ujira katika miradi ya kuboresha miundombinu ya afya, elimu na maji na kutoa elimu kwa walengwa ili kutumia ruzuku wanazopata kujikita katika kuzalisha na hatimaye kuacha kutegemea ruzuku. Hivyo, utekelezaji wa Mpango huu utaanza rasmi mara baada ya kutekelezwa kwa maagizo hayo.

Mheshimiwa Spika, Kipindi cha Pili cha Mpango wa Kunusuru Kaya Masikini kitatetekelizwa katika halmashauri zote 185 za Tanzania Bara na wilaya zote za Zanzibar katika vijiji, mitaa na shehia zote ikiwa ni pamoja na zile ambazo hazikufikiwa katika Kipindi cha Kwanza; taratibu za utekelezaji wa Kipindi cha Pili zimeboreshwa ili kuwa na walengwa wanaostahili.

Mheshimiwa Spika, aidha, kabla ya kuanza utekelezaji, Serikali itafanya tathmini ya hali ya maisha ya walengwa waliokuwemo katika kipindi cha kwanza cha Mpango huu ili kubaini kaya zilizoimarika kiuchumi na kuziondoa katika orodha ya wanufaika wa ruzuku katika kipindi cha pili. Utaratibu huu umebuniwa kwa lengo la kulinda mafanikio yao ili ruzuku kwa kaya hizi itakapositishwa wasirudi tena katika hali ya umaskini ndani ya kipindi kifupi. Utaratibu uliobuniwa ni kuipatia kila kaya mafunzo ya kuweka akiba na kuwekeza pamoja na kuwapatia mitaji ya kuanzisha shughuli za ujasiri amali kulingana na eneo ambalo wana uzoefu nalo.

Na. 15

Hitaji la Mahakama ya Wilaya – Wilaya ya Uyui

MHE. ALMASI A. MAIGE aliuliza:-

Wilaya ya Uyui haina Mahakama ya Wilaya na ina Mahakama moja tu ya Mwanzo inayotumia chumba kidogo katika jengo la Mkuu wa Wilaya ya Uyui baada ya kutelekeza Mahakama ya Mwanzo ya Upuge:-

(a) Je, ni lini Serikali itajenga Mahakama ya Wilaya ya Uyui?

(b) Je, ni kwa nini Serikali ilitelekeza Mahakama ya Mwanzo ya Upuge pamoja na majengo yake katika Kijiji cha Upuge?

WAZIRI WA KATIBA NA SHERIA alijibu:-

Mheshimiwa Spika, ninapenda kujibu swali la Mheshimiwa Almasi Athuman Maige, Mbunge wa Tabora Kaskazini lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, uhaba wa majengo ni moja ya changamoto kubwa inayoikabili Mahakama ya Tanzania, Mahitaji ya majengo ya kuendeshea shughuli za mahakama hapa nchini ni makubwa, Kwa msingi huo, mahakama imejiwekea utaratibu wa kujenga majengo haya kwa awamu kulingana na upatikanaji wa fedha.

Mheshimiwa Spika, ujenzi wa jengo la Mahakama ya Wilaya Uyui ni mionganoni mwa majengo ya Mahakama za Wilaya 33 yaliyopangwa kuanza kujengwa mwezi June, 2020 kwa ufadhilli wa Benki ya Dunia, kwa sasa mahakama ipo katika hatua za mwisho kukamilisha mchakato wa awali ili ujenzi wa majengo hayo uanze kwa muda kama ilivyo katika mpango wa mahakama.

Mheshimiwa Spika, Serikali haikulitelekeza jengo la Mahakama ya Mwanzo Upuge, sababu kubwa ilikuwa ni uchakavu wa jengo lenyewe ambalo halikuwa rafiki kuendelea kutumika kuendeshea shughuli za mahakama. Hata hivyo, tunatoa shukrani zetu za dhati kwa Ofisi ya Mkuu wa Wilaya ya Uyui kwa kutuwezesha kupata ofisi kwa ajili ya kuendelea kutoa huduma za Mahakama ya Mwanzo Upuge wakati tukiendelea na taratibu za ujenzi wa jengo la Mahakama ya Wilaya ambayo pia itakuwa na Mahakama ya Mwanzo katika jengo moja.

Na. 16

Eneo Lilitengwa Kujenga Mahakama – Hydom

MHE. FLATEI G. MASSAY aliuliza:-

Wananchi wa Hydom wameandaa eneo kwa ajili ya ujenzi wa Mahakama kwa sababu Polisi wakikamata watuhumiwa huwapeleka Mbulu Mjini kilomita 86 ilipo Mahakama ya Wilaya:-

(a) Je, ni lini Serikali itajenga Mahakama ya Hydom?

(b) Je, Serikali haioni kuwa inapata hasara sana kupeleka Mahabusu Mbulu Mjini umbali wa kilomita 86 kutoka Hydom?

WAZIRI WA KATIBA NA SHERIA alijibu:-

Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swalii la Mheshimiwa Flatei Gregory Massay, Mbunge wa Mbulu Vijijiini, lenye sehemu (a) na (b) kwa pamoja, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, uhaba wa majengo ni moja ya changamoto kubwa inayoikabili Mahakama ya Tanzania, mahitaji ya majengo ya kuendeshea shughuli za mahakama hapa nchini ni makubwa, kwa msingi huo, Mahakama imojiwekea utaratibu wa kujenga majengo haya kwa awamu kulingana na upatikanaji wa fedha.

Mheshimiwa Spika, katika Mkoa wa Manyara, Wilaya za Mbulu, Hanang, Kiteto na Simanjiro hazina majengo ya Mahakama za Wilaya. Aidha, Wilaya ya Mbulu ina Mahakama za Mwanzo tatu tu zinazofanya kazi, ambazo ni Daudi, Endagkot na Dongobesh, licha ya ukubwa wa Wilaya yenye Tarafa tano. Hivyo, Tarafa mbili za Hydom na Nambisi hazina Mahakama za Mwanzo changamoto inayowafanya wananchi wa Hydom kutembea umbali mrefu kufuata huduma za mahakama katika Mahakama ya Mwanzo Endgkot ama Dongobesh.

Mheshimiwa Spika, vigezo vinavyotumika kuainisha maeneo ya kipaumbele ni pamoja na umbali, idadi ya watu, wingi wa mashauri na shughuli za kiuchumi ambazo mara nyingi ni kiashiria cha kuongezeka kwa idadi ya mashauri. Kwa kuzingatia vigezo hivyo na mpango wetu wa ujenzi, nipende kumhakikishia Mheshimiwa Mbunge kuwa Mahakama ya Mwanzo Hydom imepangwa kujengwa mwaka 2020/2021.

Na. 17

Tatizo la Maji Mugumu

MHE. LUCY S. MAGERELI aliuliza:-

Ujenzi wa chujio la maji katika Bwawa la Manchira, ambalo ni chanzo pekee cha maji katika Mji wa Mugumu, Wilayani Serengeti umechukua muda mrefu sana na kusababisha wananchi kukosa amani na kupata maji yasiyokuwa na ubora kwa matumizi ya binadamu:-

(a) Je, Serikali ina kauli gani juu ya ujenzi wa chujio hilo na lini litakamilika?

(b) Je, ni lini Serikali itakamilisha mfumo wa usambazaji maji toka Bwawa la Manchira ili kuwafikishia wananchi wote wa Mji wa Mugumu na maeneo ya jirani huduma ya maji?

WAZIRI WA MAJI alijibu: -

Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swalii la Mheshimiwa Lucy Simon Magereli, Mbunge wa Viti Maalum, lenye sehemu (a) na (b), kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, ni kweli ujenzi wa chujio katika Bwawa la Manchira umechukua muda mrefu, sababu kuu ikiwa ni upungufu uliojitekeza katika usanifu wa chujio na udhaifu katika uwezo wa kifedha wa mkandarasi aliyekuwa anatekeleza mradi huo. Kutokana na mwenendo usioridhisha wa utekelezaji, Wizara na kuzingatia ushauri wa kitaalam

NAKALA MTANDAO(ONLINE DOCUMENT)

mnamo tarehe 8/1/2020 iliamua kuvunja mkataba wa ujenzi wa chujio hilo.

Mheshimiwa Spika, Mamlaka za Majisafi na Usafi wa Mazingira Musoma (*MUWASA*) na Mugumu (*MUGUWASA*), zimeelekezwa kutathimini na kupitia gharama zinazohitajika ili kukamilisha ujenzi wa chujio hilo kwa kutumia wataalam wa ndani (*Force Account*). Wizara itatoa fedha zitakazohitajika kukamilisha ujenzi wa chujio hilo linalohudumia Mji wa Mugumu.

Mheshimiwa Spika, katika kuimarisha upatikanaji wa huduma ya maji kwa wananchi wote wa Mji wa Mugumu na maeneo ya jirani, Serikali kupitia fedha za mkopo kutoka India, itakarabati na kupanua mtandao katika Mji wa Mugumu. Usanifu wa awali umefanyika ambapo kazi zitakazofanyika ni pamoja na ujenzi wa matenki mawili ya kuhifadhiya maji yenye ujazo wa mita 5,000 na 500, ulazaji wa bomba zenyе vipenyo mbalimbali zenyе urefu wa kilomita 200 na kutoka urefu wa sasa wa kilomita 42 na ukarabati mkubwa wa bomba za sasa na uboreshaji wa chujio.

Na. 18

Kurasimisha Wachimbaji Wadogo wa Madini – Msalala

MHE. EZEKIEL M. MAIGE aliuliza:-

Kwa kuwa Serikali imekuwa ikiwarasimisha wachimbaji wadogo wa madini:-

(a) Je, ni lini Serikali itawarasimisha Wachimbaji wadogo katika vijiji vya Busulwangili, Lwabakanga, Kakola namba Tisa na Wisolele katika Jimbo la Msalala?

(b) Je, ni sawa kwa mwenye leseni au msimamizi wa eneo la wachimbaji wadogo kupatiwa asilimia 30 ya mawe yanayochimbwa katika eneo lake?

WAZIRI WA MADINI alijibu:-

Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swalii la Mheshimiwa Ezekiel Magolyo Maige, Mbunge wa Msalala lenye sehemu (a) na (b), kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, tangu mwaka 1996, Serikali kupitia Wizara ya Madini imekuwa ikitenga maeneo maalum kwa ajili ya kurasimisha wachimbaji wadogo wa madini nchini. Hadi sasa, Serikali imetenga jumla ya maeneo 46 katika sehemu mbalimbali nchini yenye ukubwa wa hekta 281,533.69. Aidha, Serikali itaendelea kutenga maeneo kwa ajili ya wachimbaji wadogo kadri yatakavyokuwa yanapatikana.

Mheshimiwa Spika, katika Wilaya ya Kahama Serikali imeunda Kamati Maalum ya Utengaji wa Maeneo kwa mujibu wa Kifungu cha 15 na 16 cha Sheria ya Madini, Sura 123. Kamati hiyo itakuwa na jukumu la kuandaa utaratibu wa kugawa maeneo yote tengefu yakiwemo maeneo ya Kinamiyuba-IIlindi-Mwime, Buzwagi-Bumbiti na Nyangalata. Mpaka sasa jumla ya maombi 89 ya uchimbaji mdogo yamepokelewa na mchakato wa kugawa leseni hizo unaendelea. Aidha, Serikali kupitia Tume ya Madini imeifuta leseni ya utafutaji wa madini *PL 8125/2012* iliyokuwa inamiliikiwa na Kampuni ya *Liontown Tanzania Limited* iliyoko Kata ya Segese Halmashauri ya Msalala na eneo hilo linatarajiwa kutengwa kwa ajili ya wachimbaji wadogo.

Mheshimiwa Spika, kwa sasa maeneo ya Lwabakanga na Kakola namba Tisa aliyoyataja Mheshimiwa Mbunge, yapo ndani ya leseni ya uchimbaji mkubwa *SML 44/99* inayomilikiwa na mgodi wa *Bulyanhulu Gold Mine Limited*. Hivyo, eneo hilo haliwezi kutengwa kwa ajili ya shughuli za uchimbaji mdogo. Aidha, eneo la Busulwangili lipo ndani ya leseni ya utafutaji wa madini *PL 10782/2016* inayomilikiwa na Kampuni ya *Hai Nan Geology (Tanzania) Company Limited*. Hivyo, Serikali ipo katika hatua za awali za kufuta eneo hilo na kulitenga kwa ajili ya wachimbaji wadogo baada ya mmiliki wake kushindwa kufanya kazi ya utafiti.

Mheshimiwa Spika, Serikali kupitia Tume ya Madini ilitoa waraka wa ndani Na.3 ulioanza kutumika tarehe 15 Oktoba, 2019, wenyе dhumi ni la kutoa mwongozo kwa Maafisa Madini Wakazi na watumishi wengine katika kusimamia, kudhibiti shughuli za madini na mapato ya Serikali katika maeneo yenye *rush*. Waraka huo unawataka wasimamizi kuzingatia ukusanyaji wa kodi za Serikali Kuu na Halmashauri na kuweka mgawanyo wa mapato baina ya mmiliki wa duara (mchimbaji), mmiliki wa shamba na msimamizi. Aidha, kwa Mujibu wa Waraka huo mgawanyo utazingatia kodi za Serikali Kuu na Halmashauri kwanza ambazo ni mrabaha 6%, ada ya ukaguzi 1% na kodi ya huduma 0.3%. Baada ya kutolewa kodi hizo, mmiliki wa ardhi atapata 15%, mmiliki wa shamba 15% na mmiliki wa duara (mchimbaji) 70%.

MHE. EZEKIEL M. MAIGE: Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa majibu ya Serikali, naomba kuuliza maswali mawili ya nyongeza kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, swali la kwanza, kwa kuwa Serikali ilielekeza wananchi waunde vikundi vya uchimbaji ili wasimamie *rush* wenyewe, je, ni kwa nini sasa Kamishna wa Madini Kahama anaweka wasimamizi ambao si wanavikundi na utaratibu gani unatumika kuwapata wasimamizi hao?

Mheshimiwa Spika, swali la pili, kwa nini eneo la Wisolele limetolewa leseni kwa watu binafsi akiwemo mtu mmoja ambaye anajinasibu kuwa karibu na viongozi wa tume (jina nalihofadhi) aliyepata leseni zaidi ya 17 peke yake badala ya vikundi vya wachimbaji wadogo kama Waziri alivyojibu kwenye jibu la msingi?

WAZIRI WA MADINI: Mheshimiwa Spika, napenda kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Ezekiel Magolyo Maige, Mbunge wa Msalala, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, kama nilivyojibu kwenye jibu la swali la msingi kuwa, Serikali kupitia Tume ya Madini ilitoa Waraka wa Ndani Na.3 ulioanza kutumika tarehe 15 Oktoba,

2019, wenye dhumuni la kutoa mwongozo kwa Maafisa Madini Wakazi na watumishi wengine katika kusimamia, kudhibiti shughuli za madini na mapato ya Serikali katika maeneo yenye *rush*. Kwa mujibu wa Waraka huo Afisa Madini Mkazi ni Mwenyeketi wa Kamati ya Uongozi unaofuatilia na kuimarisha usimamizi katika eneo la *rush*. Kamati hiyo inajumuisha *DSO* (Katibu), *TAKUKURU* (Mjumbe), *OCD* (Mjumbe), *REMA* (Mjumbe) na Halmashauri (Mjumbe).

Mheshimiwa Spika, utaratibu unaotumika kuwapata wasimamizi wa *rush* ni kupitia Kamati ya Uongozi unaofuatilia na kuimarisha usimamizi katika eneo la *rush* kama ilivyotajwa hapo juu. Kamati hiyo huteua Wasimamizi wa *rush*, ambapo Mwenyekiti wa *rush* anapaswa kuwa na sifa zifuatazo:-

Awe mchimbaji mzoefu hasa katika usimamizi wa maeneo ya aina hiyo; awe hana historia ya wizi wa fedha za Serikali na awe mwaminifu. Wajumbe wengine kwenye usimamizi wa *rush* ni pamoja na Katibu, Mweka Hazina, Mwenyekiti wa Kijiji, Mwenyekiti wa Kitongoji, Mjumbe wa *REMA*, *TAWOMA*, mwakilishi wa eneo/shamba.

Mheshimiwa Spika, ni kweli katika eneo la Wisolele zimetolewa leseni za uchimbaji mdogo 55 kwa watu binafsi na vikundi mbalimbali. Aidha, kuna jumla ya maombi ya leseni za uchimbaji mdogo 95. Kati ya maombi hayo, maombi sita ni ya vikundi vya *Amani Gold Mine*, *Chapakazi*, *Domain Gold Group* na *Pamoja Mining Group*.

Mheshimiwa Spika, utolewaji wa leseni hizo 55 ukijumuisha leseni 17 zilizotajwa na Mheshimiwa Mbunge zilitolewa kabla ya *rush* na vikundi kuundwa. Kwa mujibu wa Sheria ya Madini, 2010 pamoja na Marekebisho yake ya 2017 mchimbaji mdogo hazuiwi kumiliki leseni zaidi ya moja.

Na. 19

Barabara ya Same - Kisiwani – Mkomazi

MHE. NAGHENJWA L. KABOYOKA aliuliza:-

(a) Je, Serikali ina mkakati gani wa kutimiza ahadi ya Mheshimiwa Rais ya kujenga kwa kiwango cha lami barabara ya Same – Kisiwani hadi Mkomazi ambayo inaunganisha Majimbo matano ya Same Magharibi, Same Mashariki, Mlalo, Mkinga na Korogwe Vijijini?

(b) Je, ni fedha kiasi gani zimetumika kuanzia mwaka 2015/2016 – 2019/2020 kwa ajili ya kukarabati barabara hiyo?

WAZIRI WA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO
alijibu:-

Mheshimiwa Spika, napenda kujibu kwa pamoja swalii la Mheshimiwa Naghenjwa Livingstone Kaboyoka, Mbunge wa Same Mashariki lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Barabara ya Same – Kisiwani – Mkomazi imekuwa ikifanyiwa matengenezo ya aina mbalimbali kila mwaka. Aidha, kuanzia Mwaka wa Fedha 2015/2016 hadi 2019/2020, kiasi cha Sh.3,299.365 kimetumika kwa ajili ya matengenezo mbalimbali ya barabara hiyo. Kufuatia kufanyika na kukamilika kwa upembuzi yakinifu pamoja na usanifu wa kina kwa kilometra zote za barabara hiyo kilometra 100.5, Serikali kuititia Wizara yangu imetenga kiasi cha shilingi bilioni tano (Shilingi milioni 5,000.00) katika Mwaka wa Fedha 2020/2021 ili kitumike kuanza ujenzi kwa barabara hiyo kwa kiwango cha lami.

NDG. STEPHEN KAGAIGAI – KATIBU WA BUNGE:

HOJA ZA SERIKALI

Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Serikali kwa Mwaka wa Fedha 2020/2021 - Ofisi ya Waziri Mkuu

SPIKA: Ahsante sana Katibu. Sasa moja kwa moja nimkaribishe Mheshimiwa Waziri Mkuu ili aweze kutuletea hoja yake ya Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Ofisi ya Waziri Mkuu kwa mwaka wa fedha 2020/2021. Mheshimiwa Waziri Mkuu, karibu sana. (*Makofii*)

WAZIRI MKUU: Mheshimiwa Spika, kama ambavyo sote tunafahamu katika kipindi cha miaka minne, kazi kubwa imefanyika na nahitaji kuiwasilisha mbele ya mbele ya Bunge lako iweze kuridhiwa sambamba na kuomba kuridhiwa kupata matumizi ya mwaka ujao, yote ambayo nimeandika naomba yaingie kwenye kumbukumbu na mimi nitafanya mapitio ya maeneo muhimu ambayo yanahitaji yanukuliwe.

Mheshimiwa Spika, sasa naomba kutoa hoja kwamba kutokana na taarifa zilizowasilishwa leo katika Bunge lako Tukufu na Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Bajeti, Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Katiba na Sheria na Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Masuala ya UKIMWI zilizochambua Bajeti ya Mfuko wa Bunge na Ofisi ya Waziri Mkuu, Bunge lako sasa lipokee na kujadili Taarifa ya Mapitio ya Utekelezaji wa Kazi za Serikali kwa mwaka 2019/2020 na Mwelekeo wa Kazi za Serikali kwa mwaka 2020/2021. Aidha, naomba Bunge lako Tukufu likubali kupitisha Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Fedha za Ofisi ya Waziri Mkuu na Taasisi zilizopo chini yake pamoja na Mfuko wa Bunge kwa mwaka wa fedha 2020/2021.

Mheshimiwa Spika, wakati tunapojadili Taarifa ya Mapitio ya Utekelezaji wa Kazi za Serikali kwa Mwaka 2019/2020 na Mwelekeo wa Kazi za Serikali kwa Mwaka 2020/2021, hatuna budi kumshukuru Mwenyezi Mungu mwingi wa rehema kwa kuendelea kutujaalia afya na uzima. Katika mwaka 2019/2020, Bunge lako Tukufu lilimpoteza aliyekuwa Mbunge wa Jimbo la Newala Vijijini, Mheshimiwa Rashid Ajali Akbar. Naungana na Mheshimiwa Rais Dkt. John Pombe Magufuli na Watanzania wenzangu kutoa salamu za pole kwa familia ya Marehemu na wanachama wa Chama cha CUF kufuatia kifo cha aliyekuwa Katibu Mkuu wa Chama cha Wananchi (CUF) Taifa, Alhaj Khalifa Suleiman Khalifa. Pia kwa masikitiko makubwa, niungane na Watanzania wote, familia na wanahabari wote nchini kwa kifo cha Mwandishi wa Habari Mwandamizi wa Shirika la Habari Tanzania (TBC), ndugu yetu tuliyefanya naye kazi vizuri hapa Bungeni, Hayati Marin Hassan Marin, kilichotokea leo alfajiri. Mungu aziweke roho za marehemu mahali pema peponi – Amina.

Mheshimiwa Spika, vilevile, Taifa letu lilikumbwa na majanga mbalimbali ikiwa ni pamoja na mafuriko nchini kote na ajali za barabaranı ambazo zilisababisha vifo, majeruhi na uharibifu wa mali. Sambamba na kutoa pole kwa ndugu, jamaa na marafiki kwa misiba iliyotokea, tuendelee kumuomba Mwenyezi Mungu ajaalie afya njema waliopata majeraha na apumzishe roho za marehemu mahali pema peponi. Amina! Vilevile, nawashukuru kwa dhati wale wote waliojitelea kwa hali na mali katika kuwasaidia majeruhi na wahanga wa matukio yote hayo.

Mheshimiwa Spika, kama tunavyofahamu, mwaka huu Serikali ya Awamu ya Tano inahitimisha kipindi cha kwanza cha miaka mitano kilichoanza mwaka 2015. Kwa msingi huo, hotuba yangu itaeleza kwa muhtasari baadhi ya mafanikio makubwa ambayo Serikali imeyapata katika kipindi cha takriban miaka mitano ya utekelezaji wa llani ya Uchaguzi ya Chama cha Mapinduzi (CCM).

Mheshimiwa Spika, hotuba hii pia inaanisha baadhi ya kazi zilizotekelizwa na Serikali kwa kuzingatia mipango na mikakati mbalimbali hususan Mpango wa Pili wa Maendeleo wa Miaka Mitano wa Mwaka 2016/2017 hadi 2020/2021 ambao ni sehemu ya utekelezaji wa Dira ya Taifa ya Maendeleo ya Mwaka 2025. Mikakati na Mipango hiyo, inatekelezwa sambamba na mipango mingine ya kikanda na kimataifa kama vile Agenda ya Mwaka 2063 ya Umoja wa Afrika na Malengo Endelevu ya Umoja wa Mataifa ya Mwaka 2030.

Mheshimiwa Spika, katika kipindi cha uongozi wa Serikali ya Awamu ya Tano, tumeshuhudia mafanikio makubwa katika kuimarisha miundombinu, huduma za kiuchumi na kijamii, utawala bora, mapambano dhidi ya rushwa na ujisadi pamoja na kuhamasisha uwekezaji. Napenda kutumia fursa hii kumpongeza sana Mheshimiwa Dkt. John Pombe Joseph Magufuli, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa uongozi wake mahiri wa Serikali ya Awamu ya Tano katika utekelezaji wa llani ya Uchaguzi ya Chama cha Mapinduzi ya Mwaka 2015 hadi 2020. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, nawapongeza sana pia, Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan, Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania; Mheshimiwa Dkt. Ali Mohamed Shein, Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi na Mheshimiwa Balozi Seif Ally Idd, Makamu wa Pili wa Rais wa Serikali ya Mapinduzi Zanzibar kwa kusimamia vyema utekelezaji wa llani ya Uchaguzi ya Chama cha Mapinduzi. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, kipekee, nakushukuru wewe binafsi, pia Mheshimiwa Naibu Spika na Wenyeviti wa Bunge kwa kuliongoza vyema Bunge lako Tukufu na Wabunge wote katika kusimamia Serikali kuhakikisha kuwa inatekeleza wajibu wake ipasavyo wa kuhudumia wananchi. Vilevile, natoa shukrani zangu za dhati kwa Kamati za Kudumu za Bunge kwa kazi kubwa ya kupitia Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara, Mikoa, Wakala, Idara zinazojitegemea na Mamlaka za Serikali za Mitaa. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, kipekee, nawashukuru sana Wajumbe wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Katiba na Sheria chini ya Uenyekiti wa Mheshimiwa Mohammed Omary Mchengerwa, Mbunge wa Jimbo la Rufiji; Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Masuala ya UKIMWI chini ya Uenyekiti wa Mheshimiwa Oscar Rwegasira Mukasa, Mbunge wa Jimbo la Biharamulo Magharibi; na Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Bajeti chini ya Uenyekiti wa Mheshimiwa Mashimba Mashauri Ndaki, Mbunge wa Jimbo la Maswa Magharibi. Maoni na ushauri wa Kamati hizo umesaidia sana kuboresha Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Fedha ya Ofisi ya Waziri Mkuu na Mfuko wa Bunge kwa Mwaka 2020/2021. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, nawashukuru Waheshimiwa Mawaziri na Naibu Mawaziri wote, Katibu Mkuu Kiongozi, Mwanasheria Mkuu wa Serikali, Makatibu Wakuu na Naibu Makatibu Wakuu, Wakuu wa Mikoa na Wilaya, Wakuu wa Idara, Mashirika, Wakala na Taasisi zote za Serikali kwa ushirikiano [mlionipa](#) katika kutekeleza majukumu ya Ofisi ya Waziri Mkuu. Aidha, nawashukuru wafanyakazi wote wa Serikali na Taasisi zake kwa kutekeleza vizuri majukumu yao

kwa weledi mkubwa na hivyo kuwezesha Serikali kutekeleza kazi zake kwa tija na ufanisi mkubwa. Vilevile, nawashukuru kwa michango yenu iliyowezesha kukamilisha Mpango na Bajeti ya Serikali ya mwaka 2020/2021. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, kwa namna ya pekee kabisa, namshukuru Mheshimiwa Jenista Joakim Mhagama, Mbunge wa Jimbo la Peramiho na Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu (Sera, Bunge, Kazi, Vijana, Ajira na Wenye Ulemavu); Mheshimiwa Angella Jasmine Kairuki, Mbunge wa Viti Maalum na Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu (Uwekezaji); Mhe. Anthony Peter Mavunde, Mbunge wa Jimbo la Dodoma Mjini na Naibu Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu (Kazi, Vijana na Ajira); na Mhe. Stella Alex Ikupa, Mbunge wa Viti Maalum na Naibu Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu (Watu Wenye Ulemavu). (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, pia nawashukuru Makatibu Wakuu, Bw. Andrew Wilson Massawe (Kazi, Vijana, Ajira na Wenye Ulemavu); Bibi Dorothy Aidan Mwaluko (Sera, Uratibu na Uwekezaji); na Bw. Tixon Tuyangine Nzunda (Waziri Mkuu na Bunge). Vilevile nawashukuru Wakurugenzi, Wakuu wa Taasisi zilizopo chini ya Ofisi ya Waziri Mkuu, Ofisi Binafsi ya Waziri Mkuu na Wafanyakazi wote kwa ushirikiano mkubwa wanaonipatia katika kutekeleza majukumu ya Ofisi ya Waziri Mkuu. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, napenda pia kuwashukuru washirika wa maendeleo zikiwemo nchi rafiki, taasisi na mashirika ya kimataifa, madhehebu ya dini na mashirika yasiyo ya kiserikali, kwa kuendelea kuunga mkono juhudzi za Serikali katika kujenga uchumi wa viwanda na kuilettea maendeleo nchi yetu. Mchango wao umekuwa muhimu kuwezesha nchi yetu kupiga hatua kubwa kimaendeleo kulingana na mipango tuliyojiwekea.

Mheshimiwa Spika, nawashukuru pia wananchi wote kwa kuendelea kuiunga mkono Serikali ya Awamu ya Tano katika kutekeleza majukumu yake ipasavyo. Aidha, nawashukuru wananchi wa Jimbo la Ruangwa, Mkoani Lindi

kwa kuendelea kushirikiana nami na kwa kuniunga mkono. Niwapongeze na kuwashukuru kwa kutekeleza shughuli za maendeleo jimboni kwa ufanisi mkubwa. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, kipekee pia namshukuru sana mke wangu mpendwa Mary; watoto wangu na familia yangu kwa ujumla kwa upendo wao, uvumilivu na maombi yao wakati wote napotekeleza majukumu yangu ya kitaifa. Nawashukuru sana. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, naomba nizungumzie Homa Kali ya Mapafu. Hivi sasa nchi yetu na dunia kwa ujumla inapitia katika kipindi kigumu. Itakumbukwa kwamba tarehe 11 Machi 2020, Shirika la Afya Duniani (*WHO*) lilitangaza mlipuko wa Homa Kali ya Mapafu ijulikanayo kama *COVID-19* inayosababishwa na virusi vya CORONA kuwa ni janga la Kimataifa. Aidha, tarehe 16 Machi, 2020 Mheshimiwa Dkt. John Pombe Joseph Magufuli Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania alitangaza kuwepo kwa ugonjwa huu hapa nchini.

Mheshimiwa Spika, tangu kugundulika kwa ugonjwa huo, Serikali inaendelea kuchukua hatua mbalimbali katika kukabiliana na ugonjwa huu ikiwa ni pamoja na kuimarissha ukaguzi, upimaji na ufuatiliaji wa wasafiri wanaoingia nchini ili kubaini wasafiri wanaoonesha dalili za ugonjwa huo au wenye viashiria hatari ili kuweza kuwatenga. Sasa tunachofanya, tumesitisha huduma za ndege kwa kuweka abiria wote kwenye nyumba maalum ya kujitenga kwa gharama zao, tumetenga pia na hosteli ili kuwapunguzia gharama kwa wale ambao hawana uwezo wa kuishi kwenye hoteli. Kadhalika, katika kukabiliana na virusi vya *CORONA*, Serikali ilitoa maelekezo yafuatayo:-

(i) Tumesitisha Mbio za Mwenge wa Uhuru na kwamba fedha zilizotengwa kwa ajili ya jukumu hilo zitumike kusaidia hatua za kukabiliana na janga la virusi vya Corona;

(ii) Tumesitisha michezo yote inayokusanya makundi ya watu ikiwemo Ligi Kuu ya Tanzania Bara, Ligi Daraja la

Kwanza, Ligi Daraja la Pili na aina ya michezo yote hapa nchini.

(iii) Kusitisha shughuli zote za elimu kuanzia elimu ya awali, hadi vyuo vikuu ili wote warudi makwao waendelee kujiunga na familia zao.

(iv) Kusitisha semina, warsha, makongamano na mikutano yote ya ndani na ya hadhara yenyenku kuhusisha mjumuiko wa watu wengi.

(v) Kuwatenga abiria waingiao nchini kwenye maeneo maalum kwa siku 14 ili kufuatilia hali zao mpaka tutakapojiridhisha kuwa hawana ugonjwa huo;

(vi) Kuwasisitiza Watanzania kufuata kanuni za kudhibiti maambukizi ikiwemo kunawa maji kwa sabuni, kujikinga unapokohoa na kupiga chafya, kutopeana mikono bila sababu, kukaa au kusimama kwa umbali unaokubalika kwa jirani yako na kadhalika na kuwaasa Watanzania wenye safari zisizo za lazima kwenda nje ya nchi hasa kwenye nchi zenyenku maambukizi ya Corona ikiwezekana wasitishe mpaka hapo hali itakapotengamaa.

Mheshimiwa Spika, Serikali inaendelea na usimamizi wa karibu sambamba na kufanya tathmini na kuchukua hatua kadhaa. Tumeunda Kamati za kitaifa tatu (3) zinazosimamia ugonjwa huu na niendelee kusisitiza kuwa sote tuzingatie maelekezo yaliyotolewa na Serikali toka tulipoanza kampeni ya kupambana na ugonjwa huu. Aidha, niwatake Watanzania kuzingatia masharti ya afya kwa kufuata ushauri unaotolewa na wataalam wetu. Mgonjwa akithibitika, atapelekwa eneo maalum bila kujali cheo chake, atalala palipoandaliwa. Watanzania wenzangu tuendelee kupuuza taarifa za uzushi zinazosambazwa na wasiotutakia mema katika mitando ya kijamii.

Mheshimiwa Spika, nianze na mafanikio ya Serikali ya Awamu ya Tano. Tarehe 20 Novemba, 2015 wakati akifungua rasmi Bunge la Kumi la Moja la Jamhuri ya Muungano wa

Tanzania Jijini Dodoma, Mheshimiwa Dkt. John Pombe Joseph Magufuli, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania aliiwaahidi wananchi wote kuwa Serikali ya Awamu ya Tano itawatumikia na kuwajali.

Mheshimiwa Spika, katika kutekeleza azma hiyo, ndani ya kipindi cha takriban miaka mitano mafanikio makubwa yamepatikana na yamesaidia kuimarisha hali ya kiuchumi na kijamii kwenye Taifa letu. Ujenzi wa miundombinu muhimu ya kiuchumi hususan ya usafiri, usafirishaji sambamba na uimarishaji wa huduma muhimu za kijamii ni mionganoni mwa masuala yaliyopewa kipaumbele na Serikali ya Awamu ya Tano. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, ujenzi wa Reli ya Kati kwa kiwango cha kimataifa (*Standard Gauge Railway*), ufufuaji wa Shirika la Ndege la Tanzania, ufufuaji wa ushirika na mali za ushirika mfano, *NCU, SHIRECU, WETCU* na Mamlaka ya Mkonge Tanzania, ujenzi wa Bwawa la Kufua Umeme la Julius Nyerere, ulinzi wa maliasili na rasilimali zetu pamoja na ujenzi na ukarabati wa miundombinu ya elimu, afya na maji ni kati ya hatua za msingi zinazochukuliwa na Serikali ya Awamu ya Tano katika kufikia uchumi wa kati unaoongozwa na viwanda ifikapo mwaka 2025.

Mheshimiwa Spika, katika kipindi hiki cha miaka mitano, tumeshuhudia miradi hiyo muhimu ikiwa katika hatua mbalimbali za utekelezaji. Kwa mfano, ujenzi wa Reli ya Kati kwa kiwango cha Kimataifa ambao hadi mwaka 2020 umetumia shilingi trilioni 2.96 na kukamilika kwa asilimia 75 kwa kipande cha Dar es Salaam hadi Morogoro na asilimia 28 kwa kipande cha Morogoro hadi Makutupora. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, Serikali inatumia gharama kubwa katika kujenga miundombinu hiyo wezeshi ya kiuchumi kwa lengo la kulifanya Taifa letu kuwa na uchumi imara wa kujitegemea na wenye kuhimili ushindani. Fedha hizo pia zimekuwa chanzo cha ajira na zabuni kwa Watanzania zinazowasaidia kuongeza kipato.

Mheshimiwa Spika, mradi huu utakapokamilika utaongeza ufanisi wa huduma za usafiri na usafirishaji wa bidhaa na abiria pamoja na kupunguza gharama za uchukuzi. Kadhalika, utachochea ukuaji wa miji na sekta nyingine kama vile kilimo, viwanda, utalii na biashara. Vilevile, mradi huu utakuwa chanzo cha ongezeko la mapato ya Serikali yatakayosaidia katika kuboresha maslahi ya watumishi na huduma za kijamii kama vile afya, elimu na maji.

Mheshimiwa Spika, vilevile, ujenzi wa Mradi wa Bwawa la Kufua Umeme wa Maji wa Julius Nyerere ambalo litakapokamilika litazalisha umeme wa Megawati 2,115. Hadi Machi 2020 mradi huo umegharimu shilingi triliioni 1.28 na umekamilika kwa asilimia 10.74. Kukamilika kwa bwawa hilo kutalihakikisha Taifa letu umeme wa uhakika na wa nafuu zaidi. Aidha, ongezeko hilo la uzalishaji wa umeme litawezesha shughuli za uzalishaji viwandani kuwa za uhakika, tija, ufanisi na gharama nafuu. Vilevile, mradi huu utachangia kwa kiasi kikubwa katika juhudini za kuhifadhi mazingira kutokana na kuongezeka kwa matumizi ya nishati ya umeme badala ya kuni. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, Serikali imefanikiwa kutekeleza Mradi wa Usambazaji wa Umeme Vijiji (REA) ambapo vijiji vilivyounganishiwa umeme nchini vimeongezeka kutoka vijiji 2,118 mwaka 2015 hadi vijiji 9,001 mwezi Machi 2020. Mradi huo pia umezinufaisha Taasisi 11,128 zikiwemo za elimu, afya, dini, mashine za kusukuma maji na huduma za biashara. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, katika kuimarisha huduma za usafiri wa anga, Serikali inaendelea kuliimarisha Shirika la Ndege la Tanzania. Hadi kufikia Machi, 2020 tayari ndege 8 mpya zenye thamani ya shilingi triliioni 1.27 zimepokelewa na kuanza kazi. Kadhalika, malipo ya awali ya shilingi bilioni 85.7 kwa ajili ya ununuzi wa ndege nyingine 3 mpya yamefanyika. Ununuzi wa ndege hizi, umeongeza ufanisi katika usafiri wa anga, kuongezeka kwa mapato ya Serikali, kuimarika kwa utalii na kuongezeka kwa fursa za ajira katika sekta ya huduma. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, bajeti ya dawa, vifaa, vifaa tiba na vitendanishi imeongezeka kutoka shilingi bilioni 31 kwa Mwaka 2015 hadi shilingi bilioni 269 kwa mwaka 2019. Serikali pia imegharamia ujenzi na uboreshaji wa miundombinu ya afya kwa kujenga zahanati 1,198, ukarabati wa vituo vya afya 487, hospitali za Halmashauri za Wilaya 69 na hospitali za rufaa za mikoa 10 za mikoa ya Njombe, Simiyu, Mara, Geita, Songwe, Katavi, Sekou Toure, Mwananyamala, Mawenzi, Manyara, hospitali za rufaa za kanda tatu za Mtwara, Mbeya na Burigi-Chato na Hospitali Maalum ya Kibong'oto na Uhuru hapa Jijini Dodoma Wilaya ya Chamwino. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, katika kipindi cha Julai 2015 hadi Januari 2020 jumla ya shilingi trilioni 3.01 zimetumika kugharamia huduma za afya. Kuongezeka kwa bajeti ya dawa na uboreshaji wa miundombinu ya afya, kumeleta mapinduzi makubwa katika sekta ya afya kwa kuimarisha afya za watanzania.

Mheshimiwa Spika, nyote mtakubaliana nami kuwa ujenzi na uboreshaji wa miundombinu ya afya, ununuzi wa dawa na vifaa vya kisasa vya tiba ni utekelezaji wa dhamira ya dhati ya Serikali ya Awamu ya Tano ya kuhakikisha kila Mtanzania anapatiwa haki yake ya kupata matibabu tena katika eneo alipo.

Mheshimiwa Spika, katika eneo la elimu, Serikali imeongeza mikopo kwa ajili ya elimu ya juu kutoka shilingi bilioni 365 mwaka 2015 hadi shilingi bilioni 450 mwaka 2019. Elimu msingi bila Ada nayo imetekelizwa kwa mafanikio makubwa na kuhakikisha watoto wote wenye umri wa kwenda shule wanaandikishwa na kupatiwa nafasi ya kwenda shule.

Mheshimiwa Spika, utekelezaji mzuri wa Mpango wa Elimumsingi bila ada, uliwezesha kuongezeka kwa idadi ya wanafunzi walioandikishwa darasa la kwanza. Kwa mfano, kabla ya kuanza kwa Mpango huo Mwaka 2015 ni wanafunzi 1,568,378 tu walioandikishwa. Aidha, baada ya kuanza utekelezaji wa Mpango Elimumsingi Bila Ada wanafunzi

2,120,667 wameweza kuandikishwa mwaka 2016. Katika kipindi cha mwaka 2015 hadi Februari 2020 jumla ya Shilingi trillioni 1.2 zimetumika kugharamia Elimumsingi bila ada.

Mheshimiwa Spika, maboresho yanayofanyika kwa upande wa elimumsingi yanazingatia uhitaji wa miundombinu ya kujifunzia na kufundishia. Kuanzia mwaka 2015 hadi Februari, 2020 vyumba vya madarasa 166,627, maabara 5,801, nyumba za walimu 57,541, matundu ya vyoo 231,612 yamejengwa na madawati 2,886,459 yamenunuliwa. Aidha, idadi ya shule za msingi zenye madarasa ya elimu ya awali imeongezeka kutoka madarasa 16,889 mwaka 2015 hadi kufikia madarasa 17,771 mwaka 2020. Kadhalika, idadi ya shule za sekondari imeongezeka kutoka shule 4,708 mwaka 2015 hadi shule 5,330 mwaka 2020.

Mheshimiwa Spika, utekelezaji wa Mpango wa Elimumsingi Bila Ada unawahakikisha watoto wote wa kitanzania hususan wale wa hali ya chini kupata haki yao ya msingi ya kupata elimu. Aidha, Mpango huo umewapunguzia wazazi mzigo wa ada na michango isiyokuwa ya lazima na hivyo kujielekeza zaidi katika kutafuta na kuwapatia mahitaji ya msingi vijana wetu kama vile sare za shule na madaftari na vitu vingine. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, kama utakavyokumbuka, katika vikao vingi vya Bunge lako Tukufu vilivyotangulia, changamoto ya maji ni suala lililoongoza kuchangiwa Bungeni na Waheshimiwa Wabunge. Katika kipindi cha takribani miaka mitano, Serikali yetu sikiu ya Awamu ya Tano imetekeleza ujenzi na ukarabati wa miradi ya maji mbalimbali ipatayo 1,423. Kati ya miradi hiyo, 792 imekamilika ikihusisha miradi 710 vijijini na miradi 82 mijini.

Vilevile Serikali ilipokea ombi la Waheshimiwa Wabunge na kuanzisha Mfuko wa Taifa wa Maji na Wakala wa Usambazaji Maji na Usafi wa Mazingira Vijijini (*RUWASA*). Lengo la Serikali ni kuhakikisha vyombo hivi vinakuwa chanzo cha uhakika cha upatikanaji wa fedha za kugharamia miradi ya maji na kusimamia utoaji wa huduma ya maji na usafi wa

mazingira. Juhudi hizi kwa pamoja zitasaidia kusogeza huduma ya maji kwa kasi zaidi karibu na wananchi katika maeneo ya mijini na vijijini.

Mheshimiwa Spika, katika kipindi cha takriban miaka mitano, Serikali imefanikiwa kulinda na kuendeleza rasilimali na maliasili za Taifa hususan madini na kuhakikisha zinatumika kwa maslahi mapana ya Taifa na watu wake. Mafanikio hayo, yametokana na Serikali kutekeleza kwa ufanisi mkubwa Mkakati wa Utekelezaji wa Sheria ya Mamlaka ya Nchi kuhusu Umiliki wa Utajiri na Maliasili za Nchi wa Mwaka 2017 na Sheria ya Mapitio na Majadiliano kuhusu Masharti Hasi katika Mikataba ya Utajiri na Maliasili za Nchi ya Mwaka 2017.

Mheshimiwa Spika, utekelezaji wa mkakati na sheria hiyo umechangia kuongezeka kwa maduhuli ya Serikali yatokanayo na sekta ya madini mwaka hadi mwaka. Maduhuli ya Serikali yameongezeka kutoka shilingi bilioni 205.2 mwaka 2015/2016, hadi Shilingi bilioni 346.6 Mwaka 2018/2019. Aidha, katika Mwaka 2019/2020 Serikali inatarajia kukusanya shilingi bilioni 471.

Mheshimiwa Spika, ukusanyaji wa mapato nao umeongezeka kutoka wastani wa Shilingi bilioni 850 kwa mwezi Mwaka 2015 hadi kufikia wastani wa shilingi triliuni 1.3 Mwaka 2019. Ongezeko hili limechangiwa na hatua za makusudi zilizochukuliwa na Serikali hususan kuimarisha matumizi ya mifumo ya ukusanyaji mapato kwa njia za kielektroniki. Lakini pia kuongeza idadi ya walipa kodi na kuibua vyanzo vipyta ya mapato. Aidha, ongezeko hilo limekuwa chachu katika utekelezaji wa miradi ya maendeleo ambayo imesaidia kuimarisha utoaji wa huduma pamoja na kusogeza huduma hizo karibu na wananchi. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, nichukue fursa hii kuwashukuru wananchi na walipa kodi wote kwa kuendelea kuitikia wito wa Serikali wa kulipa kodi kwani hatua hiyo ni muhimu katika kulifanya Taifa letu liweze kujitegemea. Serikali itaendelea kusimamia matumizi kwa lengo la kuongeza ufanisi na tija kwa mustakabali wa maendeleo ya Taifa. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, Serikali pia imefanikiwa kudhibiti matumizi ya hovyo ya fedha za Umma kwa kuziba mianya ya ukwepaji kodi sambamba na kuhakikisha kwamba wale wote wanaotakiwa kulipa kodi wanafanya hivyo. Kwa mfano, katika kipindi cha miaka mitano (2015 – 2019), Serikali imeweza kuokoa shilingi bilioni 19.83 ya mishahara kwa kuwaondoa kwenye mfumo wa malipo kama watumishi hewa 19,708 na wenyewe vyeti vya kughushi 15,411. Msingi huu tunaojenga ni muhimu katika kujenga uchumi imara na usio tegemezi. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, katika siku ya Mashujaa iliyofanyika kitaifa katika viwanja vya Mashujaa Jijini Dodoma tarehe 25 Julai, 2016, Mheshimiwa Dkt. John Pombe Joseph Magufuli, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania alitangaza na kusisitiza azma ya Serikali kuhamia Dodoma ambapo alisema, nanukuu: "...ninazungumza kutoka kwenye dhamira yangu kabla sijamaliza kipindi changu cha miaka mitano Serikali yote itakuwa hapa Dodoma..." Naomba kunukuu. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, ninapenda kuliarifu Bunge lako Tukufu na watananzia kuwa tayari Serikali imehamia Dodoma. Hadi Machi 2020, jumla ya watumishi 15,361 wa Wizara na Taasisi za Serikali wamehamia Makao Makuu ya Serikali Dodoma, ujenzi wa awali wa ofisi za Serikali katika Mji wa Serikali Mtumba umekamilika, maandalizi ya sasa ni ujenzi wa majengo ya ofisi za Serikali awamu ya pili na ujenzi wa barabara kwa kiwango cha lami katika mji huo unaendelea. Vilevile, Serikali imekamilisha mapitio ya Mpango Kabambe wa Jiji la Dodoma ambao niliuzindua tarehe 13 Februari, 2020 kwa ajili ya kusimamia shughuli za upangaji wa Jiji la Dodoma. Naielekeza Halmashauri ya Jiji la Dodoma kusimamia ipasavyo utekelezaji wa mpango huo ili kuhakikisha Jiji la Dodoma linaendelezwa kwa kuzingatia Mpango huo bila kurudia makosa yaliyofanyika katika majiji mengine. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, nyote mtakubaliana nami kuwa Serikali ya Awamu ya Tano imefanikiwa katika usimamizi madhubuti wa sheria, kanuni na taratibu za uwajibikaji wa viongozi na watumishi wa umma. Usimamizi huo, unawezesha

viongozi na watendaji wa umma kuwajibika ipasavyo kwa wananchi ambao ndiyo waajiri wao. Sambamba na hilo, nidhamu Serikalini imeongezeka kutokana na Serikali kuwachukulia hatua za kinidhamu watumishi wazembe, wadanganyifu na wasio waadilifu wameweza kuchukuliwa hatua mbalimbali.

Mheshimiwa Spika, tunapotaja mafanikio haya tuna kila sababu ya kumpongeza Mheshimiwa Dkt. John Pombe Joseph Magufuli, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwani uongozi wake mahiri na wenye uthubutu ndiyo msingi mkuu wa mafanikio yaliyopatikana. Dhana na falsafa alijojenga ya Hapa Kazi Tu imesaidia kubadili mtazamo wa Watanzania wengi ambapo sasa tunashuhudia uwajibikaji wa kiwango cha juu wa mtu mmoja mmoja, katika shughuli mbalimbali za kiuchumi na uzalishaji iwe shambani, ofisiini, kiwandani, kwenye masoko na kwingineko badala ya tabia ya awali ya baadhi ya wananchi wachache kupoteza muda mwingi katika shughuli ambazo hazina tija kwa Taifa. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, mafanikio haya katika utekelezaji wa miradi ya maendeleo na uboreshaji wa huduma za jamii yameenda sambamba na uzalishaji wa ajira zipatazo milioni 12.6 zikiwemo ajira za moja kwa moja milioni 11.7 kwenye sekta mbalimbali nchini. Kwa mfano Sekta za Afya, Elimu na Utawala zimetoa ajira za kudumu kwa kuajiri watumishi 28,403 katika mamlaka za Serikali za Mitaa.

Mheshimiwa Spika, Mradi wa reli ya kati kwa kiwango cha kimataifa umewezesha kuzalishwa ajira zipatazo 13,177 za kitaalam na zisizo za kitalaan. Kati ya hizo, ajira za kitaalam kwa wazawa ni asilimia 46.5. Pia kuititia mradi huu kumekuwa na utoaji wa zabuni zenye thamani ya Shilingi bilioni 664.7 kwa wazabuni na wakandarasi wa ndani 640.

Mheshimiwa Spika, Mradi wa umeme wa mwalimu Nyerere kuititia maporomoko ya mto Rufiji umezalisha jumla ya ajira 3,897 ikiwemo ajira za wazawa 3,422, Ufufuaji wa shirika la ndege la Tanzania (*ATCL*) pamoa na kuboresha viwanja

vya ndege jumla ya ajira 2,970,Ujenzi wa Viwanda nchini jumla ya ajira zilizozalishwa ni 41,900. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, ujenzi na uboreshaji wa miundombini mbalimbali ikiwemo Hospitali za Wilaya, vituo vya afya, Zahanati, Madarasa, Nyumba na majengo maeneo mapya ya utawala, Miradi ya barabara chini ya TARURA kwa kutumia *Force Account* jumla ya mafundi 845,348 walipata ajira za mikataba na muda.

Mheshimiwa Spika, baada ya kueleza mafanikio hayo, nyote ni mashuhuda kwamba Chama Cha Mapinduzi kiliahidhi na kimetekeleza kwa vitendo na ndiyo maana kinaendelea kuwa Chama cha mfano na cha kuigwa siyo tu Nchini, bali hata katika Bara la Afrika. Hata hivyo, mafanikio mengine yataelezwa kwa kina wakati Mawaziri watakapokuwa wanawasilisha hotuba za bajeti za Wizara zao mbele ya Bunge lako Tukufu. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, sasa naomba kutoa taarifa kuhusu utekelezaji wa Mpango wa Maendeleo wa Mwaka 2019/2020 na shughuli zitakazoteklezwa na Serikali katika Mwaka 2020/2021.

Mheshimiwa Spika, Mpango wa Maendeleo na Bajeti ya Mwaka 2020/2021 Mapendekezo ya Bajeti ya Serikali ya Mwaka 2020/2021 yamezingatia Sera na Miongozo ikiwa ni pamoja na Mpango wa Maendeleo wa Taifa wa Mwaka 2020/2021. Mpango huu ni wa mwisho katika mfululizo wa mipango ya kila mwaka wa kutekeleza Mpango wa Taifa wa Miaka Mitano (2016/2017 – 2020/2021) wenye dhima ya Kujenga Uchumi wa Viwanda ili Kuchochea Mageuzi ya Uchumi na Maendeleo ya Watu.

Mheshimiwa Spika, Mpango wa Maendeleo na Bajeti wa Mwaka 2020/2021 umezingatia yafuatayo: Dira ya Taifa ya Maendeleo ya Mwaka 2025 yenye lengo la kuiwezesha Tanzania kuwa Nchi ya hadhi ya uchumi wa kipato cha kati inayoongozwa na viwanda ifikapo Mwaka 2025. Mpango wa pili wa Maendeleo wa Taifa wa Miaka Mitano, 2016/2017 –

2020/2021; Sera na Mikakati mbalimbali; Malengo ya Maendeleo Endelevu na Makubaliano ya Kikanda na Kimataifa ambayo Serikali imeyaridhia. Aidha, Ilani ya Uchaguzi ya Chama Cha Mapinduzi ya Mwaka 2015 - 2020 imezingatiwa pamoja na Maelekezo ya Serikali yaliyoainishwa na Mheshimiwa Rais wakati wa uzinduzi rasmi wa Bunge la 11 mwezi Novemba, 2015.

Mheshimiwa Spika, lakini vilevile, Mpango umezingatia hali halisi ya utekelezaji wa Mpango wa Maendeleo wa Mwaka 2019/2020; changamoto zilizojitokeza; hali ya uchumi kitaifa, kikanda na kidunia kwa Mwaka 2019 na maoteo ya ukuaji wa uchumi kwa Mwaka 2020.

Mheshimiwa Spika, nitumie fursa hii kueleza kwa kifupi vipaumbele vyta Mpango wa Maendeleo wa Mwaka 2020/2021 ambavyo vimejikita katika masuala makuu manne yafuatayo:

- (i) Ni Ujenzi wa Msingi wa Uchumi wa Viwanda;
- (ii) Kufungamanisha ukuaji wa uchumi na maendeleo ya watu;
- (iii) Uboreshaji wa mazingira wezeshi kwa uendeshaji wa biashara na uwekezaji na Kuimarisha usimamizi wa utekelezaji wa Mpango wa Maendeleo.

Mheshimiwa Spika, katika kufikia malengo ya Mpango, Serikali itaendelea kutoa kipaumbele cha pekee katika kutekeleza miradi ya kielelezo ya kimkakati ikiwa ni pamoja na ujenzi wa reli ya Kati ya Kiwango cha Kimataifa; Mradi wa kufua umeme wa Maji wa Julius Nyerere – MW 2,115; Kuboresha Shirika la Ndege la Tanzania Mradi wa Ujenzi wa Bomba la Mafuta Ghafi kutoka Hoima nchini Uganda hadi Mkoani Tanga hapa Tanzania. Uanzishwaji wa kanda maalum za Kiuchumi na Kusomesha wataalam wengi zaidi katika fani za Ujuzi Adimu na Maalum. Hatua hizo, zitasaidia kufungamanisha ujenzi wa miundombinu wezeshi na sekta nyingine za kiuchumi ili kuongeza kasi ya maendeleo, ajira

na kipato na hatimaye kuliwezesha Taifa kupiga hatua kubwa za kimaendeleo.

Mheshimiwa Spika, nitumie fursa hii kutoa rai kwa Wafanyabiashara, Wawekezaji, Wajasiriamali, Waheshimiwa Wabunge, Viongozi na Watendaji wa Serikali, Taasisi za Dini, Asasi za Kiraia, Washirika wa Maendeleo, na Wananchi wote kwa ujumla, kushirikiana na Serikali bega bega katika kutekeleza Mpango huu ili azma ya kufikia uchumi wa katii unaoongozwa na viwanda ifikapo Mwaka 2025 iweze kutimia.

Mheshimiwa Spika, Hali ya Uchumi, uchumi wa Taifa umeendelea kuimarika ambapo katika kipindi cha Januari hadi Septemba 2019, ukuaji halisi wa Pato la Taifa ulifikia asilimia 6.9. Baadhi ya shughuli zilizochangia ukuaji huo kwa viwango vikubwa ni pamoja na ujenzi asilimia 14.8 uchimbaji wa madini na mawe asilimia 12.6; habari na mawasiliano asilimia 11, uchukuzi na uhifadhi wa mizigo asilimia 8.8 na huduma za usambazaji maji asilimia 8.5.

Mheshimiwa Spika, katika kipindi cha kuanzia Julai hadi Januari 2020, mfumuko wa bei ulikuwa wastani wa asilimia 3.7. Kiwango hiki ni chini ya lengo la Taifa la kipindi cha muda wa katili asilimia 5, na chini ya malengo ya asilimia 7.0 kwa nchi za Jumuiya ya Maendeleo Kusini mwa Afrika (*SADC*) na asilimia 8 kwa Jumuiya ya Afrika Mashariki. Hali hii inatokana na utekelezaji madhubuti wa sera za fedha na za bajeti, uhakika wa upatikanaji wa chakula na utulivu wa thamani ya shilingi ya Tanzania dhidi ya sarafu nyingine duniani.

Mheshimiwa Spika, katika Mwaka 2020/2021, Serikali itaendelea kuimarisha sekta za uzalishaji na utoaji huduma ili kuongeza kasi ya ukuaji wa Pato Halisi la Taifa.

Mheshimiwa Spika, uhakika wa upatikanaji wa chakula na utulivu wa thamani ya shilingi ya Tanzania dhidi ya sarafu nyingine duniani; katika mwaka 2020/2021, Serikali itaendelea kuimarisha sekta za uzalishaji na utoaji huduma ili kuongeza kasi ya ukuaji wa Pato Halisi la Taifa. Vilevile, Serikali

itaendelea kutekeleza mkakati na sera za uchumi wa jumla ili kukidhi kasi ya mfumuko wa bei na kuwa na mwenendo tulivu wa uchumi. Serikali pia itaendelea kuimarisha Mfumo wa Serikali wa Kielektroniki wa Ukusanyaji wa Mapato kwa kuharakisha ufungaji wa mfumo huo katika Wizara na taasisi zote za Serikali.

Mheshimiwa Spika, Hali ya Kisiasa; Ofisi ya Msajili wa Vyama vya Siasa imeendelea kusimamia utekelezaji wa sheria na maadili ya vyama vya siasa ili kuhakikisha kwamba demokrasia ya vyama vingi inaimarika pamoja na kudumisha amani, utulivu na mshikamano uliopo katika nchi yetu. Katika mwaka 2020/2021, Ofisi ya Msajili wa Vyama vya Siasa itaendelea kusimamia utekelezaji wa utoaji elimu kuhusu Sheria ya Vyama vya Siasa, Kanuni za Maadili ya Vyama vya Siasa, pamoja na Sheria ya Gharama za Uchaguzi katika uchaguzi mkuu wa mwaka 2020. Vilevile, Ofisi ya Msajili wa Vyama vya Siasa itaendelea kufuatilia uhai wa vyama vya siasa vyenye usajili wa kudumu kwa lengo la kuwawezesha wananchi kushiriki na kutoa michango yao ya mawazo na fikra kuitia vyama hivyo ili kuimarisha demokrasia na maendeleo nchini.

Mheshimiwa Spika, Uchaguzi wa Serikali za Mitaa; Serikali imeratibu na kusimamia Uchaguzi wa Serikali za Mitaa uliofanyika tarehe 24 Novemba, 2019. Uchaguzi huo ulihusisha Mitaa 4,263, Vijiji 12,319 na Vitongoji 64,384. Katika uchaguzi huo, Chama cha Mapinduzi kilipata ushindi wa kishindo wa asilimia 99.9 kwa nafasi zote zilizogombewa. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, matokeo hayo yameendelea kudhihirisha imani kubwa walionayo wananchi kwa Chama cha Mapinduzi. Hivyo, basi natoa rai kwa wananchi kuendelea kushirikiana na viongozi waliochaguliwa ili kutimiza azma ya kuwaletea maendeleo.

Mheshimiwa Spika, Maandalizi ya Uchaguzi Mkuu; Tume ya Taifa ya Uchaguzi imeanza maandalizi ya Uchaguzi Mkuu utakaofanyika mwezi Oktoba, 2020. Pamoja na mambo mengine, maandalizi hayo yanahusisha

Zoezi la Kuboresha Daftari la Kudumu la Wapiga Kura liliofanyika nchi nzima. Awamu ya kwanza ilizinduliwa tarehe 18 Julai, 2019, Mkoani Kilimanjaro na kukamilika tarehe 23 Februari, 2020 katika Mkoa wa Dar es Salaam.

Mheshimiwa Spika, uboreshaji wa daftari hili ulihusisha uandikishaji wa wapiga kura wapya ambaao wametimiza umri wa miaka 18 au watatimiza umri huo ifikapo siku ya uchaguzi mkuu mwaka huu wa 2020. Urekebishaji wa taarifa za wapiga kura walioandikishwa katika uchaguzi mkuu wa mwaka 2015 pamoja na ufitaji wa taarifa za wapiga kura waliopoteza sifa za kuwemo katika Daftari la Kudumu la Wapiga Kura. Katika zoezi hilo jumla ya wapiga kura 10,285,732 wameandikishwa na kati yao, wapiga kura wapya ni 7,043,247. Wapiga kura walioboreshewa taarifa zao ni 3,225,778 na wapiga kura waliofutwa kwenye Daftari la Kudumu la Wapiga Kura kutokana na kupoteza sifa ni 16,707. Zoezi la Uboreshaji wa Daftari la Kudumu la Wapiga Kura kwa Awamu ya Pili linatarajiwu kuanza tarehe 5 Aprili 2020 na kukamilika tarehe 26 Juni 2020. Zoezi hili litaenda sambamba na uhakiki wa taarifa za wapiga kura katika daftari hilo. Natoa wito kwa wananchi kujitokeza kwa wingi kujandikisha na kuboresha taarifa zao katika daftari hilo ili waweze kutumia haki yao ya kikatiba ya kuchagua viongozi wanaowataka.

Mheshimiwa Spika, nawasihi Watanzania kushiriki kikamilifu kwenye uchaguzi huo ambaao ratiba itatolewa na Tume ya Uchaguzi. Viongozi wa Vyama vya Siasa waoneshe mfano wa kuendesha siasa za kistaarabu zenyenye lengo la kuwaunganisha Watanzania na siyo kuwatenganisha. Hakuna kiongozi aliywahi kupata sifa nzuri kwa kuwa chanzo cha mifarakano. Hivyo basi, tudumishe utulivu, amani, mshikamano pamoja na ustaarabu wetu wa kitanzania katika kipindi chote cha kampeni na Uchaguzi Mkuu ili kulifanya Taifa letu kuendelea kuwa kisiwa cha amani na mfano wa kuigwa barani Afrika na duniani kwa ujumla. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania limeendelea kutimiza wajibu wake wa kikatiba na kikanuni kwa kufanya mikutano mitatu na huu ukiwa ni

wa nne kwa mwaka 2019/2020. Ofisi ya Bunge kwa sasa inatekeleza shughuli za Bunge kwa kutumia TEHAMA kuititia mfumo wa Bunge Mtandao (*e-Parliament*) uliotengenezwa na kusimamiwa na wataalam wa ndani wa Ofisi ya Bunge, hongera sana. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, hivi sasa Wizara, Idara na Taasisi za Serikali zinawasilisha taarifa na nyaraka mbalimbali Bungeni kwa kutumia nakala tete badala ya nakala ngumu. Hatua hii imeweza kupunguza gharama za uendeshaji hivyo kuokoa kiasi kikubwa cha fedha cha takribani shillingi bilioni 2 kilichokuwa kinatumika kila mwaka katika uandaaji na uhifadhi wa nyaraka mbalimbali zinazoandalishiwa kwa ajili ya utekelezaji wa shughuli mbalimbali za Bunge. Pia, Ofisi ya Bunge imeweza kuzindua *Bunge Mobile Application* ambayo imewezesha Waheshimiwa Wabunge pamoja na wadau wengine kupata kwa urahisi taarifa mbalimbali kama vile orodha ya shughuli za Bunge (*Order Paper*), *hansard* pamoja na sheria na miswada. Ni matumaini yangu kwamba Bunge lako Tukufu litaendelea kuisimamia Serikali ili itekeleze majukumu yake ipasavyo.

Mheshimiwa Spika, Mahakama; katika kuhakikisha wananchi wanapata haki kwa wakati na kwa gharama nafuu, Mahakama imeendelea kuimarisha huduma kwa kuweka mifumo na taratibu mbalimbali za kuwafikia wananchi katika maeneo yote nchini ili kupunguza mlundikano wa mashauri. Moja ya utaratibu unaotumika ni kuwatumia Mahakimu wenye Mamlaka ya Ziada (*Extended Jurisdiction*) kusikiliza mashauri ya Mahakama Kuu ambapo Mahakimu 195 walipewa mamlaka hiyo ya ziada. Katika kipindi cha mwaka 2019 mashauri 1,132 yalisikilizwa na kumalizwa kwa utaratibu huo.

Mheshimiwa Spika, Mahakama imeendelea kuboresha miundombinu katika ngazi mbalimbali nchini ikiwa ni pamoja na ujenzi na ukarabati wa majengo. Katika kutekeleza hilo, ujenzi wa majengo ya Mahakama Kuu katika Mikoa ya Kigoma na Mara, Mahakama ya Hakimu Mkazi katika Mikoa ya Simiyu, Manyara, Geita, Njombe, Mahakama

za Wilaya 14, pamoja na Mahakama za Mwanzo za Mlowo, Magoma, Uyole, Mtowisa, Msanzi na Mkunya umekamilika.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2020/2021, Serikali itaendelea kulinda, kuheshimu na kuzingatia haki za binadamu na kuimarisha mifumo ya usimamizi wa sheria na utoaji haki kwa kutumia TEHAMA. Vilevile, Serikali itaendelea kufanya maboresho katika mfumo wa Haki Jinai ili kuweseha shughuli za uchunguzi, upelelezi, uendeshaji wa mashauri na usikilizaji wa mashauri kufanyaika kwa ufanisi mkubwa.

Mheshimiwa Spika, Uwekezaji; Serikali imeendelea kuratibu na kusimamia shughuli za kuhamasisha na kufanikisha wawekezaji wa ndani na nje ya nchi kwa lengo la kuvutia mitaji, teknolojia na ujuzi ambaeo ni chachu ya maendeleo katika sekta mbalimbali. Serikali inaendelea kuhakikisha mazingira ya uwekezaji na blashara yanakuwa rafiki hapa nchini. Serikali imeendelea kutumia vyema uwepo wa fursa nyingi za uwekezaji na kuwepo kwenye eneo la kimkakati la kijigrafia kwa kuhudumia nchi zipatazo sita (6) ambazo hazipo kwenye mwambao wa bahari. Hali hii inaifanya nchi yetu kuwa ni lango la biashara ya kimataifa hususani katika ukanda wa nchi za Afrika Mashariki na Kati pamoja na Kusini mwa Afrika. Aidha, Serikali inaendelea kuboresha mazingiza ya uwekezaji na biashara ikiwemo kufanya tathmini ya utekelezaji wa Sera ya Taifa ya Uwekezaji ya mwaka 1996 ili kubaini changamoto za kisera, kisheria na kiutendaji zitakazopelekea kuhuisha Sera ya Uwekezaji ya Mwaka 1996 na Sheria ya Uwekezaji ya Mwaka 1997.

Mheshimiwa Spika, vilevile Serikali imeendelea kuratibu utekelezaji wa Kuboresha Mfumo wa Udhibiti wa Biashara (*Blueprint*) ambapo kupitia Mpango huo Serikali imefuta tozo 54 katika mwaka wa fedha 2019/2020 pamoja na kuondoa mwingilio wa majukumu kati ya Shirika la Viwango Tanzania (*TBS*) na Mamlaka ya Dawa na Vifaa Tiba (*TMDA*) ili kurahisisha shughuli za uwekezaji na biashara.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2019/2020, Serikali pia imeratibu mikutano ya mashauriano kati yake na

wawekezaji na wafanyabiashara kutoka ndani na nje ya nchi kwa lengo la kusikiliza na kutatua changamoto mbalimbali wanazokabiliana nazo. Katika mikutano hiyo hoja nyingi na changamoto zilipatiwa ufumbuzi na nyingine kutolewa ufanuzi ambapo pia wafanyabiashara na wawekezaji walikumbushwa pia wajibu wao katika uendeshaji biashara na uwekezaji wao. Serikali kupitia Ofisi ya Waziri Mkuu (Uwekezaji) kwa kushirikiana na Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki iliendesha mikutano kati ya Serikali na wawekezaji kutoka China, Uingereza na Marekani walioewekeza hapa nchini kwa nia ya kusikiliza na kutatua changamoto zinazowakabili na kupata maoni na ushauri zaidi.

Mheshimiwa Spika, katika kuongeza tija ya kushughulikia malalamiko ya wawekezaji, Serikali kwa kushirikiana na Taasisi ya Sekta Binafsi Tanzania (*TPSF*) imeandaa mfumo wa kielektroniki wa kupokea malalamiko na kupata mrejesho wa wawekezaji ambao utaanza kutumika katika mwaka 2020/2021. Mfumo huo utapokea maoni na ushauri kwa njia ya haraka na kuleta ufanisi katika kuwashudumia.

Mheshimiwa Spika, Mazingira ya uwekezaji na ufanyaji biashara nchini yameendelea kuimarika. Taarifa ya Benki ya Dunia ya Wepesi wa Kufanya Biashara ya mwaka 2020 iliyotolewa Oktoba, 2019 inaonesha kuwa Tanzania imepanda kwa nafasi tatu (3) juu kutoka nafasi ya 144 hadi kufikia nafasi ya 141. Lengo letu ni kufikia nafasi ya juu kufikia mMwaka 2025. Naziagiza Wizara na Taasisi zote za Serikali zinazohusika na utekelezaji wa maboresho na kuweka mazingira mazuri na rafiki ya kuratibu kwa ukaribu ili kufungua fursa zaidi kutoka kwa wawekezaji kutoka pande zote.

Mheshimiwa Spika, kwa upande wa kukuza uwekezaji, Serikali kupitia Ofisi ya Waziri Mkuu imeendelea kuhamasisha mikoa yote nchini kuandaa Makongamano ya Uwekezaji sambamba na kuzindua Miongozo ya Uwekezaji ya Mikoa inayobainisha fursa walizonazo kwenye mikoa hiyo pamoja na maeneo ya uwekezaji yaliyotengwa ili kuhamasisha na

kuvutia uwekezaji zaidi katika Mikoa hiyo. Hadi sasa, mikoa 14 ndio imezindua miongozo hiyo na mikoa yote ambayo hajakamilisha kuandaa miongozo hiyo ifanye hivyo kabra ya Septemba, 2020. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, Ofisi ya Waziri Mkuu imeendelea kuratibu makongamano ya uwekezaji yaliyofanyika hapa nchini kama vile Kongamano la Biashara na Uwekezaji kati ya Tanzania na Uganda, Tanzania na Afrika Kusini, Afrika Mashariki na Sweden na Makongamano mengine yaliyofanyika nje ya Nchi kama vile Tanzania na Burundi, *Investment for Africa* liliyofanyika nchini Misri, Kongamano liliyoandaliwa na Benki ya Maendeleo ya Afrika liliyofanyika Afrika Kusini, na Kongamano kati ya Pakistani na Afrika, liliyofanyika nchini Kenya. Tumeendelea kupokea wawekezaji wanaofika nchini kwa ajili ya kutafuta fursa za uwekezaji kutoka nchi mbalimbali.

Mheshimiwa Spika, kupitia Kitengo cha Huduma za Mahala Pamoja (*One Stop Facilitation Centre*) kilichopo Kituo cha Uwekezaji Tanzania (*TIC*) chenye watendaji kutoka Taasisi 10 wameendelea kutoa huduma za muda mfupi kwa wawekezaji wetu wanaofika hapa nchini kupitia Kituo hicho hadi kufikia Februari 2020, jumla ya miradi 146 yenye thamani ya Dola za Marekani milioni 1,514.57 inayotegemewa kutoa ajira za moja kwa moja zipatazo 26,384 ilisajiliwa ambapo miradi 52 sawa na asilimia 36 inamiliikiwa na wageni, miradi 50 sawa na asilimia 34 inamiliikiwa na Watanzania na miradi 44 sawa na asilimia 30 inamiliikiwa kwa ubia kati ya wageni na Watanzania. Katika miradi iliyosajiliwa katika mwaka huu wa fedha miradi 94 sawa na asilimia 65 ya miradi yote inahusisha sekta ya uzalishaji viwandani.

Mheshimiwa Spika, Sekta ya Uzalishaji; Viwanda; kwa kutambua umuhimu wa viwanda Serikali imeendelea kuchukua hatua madhubuti ili kuwezesha sekta hii kukua kwa haraka na kutoa mchango mkubwa zaidi katika Pato la Taifa pamoja na kupunguza umaskini. Katika kutekeleza dhana hii kwa vitendo katika mwaka 2019/2020, Serikali iliimarisha Kiwanda cha Ngozi na Bidhaa za Ngozi cha Karanga Mkoani

Kilimanjaro na kuimarisha Shirika la Nyumba (Pwani) ili kuongeza uzalishaji ikiwemo wa magari ya zimamoto ambayo yanaunganishwa hapa nchini. Vilevile, ada na tozo 54 zilifutwa ili kuondoa kero na urasimu kwa wafanyabiashara na wawekezaji katika sekta hii.

Mheshimiwa Spika, aidha, uzalishaji katika baadhi ya viwanda uliana ikiwa ni pamoja na *Pipe Industries Company Limited* (Dar es Salaam), Kiwanda cha Chai cha Kabambe (Njombe), kiwanda cha *Yalin Cashewnut Company Limited* pale Mtware, kiwanda cha *21st Century Food and Packaging* kilichopo Dar es Salaam, Kiwanda cha Kusaga Mahindi (*MeTL*, Dar es Salaam), Kiwanda cha Bidhaa za Plastiki cha *Plasco Pipelines Company Limited* kilichopo Dar es Salaam, Kiwanda cha Kupakia na Kuhifadhi Parachichi, Rungwe Avocado na Kiwanda cha Kuchakata Parachichi kwa ajili ya kutengeneza mafuta (*KUZA Afrika*).

Mheshimiwa Spika, kutokana na jitihada kubwa zinazoendelea kufanywa na Serikali za kujenga uchumi wa viwanda, jumla ya viwanda vipyta zaidi ya 4,000 vimejengwa katika mikoa mbalimbali. Viwanda vilivyojengwa vinazalisha bidhaa za ujenzi pamoja na viwanda vya kusindika mazao ya kilimo ikiwemo nafaka, matunda, mafuta ya kupikia na bidhaa za ngozi. Ujenzi wa viwanda vipyta nchini katika kipindi cha Serikali ya Awamu ya Tano, umechangia kupatikana kwa ajira mpya 482,601 nchi nzima. (*Makof!*)

Mheshimiwa Spika, sekta ya kilimo ni muhimu katika kuhakikisha usalama wa chakula, kupambana na umaskini, kuongeza ajira pamoja na kuleta maendeleo ya nchi kwa ujumla. Kwa kulitambua hilo, Serikali ya Awamu ya Tano imeendelea kutoa kipaumbele kikubwa kwenye sekta hiyo kwa lengo la kuwawezesha wakulima kupata pembejeo na zana za kisasa ili kuongeza tija katika kilimo na hivyo kuleta mageuzi ya kiuchumi.

Mheshimiwa Spika, Hali ya Upatikanaji wa Chakula; Pamoja na mambo mengine hususan kuimarika kwa hali ya hewa, mageuzi yanayofanywa katika sekta ya kilimo,

yamechangia kuimarika kwa hali ya upatikanaji wa chakula nchini na upatikanaji wa malighafi za viwanda, sambamba na kuongeza tija kwa wakulima. Katika msimu wa kilimo wa mwaka 2018/2019 uzalishaji wa mazao ya chakula kitaifa ulikuwa tani milioni 16.3 ikilinganishwa na mahitaji halisi ya tani milioni 13.6. Uzalishaji huo umeihakikishia nchi utoshelevu wa chakula kwa asilimia 118 kwa msimu wa kilimo wa mwaka 2019/2020.

Mheshimiwa Spika, Upatikanaji wa Pembejeo za Kilimo; Serikali imeendelea kuhamasisha matumizi ya pembejeo na mbinu bora za kilimo na teknolojia kwa lengo la kukifanya kilimo chetu kuwa cha kisasa zaidi na chenye tija. Hadi kufikia Februari, 2020 upatikanaji wa mbegu bora za mazao umefikia tani 71,207 ikilinganishwa na tani 57,023 za msimu wa mwaka 2018/2019. Kati ya mbegu hizo, tani 66,031 zimezalishwa nchini ambayo ni sawa na asilimia 93 na tani 5,175 sawa na asilimia 7.0 zimeingizwa kutoka nje ya nchi.

Mheshimiwa Spika, Serikali imeendelea kuimarisha upatikanaji wa mbolea nchini kwa kutumia Mfumo wa Ununuzi wa Mbolea kwa pamoja ambao umesaidia kupunguza bei ya mbolea kwa wakulima. Kutokana na mfumo huo, upatikanaji wa mbolea hadi Februari, 2020 umefikia tani 516,813 sawa na asilimia 89 ya lengo la tani 586,604. Kwa kuwa mbolea hizo hutumika kulingana na hatua mbalimbali za ukuaji wa mazao, Serikali inaendelea kuhakikisha asilimia 11 iliyobaki inapatikana na kusambazwa kwa wakulima kwa wakati. Aidha, Serikali imeendelea kuratibu upatikanaji wa viuatilifu ambapo hadi Januari, 2020, jumla ya tani 8,719 za viuatilifu zimeingizwa nchini ili kukidhi visumbufu vyta mimea na mazao.

Mheshimiwa Spika, katika kipindi cha Julai, 2019 hadi Februari, 2020, Benki ya Maendeleo ya Kilimo Tanzania imetua mikopo ya shilingi bilioni 34 kwa miradi ya kilimo 38 na kufanya jumla ya mikopo iliyotolewa kufikia shilingi bilioni 160.6 toka benki ilipoanza utoaji wa mikopo. Mikopo iliyotolewa imewanufaisha wakulima wadogo, wa kati na wakubwa wapatao milioni 2.1 na mazao ya kilimo, mifugo na uvuvi

pamoja na viwanda vidogo vya uchakataji wa mazao navyo pia vimepata mikopo. Katika kipindi hicho *TADB* imetoa mikopo ya ziada ya shilingi bilioni 31.77 kupitia Mfuko wa Dhamana kwa Wakulima Wadogo. Mikopo hiyo imewanufaisha wakulima wapatao 5,080, biashara ndogo na za katи za kilimo zipatazo 30, Vyama vya Msingi (*AMCOS*) 20 katika mikoa mbalimbali nchini na kufanikisha ununuzi wa matreka 19 katika mikoa hiyo.

Mheshimiwa Spika, Uzalishaji wa Zao la Chikichi; Serikali imedhamiria kumaliza tatizo la upatikanaji mafuta ya kula nchini kwa kuendeleza zao la chikichi sambamba na mazao mengine yanayozalisha mafuta. Uendelezaji wa zao la chikichi unahusisha kupanda kwa wingi miche mipyä yenye uzalishaji wenye tija. Serikali kupitia Taasisi ya Utafiti (*TARI*) imeanza uzalishaji wa mbegu bora za chikichi aina ya *TENERA* inayotoa mafuta mengi. Lengo ni kuzalisha mbegu bora na za kutosha zitakazowezesha wakulima kuongeza uzalishaji na hivyo kujiongezea kipato na kupunguza matumizi ya fedha za kigeni kuagiza mafuta ya kula kutoka nje ya nchi. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, hadi tarehe 15 Februari, 2020, mbegu 1,525,017 zimezalishwa ambazo zitatosha kupanda eneo la ekari 30,500. Tayari mbegu 1,026,111 zimesambazwa kwa ajili ya kuziotesha ili miche bora iweze kusambazwa kwa wakulima. Usambazaji kwa ajili ya uoteshaji umefanyika katika Halmashauri za Mkoa wa Kigoma na taasisi nyingine ikiwemo Magereza ya Kwitanga na llagala na JKT Bulombora. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2020/2021, Serikali itaendelea kuimarisha huduma za ugani, kilimo cha umwagiliaji, ushirika na upatikanaji wa pembejeo ikiwa ni pamoja na mbegu bora za mazao. Aidha, itajenga na kukarabati miundombinu ya kuhifadhi mazao ya kilimo na masoko.

Mheshimiwa Spika, zao la mkonge. Sote ni mashahidi kuwa zao la mkonge lilikatiwa tamaa na wakulima na wakulima wengi waliacha kulima zao hili. Serikali imeanza kuchukua hatua za kufufua kilimo cha mkonge na masoko

yake. Tunafufua Mamlaka ya Mkonge ili itambue mashamba yake na mali zake zote ili ianze kuhamasisha wakulima wadogo na wakubwa na kuwakaribisha wawekezaji wa sekta ya mkonge. Tunaimarisha Taasisi ya Utafiti ya Mlingano ili ianze kuzalisha miche zaidi na kuisambaza kwa wakulima. Natoa wito kwa Wizara, Wakuu wa Mikoa inayolimwa mkonge kutambua wakulima wa mkonge na wapate msaada wa kitaalam ili waweze kulima zao hili. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, mifugo. Serikali imeendelea kuimarisha sekta ya mifugo nchini ili iweze kutoa mchango mkubwa zaidi katika pato la taifa na kutoa fursa za ajira. Ili kufikia lengo hili, Serikali imehamasisha wafugaji kuendelea kuimarisha ufugaji wa kisasa, kuchakata bidhaa za mifugo kwa ajili ya mahitaji ya ndani, ikiwemo lishe bora na kuuza nje pamoja na kuhamasisha uwekezaji wa sekta binafsi. Aidha katika mwaka 2019/2020, Serikali imekarabati majosho 292, inaendelea na ukurabati wa majosho 207 na kuendelea na ujenzi wa majosho mapya 84, katika Halmashauri mbalimbali hapa nchini. Hatua hi imewezesha kuongezeka kwa majosho yanayofanya kazi kutoka 1,486 mwaka 2018, hadi majosho 1,738, mwaka 2019/2020. Aidha, Serikali imenunua lita 12,549 za dawa za kuogeshea mifugo.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2020/2021 Serikali itaendelea kuhimiza ufugaji wa kisasa pamoja na kuimarisha afya ya migufo kwa kuwezeshwaa upatikanaji wa huduma za chanjo na tiba kwa kuimarisha vituo vya utengenezaji wa chanjo za mifugo. Aidha, Serikali itaendelea kuhakikisha upatikanaji wa malisho kwa kutambua, kutenga, kumilikisha, kusimamia na kuendeleza maeneo ya malisho. Vilevile huduma za ugani zitaboreshwa na mafunzo kwa ufugaji na Maafisa Ugani yatatolewa ili kuwapatia maarifa na teknolojia zaidi kwa lengo la kuongeza tija.

Mheshimiwa Spika, uvuvi. Serikali imeendelea kuboresha sekta ndogo ya uvuvi ili iweze kuchangia kikamilifu katika pato la taifa na ajira kwa ujumla. Hatua zilizochukuliwa ni pamoja na kuondolewa kwa kodi katika zana na malighafi za uvuvi, kupambana na uvuvi haramu, kuboreshwa kwa

mialo ya kupokelea samaki kuwa ya kisasa, kuhamasisha uwekezaji katika ukuzaji wa viumbi maji pamoja na kuhamasisha sekta binafsi kuwekeza katika viwanda vya kuchakata samaki. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2020/2021, Serikali itaimarisha sekta ya uvuvi ili kuongeza mchango wa sekta hiyo katika pato la taifa na kuwaongezea wavuvi kipato. Hatua zitakazochukuliwa zitahusisha utekelezaji wa mkakati wa kujenga na kuboresha miundombinu ya uvuvi; mkakati wa kufufua Shirika la Uvuvu Tanzania; kuweka mazingira bora katika uvuvi wa Bahari Kuu kwa kuweka vivutio na wawekezaji; kuendelea kupambana na wavuvi haramu na kuhamasisha matumizi endelevu ya rasilimali za uvuvi, uhifadhi na uchakataji wa samaki ili kuimarissha mnyororo wa thamani.

Mheshimiwa Spika, sekta ya utalii. Sekta ya utalii nchi imeendelea kuimarisika ikichagizwa pamoja na mambo mengine na uwekezaji mkubwa uliofanyika katika miundombinu ya usafiri na usafirishajii na utoaji huduma katika mwaka 2019. Idadi ya watalii walioingia nchini ilifikia 1,510,151 ikilinganishwa na 1,505,702 ya mwaka 2018. Ongezeko la idadi ya watalii nchini limeongeza mapato ya Serikali yatokanayo na utalii kutoka Dola za Marekani bilioni 2.4 mwaka 2018 hadi Dola za Marekani bilioni 2.6 mwaka 2019.

Mheshimiwa Spika, katika hatua nyingine ya kuimarissha shughuli za utalii nchini, Serikali imepandisha hadhi Mapori ya Akiba sita ambayo ni Burigi (Chato), Ibanda (Kyerwa), Rumanyika (Karagwe), Nyerere, Mto Ugalla na Kigosi kuwa Hifadhi za Taifa. Lengo ni kuimarissha sekta ya utalii kwa kuwa na maeneo mengi ya hifadhi na vivutio vya watalii yatakayosaidia kuongeza wigo wa utalii na mapato yatokanayo na sekta hiyo. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2020/2021, Serikali itaendelea kuvitangaza vivutio vya utalii ndani na nje ya nchi hususan kwenye masoko ya kimkakati. Pia tutaimarisha Hifadhi za Taifa mpya sita na kukuza wigo wa mazao ya utalii na kuweka mazingira wezeshi ili sekta binafsi iweze kushiriki

kikamifu katika uwekezaji kwenye utalii. Kadhalika maeneo mengine yatakayopewa kipaumbele ni utalii wa meli, mikutano, fukwe, utamaduni, malikale, ikolojia na jiolojia. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, sekta ya madini. Usimamizi mzuri wa mikakati na sheria za ulinzi wa rasilimali na maliasili zetu umekuwa chachu ya kukua na kuimarika kwa sekta ya madini nchini. Usimamizi huo umeifanya sekta hiyo kutoa mchango mkubwa katika ukuaji wa Pato la Taifa. Mathalan, katika kipindi cha nusu ya kwanza ya mwaka 2019/2020 mchango wa sekta ya madini ulikuwa asilimia 13.7. Katika kipindi hicho, sekta ya madini ilishika nafasi ya pili katika kuchangia Pato la Taifa baada ya sekta ya ujenzi iliyochangia asilimia 16.5. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, hadi kufikia Januari 2020, maduhuli ya Serikali yaliyokusanya kupitia Sekta ya Madini ni Shilingi bilioni 284.4. Kiwango hicho ni sawa na asilimia 60.4 ya lengo la mwaka la kukusanya Shilingi bilioni 470.89. Mafanikio hayo, ni ishara tosha ya kuendelea kuimarika kwa sekta hii ya madini kufuatia usimamizi thabiti unaowekwa na Serikali. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, Serikali imeanzisha masoko ya madini nchini kote kwa lengo la kupata takwimu sahihi za mauzo ya madini, kuwasaidla wachimbaji wadogo kupata soko la uhakika, kupata bei stahiki kwa bidhaa za madini na kuondoa tatizo la utoroshaji na biashara haramu ya madini. Hatua hiyo imewezesha kuongezeka kwa mapato ya Serikali kupitia tozo za mrabaha na ada ya ukaguzi wa mauzo ya madini kwenye masoko.

Mheshimiwa Spika, hadi Januari 2020, jumla ya masoko ya madini 28 na vituo vidogo vya ununuzi wa madini 28 vimeanzishwa nchini. Kupitia masoko na vituo hivyo, katika kipindi cha Machi 2019 hadi Januari 2020, jumla ya kilogramu 9,237.34 za dhahabu; karati 12,973.14 za madini ya almasi; kilogramu 20,099.17 za madini ya bati na kilogramu 514,683.28 za madini ya vito mbalimbali ziliuzwa na kuipatia Serikali

mapato ya shilingi bilioni 66.57 ambazo zimetokana na mrabaha, ada ya ukaguzi na ushuru wa Halmashauri.

Mheshimiwa Spika, masoko ya madini yamekuwa na mchango mkubwa katika kuimarisha upatikanaji wa takwimu sahihi za madini tofauti na ilivyokuwa awali kabla ya kuanzishwa kwake. Masoko hayo yana ulinzi na usalama wa kutosha na sifa zote za kimataifa zinazohitajika katika kuendesha biashara ya madini. Hivyo, natoa rai kwa wadau wa ndani na nje ya nchi kutumia masoko na vituo vyetu ambavyo vinaendeshwa kwa misingi ya kisheria kwa kuzingatia ushindani na uwazi wa kibiashara. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, katika mwaka huu wa fedha wa 2020/2021, Serikali itaendelea kuimarisha uchimbaji mdogo na wa kati wa madini nchini; ukusanyaji wa mapato yatokanayo na madini; kuhamasisha uwekezaji katika sekta ya madini; kuimarisha shughuli za ugani na utafiti na uongezaji thamani madini na masoko.

Mheshimiwa Spika, nishati. Hali ya upatikanaji wa umeme nchini imeendelea kuimarika na kuchangia katika ukuaji wa uchumi na ustawi wa Taifa kwa ujumla. Uwezo wa mitambo ya kufua umeme nchini ni megawati 1,602.32 ambapo kati ya hizo megawati 1,565.72 zipo katika Mfumo wa Gridi ya Taifa na megawati 36.6 zipo nje ya Mfumo wa Gridi ya Taifa. Aidha, hali ya maji katika mabwawa ya Mtera, Kidatu, Kihansi, Nyumba ya Mungu na New Pangani Falls imeendelea kuwa nzuri na hivyo kutuhakikishia kuwa na umeme wa uhakika. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, pamoja na kuelezea juu ya mafanikio tuliyoyapata katika utekelezaji wa Mradi wa Kufua Umeme wa Maji wa Julius Nyerere hapo awali, Serikali vilevile inatekeleza Mradi wa Kuzalisha Umeme wa Rusumo utakaozalisha megawati 80. Kukamilika kwa miradi hii na mingine itaimarisha upatikanaji wa umeme nafuu na wa uhakika na hivyo kuchangia katika maendeleo ya ukuaji wa viwanda na uchumi.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2020/2021, Serikali itaendelea kutekeleza miradi mikubwa na ya kielelezo ya uzalishaji wa umeme hususan Mradi wa Kufua Umeme wa Maji wa Julius Nyerere (MW 2,115), upanuzi wa Mradi wa Kinyerezi I (MW 185) pamoja na kuimarisha mifumo ya usafirishaji na usambazaji wa umeme nchini. Aidha, Serikali itaendelea kutekeleza Awamu ya Tatu ya Mradi wa Kupeleka Umeme Vijijini ili kuhakikisha vijiji vilivyobaki vyote vinapatiwa umeme. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, huduma za kiuchumi, sekta ya ardhi. Ardhi ni rasilimali namba moja katika kuifikia ndoto ya Serikali ya kujenga uchumi wa viwanda. Kwa msingi huo, Serikali imeendelea kusimamia upimaji wa ardhi, mipango ya matumizi ya ardhi kuanzia ngazi ya kijiji hadi Taifa na umilikishaji ardhi kwa wananchi.

Mheshimiwa Spika, sambamba na kuimarisha utoaji huduma kwa njia ya kielektroniki, Serikali inatekeleza mpango wa kusogeza huduma za ardhi karibu na wananchi. Hadi sasa ofisi za ardhi za mikoa 26 zimeanzishwa pamoja na kuendelea kuziimarisha ofisi zote za ardhi za Halmashauri kwa kuwapatia mafunzo wataalam wa sekta ya ardhi na kununua vifaa. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2019/2020, Serikali imekamilisha awamu ya kwanza ya usimikaji wa Mfumo Unganishi wa Kuhifadhi Kumbukumbu za Ardhi katika Ofisi za Ardhi Kanda ya Dar es Salaam na Halmashauri za Manispaa ya Kinondoni na Ubungo. Lengo ni kuharakisha upimaji na utoaji hatimiliki za ardhi ili kuwawezesha wananchi wengi zaidi kumiliki ardhi kisheria na kutumia hati hizo kupata mikopo katika taasisi za fedha itakayowezesha kuanzisha na kuendeleza shughuli mbalimbali za ujasiriamali. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, mipango ya matumizi ya ardhi. Serikali imeendelea kusimamia upangaji na utekelezaji wa mipango ya matumizi ya ardhi katika ngazi ya Kanda, Wilaya na Vijiji. Lengo la Serikali ni kuhakikisha Serikali inaimarisha sekta ya ardhi.

Mheshimiwa Spika, kama ambavyo nimeeleza kwamba ziko kazi nydingi zimefanywa katika kipindi hiki cha hii miaka minne kuelekea miaka mitano na zote zimeandikwa kwenye taarifa hii, niendelee kuomba taarifa yangu yote iingie kwenye Kumbukumbu ili Waheshimiwa Wabunge na wananchi waendelee kusoma. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, pia watambue kwamba Serikali inaendelea na uboreshaji wa miundombinu ya usafiri na usafirishaji ikiwemo, madaraja, barabara kwa kujengwa kwa kiwango lami, ujenzi wa reli, umarishaji wa bandari na ujenzi wa meli mpya kwenye maeneo yote ya maziwa hapa nchini, tunaimarisha pia usafiri wa anga na viwanja vya ndege na tunaimarisha mawasiliano ya ndani na nje kupitia mifumo ya simu kuwawezesha Watanzania kufanya mawasiliano maeneo yote. Pia huduma za jamii nazo kama elimu, tumeboresha na tunaendelea kuboresha ili kuhakikisha kwamba Watanzania wote wanapata elimu ya kutosha kutoka ngazi ya awali mpaka elimu ya juu. Tunaendeleza utoaji wa huduma za maji kama ambavyo nimeeleza awali mijini na vijijini kuhakikisha kwamba wananchi wanapata huduma ya maji salama na ya kutosha.

Mheshimiwa Spika, pia tunaendelea kuimarisha sekta ya afya kwa ujenzi wa maeneo ya utoleaji huduma, ukarabati wa maeneo ya kutolea huduma ili tuweze kuimarisha afya za Watanzania. Vilevile, tunaendelea kutoa huduma kwa wenyewe mahitaji maalum ambako Ofisi ya Waziri Mkuu inacho kitengo na Naibu Waziri ambaye anaratibu watu wote wenyewe mahitaji maalum. Tunaendelea kutoa huduma hiyo na Mheshimiwa Stella Ikupa anashughulikia vizuri. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, suala la ulinzi na usalama limezingatiwa. Tunaendelea kuimarisha ulinzi na usalama kwenye mipaka yetu yote kuhakikisha kwamba nchi inabaki salama ili kuwawezesha Watanzania kutekeleza majukumu yao. Vilevile tunaendelea na usimamizi wa kazi na wafanyakazi kwenye sekta mbalimbali za umma ili watumishi wa umma waweze kutoa huduma kwa Watanzania kadri ya mahitaji ya Watanzania walioko kwenye maeneo hayo.

Mheshimiwa Spika, suala la afya na usalama mahali pa kazi limezingatiwa. Ofisi ya Waziri Mkuu nayo pia inashughulikia kwa karibu kuhakikisha kwamba watumishi wetu wa umma, wafanyakazi kwenye sekta zote binafsi na za Serikali tunahakikisha usalama wao unaendelea kuwa imara ili waweze kutumikia sekta zao.

Mheshimiwa Spika, lakini suala la utumishi umma tumeendelea kuboresha kupitia Ofisi ya Rais, Utumishi na Utawala Bora ambapo inaendelea kuratibu, kuhakiki kwa nchi nzima kama ikama inatosha ili kuwa na watumishi wa kutosha kwenye sekta zote na kila mmoja aweze kuwajibuka kama inavyotakiwa na ili aweze kutoa huduma inayotakiwa.

Mheshimiwa Spika, suala uwevezaji wananchi kiuchumi, Ofisi ya Waziri Mkuu tumeendelea kuratibu. Tunayo Kurugenzi inafanya kazi ya uwezesha jili kiuchumi na sasa hivi tunaendesha miradi ya wananchi kwenye vikundi mbalimbali kwa ngazi ya vijiji na wilaya. Tunahakikisha tunawapa ujuzi vijana wote ambao wamemaliza vyuo na wasiomaliza vyuo kila mmoja kwenye sekta ambayo anaitumikia ili aweze aweze kupata uchumi wakati wote anapoendelea shughuli zake. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, pia tunaimarisha Mfuko wa Taifa wa Maendeleo ya Vijana ambao pia vijana hao tumewaweka kwenye malengo na tumeratibu utaratibu wao kupitia kitabu changu wanaweza kupata ufanuzi zaidi. Tuna Mfuko wa Maendeleo ya Jamii (*TASAF*), unaoratibiwa na Ofisi ya Rais, umeendelea kutoa huduma zake na maboresho Awamu ya Pili yameshafika na tumeenza. Awamu hiyo ilizinduliwa rasmi na Mheshimiwa Rais. Kwa hiyo, kupitia mwaka huu wa bajeti huduma hizo zitaanza kutolewa tena.

Mheshimiwa Spika, ukuzaji ujuzi, nimeeleza kwamba sasa tunatumia vyuo vyetu vya ufundi vya taasisi binafsi na Serikali kutoa elimu ya ujuzi kwa vijana wetu kwenye vyuo hivyo mbalimbali ili kupata ujuzi waweze kujajiri na wakifanikiwa kuajiriwa kwenye sekta zilizo rasmi.

Mheshimiwa Spika, ukuzaji wa fursa za ajira. Suala la ajira ni endelevu na tunaendelea kuhakikisha kwamba ajira nayo inakuwa ni kipaumbele kuititia miradi tullyonayo lakini pia kuititia sekta rasmi na zisizo rasmi. Kama ambavyo nimetoa takwimu za awali suala la ajira liko kwenye mkakati wetu.

Mheshimiwa Spika, lakini tuna masuala ya mtambuka, vita dhidi ya rushwa, haya ni mapambano endelevu hatutalala. Popote ambako kutakuwa na taarifa za rushwa zipelekwe kwenye taasisi husika ili hatua kali zichukuliwe dhidi ya wala rushwa.

Mheshimiwa Spika, mapambano dhidi ya UKIMWI nayo pia ni sehemu ya mapambo ambayo tumeyaweka mstari wa mbele kuhakikisha kwamba tunaepukana na maambukizi mapya ya ugonjwa huu hasa kwa kuzingatia kwamba tunao mkakati wa 90/90/90 ambao sasa unatekelezwa. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, tukiwa tunaendelea na mapambano ya UKIMWI, lakini tuna mapambano dhidi ya dawa za kulevyaa ambayo pia yanasmamiwa na Ofisi ya Waziri Mkuu. Tuna mipango kazi ambayo itaendelea kusimamia na kuondoa kabisa uzalishaji, usafirishaji na matumizi ya dawa za kulevyaa hapa nchini na kulifanya taifa letu kuwa lenye vijana wenyewe afya njema ambao pia tunawatarajia kuingia kwenye uzalishaji mali hapa nchini. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, pia tunaendelea kuratibu maafa sehemu mbalimbali. Katika kipindi cha mwaka huu tumepata mvua nyingi sana na zimeleta athari katika maeneo mengi. Sasa hivi nchi nzima ina mafuriko na sasa Mto Rufiji umejaa na wananchi wengi wamepata athari vya vifo, uharibifu wa miundombinu na upotevu wa mali. Yote haya ni maeneo ambayo kwa kweli Serikali kuititia ngazi zake za Wilaya na Mkoa tunaendelea kuratibu na kushirikiana na wananchi kuhakikisha kwamba tunawasaidia kuwaondoa kwenye maeneo haya. Kwenye eneo hili tumetoa wito, wale wote

ambao wanaishi kwenye maeneo hatarishi ni vizuri sasa wakaondoka na kwenda maeneo ambayo yako salama hii ni kwa ajili ya afya zao. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, suala la mazingira nalo pia limepata fursa ya kujadiliwa kwa kina na tunalismamia. Pamoja na hilo, pia suala la Muungano, kama ambavyo unajua tunayo Wizara inashughulikia Muungano, tunaendelea na Vikao vya Pamoja vya Mabaraza ya Mawaziri kwenye shughuli ya maendeleo. Pia hata janga la CORONA nalo pia tumeunda Kamati ya Kitaifa inayojumuisha Mawaziri kutoka pande zote mbili (Bara na Visiwani) tunakaa pamoja kujadili. Wiki ijayo tutakutana kwa mara ya pili kufanya tathmini ya hatua tulioifiki na ushauri ambao tutaupata hapa ili tuone namna nzuri ya kupambana na ugonjwa huu.

Mheshimiwa Spika, uhusiano wa kimataifa nao umepata nafasi ya kusimamiwa kikamilifu ili kujenga mahusiano ya kidiplomasia kwenye nchi rafiki na Tanzania. Tunashukuru kwamba mpaka sasa mahusiano yetu na nchi mbalimbali kuanzia kwenye Ukanda wetu wa Afrika Mashariki, SADC, Bara la Afrika na nchi za nje ya Bara la Afrika yanaendelea vizuri.

Mheshimiwa Spika, sekta ya habari, utamaduni na michezo, tunaendelea kuimarisha utoaji matangazo yaliyo sahihi maeneo yote nchini, kuboresha usikivu, lakini pia tunaendelea kusisitiza kudumisha utamaduni wetu. Vilevile wataalam wetu wa lugha ya Kiswahili waendelee kuhakikisha lugha ya Kiswahili inatumika maeneo yote kama ilivyokubalika na baadhi ya Kanda kama vile Kanda ya SADC.

Mheshimiwa Spika, hitimisho kama nilivyotangulia kueleza katika kipindi cha takribani miaka mitano tangu Serikali ya Awamu ya Tano chini ya uongozi mahiri wa

Mheshimiwa Dkt. John Pombe Magufuli, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania toka iingie madarakani tumeshuhudia mafanikio makubwa ya kiuchumi na kijamii ambayo tunaendelea kuyaona. Mafanikio hayo ni ishara tosha kwamba ahadi za Chama cha Mapinduzi ndani ya kipindi hiki cha miaka mitano zinatekelezwa vyema kwa mafanikio makubwa. Hivyo basi katika mwaka huu Serikali pamoja na mambo mengine itaweka mkazo katika masuala yote ambayo nimeyaeleza hapa ili tuhakikishe kwamba nchi inapata huduma zake kupitia utekelezaji wa ilani hii. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, natoa wito kwa kila mwananchi kuendelea kuunga mkono jitihada kubwa zinazofanywa na Serikali yetu chini ya uongozi wa Kiongozi wetu Mheshimiwa Magufuli kwa kufanya kazi kwa bidii, weledi, uadilifu, tija na ufanisi, uaminifu na kupiga vita rushwa. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, sasa nitoe Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Fedha za Ofisi ya Waziri Mkuu na Ofisi ya Bunge kwa Mwaka 2020/2021. Kwa mwaka huu wa 2020/2021 Ofisi ya Waziri Mkuu na Taasisi zilizo chini yake inaliomba Bunge lako tukufu liidhinishe jumla ya shilingi 312,802,520,000, Kati ya fedha hizo shilingi 88,829,156,000 ni kwa ajili ya matumizi ya kawaida na shilingi 228,373,364,000 ni kwa ajili ya matumizi ya maendeleo.

Mheshimiwa Spika, vilevile naliomba Bunge lako Tukufu liidhinishe jumla ya shilingi 121,786,257,000 kwa ajili ya Mfuko wa Bunge. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, kati ya fedha hizo shilingi 113,567,647,000 ni kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida na shilingi 8,218,610,000 ni kwa ajili ya Matumizi ya Maendeleo.

WAZIRI WA FEDHA NA MIPANGO: Mheshimiwa Spika, naafiki.

**HOTUBA YA WAZIRI MKUU WA JAMHURI YA MUUNGANO WA
TANZANIA, MHESHIMIWA KASSIM M. MAJALIWA (MB.),
KUHUSU MAPITIO NA MWELEKEO WA KAZI ZA SERIKALI NA
MAKADIRIO YA MAPATO NA MATUMIZI YA FEDHA ZA OFISI
YA WAZIRI MKUU NA OFISI YA BUNGE
KWA MWAKA 2020/2021 – KAMA ILIVYOWASILISHWA MEZANI**

UTANGULIZI

1. ***Mheshimiwa Spika***, naomba kutoa hoja kwamba kutokana na taarifa zilizowasilishwa leo katika Bunge lako Tukufu na Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Bajeti, Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Katiba na Sheria na Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Masuala ya UKIMWI zilizochambua Bajeti ya Mfuko wa Bunge na Ofisi ya Waziri Mkuu, Bunge lako sasa lipokee na kujadili Taarifa ya Mapitio ya Utekelezaji wa Kazi za Serikali kwa Mwaka 2019/2020 na Mwelekeo wa Kazi za Serikali kwa Mwaka 2020/2021. Aidha, naomba Bunge lako Tukufu likubali kuitisha Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Fedha ya Ofisi ya Waziri Mkuu na Taasisi zilizopo chini yake pamoja na Mfuko wa Bunge kwa Mwaka 2020/2021.
2. ***Mheshimiwa Spika***, wakati tunapojadili Taarifa ya Mapitio ya Utekelezaji wa Kazi za Serikali kwa Mwaka 2019/2020 na Mwelekeo wa Kazi za Serikali kwa Mwaka 2020/2021 hatunabudi kumshukuru Mwenyezi Mungu mwingi wa rehema kwa kuendelea kutujaalia afya na uzima.
1. ***Mheshimiwa Spika***, katika Mwaka 2019/2020, Bunge lako Tukufu lilimpoteza aliyekuwa Mbunge wa Jimbo la Newala Vijiji, Mheshimiwa Rashid Ajali Akbar. Pia naungana na Mheshimiwa Dkt. John Pombe Joseph Magufuli, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Watanzania wenzangu kutoa salam za pole kwa familia ya Marehemu na wanachama wa CUF kufuatia kifo cha aliyekuwa Katibu Mkuu wa Chama cha Wananchi (CUF) Taifa Alhaji Khalifa Suleiman Khalifa. Pia kwa masikitiko makubwa niungane na wananchi wote, familia na wanahabari wote nchini kwa kifo cha Mwandishi wa Habari Mwandamizi wa Shirika la Habari

Tanzania (TBC) ndugu yetu Marin Hassan Marin kilichotokea leo alfajiri, Mungu aziweke roho za marehemu mahali pema peponi – Amina. Vilevile, Taifa letu lilikumbwa na majanga mbalimbali ikiwa ni pamoja na mafuriko nchini kote na ajali za barabarani ambazo zilisababisha vifo, majeruhi na uharibifu wa mali.

4. ***Mheshimiwa Spika***, sambamba na kutoa pole kwa ndugu, jamaa na marafiki kwa misiba iliyotokea, tuendelee kumuomba Mwenyezi Mungu awajaalie afya njema waliopata majeraha na azipumzishe roho za marehemu mahali pema peponi. **Amina!** Vilevile, nawashukuru kwa dhati wale wote waliojitelea kwa hali na mali katika kuwasaidia majeruhi na wahanga wa matukio hayo.

5. ***Mheshimiwa Spika***, kama tunavyofahamu, mwaka huu Serikali ya Awamu ya Tano inahitimisha kipindi cha kwanza cha miaka mitano kilichoanza Mwaka 2015. Kwa msingi huo, hotuba yangu itaeleza kwa muhtasari baadhi ya mafanikio makubwa ambayo Serikali imeyapata katika kipindi cha takriban miaka mitano ya utekelezaji wa llani ya Uchaguzi ya Chama Cha Mapinduzi (CCM).

6. ***Mheshimiwa Spika***, hotuba hii inaanisha baadhi ya kazi zilizotekelawa na Serikali kwa kuzingatia mipango na mikakati mbalimbali hususan Mpango wa Pili wa Maendeleo wa Miaka Mitano wa Mwaka 2016/2017 hadi 2020/2021 ambao ni sehemu ya utekelezaji wa Dira ya Taifa ya Maendeleo ya Mwaka 2025. Mikakati na Mipango hiyo, inatekelezwa sambamba na mipango mingine ya kikanda na kimataifa kama vile Agenda ya Mwaka 2063 ya Umoja wa Afrika na Malengo Endelevu ya Umoja wa Mataifa ya Mwaka 2030.

7. ***Mheshimiwa Spika***, katika kipindi cha uongozi wa Serikali ya Awamu ya Tano, tumeshuhudia mafanikio makubwa katika kuimarisha miundombinu, huduma za kiuchumi na kijamii, utawala bora, mapambano dhidi ya rushwa na ujisadi pamoja na kuhamasisha uwekezaji. Ningependa kutumia fursa hii kumpongeza Mheshimiwa Dkt.

John Pombe Joseph Magufuli, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa uongozi wake mahiri wa Serikali ya Awamu ya Tano katika utekelezaji wa Ilani ya Uchaguzi ya Chama Cha Mapinduzi ya Mwaka 2015 hadi 2020. Nawapongeza pia, Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan, Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania; Mheshimiwa Dkt. Ali Mohamed Shein, Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi na Mheshimiwa Balozi Seif Ally Idd, Makamu wa Pili wa Rais wa Serikali ya Mapinduzi Zanzibar kwa kusimamia vyema utekelezaji wa Ilani ya Uchaguzi ya Chama Cha Mapinduzi.

8. ***Mheshimiwa Spika***, kipekee nakushukuru wewe binafsi, pia Mheshimiwa Naibu Spika na Wenyezeti wa Bunge kwa kuliongoza vyema Bunge lako Tukufu na Wabunge wote katika kusimamia Serikali kuhakikisha kuwa inatekeleza wajibu wake ipasavyo wa kuhudumila wananchi. Vilevile, natoa shukrani zangu za dhati kwa Kamati za Kudumu za Bunge kwa kazi kubwa ya kupitia Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara, Mikoa, Wakala, Idara zinazojitegemea na Mamlaka za Serikali za Mitaa. Kipekee, nawashukuru sana Wajumbe wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Katiba na Sheria chini ya uenyekiti wa Mhe. Mohammed Omary Mchengerwa, Mbunge wa Jimbo la Rufiji; Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Masuala ya UKIMWI chini ya uenyekiti wa Mhe. Oscar Rwegasira Mukasa, Mbunge wa Jimbo la Biharamulo Magharibi na Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Bajeti chini ya uenyekiti wa Mhe. Mashimba Mashauri Ndaki, Mbunge wa Jimbo la Maswa Magharibi. Maoni na ushauri wa Kamati hizo umesaidia sana kuboresha Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Fedha ya Ofisi ya Waziri Mkuu na Mfuko wa Bunge kwa Mwaka 2020/2021.

9. ***Mheshimiwa Spika***, nawashukuru Waheshimiwa Mawaziri na Naibu Mawaziri, Katibu Mkuu Kiongozi, Mwanasheria Mkuu wa Serikali, Makatibu Wakuu na Naibu Makatibu Wakuu, Wakuu wa Mikoa na Wilaya, Wakuu wa Idara, Mashirika, Wakala na Taasisi zote za Serikali kwa ushirikiano mlionipatia katika kutekeleza majukumu ya Ofisi ya Waziri Mkuu. Aidha, nawashukuru wafanyakazi wote wa

Serikali na Taasisi zake kwa kutekeleza majukumu yao kwa weledi mkubwa na hivyo, kuwezesha Serikali kutekeleza kazi zake kwa tija na ufanisi. Vilevile, nawashukuru kwa michango yenu iliyowezesha kukamilisha Mpango na Bajeti ya Serikali ya Mwaka 2020/2021.

10. ***Mheshimiwa Spika***, kwa namna ya pekee kabisa, namshukuru Mhe. Jenista Joakim Mhagama, Mbunge wa Jimbo la Peramiho na Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu (Sera, Bunge, Kazi, Vijana, Ajira na Wenye Ulemavu); Mhe. Angellah Jasmine Kairuki, Mbunge wa Viti Maalum na Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu (Uwekezaji); Mhe. Anthony Peter Mavunde, Mbunge wa Jimbo la Dodoma Mjini na Naibu Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu (Kazi, Vijana na Ajira); Mhe. Stella Alex Ikupa, Mbunge wa Viti Maalum na Naibu Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu (Watu Wenye Ulemavu); Makatibu Wakuu Bw. Andrew Wilson Massawe (Kazi, Vijana, Ajira na Wenye Ulemavu), Bibi Dorothy Aidan Mwaluko (Sera, Uratibu na Uwekezaji) na Bw. Tixon Tuyangine Nzunda (Waziri Mkuu na Bunge) na Wakurugenzi, Wakuu wa Taasisi zilizopo chini ya Ofisi ya Waziri Mkuu, ofisi Binafsi ya Waziri Mkuu na Wafanyakazi wote kwa ushirikiano mkubwa wanaonipatia katika kutekeleza majukumu ya Ofisi ya Waziri Mkuu.

11. ***Mheshimiwa Spika***, napenda pia kuwashukuru washirika wa maendeleo zikiwemo nchi rafiki, taasisi na mashirika ya kimataifa, madhehebu ya dini na mashirika yasiyo ya kiserikali, kwa kuendelea kuunga mkono juhudzi za Serikali katika kujenga uchumi wa viwanda na kuiletea nchi yetu maendeleo. Mchango wao umekuwa muhimu kuwezesha nchi yetu kupiga hatua kubwa kimaendeleo kulingana na mipango tuliojiwekea.

12. ***Mheshimiwa Spika***, ninawashukuru wananchi wote kwa kuendelea kuiunguza mkono Serikali ya Awamu ya Tano katika kutekeleza majukumu yake ipasavyo. Aidha, nawashukuru wananchi wa Jimbo la Ruangwa kwa kuendelea kushirikiana nami na kwa kuniunga mkono. Niwapongeze na kuwashukuru kwa kutekeleza shughuli za maendeleo jimboni kwa ufanisi. Kipekee, namshukuru sana

mke wangu mpendwa, Mary; watoto wangu na familia yangu kwa ujumla kwa upendo wao, uvumilivu na maombi yao wakati wote ninapotekeleza majukumu yangu ya kitaifa. Nawashukuru sana.

Homa Kali ya Mapafu

13. ***Mheshimiwa Spika***, hivi sasa nchi yetu na dunia kwa ujumla inapitia katika kipindi kigumu. Itakumbukwa kwamba, tarehe 11 Machi 2020, Shirika la Afya Duniani (WHO) ilitangaza mlipuko wa Homa Kali ya Mapafu ijulikanayo kama *COVID-19* inayosababishwa na virusi vya CORONA kuwa ni janga la Kimataifa. Aidha, tarehe 16 Machi, 2020 Mheshimiwa Dkt. John Pombe Joseph Magufuli ilitangaza kuwepo kwa mgonjwa wa kwanza nchini.

14. ***Mheshimiwa Spika***, tangu kugundulika kwa ugonjwa huo, Serikali inaendelea kuchukua hatua mbalimbali katika kukabiliana na ugonjwa huu ikiwa ni pamoja na kuimarisha ukaguzi, upimaji na ufuatilaji wa wasafiri wanaoingia nchini ili kubaini wasafiri wanaoonesha dalili za ugonjwa au wenye viashiria hatari hata hivyo mashirika mengi yamesitisha ndege zao kwa kukosa abiria. Abiria waingiao wote hupelekwa nyumba ya kujitenga kwa gharama zao, tumetenga na hostel ili kuwapunguzia gharama. Kadhalika, katika kukabiliana na virusi vya *CORONA*, Serikali ilitoa maelekezo yafuatayo:

Moja: Kusitisha Mbio za Mwenge wa Uhuru na kwamba fedha zilizotengwa kwa ajili ya jukumu hilo zitumike kusaidia hatua za kukabiliana na janga la virusi vya Corona;

Mbili: Kusitisha michezo yote inayokusanya makundi ya watu ikiwemo ligi kuu ya Tanzania Bara, ligi daraja la kwanza, ligi daraja la pili na aina nyingine za michezo;

Tatu: Kusitisha shughuli zote za elimu kuanzia elimu ya awali, msingi, Sekondari, vyuo vya kati hadi vyuo vikuu;

- Nne:** Kusitisha Semina, Warsha, Makongamano na Mikutano yote ya ndani na ya hadhara yenyeye kuhusisha mjumuiko wa watu wengi;
- Tano:** Kuwatenga abiria waingiao nchini kwenye maeneo maalum kwa siku 14 ili kufuatilia hali zao mpaka tutakapojiridhisha kuwa hana ugonjwa;
- Sita:** Kuwasisitiza watanzania kufuata kanuni za kudhibiti maambukizi ikiwemo kunawa maji kwa sabuni, kukinga unapokohoa na kupiga chafya, kutopeana mikono bila sababu, kukaa au kusimama kwa umbali na jirani yako n.k; na
- Saba:** Kuwaasa Watanzania wenye safari zisizo za lazima kwenye nchi zenyeye maambukizi ya virusi vyta Corona, kusitisha safari hizo, na hatua zingine zitafuata.

15. ***Mheshimiwa Spika***, serikali inaendelea na usimamizi wa karibu sambamba na kufanya tathmini na kuchukua hatua kadhaa. Tumeunda Kamati za kitaifa tatu (3) zinazosimamia ugonjwa huu, niendelee kusisitiza kuwa sote tuzingatie maelekezo yaliyotolewa na Serikali toka tulipoanza kampeni ya kupambana na ugonjwa huu. Aidha, niwatake Watanzania kuzingatia masharti ya afya kwa kufuata ushauri unaotolewa na wataalam. Mgonjwa akithibitika, atapelekwa eneo maalum bila kujali cheo chake, atalala palipoandaliwa. Watanzania wenzangu tuendelee kupuuza taarifa za uzushi zinazosambazwa katika mitandao ya kijamii.

MAFANIKIO YA SERIKALI YA AWAMU YA TANO

16. ***Mheshimiwa Spika***, tarehe 20 Novemba 2015 wakati akifungua rasmi Bunge la Kumi na Moja la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania jijini Dodoma, Mheshimiwa Dkt. John Pombe Joseph Magufuli, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania aliwaahidi wananchi wote kuwa Serikali ya Awamu ya Tano itawatumikia na kuwajali.

17. ***Mheshimiwa Spika***, katika kutekeleza azma hiyo, ndani ya kipindi cha takriban miaka mitano mafanikio makubwa yamepatikana na yamesaidia kuimarisha hali ya kiuchumi na kijamii kwenye Taifa letu. Ujenzi wa miundombinu muhimu ya kiuchumi hususan ya usafiri na usafirishaji sambamba na uimarishaji wa huduma muhimu za kijamii ni mionganoni mwa masuala yaliyopewa kipaumbele na Serikali ya Awamu ya Tano.
18. ***Mheshimiwa Spika***, ujenzi wa Reli ya Kati kwa kiwango cha kimataifa (*Standard Gauge Railway*), ufufuaji wa Shirika la Ndege la Tanzania, ufufuaji wa ushirika na mali za ushirika mfano, NCU, SHIRECU, WETCU na Mamlaka ya Mkonge Tanzania, ujenzi wa Bwawa la Kufua Umeme la Julius Nyerere, ulinzi wa maliasili na rasilimali zetu pamoja na ujenzi na ukarabati wa miundombinu ya Elimu, Afya na Maji ni kati ya hatua za msingi zinazochukuliwa na Serikali ya Awamu ya Tano katika kufikia uchumi wa kati unaoongozwa na viwanda ifikapo Mwaka 2025.
19. ***Mheshimiwa Spika***, katika kipindi hiki cha miaka mitano, tumeshuhudia miradi hiyo muhimu ikiwa katika hatua mbalimbali za utekelezaji. Kwa mfano, ujenzi wa Reli ya Kati kwa kiwango cha Kimataifa ambao hadi Machi 2020 umetumia Shilingi trilloni 2.96 na kukamilika kwa asilimia 75 kwa kipande cha Dar es Salaam hadi Morogoro na asilimia 28 kwa kipande cha Morogoro hadi Makutupora.
20. ***Mheshimiwa Spika***, Serikali inatumia gharama kubwa katika kujenga miundombinu hiyo wezeshi ya kiuchumi kwa lengo la kulifanya Taifa letu kuwa na uchumi imara wa kujitegemea na wenyewe kuhimili ushindani. Fedha hizo pia zimekuwa chanzo cha ajira na zabuni kwa Watanzania zinazowasaidia kuongeza kipato.
21. ***Mheshimiwa Spika***, mradi huu utakapokamilika utaongeza ufanisi wa huduma za usafiri na usafirishaji wa bidhaa na abiria pamoja na kupunguza gharama za uchukuzi. Kadhalika, utachochaea ukuaji wa miji na sekta nyingine kama vile kilimo, viwanda, utalii na biashara. Vilevile,

mradi huu utakuwa chanzo cha ongezeko la mapato ya Serikali yatakayosaidia katika kuboresha maslahi ya watumishi na huduma za kijamii kama vile afya, elimu na maji.

22. ***Mheshimiwa Spika***, vilevile, ujenzi wa Mradi wa Bwawa la Kufua Umeme wa Maji wa Julius Nyerere ambalo litakapokamilika litazalisha umeme wa Megawati 2,115. Hadi Machi 2020 mradi huo umegharimu Shilingi trillioni 1.28 na umekamilika kwa asilimia 10.74. Kukamilika kwa bwawa hilo kutalihakikishia Taifa letu umeme wa uhakika na wa nafuu zaidi. Aidha, ongezeko hilo la uzalishaji wa umeme litawezesha shughuli za uzalishaji viwandani kuwa za uhakika, tija, ufanisi na gharama nafuu. Vilevile, mradi huu utachangia kwa kiasi kikubwa katika juhudini za kuhifadhi mazingira kutokana na kuongezeka kwa matumizi ya nishati ya umeme kwa watu wengi.

23. ***Mheshimiwa Spika***, Serikali imefanikiwa kutekeleza Mradi wa Usambazaji wa Umeme Vijiji (REA) ambapo vijiji vilivyounganishiwa umeme nchini vimeongezeka kutoka vijiji 2,118 Mwaka 2015 hadi vijiji 9,001 mwezi Machi 2020. Mradi huo pia umezinufaisha Taasisi 11,128 zikiwemo za elimu, afya, dini, mashine za kusukuma maji na huduma za biashara.

24. ***Mheshimiwa Spika***, katika kuimarisha huduma za usafiri wa anga, Serikali inaendelea kuliimarisha Shirika la Ndege la Tanzania. Hadi kufikia Machi, 2020 tayari ndege 8 mpya zenyewe thamani ya Shilingi trillioni 1.27 zimepokelewa na kuanza kazi. Kadhalika, malipo ya awali ya Shilingi bilioni 85.7 kwa ajili ya ununuzi wa ndege nyingine 3 mpya yamefanyika. Ununuzi wa ndege hizi, umeongeza ufanisi katika usafiri wa anga, kuongezeka kwa mapato ya Serikali, kuimarika kwa utalii na kuongezeka kwa fursa za ajira katika sekta ya huduma.

25. ***Mheshimiwa Spika***, bajeti ya dawa, vifaa, vifaa tiba na vitendanishi imeongezeka kutoka Shilingi bilioni 31 kwa Mwaka 2015 hadi Shilingi bilioni 269 kwa Mwaka 2019. Serikali pia imegharamia ujenzi na uboreshaji wa miundombinu ya afya kwa kujenga zahanati 1,198, ukarabati wa vituo vya afya

487, hospitali za Halmashauri za Wilaya 69 na hospitali za rufaa za mikoa 10 za Njombe, Simiyu, Mara, Geita, Songwe, Katavi, Sekou Toure, Mwananyamala, Mawenzi, Manyara, hospitali za rufaa za kanda 3 za Mtwara, Mbeya na Burigi-Chato na Hospitali Maalum ya Kibong'oto na Uhuru - Chamwino. Katika kipindi cha Julai 2015 hadi Januari 2020 jumla ya Shilingi triliioni 3.01 zimetumika kugharamia huduma za afya. Kuongezeka kwa bajeti ya dawa na uboreshaji wa miundombinu ya afya, kumeleta mapinduzi makubwa katika sekta ya afya kwa kuimarisha afya za Watanzania.

26. ***Mheshimiwa Spika***, nyote mtakubaliana nami kuwa ujenzi na uboreshaji wa miundombinu ya afya, ununuzi wa dawa na vifaa vya kisasa vya tiba ni utekelezaji wa dhamira ya dhati ya Serikali ya Awamu ya Tano ya kuhakikisha kila Mtanzania anapatiwa haki yake ya kupata matibabu tena katika eneo alipo.
27. ***Mheshimiwa Spika***, katika eneo la elimu, Serikali imeongeza mikopo kwa ajili ya elimu ya juu kutoka Shilingi bilioni 365 Mwaka 2015 hadi Shilingi bilioni 450 Mwaka 2019. Elimumsingi bila Ada nayo imetekelizwa kwa mafanikio makubwa na kuhakikisha watoto wote wenye umri wa kwenda shule wanaandikishwa na kupatiwa elimu.
28. ***Mheshimiwa Spika***, utekelezaji mzuri wa Mpango wa Elimumsingi bila Ada, uliwezesha kuongezeka kwa idadi ya wanafunzi walioandikishwa darasa la kwanza. Kwa mfano, kabla ya kuanza kwa Mpango huo Mwaka 2015 ni wanafunzi 1,568,378 walioandikishwa. Aidha, baada ya kuanza utekelezaji wa Mpango Elimumsingi Bila Ada wanafunzi 2,120,667 waliandikishwa Mwaka 2016. Katika kipindi cha mwaka 2015 hadi Februari 2020 jumla ya Shilingi triliioni 1.2 zimetumika kugharamia Elimumsingi Bila Ada.
29. ***Mheshimiwa Spika***, maboresho yanayofanyika kwa upande wa elimumsingi yanazingatia uhitaji wa miundombinu ya kujifunzia na kufundishia. Kuanzia Mwaka 2015 hadi Februari, 2020 vyumba vya madarasa 166,627, maabara 5,801, nyumba za walimu 57,541, matundu ya vyoo

231,612 yamejengwa na madawati 2,886,459 yamenunuliwa. Aidha, idadi ya shule za msingi zenyne madarasa ya elimu ya awali imeongezeka kutoka madarasa 16,889 Mwaka 2015 hadi kufikia madarasa 17,771 Mwaka 2020. Kadhalika, idadi ya shule za sekondari imeongezeka kutoka shule 4,708 Mwaka 2015 hadi shule 5,330 Mwaka 2020.

30. ***Mheshimiwa Spika***, utekelezaji wa Mpango wa Elimumsingi Bila Ada unawahakikishia watoto wote wa kitanzania hususan wale wa hali ya chini kupata haki yao ya msingi ya kupata elimu. Aidha, Mpango huo umewapunguzia wazazi mzigo wa ada na michango isiyokuwa ya lazima na hivyo kujielekeza zaidi katika kutafuta na kuwapatia mahitaji ya msingi vijana wetu kama vile sare za shule na madaftari.

31. ***Mheshimiwa Spika***, kama utakavyokumbuka, katika vikao vingi vya Bunge Iako Tukufu viliviotangulia, changamoto ya maji ni suala lililoongoza kuchangiwa Bungeni na Waheshimiwa Wabunge. Katika kipindi cha takribani miaka mitano, Serikali yetu sikivu ya Awamu ya Tano imetekeleza ujenzi na ukarabati wa miradi ya maji 1,423. Kati ya miradi hiyo, 792 imekamilika ikihusisha miradi 710 vijijini na miradi 82 mijini. Vilevile, Serikali ilipokea ombi la Waheshimiwa Wabunge na kuanzisha Mfuko wa Taifa wa Maji na Wakala wa Usambazaji Maji na Usafi wa Mazingira Vijijini (RUWASA). Lengo la Serikali ni kuhakikisha vyombo hivi vinakuwa chanzo cha uhakika cha upatikanaji wa fedha za kugharamia miradi ya maji na kusimamia utoaji wa huduma ya maji na usafi wa mazingira. Juhudi hizi kwa pamoja zitasaidia kusogeza huduma ya maji kwa kasi zaidi karibu na wananchi katika maeneo ya mijini na vijijini.

32. ***Mheshimiwa Spika***, katika kipindi cha takriban miaka mitano, Serikali imefanikiwa kulinda na kuendeleza rasilimali na maliasili za Taifa hususan madini na kuhakikisha zinatumika kwa maslahi mapana ya Taifa na watu wake. Mafanikio hayo, yametokana na Serikali kutekeleza kwa ufanisi mkubwa Mkakati wa Utekelezaji wa Sheria ya Mamlaka ya Nchi kuhusu Umiliki wa Utajiri na Maliasili za Nchi wa Mwaka 2017 na Sheria

ya Mapitio na Majadiliano kuhusu Masharti Hasi katika Mikataba ya Utajiri na Maliasili za Nchi ya Mwaka 2017.

33. ***Mheshimiwa Spika***, utekelezaji wa mkakati na sheria hiyo umechangia kuongezeka kwa maduhuli ya Serikali yatokanayo na sekta ya madini mwaka hadi mwaka. Maduhuli ya Serikali yameongezeka kutoka Shilingi bilioni 205.2 Mwaka 2015/2016, hadi Shilingi bilioni 346.6 Mwaka 2018/2019. Aidha, katika Mwaka 2019/2020 Serikali inatarajia kukusanya Shilingi bilioni 471.

34. ***Mheshimiwa Spika***, ukusanyaji wa mapato nao umeongezeka kutoka wastani wa Shilingi bilioni 850 kwa mwezi Mwaka 2015 hadi kufikia wastani wa Shilingi trilioni 1.3 Mwaka 2019. Ongezeko hili limechangiwa na hatua za makusudi zilizochukuliwa na Serikali hususan kuimarisha matumizi ya mifumo ya ukusanyaji mapato kwa njia za kielektroniki, kuongeza idadi ya walipa kodi na kuibua vyanzo vipyta vya mapato. Aidha, ongezeko hilo limekuwa chachu katika utekelezaji wa miradi ya maendeleo ambayo imesaidia kuimarisha utoaji wa huduma pamoja na kusogea huduma hizo karibu na wananchi.

35. ***Mheshimiwa Spika***, nichukue fursa hii kuwashukuru wananchi na walipa kodi wote kwa kuendelea kuitikia wito wa Serikali wa kulipa kodi kwani hatua hiyo ni muhimu katika kulifanya Taifa letu kujitegemea. Serikali itaendelea kusimamia matumizi kwa lengo la kuongeza ufanisi na tija kwa mustakabali wa maendeleo ya Taifa.

36. ***Mheshimiwa Spika***, Serikali pia imefanikiwa kudhibiti matumizi ya hovyo ya fedha za Umma kwa kuziba mianya ya ukwepaji kodi sambamba na kuhakikisha kwamba wale wote wanaotakiwa kulipa kodi wanafanya hivyo. Kwa mfano, katika kipindi cha miaka mitano (2015 – 2019), Serikali imeweza kuokoa Shilingi bilioni 19.83 ya mishahara kwa kuwaondoa kwenye mfumo wa malipo watumishi hewa 19,708 na wenye vyeti vya kughushi 15,411. Msingi huu tunaojenga ni muhimu katika kujenga uchumi imara na usio tegemezi.

37. **Mheshimiwa Spika**, katika siku ya Mashujaa iliyofanyika kitaifa katika viwanja vya Mashujaa Jijini Dodoma tarehe 25 Julai 2016, Mheshimiwa Dkt. John Pombe Joseph Magufuli, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania alitangaza na kusisitiza azma ya Serikali kuhamia Dodoma ambapo alisema, nanukuu:

“.....ninazungumza kutoka kwenye dhamira yangu kabla sjamaliza kipindi changu cha miaka mitano Serikali yote itakuwa hapa Dodoma.....”

38. **Mheshimiwa Spika**, ninapenda kuliarifu Bunge lako Tukufu na watanzania kuwa tayari Serikali imehamia Dodoma. Hadi Machi 2020, jumla ya watumishi 15,361 wa Wizara na Taasisi za Serikali wamehamia Makao Makuu ya Serikali Dodoma, ujenzi wa awali wa ofisi za Serikali katika Mji wa Serikali Mtumba umekamilika, maandalizi ya ujenzi wa majengo ya ofisi za Serikali awamu ya pilli na ujenzi wa barabara kwa kiwango cha lami katika mji huo unaendelea. Vilevile, Serikali imekamilisha mapitio ya Mpango Kabambe wa Jiji la Dodoma ambao niliuzindua tarehe 13 Februari 2020 kwa ajili ya kusimamia shughuli za upangaji wa Jiji la Dodoma. Naielekeza Halmashauri ya Jiji la Dodoma kusimamia ipasavyo utekelezaji wa mpango huo ili kuhakikisha Jiji la Dodoma linaendelezwa kwa kuzingatia Mpango huo.

39. **Mheshimiwa Spika**, nyote mtakubaliana nami kuwa Serikali ya Awamu ya Tano imefanikiwa katika usimamizi madhubuti wa sheria, kanuni na taratibu za uwajibikaji wa viongozi na watumishi wa umma. Usimamizi huo, umewezesha viongozi na watendaji wa umma kuwajibika ipasavyo kwa wananchi ambao ndiyo waajiri wao. Sambamba na hilo, nidhamu Serikalini imeongezeka kutokana na Serikali kuwachukulia hatua za kinidhamu watumishi wazembe, wadanganyifu na wasio waadilifu.

40. **Mheshimiwa Spika**, tunapotaja mafanikio haya tuna kila sababu ya kumpongeza Mheshimiwa Dkt. John Pombe Joseph Magufuli, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwani uongozi wake mahiri na wenye uthubutu ndiyo msingi mkuu wa mafanikio yaliyopatikana. Dhana na falsafa

aliyojenga ya **Hapa Kazi Tu** imesaidia kubadili mtazamo wa Watanzania wengi ambapo sasa tunashuhudia uwajibikaji wa kiwango cha juu wa mtu mmoja mmoja, katika shughuli mbalimbali za kiuchumi na uzalishaji iwe shambani, ofisini, kiwandani, sokoni na kwingineko badala ya tabia ya awali ya baadhi ya wananchi wachache kupoteza muda mwingu katika shughuli zisizokuwa na tija kwa Taifa.

41. ***Mheshimiwa Spika, mafanikio*** haya katika utekelezaji wa miradi ya maendeleo na uboreshaji wa huduma za jamii yameenda sambamba na uzalishaji wa ajira zipatazo **milioni 12.6** zikiwemo ajira za moja kwa moja milioni 11.7 kwenye sekta mbalimbali nchini. Kwa mfano:

- Sekta za Afya, Elimu na Utawala zimetoa ajira za kudumu kwa kuajiri watumishi 28,403 katika mamlaka za Serikali za Mitaa,
- Mradi wa reli ya kati kwa kiwango cha kimataifa umewezesha kuzalishwa ajira **zipatazo 13,177** za kitaalam na zisizo za kitalaam. Kati ya hizo, ajira za kitaalam kwa wazawa ni asilimia 46.5. Pia kupitia mradi huu kumekuwa na utoaji wa zabuni zenye thamani ya Shilingi bilioni 664.7 kwa wazabuni na wakandarasi wa ndani 640,
- Mradi wa umeme wa mwalimu Nyerere kupitia maporomoko ya mto Rufiji umezalisha jumla ya **ajira 3,897** ikiwemo ajira za wazawa 3,422,
- Ufufuaji wa shirika la ndege la Tanzania (ATCL) pamoja na kuboresha viwanja vya ndege **jumla ya ajira 2,970**,
- Ujenzi wa Viwanda nchini jumla ya ajira zilizozalishwa ni **41,900**.
- Ujenzi na uboreshaji wa miundombinu mbalimbali ikiwemo Hospitali za Wilaya, vituo vya afya, Zahanati, Madarasa, Nyumba na majengo maeneo mapya ya utawala, Miradi ya barabara chini ya TARURA kwa

kutumia force Account jumla **ya mafundi 845,348** walipata ajira za mikataba na muda.

42. ***Mheshimiwa Spika***, baada ya kueleza mafanikio hayo, nyote ni mashuhuda kwamba **Chama Cha Mapinduzi kiliahidi na kimetekeleza kwa vitendo na ndiyo maana kinaendelea kuwa Chama cha mfano na cha kuigwa siyo tu Nchini, bali hata katika Bara la Afrika**. Hata hivyo, mafanikio mengine yataelezwa kwa kina wakati Mawaziri watakapokuwa wanawasilisha hotuba za bajeti za Wizara zao.

43. ***Mheshimiwa Spika***, sasa naomba kutoa taarifa kuhusu utekelezaji wa Mpango wa Maendeleo wa Mwaka 2019/2020 na shughuli zitakazoteklezwa na Serikali katika Mwaka 2020/2021.

MPANGO WA MAENDELEO NA BAJETI YA MWAKA 2020/2021

44. ***Mheshimiwa Spika***, Mapendekezo ya Bajeti ya Serikali ya Mwaka 2020/2021 yamezingatia Sera na Miongozo ikiwa ni pamoa na Mpango wa Maendeleo wa Taifa wa Mwaka 2020/2021. Mpango huu ni wa mwisho katika mfululizo wa mipango ya kila mwaka wa kutekeleza Mpango wa Taifa wa Miaka Mitano (2016/2017 – 2020/2021) wenye dhima ya Kujenga Uchumi wa Viwanda ili Kuchochea Mageuzi ya Uchumi na Maendeleo ya Watu.

45. ***Mheshimiwa Spika***, Mpango wa Maendeleo na Bajeti wa Mwaka 2020/2021 umezingatia yafuatayo: Dira ya Taifa ya Maendeleo ya Mwaka 2025 yenye lengo la kuiwezesha Tanzania kuwa Nchi ya hadhi ya uchumi wa kipato cha kati inayoongozwa na viwanda ifikapo Mwaka 2025; Mpango wa Pili wa Maendeleo wa Taifa wa Miaka Mitano, 2016/2017 – 2020/2021; Sera na Mikakati mbalimbali; Malengo ya Maendeleo Endelevu na Makubaliano ya Kikanda na Kimataifa ambayo Serikali imeyaridhia. Aidha, Ilani ya Uchaguzi ya Chama Cha Mapinduzi ya Mwaka 2015 - 2020 imezingatiwa pamoa na Maelekezo ya Serikali yaliyoainishwa na Mheshimiwa Rais wakati wa uzinduzi rasmi wa Bunge la

11 mwezi Novemba 2015. Vilevile, Mpango umezingatia hali halisi ya utekelezaji wa Mpango wa Maendeleo wa Mwaka 2019/2020; changamoto zilizojitokeza; hali ya uchumi kitaifa, kikanda na kidunia kwa Mwaka 2019 na maoteo ya ukuaji wa uchumi kwa Mwaka 2020.

46. ***Mheshimiwa Spika***, nitumie fursa hii kueleza kwa kifupi vipaumbele vya Mpango wa Maendeleo wa Mwaka 2020/2021 ambavyo vimejikita katika masuala makuu manne yafuatayo: Ujenzi wa Msingi wa Uchumi wa Viwanda; Kufungamanisha ukuaji wa uchumi na maendeleo ya watu; Uboreshaji wa mazingira wezeshi kwa uendeshaji wa biashara na uwekezaji na Kuimarissha usimamizi wa utekelezaji wa Mpango wa Maendeleo. Katika kufikia malengo ya Mpango, Serikali itaendelea kutoa kipaumbele cha pekee katika kutekeleza miradi ya kielelezo ya kimkakati ikiwa ni pamoja na: Ujenzi wa Reli ya Kati ya Kiwango cha Klmataifa; Mradi wa kufua umeme wa Maji wa Julius Nyerere – MW 2,115; Kuboresha Shirika la Ndege la Tanzania (ATCL); Mradi wa Ujenzi wa Bomba la Mafuta Ghafi kutoka Hoima (Uganda) hadi Tanga (Tanzania); Uanzishwaji wa kanda maalum za Kiuchumi na Kusomesha wataalam wengi zaidi katika fani za Ujuzi Adimu na Maalum. Hatua hizo, zitasaidia kufungamanisha ujenzi wa miundombinu wezeshi na sekta nyingine za kiuchumi ili kuongeza kasi ya maendeleo, ajira na kipato na hatimaye kuliwezesha Taifa kupiga hatua kubwa za kimaendeleo.

47. ***Mheshimiwa Spika***, nitumie fursa hii kutoa rai kwa Wafanyabiashara, Wawekezaji, Wajasiriamali, Wabunge, Viongozi na Watendaji wa Serikali, Taasisi za Dini, Asasi za Kiraia, Washirika wa Maendeleo, na Wananchi wote kwa ujumla, kushirikiana na Serikali bega kwa bega katika kutekeleza Mpango huu ili azma ya kufikia uchumi wa kati unaoongozwa na viwanda ifikapo Mwaka 2025 iweze kutimia.

HALI YA UCHUMI

48. ***Mheshimiwa Spika***, uchumi wa Taifa umeendelea kuimariika ambapo katika kipindi cha Januari hadi Septemba

2019, ukuaji halisi wa Pato la Taifa ulifikia asilimia 6.9. Baadhi ya shughuli zilizochangia ukuaji huo kwa viwango vikubwa ni pamoja na ujenzi asilimia 14.8; uchimbaji wa madini na mawe asilimia 12.6; habari na mawasiliano asilimia 11.0; uchukuzi na uhifadhi wa mizigo asilimia 8.8 na huduma za usambazaji maji asilimia 8.5.

49. ***Mheshimiwa Spika***, katika kipindi cha kuanzia Julai hadi Januari 2020, mfumuko wa bei ulikuwa wastani wa asilimia 3.7. Kiwango hiki ni chini ya lengo la Taifa la kipindi cha muda wa kati la asilimia 5.0, na chini ya malengo ya asilimia 7.0 kwa nchi za Jumuiya ya Maendeleo Kusini mwa Afrika (SADC) na asilimia 8.0 kwa Jumuiya ya Afrika Mashariki. Hali hii inatokana na utekelezaji madhubuti wa sera za fedha na za bajeti, uhakika wa upatikanaji wa chakula na utulivu wa thamani ya Shilingi ya Tanzania dhidi ya sarafu nyingine duniani.

50. ***Mheshimiwa Spika***, katika Mwaka 2020/2021, Serikali itaendelea kuimarisha sekta za uzalishaji na utoaji huduma ili kuongeza kasi ya ukuaji wa Pato Halisi la Taifa. Vilevile, Serikali itaendelea kutekeleza mikakati na sera za uchumi jumla ili kudhibiti kasi ya mfumuko wa bei na kuwa na mwenendo tulivu wa uchumi. Serikali pia, itaendelea kuimarisha Mfumo wa Serikali wa Kielektroniki wa Ukusanyaji wa Mapato (GePG) kwa kuharakisha ufungaji wa mfumo huo katika wizara na taasisi za Serikali.

HALI YA SIASA

51. ***Mheshimiwa Spika***, Ofisi ya Msajili wa Vyama vyta Siasa imeendelea kusimamia utekelezaji wa sheria na maadili ya vyama vyta siasa ili kuhakikisha demokrasia ya vyama vingi inaimarika pamoja na kudumisha amani, utulivu na mshikamano uliopo katika nchi yetu.

52. ***Mheshimiwa Spika***, katika Mwaka 2020/2021, Ofisi ya Msajili wa Vyama vyta Siasa itaendelea kusimamia utekelezaji na utoaji elimu kuhusu Sheria ya Vyama vyta Siasa, Kanuni za

Maadili ya Vyama vya Siasa, pamoja na Sheria ya Gharama za Uchaguzi katika Uchaguzi Mkuu wa Mwaka 2020. Vilevile, Ofisi ya Msajili wa Vyama vya Siasa itaendelea kufuatilia uhai wa Vyama vya Siasa vyenye usajili wa kudumu kwa lengo la kuwawezesha wananchi kushiriki na kutoa michango yao ya mawazo na fikra kupitia vyama hivyo ili kuimarisha demokrasia na maendeleo nchini.

Uchaguzi wa Serikali za Mitaa

53. ***Mheshimiwa Spika***, Serikali imeratibu na kusimamia Uchaguzi wa Serikali za Mitaa uliofanyika tarehe 24 Novemba 2019. Uchaguzi huo ulihusisha Mitaa 4,263, Vijiji 12,319 na Vitongoji 64,384. Katika uchaguzi huo, Chama Cha Mapinduzi kilipata ushindi wa kishindo wa asilimia 99.9 kwa nafasi zote zilizogombewa. Matokeo hayo yameendelea kudhihirisha imani kubwa walijonayo wananchi kwa Chama Cha Mapinduzi. Hivyo, basi natoa rai kwa wananchi kuendelea kushirikiana na viongozi waliochaguliwa ili kutimiza azma ya kuwaleta maendeleo.

Maandalizi ya Uchaguzi Mkuu

54. ***Mheshimiwa Spika***, Tume ya Taifa ya Uchaguzi imeanza maandalizi ya Uchaguzi Mkuu utakaofanyika mwezi Oktoba 2020. Pamoja na mambo mengine, maandalizi hayo yanahuisha Zoezi la Kuboresha Daftari la Kudumu la Wapiga Kura lililofanyika nchi nzima. Awamu ya kwanza ilizinduliwa tarehe 18 Julai, 2019 Mkoani Kilimanjaro na kukamilika tarehe 23 Februari, 2020 katika Mkoa wa Dar es Salaam.

55. ***Mheshimiwa Spika***, uboreshaji wa daftari hili ulihusisha: Uandikishaji wa Wapiga Kura wapya ambaao wametimiza umri wa miaka 18 au watatimiza umri huo ifikapo siku ya Uchaguzi Mkuu wa Mwaka 2020; urekebishaji wa taarifa za Wapiga Kura walioandikishwa katika Uchaguzi Mkuu wa Mwaka 2015 pamoja na ufutaji wa taarifa za Wapiga Kura waliopoteza sifa za kuwemo katika Daftari la Kudumu la Wapiga Kura.

56. ***Mheshimiwa Spika***, katika zoezi hilo, jumla ya Wapiga Kura 10,285,732 wameandikishwa na kati yao, Wapiga Kura wapya ni 7,043,247, Wapiga Kura walioboreshewa taarifa zao ni 3,225,778 na Wapiga Kura waliofutwa kwenye Daftari la Kudumu la Wapiga Kura kutokana na kupoteza sifa ni 16,707. Zoezi la Uboreshaji wa Daftari la Kudumu la Wapiga Kura kwa Awamu ya Pili linatarajija kuanza tarehe 5 Aprili 2020 na kukamilika tarehe 26 Juni 2020. Zoezi hili litaenda sambamba na uhakiki wa taarifa za wapiga kura katika daftari hilo. Natoa wito kwa Wananchi kujitokeza kwa wingi kuijandikisha na kuboresha taarifa zao katika daftari hilo, ili wawze kutumia haki yao ya Kikatiba ya kuchagua viongozi wanaowataka.

57. ***Mheshimiwa Spika***, niwasihii Watanzania kushiriki kikamilifu kwenye Uchaguzi Mkuu ujao kwa kufuata sheria, kanuni na taratibu za Nchi. Viongozi wa Vyama vyta Siasa waoneshe mfano wa kuendesha siasa za kistaarabu zenye lengo la kuwaunganisha watanzania na siyo kuwatenganisha. Hakuna kiongozi aliyewahi kupata sifa nzuri kwa kuwa chanzo cha mifarakano. Hivyo basi, tudumishe utulivu, amani, mshikamano pamoja na ustaarabu wetu wa kitanzania katika kipindi chote cha kampeni na Uchaguzi Mkuu ili kulifanya Taifa letu kuendelea kuwa kisiwa cha amani na mfano wa kuigwa barani Afrika na duniani kwa ujumla.

BUNGE

58. ***Mheshimiwa Spika***, Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania limeendelea kutimiza wajibu wake wa kikatiba na kikanuni kwa kufanya mikutano mitatu na huu ukiwa ni wa nne kwa mwaka 2019/2020. Ofisi ya Bunge kwa sasa inatekeleza shughuli za Bunge kwa kutumia TEHAMA kuititia mfumo wa Bunge Mtandao (*e-Parliament*) uliotengenezwa na kusimamiwa na wataalam wa ndani wa Ofisi ya Bunge. Hivi sasa Wizara, Idara na Taasisi za Serikali zinawasilisha taarifa na nyaraka mbalimbali Bungeni kwa kutumia nakala tete badala ya nakala ngumu. Hatua hii imeweza kupunguza gharama za uendeshaji hivyo kuokoa kiasi kikubwa cha fedha cha takribani Shilingi bilioni 2 kilichokuwa kinatumika kila mwaka katika uandaaji na uhifadhi wa nyaraka mbalimbali

zinazoandaliwa kwa ajili ya utekelezaji wa shughuli mbalimbali za Bunge. Pia, Ofisi ya Bunge imeweza kuzindua '*Bunge Mobile Application*' ambayo imewezesha Waheshimiwa Wabunge pamoja na wadau mbalimbali kupata kwa urahisi taarifa mbalimbali kama vile orodha ya shughuli za Bunge (*Order Paper*), *Hansard* pamoja na sheria na miswada. Ni matumaini yangu kwamba Bunge lako Tukufu litaendelea kuisimamia Serikali ili itekeleze majukumu yake ipasavyo.

MAHAKAMA

59. ***Mheshimiwa Spika***, katika kuhakikisha wananchi wanapata haki kwa wakati na kwa gharama nafuu, Mahakama imeendelea kuimarisha huduma kwa kuweka mifumo na taratibu mbalimbali za kuwafikia wananchi katika maeneo yote nchini ili kupunguza mlundikano wa mashauri. Mojawapo ya utaratibu unaotumika ni kuwatumia Mahakimu wenye Mamlaka ya Ziada (*Extended Jurisdiction*) kusikiliza mashauri ya Mahakama Kuu ambapo Mahakimu 195 walipewa Mamlaka hiyo ya ziada. Katika kipindi cha Mwaka 2019 mashauri 1,132 yalisikilizwa na kumalizwa kwa utaratibu huo.
60. ***Mheshimiwa Spika***, Mahakama imeendelea kuboresha miundombinu katika ngazi mbalimbali nchini ikiwa ni pamoja na ujenzi na ukarabati wa majengo. Katika kutekeleza hilo, ujenzi wa majengo ya Mahakama Kuu katika Mikoa ya Kigoma na Mara, Mahakama ya Hakimu Mkazi katika Mikoa ya Simiyu, Manyara, Geita, Njombe, Mahakama za Wilaya 14, pamoja na Mahakama za Mwanza za Mlowo, Magoma, Uyole, Mtowisa, Msanzi na Mkunya umekamilika.
61. ***Mheshimiwa Spika***, katika Mwaka 2020/2021, Serikali itaendelea kulinda, kuheshimu na kuzingatia haki za binadamu na kuimarisha mifumo ya usimamizi wa sheria na utoaji Haki kwa kutumia TEHAMA. Vilevile, Serikali itaendelea kufanya maboresho katika mfumo wa Haki Jinai ili kuwezesha shughuli za uchunguzi, upelelezi, uendeshaji wa mashauri na usikilizaji wa mashauri kufanyika kwa ufanisi.

UWEKEZAJI

62. ***Mheshimiwa Spika***, Serikali imeendelea kuratibu na kusimamia shughuli za kuhamasisha na kufanikisha wawekezaji wa ndani na nje ya nchi kwa lengo la kuvutia mitaji, teknolojia na ujuzi ambao ni chachu ya maendeleo katika sekta mbalimbali. Serikali imeendelea kuhakikisha mazingira ya uwekezaji na biashara yanakuwa rafiki.

63. ***Mheshimiwa Spika***, Serikali imeendelea kutumia vyema uwepo wa fursa nyingi za uwekezaji na kuwepo kwenye eneo la kimkakati la kijigrafia kwa kuhudumia nchi zipatazo 6 ambazo hazipo kwenye mwambao wa bahari. Hali hii inaifanya nchi yetu kuwa lango la biashara ya kimataifa hususani katika ukanda wa nchi za Afrika Mashariki na Kati pamoja na Kusini mwa Afrika. Aidha, Serikali inaendelea kuboresha mazingiza ya uwekezaji na biashara ikiwemo kufanya tathmini ya utekelezaji wa Sera ya Taifa ya Uwekezaji ya Mwaka 1996 ili kubaini changamoto za kisera, kisheria na kiutendaji zitakazopelekea kuhuisha Sera ya Uwekezaji ya Mwaka 1996 na Sheria ya Uwekezaji ya Mwaka 1997.

64. ***Mheshimiwa Spika***, vilevile, Serikali imeendelea kuratibu utekelezaji wa Kuboresha Mfumo wa Udhibiti wa Biashara (*Blueprint*) ambapo kupitia Mpango huo Serikali imefuta tozo mbalimbali 54 katika Mwaka wa Fedha 2019/2020 pamoja na kuondoa mwingiliano wa majukumu kati ya Shirika la Viwango Tanzania (TBS) na Mamlaka ya Dawa na Vifaa Tiba (TMDA) ili kurahisisha shughuli za uwekezaji na biashara.

65. ***Mheshimiwa Spika***, katika Mwaka 2019/2020 Serikali pia imeratibu mikutano ya mashauriano kati yake na wawekezaji na wafanyabiashara kutoka ndani na nje ya nchi kwa lengo la kusikiliza na kutatua changamoto mbalimbali wanazokabiliana nazo. Katika mikutano hiyo hoja nyingi na changamoto zilipatiwa ufumbuzi na nyingine kutolewa ufanuzi ambapo pia wafanyabiashara na wawekezaji walikumbushwa wajibu wao katika uendeshaji biashara na uwekezaji wao.

66. **Mheshimiwa Spika**, Serikali kuititia Ofisi ya Waziri Mkuu (Uwekezaji) kwa kushirikiana na Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki iliendesha mikutano kati ya Serikali na wawekezaji kutoka China, Uingereza na Marekani waliowekeza hapa nchini. Kwa nia ya kusikiliza na kutatua changamoto zinazowakabili na kupata maoni na ushauri zaidi.
67. **Mheshimiwa Spika**, katika kuongeza njia za kushughulikia malalamiko ya wawekezaji, Serikali kwa kushirikiana na Taasisi ya Sekta Binafsi Tanzania (TPSF) imeandaa mfumo wa kielektroniki wa kupokea malalamiko na kupata mrejesho wa wawekezaji (*Online Complaints and Feedback Platform*) ambao utaanza kutumika katika Mwaka 2020/2021. Mfumo huo utapokea maoni na ushauri kwa njia ya haraka na kuleta ufanisi katika kuwashudumia.
68. **Mheshimiwa Spika**, Mazingira ya uwekezaji na ufanyaji biashara nchini yameendelea kuimarika. Taarifa ya Benki ya Dunia ya Wepesi wa Kufanya Biashara (*Ease of Doing Business Report*) ya Mwaka 2020 iliyotolewa Oktoba 2019 inaonesha kuwa Tanzania imepanda kwa nafasi tatu (3) kutoka nafasi ya 144 hadi kufikia nafasi ya 141. Lengo letu ni kufikia nafasi ya juu kufikia Mwaka 2025. Naziagiza Wizara na Taasisi zote za Serikali zinazohusika na utekelezaji wa maboresho na kuweka mazingira mazuri na rafiki ya kuratibu kwa ukaribu ili kufungua fursa zaidi.
69. **Mheshimiwa Spika**, kwa upande wa kukuza uwekezaji, Serikali kuititia Ofisi ya Waziri Mkuu imeendelea kuhamasisha Mikoa yote nchini kuandaa Makongamano ya Uwekezaji sambamba na kuzindua Miongozo ya Uwekezaji ya Mikoa inayobainisha fursa za uwekezaji za Mikoa pamoja na maeneo ya uwekezaji yaliyotengwa ili kuhamasisha na kuvutia uwekezaji zaidi katika Mikoa hiyo. Hadi sasa, Mikoa 14 ya Ruvuma, Songwe, Pwani, Lindi, Kagera, Mtwara, Geita, Kilimanjaro, Simiyu, Manyara, Dodoma, Mwanza, Kigoma na Morogoro imezindua miongozo hiyo. Mikoa yote ambayo hajakamilisha kuandaa miongozo hiyo ifanye hivyo kabla ya Septemba 2020.

70. ***Mheshimiwa Spika***, Ofisi ya Waziri Mkuu imeendelea kuratibu makongamano ya uwekezaji yaliyofanyika hapa nchini kama vile Kongamano la Biashara na Uwekezaji kati ya Tanzania na Uganda, Tanzania na Afrika Kusini; Afrika Mashariki na Sweden na Makongamano mengine yaliyofanyika nje ya Nchi kama vile Tanzania na Burundi; "Investment for Africa" liliofanyika nchini Misri; Kongamano lilioloandaliwa na Benki ya Maendeleo ya Afrika (AfDB) liliofanyika Afrika Kusini; na Kongamano kati ya Pakistani na Afrika liliofanyika nchini Kenya. Tumeendelea kupokea wawekezaji wanaofika nchini kwa ajili ya kutafuta fursa za uwekezaji kutoka Nchi mbalimbali.

71. ***Mheshimiwa Spika***, Serikali inahakikisha maeneo ya uwekezaji yanatengwa na kuendelezwa kwa kuwekewa miundombinu ya msingi ya maji, umeme, mawasiliano na barabara. Hadi Februari 2020, jumla ya hekta 854,821.61 zimetengwa kwa ajili ya uwekezaji katika Halmashauri zote nchini.

72. ***Mheshimiwa Spika***, kuititia kitengo cha Huduma za Mahala Pamoja (*One Stop Facilitation Centre*) kilichopo Kituo cha Uwekezaji Tanzania (TIC) chenye watendaji kutoka Taasisi 10 wameendelea kutoa huduma za muda mfupi kwa wawekezaji wetu kuititia Kituo hicho hadi kufikia Februari 2020, jumla ya miradi 146 yenye thamani ya Dola za Marekani Milioni 1,514.57 inayotegemewa kutoa ajira za moja kwa moja zipatazo 26,384 ilisajiliwa ambapo miradi 52 sawa na asilimia 36 inamilikiye na wageni, miradi 50 sawa na asilimia 34 inamilikiye na Watanzania na miradi 44 sawa na asilimia 30 inamilikiye kwa ubia kati ya wageni na Watanzania. Katika miradi iliyosajiliwa katika Mwaka huu wa Fedha miradi 95 sawa na asilimia 65 ya miradi yote inahusisha sekta ya uzalishaji viwandani.

SEKTA ZA UZALISHAJI

Viwanda

73. ***Mheshimiwa Spika***, kwa kutambua umuhimu wa viwanda Serikali imeendelea kuchukua hatua madhubuti ili

kuwezesha sekta hii kukua kwa haraka na kutoa mchango mkubwa zaidi katika Pato la Taifa pamoja na kupunguza umaskini. Katika kutekeleza dhana hii kwa vitendo katika mwaka 2019/2020, Serikali iliimarisha kiwanda cha Ngozi na Bidhaa za Ngozi cha Karanga (Moshi) na kuimarisha Shirika la Nyumbu (Pwani) ili kuongeza uzalishaji ikiwemo wa magari ya zimamoto. Vilevile, ada na tozo 54 zilifutwa ili kuondoa kero na urasimu kwa wafanyabiashara na wawekezaji katika sekta hii. Aidha, uzalishaji katika baadhi ya viwanda ulianza ikiwa ni pamoja na Pipe Industries Co. Limited (Dar es Salaam), Kiwanda cha Chai cha Kabambe (Njombe), kiwanda cha Yalin Cashewnut Co. Limited (Mtwara), kiwanda cha 21st Century Food and Packaging (Dar es Salaam), kiwanda cha kusaga mahindi (MeTL, Dar es Salaam), kiwanda cha bidhaa za plastiki cha Plasco Pipelines Co. Ltd (Dar es Salaam), kiwanda cha kupakia na kuhifadhi parachichi, Rungwe Avocado na kiwanda cha kuchakata parachichi kwa ajilli ya kutengeneza mafuta (KUZA Afrika).

74. ***Mheshimiwa Spika***, kutohana na jitihada kubwa zinazoendelea kufanya na Serikali za kujenga uchumi wa viwanda, jumla ya viwanda vipyta zaidi ya 4,000 vimejengwa katika mikoa mbalimbali. Viwanda vilivyojengwa vinazalisha bidhaa za ujenzi; pamoja na viwanda vya kusindika mazao ya kilimo ikiwemo nafaka, matunda, mafuta ya kupikia na bidhaa za ngozi. Ujenzi wa viwanda vipyta nchini, katika kipindi cha Serikali ya awamu ya tano, umechangia kupatikana kwa ajira mpya 482,601 nchi nzima.

75. ***Mheshimiwa Spika***, katika mwaka 2020/2021, Serikali itaendelea kuondoa kero zinazokwamisha ufanisi na ukuaji wa sekta ya viwanda. Aidha, Serikali itaimarisha ushindani katika soko kwa kuzingatia sheria na kanuni za ushindani sawa hususan wa bidhaa zinazozalishwa ndani ya nchi kama vile nondo, mabomba ya plastiki, nguo na mavazi, bidhaa za ngozi na marumaru. Lengo ni kuimarisha msingi wa ukuaji wa sekta ya viwanda nchini pamoja na kuvutia sekta binafsi kuwekeza au kushirikiana na Serikali kuwekeza kwenye viwanda.

Kilimo

76. **Mheshimiwa Spika**, sekta ya kilimo ni muhimu katika kuhakikisha usalama wa chakula, kupambana na umaskini, kuongeza ajira pamoja na kuleta maendeleo ya Nchi kwa ujumla. Kwa kulitambua hilo, Serikali ya Awamu ya Tano imeendelea kutoa kipaumbele kikubwa kwenye sekta hiyo kwa lengo la kuwawezesha wakulima kupata pembejeo na zana za kisasa ili kuongeza tija katika kilimo na hivyo kuleta mageuzi ya kiuchumi.

Hali ya Upatikanaji wa Chakula

77. **Mheshimiwa Spika**, pamoja na mambo mengine hususan kuimarika kwa hali ya hewa, mageuzi yanayofanywa katika sekta ya kilimo, yamechangia kuimarika kwa hali ya upatikanaji wa chakula nchini na upatikanaji wa malighafi za viwanda, sambamba na kuongeza tija kwa wakulima. Katika msimu wa kilimo wa Mwaka 2018/2019, uzalishaji wa mazao ya chakula kitaifa ulikuwa tani milioni 16.3 ikilinganishwa na mahitaji halisi ya tani milioni 13.6. Uzalishaji huo umeihakikisha Nchi utoshelevu wa chakula kwa asilimia 118 kwa msimu wa kilimo wa Mwaka 2019/2020.

Upatikanaji wa Pembejeo za Kilimo

78. **Mheshimiwa Spika**, Serikali imeendelea kuhamasisha matumizi ya pembejeo na mbinu bora za kilimo na teknolojia kwa lengo la kukifanya kilimo chetu kuwa cha kisasa zaidi na chenye tija. Hadi kufikia Februari 2020, upatikanaji wa mbegu bora za mazao umefikia tani 71,207 ikilinganishwa na tani 57,023 za msimu wa Mwaka 2018/2019. Kati ya mbegu hizo, tani 66,031 zimezalishwa nchini ambayo ni sawa na asilimia 93 na tani 5,175 sawa na asilimia 7 zimeingizwa kutoka nje ya nchi.

79. **Mheshimiwa Spika**, Serikali imeendelea kuimarisha upatikanaji wa mbolea nchini kwa kutumia Mfumo wa Ununuzi wa Mbolea kwa Pamoja ambao umesaidia kupunguza bei ya mbolea kwa wakulima. Kutokana na mfumo huo, upatikanaji wa mbolea hadi Februari 2020 umefikia tani 516,813 sawa na asilimia 89 ya lengo la tani 586,604. Kwa kuwa mbolea hizo hutumika kulingana na hatua

mbalimbali za ukuaji wa mazao, Serikali inaendelea ku hakikisha asilimia 11 iliyobaki inapatikana na kusambazwa kwa wakulima kwa wakati. Aidha, Serikali imeendelea kuratibu upatikanaji wa viuatilifu ambapo hadi Januari 2020, jumla ya tani 8,719 za viuatilifu zimeingizwa nchini ili kudhibiti visumbufo vya mimea na mazao.

Benki ya Maendeleo ya Kilimo Tanzania (TADB)

80. ***Mheshimiwa Spika***, katika kipindi cha Julai 2019 hadi Februari 2020, Benki ya Maendeleo ya Kilimo Tanzania (TADB), imetoa mikopo ya Shilingi bilioni 34 kwa miradi ya kilimo 38 na kufanya jumla ya mikopo iliyotolewa kufikia Shilingi bilioni 160.6 toka Benki ilipoanza utoaji wa mikopo. Mikopo iliyotolewa imewanufaisha wakulima wadogo, wa kati na wakubwa wapatao milioni 2.1 wa mazao ya kilimo, mifugo na uvuvi pamoja na viwanda vidogo vya uchakataji wa mazao.

81. ***Mheshimiwa Spika***, katika kipindi hicho TADB imetoa mikopo ya ziada ya Shilingi bilioni 31.77 kupitia Mfuko wa Dhamana kwa Wakulima Wadogo. Mikopo hiyo imewanufaisha wakulima wapatao 5,080, biashara ndogo na za kati za kilimo zipatazo 30, Vyama vya Msingi (AMCOS) 20 katika mikoa mbalimbali nchini pamoja na kufanikisha ununuzi wa matrekta 19 katika mikoa hiyo.

Uzalishaji wa Zao la Chikichi

82. ***Mheshimiwa Spika***, Serikali imedhamiria kumaliza tatizo la upatikanaji wa mafuta ya kula nchini kwa kuendeleza zao la chikichi sambamba na mazao mengine yanayozalisha mafuta. Uendelezaji wa zao la chikichi unahuisha kupanda kwa wingi miche mipyä yenye uzalishaji wenye tija. Serikali kupitia Taasisi ya Utafiti wa Kilimo nchini (TARI) imeanza uzalishaji wa mbegu bora za chikichi aina ya TENERA inayotoa mafuta mengi. Lengo ni kuzalisha mbegu bora na za kutosha zitakazowezesha wakulima kuongeza uzalishaji na hivyo kujiongezea kipato na kupunguza matumizi ya fedha za kigeni kuagiza mafuta ya kula kutoka nje ya nchi.

83. ***Mheshimiwa Spika***, hadi tarehe 15 Februari 2020, mbegu 1,525,017 zimezalishwa ambazo zitatosha kupanda eneo la ekari 30,500. Tayari mbegu 1,026,111 zimesambazwa kwa ajili ya kuziotesha ili miche bora iweze kusambazwa kwa wakulima. Usambazaji kwa ajili ya uoteshaji umefanyika katika halmashauri za mkoa wa Kigoma na taasisi nyingine ikiwemo Magereza ya Kwitanga na llagala na JKT Bulombora.

84. ***Mheshimiwa Spika***, katika Mwaka 2020/2021, Serikali itaendelea kuimarisha huduma za ugani, kilimo cha umwagiliaji, ushirika na upatikanaji wa pembejeo ikiwa ni pamoja na mbegu bora za mazao. Aidha, itajenga na kukarabati miundombinu ya kuhifadhi mazao ya kilimo na masoko.

Zao la Mkonge

85. ***Mheshimiwa Spika***, sote ni mashahidi kuwa zao la Mkonge lilikatiwa tamaa na wakulima na wakulima wengi waliacha kulima zao hili. Serikali imeanza kuchukua hatua za kufufua kilimo cha Mkonge na masoko yake. Tunafufua mamlaka ya Mkonge ili itambue mashamba yake na mali zingine ili ianze kuhamasisha wakulima wadogo na wakubwa na kukaribisha uwekezaji wa sekta ya Mkonge. Tunaimarisha Taasisi ya Utafiti ya Mlingano ili izalishe miche zaidi na kuisambaza kwa wakulima. Natoa wito kwa Wizara, Wakuu wa Mikoa inakolima Mkonge kutambua wakulima wa Mkonge na wapate msaada wa kitaalam.

Mifugo

86. ***Mheshimiwa Spika***, Serikali imeendelea kuimarisha sekta ya mifugo nchini ili iweze kutoa mchango mkubwa zaidi katika Pato la Taifa na kutoa fursa za ajira. Ili kufikia lengo hili, Serikali imehamasisha wafugaji kuendelea kuimarisha ufugaji wa kisasa, kuchakata bidhaa za mifugo kwa ajili ya mahitaji ya ndani, ikiwemo lishe bora na kuuza nje pamoja na kuhamasisha uwekezaji wa sekta binafsi. Aidha, katika Mwaka 2019/2020, Serikali imekarabati majosho 292, inaendelea na ukarabati wa majosho 207 na kuendelea na ujenzi wa

majosho mapya 84 katika halmashauri mbalimbali nchini. Hatua hii imewezesha kuongezeka kwa majosho yanayofanya kazi kutoka 1,486 Mwaka 2018/2019 hadi majosho 1,738 Mwaka 2019/2020. Aidha, Serikali imenunua lita 12,549 za dawa za kuogesha mifugo.

87. ***Mheshimiwa Spika***, katika Mwaka 2020/2021 Serikali itaendelea kuhimiza ufgaji wa kisasa pamoja na kuimarisha afya ya mifugo kwa kuwezesha upatikanaji wa huduma za chanjo na tiba kwa kuimarisha vituo vya utengenezaji wa chanjo za mifugo. Aidha, Serikali itaendelea kuhakikisha upatikanaji wa malisho kwa kutambua, kutenga, kumilikisha, kusimamia na kuendeleza maeneo ya malisho. Vilevile, huduma za ugani zitaboreshw na mafunzo kwa wafugaji na maafisa ugani yatatolewa ili kuwapatia maarifa na teknolojia mbalimbali kwa lengo la kuongeza tija.

Uvuvi

88. ***Mheshimiwa Spika***, Serikali imeendelea kuboresha Sekta ndogo ya Uvuvi ili iweze kuchangia kikamilifu katika Pato la Taifa na ajira kwa ujumla. Hatua zilizochukuliwa ni pamoja na kuondolewa kwa kodi katika zana na malighafi za uvuvi, kupambana na uvuvi haramu, kuboreshwa kwa mialo ya kupokelea samaki na kuwa ya kisasa, kuhamasisha uwekezaji katika ukuzaji wa viumbwe maji pamoja na kuhamasisha sekta binafsi kuwekeza katika viwanda vya kuchakata samaki.

89. ***Mheshimiwa Spika***, katika Mwaka 2020/2021, Serikali itaimarisha sekta ya uvuvi ili kuongeza mchango wa sekta hiyo katika pato la Taifa na kuwaongezea wavuvi kipato. Hatua zitakazochukuliwa zitahusisha, utekelezaji wa Mkakati wa kujenga na kuboresha miundombinu ya uvuvi, mkakati wa kufufua Shirika la Uvuvi Tanzania, kuweka mazingira bora katika uvuvi wa bahari kuu kwa kuweka vivutio kwa wawekezaji, kuendelea kupambana na wavuvi haramu na kuhamasisha matumizi endelevu ya rasilimali za uvuvi, uhifadhi na uchakataji wa samaki ili kuimarisha mnyororo wa thamani.

Utalii

90. **Mheshimiwa Spika**, sekta ya utalii nchini imeendelea kuimarika ikichagizwa pamoja na mambo mengine na uwekezaji mkubwa uliofanyika katika miundombinu ya usafiri na usafirishaji na utoaji huduma. Katika Mwaka 2019, idadi ya watalii walioingia nchini ilifikia 1,510,151 ikilinganishwa na 1,505,702 Mwaka 2018. Ongezeko la idadi ya watalii nchini limeongeza mapato ya Serikali yatokanayo na utalii kutoka Dola za Marekani bilioni 2.4 Mwaka 2018 hadi Dola za Marekani bilioni 2.6 Mwaka 2019.

91. **Mheshimiwa Spika**, katika hatua nyingine ya kuimarisha shughuli za utalii nchini, Serikali imepandisha hadhi Mapori ya Akiba 6 ambayo ni Burigi (Chato), Ibanda (Kyerwa), Rumanyika (Karagwe), Nyerere, Mto Ugalla na Kigosi kuwa Hifadhi za Taifa. Lengo ni kuimarisha Sekta ya Utalii kwa kuwa na maeneo mengi ya hifadhi na vivutio vya watalii yatakayosaidia kuongeza wigo wa utalii na mapato yatokanayo na sekta hiyo.

92. **Mheshimiwa Spika**, katika Mwaka 2020/2021, Serikali itaendelea kuvitangaza vituo vya utalii ndani na nje ya nchi hususan kwenye masoko ya kimkakati, kuimarisha hifadhi mpya 6 za Taifa, kukuza wigo wa mazao ya utalii na kuweka mazingira wezeshi ili sekta binafsi ishiriki kikamilifu katika uwekezaji kwenye utalii. Kadhalika, maeneo mengine yatakayopewa kipaumbele ni utalii wa meli, mikutano, fukwe, utamaduni, malikale, ikolojia na jiolojia.

Madini

93. **Mheshimiwa Spika**, usimamizi mzuri wa mikakati na sheria za ulinzi wa rasilimali na maliasili zetu umekuwa chachu ya kukua na kuimarika kwa sekta ya Madini nchini. Usimamizi huo umeifanya sekta hiyo kutoa mchango mkubwa katika ukuaji wa Pato la Taifa. Mathalan, katika kipindi cha nusu ya kwanza ya Mwaka 2019/2020 mchango wa Sekta ya madini ulikuwa asilimia 13.7. Katika kipindi hicho, sekta ya madini ilishika nafasi ya pili katika kuchangia Pato la Taifa baada ya sekta ya ujenzi iliyochangia asilimia 16.5.

94. ***Mheshimiwa Spika***, hadi kufikia Januari 2020, maduhuli ya Serikali yaliyokusanya kupitia Sekta ya Madini ni Shilingi bilioni 284.4. Kiwango hicho ni sawa na asilimia 60.4 ya lengo la mwaka la kukusanya Shilingi bilioni 470.89. Mafanikio hayo, ni ishara tosha ya kuendelea kuimarika kwa sekta hii kufuatia usimamizi thabiti unaowekwa na Serikali.
95. ***Mheshimiwa Spika***, Serikali imeanzisha masoko ya madini nchini kwa lengo la kupata takwimu sahihi za mauzo ya madini, kuwasaidia wachimbaji wadogo kupata soko la uhakika, kupata bei stahiki kwa bidhaa za madini na kuondoa tatizo la utoroshaji na biashara haramu ya madini. Hatua hiyo imewezesha kuongezeka kwa mapato ya Serikali kupitia tozo za mrabaha na ada ya ukaguzi wa mauzo ya madini kwenye masoko.
96. ***Mheshimiwa Spika***, hadi Januari 2020, jumla ya masoko ya madini 28 na vituo vidogo vya ununuzi wa madini 28 vimeanzishwa nchini. Kupitia masoko na vituo hivyo, katika kipindi cha Machi 2019 hadi Januari 2020, jumla ya kilogramu 9,237.34 za dhahabu; karati 12,973.14 za madini ya almasi; kilogramu 20,099.17 za madini ya bati na kilogramu 514,683.28 za madini ya vito mbalimbali ziliuzwa na kuipatia Serikali mapato ya Shilingi bilioni 66.57 ambazo zimetokana na mrabaha, ada ya ukaguzi na ushuru wa Halmashauri.
97. ***Mheshimiwa Spika***, masoko ya madini yamekuwa na mchango mkubwa katika kuimarisha upatikanaji wa takwimu sahihi za madini tofauti na ilivyokuwa awali kabla ya kuanzishwa kwake. Masoko hayo, yana ulinzi na usalama wa kutosha na sifa zote za kimataifa zinazohitajika katika kuendesha biashara ya madini. Hivyo, natoa rai kwa wadau wa ndani na nje ya nchi kutumia masoko na vituo hivyo ambavyo vinaendeshwa kwa misingi ya kisheria kwa kuzingatia ushindani na uwazi wa kibiashara.
98. ***Mheshimiwa Spika***, katika Mwaka 2020/2021, Serikali itaendelea kuimarisha uchimbaji mdogo na wa kati wa madini nchini; ukusanyaji wa mapato yatokanayo na madini; kuhamasisha uwekezaji katika Sekta ya Madini; kuimarisha

shughuli za ugani na utafiti, uongezaji thamani madini na masoko.

Nishati

99. ***Mheshimiwa Spika***, hali ya upatikanaji wa umeme nchini imeendelea kuimarika na kuchangia katika ukuaji wa uchumi na ustawi wa Taifa kwa ujumla. Uwezo wa mitambo ya kufua umeme nchini ni Megawati 1,602.32 ambapo kati ya hizo Megawati 1,565.72 zipo katika Mfumo wa Gridi ya Taifa na Megawati 36.6 zipo nje ya Mfumo wa Gridi ya Taifa. Aidha, hali ya maji katika mabwawa ya Mtera, Kidatu, Kihansi, Nyumba ya Mungu na *New Pangani Falls* imeendelea kuwa nzuri na hivyo kutuhakikisha kuwa na umeme wa uhakika.

100. ***Mheshimiwa Spika***, pamoja na kuelezea juu ya mafanikio tuliyoyapata katika utekelezaji wa Mradi wa Kufua Umeme wa Maji wa Julius Nyerere hapo awali, Serikali vilevile inatekeleza Mradi wa Kuzalisha Umeme wa Rusumo utakaozalisha Megawati 80. Kukamilika kwa miradi hii na mingine itaimarisha upatikanaji wa umeme nafuu na wa uhakika na hivyo kuchangia katika maendeleo ya ukuaji wa viwanda na uchumi.

101. ***Mheshimiwa Spika***, katika Mwaka 2020/2021, Serikali itaendelea kutekeleza miradi mikubwa na ya kielelezo ya uzalishaji wa umeme hususan Mradi wa Kufua Umeme wa Maji wa Julius Nyerere (MW 2,115), upanuzi wa Mradi wa Kinyerezi I (MW 185) pamoja na kuimarisha mifumo ya usafirishaji na usambazaji wa umeme nchini. Aidha, Serikali itaendelea kutekeleza Awamu ya Tatu ya Mradi wa Kupeleka Umeme Vijijini ili kuhakikisha vijiji vilivyobaki vinapatiwa umeme.

HUDUMA ZA KIUCHUMI

Ardhi

102. ***Mheshimiwa Spika***, ardhi ni rasilimali namba moja katika kuifikia ndoto ya Serikali ya kujenga uchumi wa viwanda. Kwa msingi huo, Serikali imeendelea kusimamia

upimaji wa ardhi, mipango ya matumizi ya ardhi kuanzia ngazi ya kijiji hadi Taifa na umilikishaji ardhi kwa wananchi. Sambamba na kuimarisha utoaji huduma kwa njia ya kielektroniki, Serikali inatekeleza mpango wa kusogezza huduma za ardhi karibu na wananchi. Hadi sasa ofisi za ardhi za mikoa 26 zimeanzishwa pamoja na kuendelea kuziimarisha ofisi zote za ardhi za Halmashauri kwa kuwapatia mafunzo wataalam wa sekta ya ardhi na kununua vifaa.

103. ***Mheshimiwa Spika***, katika Mwaka 2019/2020, Serikali imekamilisha awamu ya kwanza ya usimikaji wa Mfumo Unganishi wa Kuhifadhi Kumbukumbu za Ardhi katika Ofisi za Ardhi Kanda ya Dar es Salaam na Halmashauri za Manispaa ya Kinondoni na Ubungo. Lengo ni kuharakisha upimaji na utoaji hatimiliki za ardhi ili kuwawezesha wananchi wengi zaidi kumiliki ardhi kisheria na kutumia hati hizo kupata mikopo katika taasisi za fedha itakayowezesha kuanzisha na kuendeleza shughuli mbalimbali za ujasiriamali.

Mipango ya Matumizi ya Ardhi

104. ***Mheshimiwa Spika***, Serikali imeendelea kusimamia upangaji na utekelezaji wa mipango ya matumizi ya ardhi katika ngazi ya Kanda, Wilaya na Vijiji. Lengo la Serikali ni kuharakisha upatikanaji wa ardhi kwa ajili ya makazi na shughuli mbalimbali ikiwemo kilimo, ufugaji, biashara na uwekezaji. Katika kipindi cha Julai 2019 hadi Februari 2020, mipango ya matumizi ya ardhi ya vijiji 132 imeandalisha katika Wilaya 27.

105. ***Mheshimiwa Spika***, sambamba na uandaaji wa Mipango ya Matumizi ya Ardhi, Serikali imeendelea kutatua migogoro ya matumizi ya ardhi katika maeneo mbalimbali. Katika Mwaka 2019/2020 Mheshimiwa Rais wetu mpandwa Dkt. John Pombe Joseph Magufuli ametoa kibali kwa vijiji 920 kati ya vijiji 975 vilivyokuwemo ndani ya hifadhi na mapori ya akiba kuhalalishwa rasmi kwa ajili ya shughuli za kiuchumi na kijamii. Hatua hiyo itapunguza migogoro iliyokuwa ikiendelea katika maeneo mbalimbali nchini na hivyo kuwawezesha wananchi kutumia muda mwingu katika shughuli za uzalishaji.

Miundombinu ya Usafiri na Usafirishaji

106. ***Mheshimiwa Spika***, sekta ya miundombinu hususan ya usafiri na usafirishaji ndio kiunganishi cha sekta za uchumi wa nchi ili kuwezesha shughuli za uzalishaji mali na utoaji huduma katika jamii. Kuimarika kwa sekta hii, ni kichocheo muhimu katika kukua kwa uchumi na maendeleo ya wananchi kwa ujumla.

107. ***Mheshimiwa Spika***, kwa kutambua umuhimu wa sekta hii Serikali ya Awamu ya Tano ilichukua hatua za makusudi kuanza ujenzi mkubwa wa barabara, madaraja, vivuko, ufufuaji na ujenzi wa reli mpya, uimarishaji wa usafiri wa majini, na uboreshaji wa usafiri wa anga ili kuchochaea ukuaji wa uchumi kwa kurahisisha huduma za uchukuzi na usafirishaji wa watu na bidhaa.

Barabara na Madaraja

108. ***Mheshimiwa Spika***, katika Mwaka 2019/2020, Serikali imepata mafanikio makubwa katika kujenga mtandao wa barabara za kiwango cha lami nchini. Serikali imeendelea kuhakikisha mikoa yote inaunganishwa na mtandao wa barabara za lami ili kurahisisha usafirishaji wa watu na bidhaa.

109. ***Mheshimiwa Spika***, katika kipindi hicho jumla ya kilomita 399.07 za barabara kuu na barabara za mikoa zilijengwa kwa kiwango cha lami. Aidha, kilomita 56 za barabara kuu zillifanyiwa ukarabati kwa kiwango cha lami na kilomita 84 za barabara za mikoa zillifanyiwa ukarabati kwa kiwango cha changarawe. Hadi kufikia Februari 2020, jumla ya kilomita 6,960 zimefanyiwa matengenezo ya kawaida, kilomita 1,444 zimefanyiwa matengenezo maalum na madaraja 416 yamefanyiwa matengenezo.

110. ***Mheshimiwa Spika***, katika kuondoa msongamano wa magari Jijini Dar es Salaam, Serikali inaendelea na ujenzi wa barabara ya njia 8 kutoka Kimara hadi Kibaha yenye urefu wa Kilomita 19 ambapo ujenzi umefikia asilimia 63. Mradi

mwingine ni ujenzi wa *Ubungo Interchange* ambao umefikia asilimia 65.

111. ***Mheshimiwa Spika***, miradi mingine inayotekelawa ni pamoja na ujenzi wa Daraja la Tanzanite (Salender) lenye urefu wa Kilomita 6.2 uliofikia asilimia 25 na kuanza maandalizi ya ujenzi wa daraja la Kigongo - Busisi lenye urefu wa kilomita 3.2 na upana wa mita 28.45. Aidha, kati ya Julai 2019 hadi Januari 2020 Serikali imetoa Shilingi bilioni 703.6 kwa ajili ya utekelezaji wa miradi ya barabara na madaraja nchini.

112. ***Mheshimiwa Spika***, katika Mwaka 2020/2021, Serikali itaendelea na utekelezaji wa miradi mikubwa niliyoitaja pamoja na mingine inayoendelea. Vilevile, Serikali itaanza ujenzi wa barabara na madaraja mapya ili kuwahakikisha wananchi, wawekezaji na wafanyabiashara huduma bora na za uhakika za usafirishaji katika kipindi chote cha mwaka.

Reli

113. ***Mheshimiwa Spika***, kama nilivyoeleza hapo awali, moja ya mafanikio makubwa tuliyoyapata katika eneo la reli ni kuendelea na ujenzi wa Reli ya Kati kwa Kiwango cha Kimataifa. Nikiri pia kuwa, katika kipindi hiki, Serikali inajivunia kurejesha huduma ya reli kati ya Dar es Salaam na Moshi ambayo ilisimama kwa zaidi ya miaka 20 na kufufuliwa kwa huduma ya reli kati ya Tanga na Moshi iliyo simama kwa takribani miaka 12 ambapo hadi Machi 2020 jumla ya abiria 33,459 na mizigo tani 5,080 imesafirishwa kuitia reli hizo. Aidha, ukarabati wa reli ya kati kutoka Dar es Salaam hadi Isaka nao unaendelea kwa kuondoa reli zote nyepesi na kuweka reli mpya nzito. Ukarabati huo umewezesha kurejea kwa huduma za usafiri wa abiria na mizigo na hivyo kurahisisha usafirishaji, kupunguza kero ya usafiri na ajali za barabarani.

114. ***Mheshimiwa Spika***, katika Mwaka 2020/2021, Serikali itakamilisha ujenzi wa reli ya kati kwa kiwango cha kimataifa kwa kipande cha Dar es Salaam – Morogoro na kuendelea na ujenzi wa kipande cha Morogoro – Makutupora sambamba na kukarabati miundombinu mingine ya reli.

Bandari

115. ***Mheshimiwa Spika***, katika eneo la bandari, Serikali imeendelea kuboresha na kuimarishe miundombinu ya bandari zilizopo katika mwambao wa pwani na maziwa kwa lengo la kuendeleza huduma ya usafiri wa majini ndani ya nchi na nchi jirani. Katika Mwaka 2019/2020, Serikali imekamilisha ujenzi wa gati namba 1, 2, 3 na gati la kupakia na kupakua magari (*RoRo Berth*) katika Bandari ya Dar es Salaam. Kazi ya ukarabati wa gati namba 5 hadi 7 inaendelea.

116. ***Mheshimiwa Spika***, kwa upande wa Bandari ya Mtwara, ujenzi wa Gati lenye urefu wa mita 300 umefikia asilimia 60 wakati ukarabati wa Gati namba 2 na uongezaji wa kina cha Bandari ya Tanga unaendelea na umefikia asilimia 60. Ujenzi na ukarabati wa bandari zetu utaifanya nchi yetu kuendelea kuwa lango muhimu la uagizaji na uingizaji bidhaa kuelekea nchi jirani.

Ujenzi wa Meli

117. ***Mheshimiwa Spika***, Serikali inafanya kazi changamoto ya utoaji wa huduma za usafiri katika Maziwa Makuu ya Victoria, Tanganyika na Nyasa. Kwa upande wa ziwa Nyasa, tayari ujenzi wa Meli ya MV Mbeya yenye uwezo wa kubeba abiria 200 na tani 200 za mizigo umekamilika. Vilevile, tarehe 8 Desemba 2019, Mheshimiwa Rais Dkt. John Pombe Joseph Magufuli aliweka jiwe la msingi la ujenzi wa chelezo, meli mpya ya MV Mwanza na ukarabati wa Meli za MV Victoria na MV Butiama.

118. ***Mheshimiwa Spika***, hadi kufikia Februari 2020, ujenzi wa meli ya MV Mwanza itakayokuwa na uwezo wa kubeba abiria 1,200 na tani 400 za mizigo ulikuwa umefikia asilimia 52. Aidha, ujenzi wa chelezo umefikia asilimia 80, ukarabati wa meli za MV Victoria asilimia 75 na MV Butiama asilimia 70. Katika Mwaka 2020/2021, Serikali itaendelea kuboresha huduma za usafiri kwa njia ya maji ikiwa ni pamoja na kukamilisha miradi inayoendelea, kukarabati vyombo vilivyopo na kununua vyombo vipyta.

Usafiri wa Anga na Viwanja vyta Ndege

119. ***Mheshimiwa Spika***, pamoja na mafanikio niliyoyaeleza hapo awali kuhusu kufufua Shirika la Ndege Tanzania, katika Mwaka 2019/2020 Serikali imeendelea kuhakikisha kuwa anga la Tanzania ni salama ili kuimarisha utoaji wa huduma za usafiri wa anga. Aidha, Serikali inakamilisha usimikaji wa mfumo wa rada 4 za kuongozea ndege za kiraia katika viwanja vyta Ndege vyta Julius Nyerere, Kilimanjaro, Mwanza na Songwe.

120. ***Mheshimiwa Spika***, Serikali imeendelea kuboresha viwanja vyta Ndege mbalimbali vilivyopo nchini. Hadi kufikia Februari, 2020 Serikali imekamilisha ujenzi wa jengo la tatu la abiria katika Kiwanja cha Ndege cha Kimataifa cha Julius Nyerere. Kukamilika kwa jengo hilo kunawezesha kuwashudumia abiria milioni 6 kwa mwaka na hivyo kuongeza mapato. Serikali pia, imekamilisha upanuzi wa Kiwanja cha Ndege cha Mwanza na inaendelea na ujenzi wa jengo la abiria katika uwanja huo. Jengo hilo ambalo litagharimu Shilingi bilioni 13.26 litahudumia abiria 400,000 kwa mwaka. Vilevile, Serikali inaendelea na ujenzi na ukarabati wa viwanja vyta Ndege vyta Mtwara, Songea, Geita, Nachingwea, Iringa na Musoma.

121. ***Mheshimiwa Spika***, katika Mwaka 2020/2021, Serikali itaendelea kuboresha usafiri wa anga nchini ili kuhakikisha kuwa Tanzania inakuwa kitovu cha usafiri wa anga kwa nchi za Afrika Mashariki na Kati. Katika kufanikisha azma hiyo, Serikali itaendelea kuhakikisha kuwa usalama na miundombinu ya viwanja vyta Ndege inaboreshwa.

Mawasiliano

122. ***Mheshimiwa Spika***, katika eneo la mawasiliano Serikali imeendelea na zoezi la usajili wa laini za simu kwa njia ya biometria Nchi nzima. Hadi mwisho wa mwezi Februari, 2020 jumla ya laini milioni 31.4 kati ya laini milioni 43.9 zilikuwa zimesajiliwa. Idadi hii ni sawa na asilimia 71 ya zoezi zima la usajili. Nitoe wito kwa wananchi waliopata namba za

vitambulisho vya Taifa kukamilisha usajili wa laini zao kwa njia ya biometria ili waendelee kupata huduma za mawasiliano. Zoezi hili lina umuhimu kwa Taifa kwani linasaidia kuimarisha usalama wa watumiaji wa huduma za mawasiliano nchini na Taifa kwa ujumla.

123. ***Mheshimiwa Spika***, Serikali pia, imeendelea kusimamia mtambo wa *Telecommunications Traffic Monitoring System (TTMS)* ili kuhakikisha kuwa tunapata mapato stahiki kutokana na huduma za mawasiliano. Mfumo huu umeongeza ufanisi katika kusimamia huduma ya mawasiliano ya simu nchini. Katika kipindi cha Julai, 2019 hadi Februari, 2020 jumla ya miamala bilioni 2 yenye thamani ya Shilingi trillioni 12.2 imefanyika ambapo Serikali imepata mapato ya Shilingi bilioni 7.3.

124. ***Mheshimiwa Spika***, katika Mwaka 2020/2021, Serikali itaendelea kushirikiana na makampuni ya simu kuboresha huduma za mawasiliano hususan maeneo ya pembezoni ili kuongeza kasi ya mawasiliano ya kimtandao kwa wananchi wa maeneo hayo. Aidha, Serikali itaendelea na ujenzi wa Mkongo wa Taifa wa Mawasiliano ili kufikisha huduma katika Makao Makuu ya Wilaya zote nchini pamoja na kuanza ujenzi wa Kituo cha Data Dodoma.

HUDUMA ZA JAMII

Elimu

125. ***Mheshimiwa Spika***, elimu ya kisasa na hasa yenye mwelekeo wa sayansi na teknolojia ina nafasi ya pekee katika kufanikisha ujenzi wa msingi wa uchumi wa kisasa wa Taifa linalojitegemea. Kwa kutambua umuhimu huo na kama nilivyooleza awali Serikali ilianzisha na kutekeleza Mpango wa Elimumsingi Bila Ada ili kuhakikisha kila mtoto mwenye umri wa kwenda shule anaandikishwa.

126. ***Mheshimiwa Spika***, katika hatua nyingine ya kuboresha elimu ya sekondari ninayo furaha kuliarifu Bunge lako Tukufu kuwa tarehe 31 Machi, 2020 Benki ya Dunia imeridhia kuipatia Tanzania mkopo wa Dola za Marekani

Milioni 500 sawa na takriban shilingi trillioni 1.14 kwa ajili ya kutekeleza mpango wa maboresho ya elimu ya sekondari nchini.

127. ***Mheshimiwa Spika***, Benki ya Dunia imeridhia kuipatia Tanzani mkopo huo baada ya kuridhishwa na utekelezaji wa sera ya Elimumsingi Bila Ada. Hivyo, mpango huu utaimarisha usalama wa watoto shulenii, kuongeza uandikishaji katika shule za sekondari na elimu mbadala, kuimarisha mafunzo kwa walimu na matumizi ya TEHAMA katika kufundisha hususan masomo ya sayansi.

128. ***Mheshimiwa Spika***, utekelezaji wa mpango huo utaongeza wigo wa elimu ya sekondari hususan kwa watoto wa kike na kuwawezesha wavulana na wasichana kukamilisha elimu hiyo. Serikali itaendelea kusimamia utekelezaji wa sera ya Elimumsingi Bila Ada kwa lengo la kuwawezesha watoto wetu wa kike kupata elimu ya sekondari na stadi za kazi, kuondoa vikwazo kwa watoto wa kike kupata elimu ya sekondari, kuimarisha matumizi ya TEHAMA katika ufundishaji na ujifunzaji pamoja na uratibu, usimamizi na tathmini ya ubora wa elimu ya sekondari.

129. ***Mheshimiwa Spika***, kwa upande wa elimu ya juu, Serikali imeongeza wigo wa upatikanaji wa mikopo kwa wanafunzi wa elimu ya juu na kutoa kipaumbele kwa watu wenye mahitaji maalum. Katika Mwaka 2019/2020, Serikali imeongeza fursa za upatikanaji wa elimu ya juu kwa kutoa mikopo kwa wanafunzi 130,883 ikilinganishwa na wanafunzi 122,754 kwa Mwaka 2018/2019. Aidha, Shilingi bilioni 450 zilitumika katika kipindi hicho ikilinganishwa na Shilingi bilioni 424.8 kwa Mwaka 2018/2019.

130. ***Mheshimiwa Spika***, katika Mwaka 2020/2021, Serikali itaendelea kusimamia utekelezaji wa Mpango wa Elimumsingi Bila Ada, kutoa mikopo kwa wanafunzi wa elimu ya juu na kuhimiza uwekezaji kwa kushirikiana na sekta binafsi hususan katika kuboresha miundombinu, vifaa vya kufundishia na kujifunzia na kuendeleza rasilimali watu ikiwa ni pamoja na kutoa mafunzo kwa walimu.

Maji

Upatikanaji wa Maji Vijijini

131. ***Mheshimiwa Spika***, Serikali kwa kushirikiana na wadau wa maendeleo imeendelea kutekeleza Programu ya Maendeleo ya Sekta ya Maji kwa lengo la kuongeza upatikanaji wa huduma ya maji safi na salama kwa wananchi wote hususan wale wanaoishi maeneo ya vijijini. Katika Mwaka 2019/2020, jumla ya miradi 94 ya maji yenye vituo vya kuchotea maji 2,495 katika maeneo mbalimbali vijijini imekamilika. Aidha, miradi 558 ipo katika hatua mbalimbali za utekelezaji.

132. ***Mheshimiwa Spika***, kutokana na juhudi kubwa za Serikali katika utekelezaji wa miradi hiyo, hadi Desemba 2019, upatikanaji wa huduma ya maji katika maeneo ya vijijini umefikia asilimia 64.8. Vilevile, ili kuboresha utoaji wa huduma ya maji vijijini, Serikali imeanzisha Wakala wa Usambazaji Maji na Usafi wa Mazingira Vijijini (*RUWASA*) wenye jukumu la kutekeleza miradi na kusimamia utoaji wa huduma za maji na usafi wa mazingira vijijini.

Upatikanaji wa Maji Mijini

133. ***Mheshimiwa Spika***, kwa upande wa maji mijini, Serikali imetekeleza miradi mipya ya maji katika Jiji la Dodoma na Dar es Salaam pamoja na maeneo ya Kibaha, Bagamoyo na Kisarawe. Aidha, Serikali pia imeboresha miundombinu ya upatikanaji wa huduma ya maji katika miji mikuu ya mikoa, wilaya, miji midogo na maeneo yanayohudumiwa na miradi ya maji ya kitaifa ya Chalinze, Mugango – Kiabakari, Maswa, Wanging'ombe, Masasi - Nachingwea na Kahama – Shinyanga. Utekelezaji wa miradi hiyo umewezesha upatikanaji wa maji katika miji ya mikoa kufikia asilimia 85.

134. ***Mheshimiwa Spika***, katika Mwaka 2020/2021, Serikali itaifanyia mapitio Sera ya Taifa ya Maji ya Mwaka 2002 ili kuzingatia masuala mapya ikiwa ni pamoja na mabadiliko ya tabianchi, kutilia mkazo suala la usafi wa mazingira na

matumizi ya vyanzo vya maji chini ya ardhi. Serikali pia, itakamilisha miradi inayoendelea, kuanza miradi mipya ya maji na kuanza upembuzi yakinifu na usanifu wa kina wa mradi wa kutoa maji Ziwa Victoria kupeleka Singida hadi Dodoma.

Afya

Ujenzi na Ukarabati wa Hospitali

135. **Mheshimiwa Spika**, Serikali inaendelea na miradi ya ujenzi wa hospitali za Rufaa za Mikoa, ikiwemo ujenzi wa hospitali za Mikoa mipya ya Geita, Simiyu, Songwe, Katavi, Njombe (Mgondechi). Vilevile, Serikali inaendelea na ujenzi wa hospitali za Mikoa ya Mara, Singida na Shinyanga pamoja na ujenzi wa hospitali za Wilaya katika Halmashauri 70 nchini. Vilevile, Serikali inajenga Hospitali ya Uhuru wilayani Chamwino, Dodoma na hospitali za rufaa za kanda za Mtwara, Mbeya na Burigi - Chato.

Huduma za Afya za Kibingwa

136. **Mheshimiwa Spika**, Serikali inaendelea kuimarisha huduma za kibingwa bobezi (*superspecialist*) katika Hospitali za Rufaa za Kanda, Hospitali Maalum na Hospitali ya Taifa. Utoaji wa huduma hizo umewevesha wananchi wengi kupata huduma ambazo awali zilikuwa zinapatikana nje ya Nchi. Katika kipindi cha Julai hadi Machi 2020, Hospitali ya Taifa Muhimbili, Hospitali ya Rufaa ya Benjamina Mkapa, MOI na Taasisi ya Moyo ya Jakaya Kikwete zimetoa huduma mbalimbali za kibingwa kwa wagonjwa wa ndani na nje ya Nchi.

137. **Mheshimiwa Spika**, katika kipindi cha Julai 2019 hadi Machi 2020, idadi ya wagonjwa waliopata huduma za kibingwa bobezi katika hospitali hizo ni 1,970. Kati yao, wagonjwa 18 walipata huduma za kupandikiza figo, 330 walipata huduma ya upasuaji wa uti wa mgongo, 730 upasuaji wa ubongo, 507 upasuaji wa moyo kwa kufungua kifua, 610 upasuaji wa moyo kuititia tundu dogo, 101 upasuaji wa mishipa ya damu na watoto 284 walifanyiwa upasuaji wa vichwa vikubwa na mgongo wazi.

138. **Mheshimiwa Spika**, Taasisi ya Saratani ya *Ocean Road* imetoa tiba mionzi kwa wagonjwa 110,979 ikilinganishwa na wagonjwa 52,890 Mwaka 2018. Kati ya wagonjwa hao, 5,788 walipatiwa tiba ya mionzi. Ongezeko la tiba mionzi kwa wagonjwa limetokana na uwepo wa mitambo mipya miwili kwa ajili ya tiba ya saratani (LINAC) ambayo imesaidia kupunguza muda wa wagonjwa kusubiri tiba mionzi kutoka wiki nne Mwaka 2018 hadi wiki mbili Mwaka 2020.

139. **Mheshimiwa Spika**, katika Mwaka 2020/2021, Serikali itaendelea kuimarisha miundombinu ya afya ikiwemo ukarabati na ujenzi wa hospitali, vituo vya afya na zahanati. Vilevile, itaendelea kuimarisha upatikanaji wa dawa, vifaa na vifaa tiba pamoja na kuboresha huduma za kibingwa za afya na ubobezi katika Hospitali ya Taifa, Hospitali Maalum na Hospitali za Rufaa za Kanda ili kuziwezesha kutoa huduma bora zaldi za kibingwa nchini.

Huduma kwa Watu Wenye Ulemavu

140. **Mheshimiwa Spika**, watu wenye ulemavu wanayo haki kwa mujibu wa Katiba ya kutambuliwa utu wao, kuendelezwa, kuheshimiwa na kulindwa dhidi ya vitendo vinavyoshusha utu wao ikiwemo ubaguzi, uonevu, ukatili na mila potofu. Katika Mwaka 2019/2020, Serikali imeendelea kusimamia utekelezaji wa miongozo na mipango mbalimbali inayolenga kuongeza upatikanaji wa haki na ustawi wa Watu Wenye Ulemavu na kuhakikisha huduma zinazotolewa katika ngazi zote kwa ajili ya Watu Wenye Ulemavu na wenye mahitaji maalum zinatolewa kwa haki na usawa.

141. **Mheshimiwa Spika**, katika kukabiliana na changamoto zinazowakabili Watu Wenye Ulemavu hususan kiuchumi, Serikali imezielekeza Halmashauri kutenga asilimia 2 ya mapato yake ya ndani kwa ajili ya kutoa mikopo kwa Watu Wenye Ulemavu. Kupitia mikopo hiyo jumla ya vikundi 160 vya Watu Wenye Ulemavu vimeundwa na vilipatiwa mikopo yenye thamani ya Shilingi bilioni 3.87. Pamoja na hatua tuliyofikia napenda kutoa rai kwa Halmashauri zote nchini kutoa fedha hizi ili ziweze kutatua changamoto za

kiuchumi zinazowakabili Watu Wenye Ulemavu kama ilivyokusudiwa na Serikali.

142. ***Mheshimiwa Spika***, vilevile, Serikali imefanikiwa kuanzisha Mfuko wa Watu Wenye Ulemavu na kufungua akaunti kwa lengo la kuwawezesha kiuchumi ikiwa ni pamoja na kuwajengea uwezo wa kuanzisha miradi mbalimbali ya uzalishaji. Serikali itatumia Mfuko huo kuratibu upatikanaji wa rasilimali fedha kutoka kwa wadau ili kuhakikisha Mfuko huo unakidhi malengo ya uanzishwaji wake.

143. ***Mheshimiwa Spika***, Serikali pia, iliwezesha uendeshaji wa Baraza la Ushauri la Taifa la Watu Wenye Ulemavu ambalo limekuwa likitekeleza majukumu yake kwa mujibu wa Sheria ya Watu wenye Ulemavu Na 9. ya Mwaka 2010. Aidha, wajumbe wa Baraza hilo wamepatiwa mafunzo kuhusu Sera, Sheria, miongozo na mipango inayowahusu Watu Wenye Ulemavu ili waweze kutekeleza majukumu yao kwa ufanisi.

144. ***Mheshimiwa Spika***, katika Mwaka 2019/2020, wahitimu wa vyuo vikuu 167 wenye ulemavu, walipatiwa mafunzo ya kukuza ujuzi kupitia Programu ya Miaka Mitano ya Kukuza Ujuzi. Serikali itaendelea kuwahamasisha wahitimu wenye ulemavu kujandikisha kwenye daftari la wanaotafuta ajira ili kupata fursa ya kuajiriwa pale nafasi zinapotangazwa. Aidha, Serikali imefanya jithada na kufanikiwa kufufua vyuo vitatu vyta mafunzo ya ufundi kwa Watu Wenye Ulemavu. Vyuo hivyo ni Mirongo (Mwanza), Ruwanzari (Tabora) na Masiwani (Tanga).

145. ***Mheshimiwa Spika***, katika kipindi cha Mwaka 2020/2021, Serikali itaendelea kuweka mazingira wezeshi na rafiki kwa Watu Wenye Ulemavu ili kushiriki kikamilifu katika maendeleo ya Taifa. Baadhi ya shughuli zitakazopewa kipaumbele ni pamoja na kukamilisha maandalizi ya Mfuko wa Taifa wa Huduma kwa Watu Wenye Ulemavu, kuratibu maadhimisho ya Siku za Kitaifa na Kimataifa za Watu Wenye Ulemavu na kusimamia utekelezaji wa majukumu ya Baraza la Taifa la Ushauri kwa Watu Wenye Ulemavu. Vilevile, Serikali

itaendeleza vyuo vya mafunzo ya ufundi kwa Watu Wenye Ulemavu.

ULINZI NA USALAMA

146. ***Mheshimiwa Spika***, hali ya amani na usalama ndani ya mipaka ya Tanzania ni shwari. Vyombo vyetu vya ulinzi na usalama vinatekeleza majukumu yake ya kulinda mipaka ya Nchi, kudumisha amani, usalama wa raia na mali zao pamoja na kufundisha wananchi ulinzi wa umma. Serikali imeendelea kuiliimarisha na kuliongezea uwezo Jeshi la Wananchi wa Tanzania kwa kulipatia vifaa na zana bora za kisasa pamoja na kutoa mafunzo na mazoezi stahiki kwa wanajeshi ili kuliwezesha Jeshi kutekeleza majukumu yake ya msingi ya ulinzi wa mipaka ya Nchi yetu.

147. ***Mheshimiwa Spika***, vyombo vyetu vya ulinzi na usalama vimekuwa na mchango mkubwa katika kukabiliana na majanga na matukio yenyе kuleta athari kwa watu na mali zao na kutekeleza shughuli mbalimbali za kiuchumi hususan ujenzi, uendelezaji viwanda na shughuli za kilimo. Nitumie fursa hii kuvipongeza vyombo hivyo hususan Jeshi la Wananchi wa Tanzania na Jeshi la Magereza kwa kushiriki ipasavyo katika ujenzi wa Mji wa Serikali Mtumba, Dodoma.

148. ***Mheshimiwa Spika***, Serikali imeendelea kuimarisha usalama wa raia na mali zao na kutokana na juhudhi hizo, hali ya ulinzi na usalama imeendelea kuimarika na uhalifu kupungua kwa asilimia 2.8 kwa makosa makubwa ya jinai ikilinganishwa na Mwaka 2018/2019. Halikadhalika, ajali za barabarani zimepongua kwa asilimia 25.7 ikilinganishwa na Mwaka 2018/2019.

149. ***Mheshimiwa Spika***, katika kukabiliana na changamoto ya uhamiaji haramu, Serikali ipo katika hatua za mwisho za uwekaji wa mfumo wa kielektroniki wa usimamizi wa mipaka (*e-Border Management System*). Kukamilika kwa mfumo huo kutawezesha utoaji wa huduma bora za uhamiaji, kuimarisha ulinzi na usalama wa mipaka na kuongeza udhibiti katika ukusanyaji wa maduhuli ya Serikali.

150. ***Mheshimiwa Spika***, nitumie fursa hii kuwakumbusha wananchi wote kwamba msingi wa usalama wa raia na mali zao ni jukumu letu sote. Hivyo, ni muhimu wananchi wote tushirikiane na vyombo vyatofauti na usalama kubaini wahalifu pamoja na vitendo vinavyohatarisha usalama wetu kwa kutoa taarifa kwenye vyombo husika.

151. ***Mheshimiwa Spika***, katika Mwaka 2020/2021, Serikali itaendelea kulinda mipaka ya nchi yetu, kuimarisha usalama wa raia na mali zao ili kuhakikisha wananchi wanaishi na kufanya shughuli za maendeleo kwa amani. Vilevile Serikali itaendelea kuboresha mazingira ya kazi na zana za kisasa zinazoendana na teknolojia ya kisasa pamoja na kuendelea kuhamasisha na kuelimisha wananchijuu ya masuala ya ulinzi, uzalendo, usalama na umuhimu wa kushiriki katika ulinzi.

USIMAMIZI WA KAZI NA WAFANYAKAZI

Kazi na Wafanyakazi

152. ***Mheshimiwa Spika***, azma ya Serikali ni kuona wafanyakazi na wananchi kwa ujumla wanafanya kazi za staha na katika mazingira yanayokubalika. Katika kutekeleza azma hiyo, Serikali imeendelea kusimamia viwango vyatofauti na wafanyakazi, afya na usalama mahali pa kazi, na kusimamia Vyama vyatofauti na Waajiri.

153. ***Mheshimiwa Spika***, katika kusimamia viwango vyatofauti na wafanyakazi, Serikali imeendelea kusimamia utekelezaji wa Sheria za Kazi kwa kufanya kaguzi na kutoa elimu kwa wafanyakazi na waajiri. Aidha, mpaka kufikia mwezi Februari, 2020 kaguzi 3,663 zilifanyika katika maeneo mbalimbali ya kazi, ikiwa ni sawa na asilimia 76.3 ya lengo liliopangwa. Kupitia kaguzi hizo, waajiri 36 na raia wa kigeni 82 walifkishwa Mahakamani kwa kukiuka sheria za kazi ambapo, baada ya kupatikana na hatia walitozwa faini ya jumla ya Shilingi milioni 872.

154. ***Mheshimiwa Spika***, sambamba na hilo Serikali imeendelea kusimamia utekelezaji wa Sheria ya Kuratibu Ajira za Wageni Nchini. Hadi kufikia mwezi Februari, 2020 jumla ya

vibali vya kazi 6,625 vilitolewa kwa wageni na maombi 984 ya vibali vya kazi yalikataliwa kutokana na kutokidhi vigezo na masharti yallyowekwa kwa mujibu wa Sheria. Vilevile, katika jitihada za kuongeza ufanisi, Serikali imejenga Mfumo wa Kielektroniki wa Vibali vya Kazi (*On Line Work Permit Application and Information System*) pamoja na kuanza kutoa mafunzo ya matumizi yake kabla ya kuzinduliwa na kuanza kutumika.

Afy na Usalama Mahali pa Kazi

155. ***Mheshimiwa Spika***, katika kusimamia na kudhibiti afya na usalama Mahali pa Kazi, Serikali kupitia Wakala wa Afya na Usalama mahali pa Kazi imeendelea kufanya kaguzi mbalimbali katika maeneo ya kazi. Aidha, kwa Mwaka 2019/2020, jumla ya sehemu za kazi 2,270 zilisajiliwa, kaguzi 8,662 zilifanyika na wafanyakazi 93,575 walipimwa afya.

156. ***Mheshimiwa Spika***, katika Mwaka 2020/2021, Serikali itaendelea kusajili vyama vya wafanyakazi, sehemu mpya za kazi, kufanya kaguzi za kawaida, kaguzi maalum, kupima afya za wafanyakazi na kutoa elimu ya Afya na Usalama kwa Wajasiriamali wadogo na wa kat.

UTUMISHI WA UMMA

157. ***Mheshimiwa Spika***, Serikali imeendelea na jitihada mbalimbali za kuhakikisha utendaji kazi wenye tija kwa kuboresha vitendea kazi, kuongeza na kuwajengea uwezo watumishi. Hadi kufikia mwezi Machi 2020, Serikali imetoe ajira mpya na mbadala 6,975 na kuwapandisha vyeo Watumishi 290,625 wa Kada mbalimbali. Aidha, Serikali imelipa Shilingi bilioni 130.4 kwa Watumishi wa Umma 100,684 waliokuwa wanadai madeni mbalimbali na uhakiki wa Watumishi 36,981 wenye madeni ya Shilingi bilioni 88.389 unaendelea. Uhakiki huo ukikamilika madeni hayo yatalipwa.

158. ***Mheshimiwa Spika***, nitumie fursa hii kuwashukuru wafanyakazi wote kwa mchango wao mkubwa katika kujenga Taifa letu. Napenda kuwahakikishia watumishi wote

kuwa, katika mwaka 2020/2021, Serikali itaendelea kuweka mazingira bora ya kufanya kazi ili Watumishi wa Umma wafanye kazi kwa weledi, juhud, uadilifu na uwajibikaji.

UWEZESHAJI WANANCHI KIUCHUMI

159. ***Mheshimiwa Spika***, Serikali imeendelea kusimamia utekelezaji wa Sera ya Taifa ya Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi ya Mwaka 2004 kwa lengo la kuwakwamua Kiuchumi. Katika kutekeleza azma hiyo, Serikali imefanikiwa kuongeza ushiriki wa Watanzania kwenye miradi ya kielelezo na kimkakati ikiwemo Mradi wa Ujenzi wa Reli ya Kati kwa Kiwango cha Kimataifa na Mradi wa Kufua Umeme wa Maji wa Julius Nyerere ambapo Watanzania 250,000 wameajiriwa katika nafasi mbalimbali zenyenje ujuzi wa juu, kati na chini, ikilinganishwa na wageni 1,338. Idadi hiyo ni sawa na asilimia 99 ya ajira zote kwenye miradi hiyo. Aidha, Shilingi bilioni 170 zililipwa kwa kampuni za kitanzania ambazo zilipata kazi katika miradi ya kielelezo na kimkakati inayotekelizwa nchini.

160. ***Mheshimiwa Spika***, katika Mwaka 2020/2021, Serikali itaendelea kuzitumia Taasisi zake za ndani za masuala ya ujuzi na teknolojia zikiwemo Vyuo vya VETA, Chuo cha Ufund Dar es salaam (DIT), Chuo cha Ubaharia Dar es Salaam (DMI) na vyuo vya ufundi vya Don Bosco katika kuandaa na kufundisha programu zitakazowezesha Watanzania kushiriki katika miradi ya kimkakati, kujiajiri na kuajiriwa katika maeneo mbalimbali.

161. ***Mheshimiwa Spika***, kufuatia utekelezaji wa maelekezo ya Serikali kuwa kila Halmashauri itenye asilimia 10 ya makusanyo yake kwa Wanawake, Vijana na Wenye Ulemavu, Halmashauri zilitenga jumla ya Shilingi bilioni 54.1 na kutoa jumla ya Shilingi bilioni 25.4 kwa Wanawake, Vijana na Wenye Ulemavu. Kati ya fedha hizo; Shilingi 12.9 bilioni zilitolewa kwa wanawake, Shilingi 9.5 bilioni zilitolewa kwa vijana na Shilingi bilioni 2.9 zilitolewa kwa watu wenye ulemavu. Napenda kusitiza Halmashauri zote nchini kuendelea kutenga na kutoa mikopo hiyo kwa walengwa ili waweze kuinua hali zao kiuchumi na kuongeza mchango wao katika kujenga uchumi wa Taifa.

162. ***Mheshimiwa Spika***, katika Mwaka 2019/2020, Serikali imeendelea kusimamia uanzishwaji wa vituo maalum vya uwezeshaji katika mikoa mbalimbali nchini. Lengo ni kuwawezesha wananchi kupata taarifa mbalimbali kuhusu fursa za uwezeshaji, usajili na uendelezaji wa biashara, upatikanaji wa mitaji na mafunzo ya kuongeza thamani ya mazao na bidhaa mbalimbali.

Mfuko wa Taifa wa Maendeleo ya Vijana

163. ***Mheshimiwa Spika***, ili kutumia kundi la vijana kama fursa muhimu kwa maendeleo ya Taifa, Serikali imeendelea na uboreshaji wa Mfuko wa Maendeleo ya Vijana. Katika Mwaka 2019/2020, Mfuko wa Taifa wa Maendeleo ya Vijana umetoa mikopo yenye thamani ya Shilingi bilioni 3.2 ambapo vikundi 586 vyenye jumla ya vijana 4,222 kutoka katika Halmashauri 155 walipata mikopo hiyo.

Mfuko wa Maendeleo ya Jamii (TASAF)

164. ***Mheshimiwa Spika***, mnamo tarehe 17 Februari 2020, Mheshimiwa Dkt. John Pombe Joseph Magufuli, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania alizindua Kipindi cha Pili cha Mpango wa Kunusuru Kaya Maskini katika Awamu ya Tatu ya TASAF utakaoteklezwa Tanzania Bara na Zanzibar. Kuzinduliwa kwa kipindi hiki cha Pili cha Mpango huo, kunadhihirisha nia ya Serikali ya Awamu ya Tano katika kutetea wanyonge na wasiojiweza.

165. ***Mheshimiwa Spika***, Mpango huu umewezesha kaya maskini kuongeza kipato, fursa na uwezo wa kugharamia mahitaji muhimu pamoja na kujenga rasilimali watu. Mathalan, kipindi cha Kwanza cha TASAF Awamu ya Tatu kilihudumia kaya milioni 1.1 zenyе watu milioni 5.2 katika Halmashauri 159 za Tanzania Bara na wilaya zote za Zanzibar.

166. ***Mheshimiwa Spika***, kuititia Mpango huu wa TASAF kaya maskini zimemudu kujunga na Mfuko wa Bima ya Afya ya Jamii pamoja na kujikwamua dhidi ya umaskini. Kwa mfano, asilimia 32 ya kaya zilijiunga na Bima ya Afya ya Jamii

ikilinganishwa na asilimia 11 kabla ya mpango wa TASAF. Aidha, katika kipindi cha Mwaka 2011/2012 hadi 2017/2018 umaskini wa mahitaji ya msingi kwa Tanzania Bara, ulipungua kwa asilimia 1.8 na wa chakula kwa asilimia 1.7. Aidha, takwimu zinaonesha pia kuwa, umaskini uliokithiri umepungua ~~kutoka asilimia 28.2 hadi asilimia 26.1~~ Kunipungua huko

167. ***Mheshimiwa Spika***, katika Mwaka 2020/2021, Serikali itafanya utambuzi na uhakiki wa hali za ustawi wa maisha ya walengwa wa Mpango wa Kunusuru Kaya Maskini katika Halmashauri 101. Lengo ni kubaini kaya ambazo si maskini tena sambamba na kuandikisha kaya mpya 235,647 ambazo hazikufikiwa katika kipindi cha kwanza cha Mpango. Natoa ~~wito kwa woto waliongowa dhamaana ya kutokoloza Mpango~~

Ukuzaji Ujuzi

168. ***Mheshimiwa Spika***, suala la ukuzaji ujuzi wa nguvukazi nchini ni mionganoni mwa ajenda muhimu ya kisera katika kuwezesha wananchi kujikwamua kiuchumi. Serikali imeendelea kuwezesha wananchi wake kuititia Programu ya Kukuza Ujuzi Nchini kwa lengo la kuwapatia ujuzi na stadi za kazi hasa kundi la vijana, wanawake na Watu Wenye ~~Ulimwengu. Ujuzi huo litawawozesha kiumidu lishindani katika~~

169. ***Mheshimiwa Spika***, katika Mwaka 2019/2020, jumla ya vijana 30,099 wamevezeshwa kupata ujuzi kuititia programu hiyo. Katika yao, vijana 5,875 wamepata mafunzo ya uanagenzi katika fani za ufundi stadi katika maeneo mbalimbali. Mafunzo haya yamefanyika katika Mikoa 13 ya Tanzania Bara ambayo ni Arusha, Dar es Salaam, Dodoma, Lindi, Geita, Mara, Kilimanjaro, Iringa, Morogoro, Kagera, Singida, Shinyanga na Ruvuma. Aidha, jumla ya vijana 5,395 wamepewa mafunzo na kurasimishiwa ujuzi walioupata

kupitia mfumo usio rasmi wa mafunzo kupitia VETA katika fani za uachi, usoromalo, ushoni, ufundibomba, ushomlozai na

170. *Mheshimiwa Spika*, katika kuhakikisha wahitimu wa elimu ya juu wanapata uzoefu wa kazi ili kuwawezesha kupata ajira, jumla ya wahitimu 2,115 wamewezeshwa kupata mafunzo ya uzoefu kazini kupitia viwanda na kampuni mbalimbali nchini. Kati yao, wahitimu 100 wa fani ya kilimo wamewezeshwa kwenda nchini Israeli kuhudhuria mafunzo ya uzoefu kazini katika kilimo cha kisasa kwa muda wa mwaka mmoja. Aidha, vijana wengine 3,200 wataanza mafunzo mwanzo hili wa Aprili 2020. Nichukuu fursa hii kuzichukuru taasisi

171. *Mheshimia Spika*, kwa Mwaka 2020/2021, Serikali itaendelea kutoa mafunzo ya ujuzi wa kujiajiri na stadi za kazi kwa vijana katika fani mbalimbali. Aidha, Serikali itaendelea

Ukuzaji wa Fursa za Ajira

172. *Mheshimiwa Spika*, sambamba na ukuzaji ujuzi, Serikali pia imeendelea kuratibu juhudzi za ukuzaji wa fursa za ajira. Katika kipindi cha Julai hadi Februari 2020, jumla ya ajira 1,577,622 zimezalishwa katika sekta mbalimbali ambapo ajira 579,518 zimezalishwa na sekta rasmi na ajira 998,104 zimezalishwa na sekta isyo rasmi. Serikali pia, imeendelea na utoaji wa huduma za ajira ili kuwezesha watafutakazi kumudu ushindani wa soko la ajira. Hadi kufikia tarehe 31 Januari 2020, jumla ya watafutakazi 6,756 wamesajiliwa na Kitengo cha Huduma za Ajira ili kupatiwa huduma mbalimbali za ajira hususan, ushauri nasihi (*vocational guidance and employment counselling*) na mafunzo ya kumudu ushindani

ushauri nasihi pamoja na mafunzo hayo walikuwa 5,266.

NAKALA MTANDAO(ONLINE DOCUMENT)

173. ***Mheshimiwa Spika***, katika Mwaka 2020/2021, Serikali itaendelea kutekeleza mikakati mbalimbali ya ukuzaji wa fursa za ajira. Mikakati hiyo ni pamoja na kuwawezesha vijana wabunifu na makundi mbalimbali ya vijana na wanawake ~~kuimbarisha shughuli za uzalishaji mali na ujasiriamali ili wawazo~~

HIFADHI YA JAMII

Usimamizi na Udhibiti wa Sekta ya Hifadhi ya Jamii

174. ***Mheshimiwa Spika***, katika Mwaka 2019/2020, Serikali imeendelea kutekeleza programu ya maboresho ya Sekta ya Hifadhi ya Jamii kwa kuhakikisha kuwa Kinga ya Jamii inawafikia wananchi walio wengi. Maboresho yaliyofanyika yamelenga kuongeza ufanisi katika sekta ya hifadhi ya jamii. Vilevile, Serikali imeanza kutekeleza kipindi cha Mpito cha ~~mizaka mitano (2019 – 2023) cha kuondoleza kuboresha Sekta~~

Mifuko ya Pensheni

175. ***Mheshimiwa Spika***, Mifuko ya Pensheni ya NSSF na PSSSF imekuwa ikifanya kazi muhimu ya kulipa pensheni pamoja na mafao mengine kwa wastaifu katika sekta za umma na binafsi. Katika kipindi cha Julai hadi Desemba 2019, Mifuko hiyo illipa pensheni, malipo ya mkupuo pamoja na mafao mengino yenye iumla ya Shilingi trilioni 1.4 kwa

176. ***Mheshimiwa Spika***, katika Mwaka 2020/2021, Serikali itaboresha uchakataji wa mafao ili kulipa mafao stahiki na ~~kwa wakati na kuimbarisha ukusanyaji wa michango na~~

MASUALA MTAMBUKA

Vita Dhidi ya Rushwa

177. ***Mheshimiwa Spika***, jitihada za kuinua uchumi na kuungeza huduma za jamii hazitaleta manufaa kwa wananchi na kuondoa umasikini iwapo adui rushwa ataendelea kulitafuna Taifa letu. Rushwa ni adui wa haki, maendeleo na ustawi wa wananchi, pia ni moja ya changamoto kubwa inayoikabili Nchi yetu na dunia kwa ujumla.

178. ***Mheshimiwa Spika***, kwa kutambua hilo, Serikali ya Awamu ya Tano inatekeleza mikakati mbalimbali ya kupambana na rushwa ambayo imeweza kupunguza vitendo vya rushwa kwa kiasi kikubwa nchini. Mikakati hiyo ni pamoja na Mkakati wa Taifa Dhidi ya Rushwa na Mpango wa Utekelezaji Awamu ya Tatu wa Mwaka 2017 - 2022. Hii inadhihirishwa na matokeo ya tafiti zilizofanywa Mwaka 2019 na Taasisi za Kitaifa na Kimataifa na kuonesha kuwa Tanzania inafanya vizuri katika kudhibiti vitendo vya rushwa na ujisadi. Aidha, kiashiria cha *Corruption Perception Index (CPI)* cha taasisi ya *Transparency International* kimeonesha Tanzania imefikia kiwango cha asilimia 37 na kushika nafasi ya 96 katika nchi 180 ikilinganishwa na kiwango cha asilimia 30 katika nafasi ya 119 Mwaka 2015.

179. ***Mheshimiwa Spika***, katika Mwaka 2019/2020, Serikali imeokoa kiasi cha Shilingi bilioni 47.3 zikiwa ni thamani ya mali na fedha taslimu zilizotokana na operesheni mbalimbali za kiuchunguzi zilizofanyika nchini. Serikali pia, ilifanya ufuatilaji katika miradi 244 ya maendeleo iliyo husisha sekta za Afya, Elimu, Maji, Ujenzi na Nishati yenyeye thamani ya Shilingi trillioni 9.86 ili kuhakikisha inatekelezwa kulingana na thamani halisi ya fedha.

180. ***Mheshimiwa Spika***, katika Mwaka 2020/2021, Serikali itaendelea kuimarisha mifumo mbalimbali kwenye Sekta za Umma katika ngazi zote nchini ili kubaini na kupendekeza

njia madhubuti za kuziba mianya ya rushwa na kuboresha utoaji wa huduma kwa wananchi. Aidha, Serikali itaendelea kufuatilia miradi ya maendeleo ili kuhakikisha inatekelezwa kulingana na thamani ya fedha zilizotolewa kwa ajili hiyo.

Mapambano Dhidi ya UKIMWI

181. ***Mheshimiwa Spika***, Serikali kwa kushirikiana na wadau inaendelea kutekeleza Mpango Mkakati wa Nne wa Taifa wa Kudhibiti UKIMWI wa Mwaka 2018/2019 - 2022/2023 ambao unalenga kutekeleza malengo ya dunia yenye mwelekeo wa kupambana na UKIMWI ili kufikia TISINI TATU (90:90:90). Katika kutekeleza malengo hayo, lengo la 90 ya kwanza ni kuhakikisha asilimia 90 ya watu wanapima na kujua hali zao ambapo hadi Desemba 2019 wenye VVU na waliopima na kujua hali zao ilikuwa asilimia 80.1 ikilinganishwa na asilimia 75 kwa Mwaka 2018. Lengo la 90 ya pili ni kuhakikisha asilimia 90 ya waliokutwa na VVU wanaanzishiwa dawa za kufubaza VVU ambapo walioanza dawa za ARV na kubaki katika dawa ni asilimia 98.8 ikilinganishwa na asilimia 98 kwa Mwaka 2018. Lengo la 90 ya tatu ni kuhakikisha asilimia 90 ya wanaoanzishiwa dawa za ARV kinga zao za mwili zinaimarika ambapo lengo hili limefikiwa kwa asilimia 92 ikilinganishwa na asilimia 88 kwa Mwaka 2018.

182. ***Mheshimiwa Spika***, kutokana na juhudzi za dhati zilizofanywa na Serikali, hali ya maambukizi ya UKIMWI inaonesha kuna Watanzania takribani milioni 1.6 wanaoishi na VVU ambapo kiwango cha maambukizi kimeshuka kutoka asilimia 7 ya Mwaka 2014 hadi kufikia asilimia 4.7 kwa Mwaka 2020.

183. ***Mheshimiwa Spika***, mafanikio hayo yamechangiwa na jitihada mbalimbali za Serikali ikiwa ni pamoa na kupitia miongozo na Sheria mbalimbali ambapo umri wa vijana kupima VVU bila ya kuambatana na wazazi au walezi wao umeshushwa kutoka miaka 18 hadi 15. Aidha, dawa mpya ya ARV yenye ufanisi (*Dolutegravir*) imeruhusisha kuingizwa na kutumika nchini ambapo hadi Desemba 2019 asilimia 53 ya watu wanaoishi na virusi vyta UKIMWI (WAVIU) wameanza

kutumia dawa hiyo. Serikali pia imeridhia mfumo wa watu kujipima wenyewe.

184. ***Mheshimiwa Spika***, katika Mwaka 2020/2021, Serikali itaendelea kufanya jitihada za kupunguza kasi ya maambukizi katika jamii kwa kuhamasisha upatikanaji wa rasilimali muhimu kwa ajili ya mapambano dhidi ya UKIMWI; kupunguza kiwango cha maambukizi ya VVU kutoka kwa mama kwenda kwa mtoto na kuimarisha huduma za elimu ya UKIMWI.

Mapambano Dhidi ya Dawa za Kulevya

185. ***Mheshimiwa Spika***, Tanzania imeendelea kuwa mfano wa kuigwa kimataifa katika kudhibiti na kupambana na dawa za kulevya. Nchi yetu imefanikiwa kwa ufanisi mkubwa kudhibiti uzalishaji, uuzaaji, usambazaji na matumizi ya dawa za kulevya. Mafanikio hayo, yamewezesha waathirika wengi hasa vijana kubadilika na kujihusisha katika shughuli za uzalishaji mali pamoja na kuipatia sifa Tanzania kutoka kwa Jumuiya ya Kimataifa.

186. ***Mheshimiwa Spika***, katika kikao cha 63 cha Kamisheni ya Shirika la Umoja wa Mataifa linaloshughulikia Dawa za Kulevya na Uhalifu kilichofanyika Machi 2020, Tanzania ilipongezwa kwa kufanikiwa kwa kiasi kikubwa katika kutekeleza miongozo ya Umoja wa Mataifa ya kudhibiti na kupambana na dawa za kulevya.

187. ***Mheshimiwa Spika***, katika kipindi cha Julai 2019 hadi Januari 2020 Serikali ilifanikiwa kukamata watuhumiwa wa dawa za kulevya 6,350. Katika kipindi hicho, kilogramu 34.986 za heroine na kilogramu 1.556 za cocaine zilikamatwa. Kadhalika, tani 10.559 za bangi, tani 6.016 za mirungi na mashamba ya bangi 9 yenye jumla ya ekari 4.25 yaliteketezwa.

188. ***Mheshimiwa Spika***, pamoja na kukamata watuhumiwa na madawa ya kulevya, Serikali imeendelea kutoa elimu kwa umma kuhusu athari za matumizi ya dawa za kulevya kuititia vyombo vya habari na mitandao ya kijamii. Elimu kuhusu dawa za kulevya na UKIMWI pia imetolewa kwa

wasanii 600 pamoja na makundi maalum ikiwemo Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Masuala ya UKIMWI pamoja na viongozi wa mbio za Mwenge. Elimu hiyo, imesaidia kujenga uelewa wa pamoja juu ya athari na namna ya kupambana na kudhibiti dawa za kulevya nchini.

189. ***Mheshimiwa Spika***, katika hatua nyingine, Serikali imefanya ukaguzi wa kampuni 58 zinazojihusisha na biashara ya kemikali bashirifu na usafirishaji wa vifurushi. Kupitia ukaguzi huo, imegundulika kuwa baadhi ya kampuni hizo hutumia majina bandia katika kuingiza kemikali bashirifu na kusafirisha vifurushi vyta dawa za kulevya. Katika kukabiliana na tatizo hilo, Serikali imefanikiwa kukamata watuhumiwa 7 na zaidi ya kilo 890 za dawa za kulevya aina ya mirungi katika Ofisi za Posta zilizokuwa na majina bandia kama vile mlonge na majani ya chai zikisafirishwa kwenda nchi za Ulaya, Marekani na Canada.

190. ***Mheshimiwa Spika***, katika kukabiliana na hali hiyo, Serikali imeimarisha ukaguzi katika kampuni zinazosafirisha vifurushi kwenda nje ya nchi zikiwemo Ofisi za Posta. Aidha, katika kuboresha shughuli za ukaguzi wa kemikali bashirifu na dawa tiba zenye asili ya kulevya, Serikali imeandaa miongozo ya ukaguzi na uchukuaji sampuli itakayosaidia kufanya ukaguzi wenye ufanisi kubaini usafirishaji dawa za kulevya, kemikali bashirifu na dawa tiba zenye asili ya kulevya.

191. ***Mheshimiwa Spika***, kwa upande wa tiba dhidi ya waathirika wa dawa za kulevya, Serikali inapanua wigo wa utoaji huduma za tiba kwa kujenga na kuanzisha vituo vyta utoaji wa huduma ya *methadone* katika Mikoa ya Tanga na Pwani. Hadi sasa, zaidi ya watumiaji 8,200 wanapata huduma za tiba ya *methadone* kila siku katika vituo vilivyopo katika mikoa ya Dar es Salaam, Mwanza, Mbeya, Tanga na Pwani.

192. ***Mheshimiwa Spika***, katika Mwaka 2020/2021, Serikali itaendelea kudhibiti uingizaji, usafirishaji na matumizi ya dawa za kulevya kwa kutoa elimu kwa umma juu ya madhara ya matumizi na biashara ya dawa za kulevya na kuongeza huduma za tiba kwa waathirika wa dawa za kulevya.

Uratibu wa Maafa

193. ***Mheshimiwa Spika***, katika kipindi cha Mwaka 2019/2020, Nchi yetu imekumbwa na maafa mbalimbali ikiwemo mafuriko, maporomoko ya ardhi na majanga ya moto. Wananchi wa Bonde la Mto Rufiji wamepata athari ya mafuriko ambako serikali kupitia Mkoa na Wilaya, pia Ofisi ya Waziri Mkuu inashirikiana na Viongozi wa Wilaya kutoa huduma kadiri tathmini inavyoendelea. Maeneo mengi nchini yameendelea kupata mafuriko na kuathiri shughuli za wananchi. Kufuatia hali hiyo, Serikali imechukua hatua mbalimbali katika kukabili na kurejesha hali ikiwa ni pamoja na kujenga miundombinu ya barabara, umeme, reli na majengo ya umma yaliyoathirika na kutoa misaada ya kibinadamu kwa waathirika.

194. ***Mheshimiwa Spika***, Serikali pia imeendelea kutoa elimu kwa umma pamoja na kuzijengea uwezo Kamati za Usimamizi wa Maafa katika ngazi zote. Lengo ni kuongeza uelewa na kuimarisha ustahimilivu dhidi ya majanga kwa kupunguza vihatarishi na vyanzo vinavyoweza kusababisha maafa. Aidha, kutokana na mvua nyingi zinazoendelea kunyesha nchini, naelekeza wakuu wote wa Mikoa na Wilaya kuhakikisha wananchi walioweka makazi katika maeneo hatarishi ikiwemo kandokando ya mito na mabonde wanahama mara moja katika maeneo hayo ili kupunguza madhara yanayoendelea kujitokeza katika jamii.

195. ***Mheshimiwa Spika***, katika Mwaka 2020/2021, Serikali itaendelea kuimarisha mifumo ya utoaji wa taarifa za tahadhari za awali na kuzingatia Wasifu wa Janga la Mafuriko na Ukame nchini. Wasifu huo, unajumuisha taarifa za ramani ya maeneo hatarishi, rasilimali, miundombinu muhimu katika maeneo hayo, hatari ya kudhurika na makadirio ya hasara za kiuchumi kutokana na madhara ya mafuriko na ukame.

Mazingira

196. ***Mheshimiwa Spika***, Serikali imeendelea kuchukua hatua mbalimbali kukabiliana na uharibifu wa mazingira

ikiwemo kuhamasisha upandaji miti, usafi na utunzaji wa mazingira sambamba na kuanza mradi wa usambazaji gesi majumbani na kupiga marufuku matumizi ya mifuko ya plastiki.

197. ***Mheshimiwa Spika***, katika Mwaka 2019/2020, Serikali imeendelea kutekeleza mradi wa usambazaji wa gesi majumbani, viwandani na katika magari. Hadi kufikia Desemba 2019, Serikali imekamilisha ujenzi wa miundombinu ya usambazaji gesi asilia na kuunganisha nyumba 125 na Taasisi 4 mkoani Mtwara. Aidha, viwanda 48 vimeunganishwa na gesi asilia ikiwemo viwanda vya Coca Cola, Tanzania Breweries Ltd, Kiwanda cha Cement cha Wazo Hill vilivvopo Dar es Salaam na kiwanda cha Saruji cha Dangote kilichopo Mtwara. Halikadhalika, ujenzi wa miundombinu ya kuunganisha nyumba 185 na Taasisi 4 jijini Dar es Salaam nao umekamilika.

198. ***Mheshimiwa Spika***, Serikali pia imefanikiwa kusimamia utekelezaji wa katazo la matumizi ya mifuko ya plastiki hapa nchini. Katika Mwaka 2019/2020, tani 259.2 za mifuko ya plastiki zilikusanywa nchi nzima. Kati ya hizo, tani 171.5 zilitketezwa na tani 86.7 zilirejelezwa katika viwanda mbalimbali hapa nchini. Aidha, Serikali imeendelea kusimamia ubora na matumizi ya mifuko mbadala.

199. ***Mheshimiwa Spika***, katazo la mifuko ya plastiki limetoa fursa za kuzalisha mifuko mbadala ambapo wadau wengi wamejitezea kuwekeza katika sekta hiyo. Kwa mfano, hadi sasa idadi ya viwanda vipyta vinavyozalisha mifuko mbadala vimefikia 7. Kati ya hivyo viwanda 6 vipo Dar es Salaam na kimoja kipo Arusha.

200. ***Mheshimiwa Spika***, nitumie fursa hii kuziagiza Halmashauri zote nchini kuendelea kutunza mazingira ili kukabiliana na uharibifu wa mazingira unaotokana na shughuli mbalimbali za kibinadamu na mabadiliko ya tabianchi.

201. **Mheshimiwa Spika**, katika Mwaka 2020/2021, pamoja na mambo mengine, Serikali itaendelea na zoezi la kuunganisha viwanda na nyumba nyingi zaidi kwenye mtandao wa matumizi ya gesi asilia katika Mikoa ya Dar es Salaam na Mtwara. Vilevile, Serikali itaimarisha juhudzi za kuhifadhi na kulinda mazingira kwa kutekeleza miradi mbalimbali.

MUUNGANO

202. **Mheshimiwa Spika**, Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania imeendelea kushirikiana vyema na Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar katika kuuendeleza na kuudumisha Muungano wetu. Katika Mwaka 2019/2020, vikao mbalimbali vya Wataalam na Makatibu Wakuu vilifanyika na kujadili masuala ya uvuvi kwenye ukanda wa bahari kuu, na hoja za fedha na biashara baina ya Zanzibar na Tanzania Bara. Aidha, maandalizi ya vikao vya pamoja vya Mawaziri wa SMT na SMZ yamefanyika ikiwemo na kuundwa kwa kamati ya kitaifa inayoratibu ugonjwa wa Corona.

203. **Mheshimiwa Spika**, nitumie fursa hii kuwapongeza Mheshimiwa Dkt. John Pombe Joseph Magufuli, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Mheshimiwa Dkt. Ali Mohamed Shein, Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi kwa kuendelea kuenzi dhamira ya Waasisi wa Muungano.

204. **Mheshimiwa Spika**, ndugu zetu Wachina wanao msemo maarufu usemao, "*When we drink water from the well, we should not forget those who dug it.*" Msemo huu humaanisha kuwa, tunapokunywa maji kutoka kwenye kisima basi tuisahau fadhila za waliochimba kisima hicho. Hivyo basi, nasi hatuna budi kuendelea kuenzi na kuheshimu juhudzi za Waasisi wa Muungano wetu Hayati Baba wa Taifa, Mwalimu Julius Kambarage Nyerere na Hayati Mzee Abeid Amani Karume kwa kutuachia alama ya Muungano ambao umekuwa funzo kwa mataifa mengine. Kwa msingi huo, Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania itaendelea kushirikiana na Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar katika

kutekeleza wajibu wake wa kikatiba na kisheria wa kuuenzi na kuulinda Muungano wetu sambamba na kudumisha amani na utulivu katika pande zote mbili za Muungano.

205. ***Mheshimiwa Spika***, nitumie fursa hii pia kuwashukuru wananchi wote wa Unguja na Pemba ambao sio tu walnipokea vizuri, lakini pia walnipatia ushirikiano mkubwa wakati wa ziara yangu ya kikazi mwezi Januari 2020 kwa ajili ya kukagua utekelezaji wa Ilani ya Uchaguzi ya Chama Cha Mapinduzi ya mwaka 2015 hadi 2020 kwa upande wa Zanzibar.

206. ***Mheshimiwa Spika***, katika Mwaka 2020/2021, Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania itaendelea kushirikiana na Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kwa kuimarisha ziara na ushiriki wa viongozi wakuu katika matukio muhimu ya kitaifa sambamba na kufanya mikutano ya mashauriano ya viongozi na watendaji kwa lengo la kuimarisha Muungano wetu.

UHUSIANO WA KIMATAIFA

207. ***Mheshimiwa Spika***, Tanzania imeendelea kuwa na ushawishi mkubwa katika kutekeleza majukumu yake mbalimbali ya kidiplomasia kwa mujibu wa Katiba ya Nchi, Sheria, Kanuni na Taratibu zilizopo. Aidha, mahusiano kati ya Tanzania na Jumuiya ya Kimataifa yameendelea kuimarika.

208. ***Mheshimiwa Spika***, kuimarika kwa mahusiano na ushawishi wetu kwa Jumuiya ya Kimataifa kumewezesha Tanzania kuanzisha Balozi mpya 2 katika nchi rafiki katika Mwaka 2019/2020. Balozi hizo ni Windhoek – Namibia na Havana – Cuba. Sanjari na hilo, Tanzania imeendelea kuridhia na kutekeleza Itifaki na Mikataba mbalimbali ya Kikanda na Kimataifa.

209. ***Mheshimiwa Spika***, katika Mwaka 2020/2021, Tanzania itaendelea kuridhia na kutekeleza mikataba mbalimbali ya kimataifa na kikanda sambamba na kuheshimu misingi ya mahusiano na mataifa engine duniani. Aidha, kupitia

ushirikiano mzuri uliopo na ushawishi wetu kwenye jumuiya za kikanda na kimataifa, Tanzania italinda uhuru wa kujamulia mambo yake yenewe, na kujenga umoja na mtangamano wa kikanda wa Bara la Afrika. Halikadhalika, Tanzania itashiriki kikamilifu katika kuendeleza siasa ya kutofungamana na upande wowote kama dira na msimamo wetu katika mahusiano baina yetu na Nchi nyingine katika Jumuiya ya Kimataifa.

210. ***Mheshimiwa Spika***, kwa upande mwingine Serikali itaendelea kuweka mkazo katika kukuza ushirikiano kwenye nyanja za biashara, uwekezaji, masoko ya bidhaa zetu, utalii na lugha ya Kiswahili ili kuchochea maendeleo ya Nchi.

HABARI, UTAMADUNI NA MICHEZO

211. ***Mheshimiwa Spika***, katika Mwaka 2019/2020 Serikali imeendelea kutekeleza mikakati ya kuimarisha upatikanaji wa habari, kurasimisha kazi za kitamaduni, sanaa na ubunifu na kuhakikisha watendaji wa kazi hizo wanapata maslahi yanayoendana na kazi zao. Aidha, Serikali imeendelea kuhakikisha kwamba lugha ya Kiswahili inaendelezwa ndani na nje ya Nchi na kutumika kama bidhaa ya soko na chanzo cha ajira kwa wataalam wa lugha yetu ya Kiswahili.

212. ***Mheshimiwa Spika***, Mkutano wa 39 wa Wakuu wa Nchi na Serikali wa Nchi za Jumuiya ya Maendeleo Kusini mwa Afrika (SADC) uliofanyika Tanzania tarehe 17 na 18 Agosti, 2019 jijini Dar es Salaam ulipitisha lugha adhimu ya Kiswahili kuwa moja ya lugha rasmi za Jumuiya hiyo. Serikali imeandaa Miongozo ya Ufundishaji Kiswahili kwa Wageni na kubainisha mahitaji ya uandaaji wa Mitaala ya kufundishia Kiswahili katika Nchi za kigeni. Aidha, kupitia kanzidata ya usajili wa Wataalam wa Kiswahili iliyopo Baraza la Kiswahili Tanzania (BAKITA), jumla ya wataalam 1,159 wamesajiliwa hadi mwezi Machi, 2020.

213. ***Mheshimiwa Spika***, nitumie fursa hii kulipongeza Shirika la Utangazaji la Taifa (TBC) kufuatia maboresho muhimu kwenye mfumo wa urushaji matangazo. Tarehe 30 Machi,

2020 TBC iliweka jiwe la msingi wa ujenzi wa jengo la studio na kuzindua programu tumizi na tovuti ya Safari Channel. Maboresho hayo yataimarisha mfumo mzima wa urushaji matangazo hususan taarifa ya habari (Aridhio).

214. ***Mheshimiwa Spika***, katika Mwaka 2020/2021, Serikali itaendelea kusimamia utekelezaji wa Sheria ya Huduma za Habari Na. 12 ya Mwaka 2016 na kuratibu na kusimamia maendeleo ya michezo nchini ikiwemo ushiriki wa timu za Taifa katika mashindano mbalimbali ya Kimataifa.

HITIMISHO

215. ***Mheshimiwa Spika***, kama nilivyo tangulia kueleza, katika kipindi cha takriban miaka mitano tangu Serikali ya Awamu ya Tano chini ya uongozi mahiri wa Mheshimiwa Dkt. John Pombe Joseph Magufuli, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania iingie madarakani tumeshuhudia mafanikio makubwa ya kiuchumi na kijamii.

216. ***Mheshimiwa Spika***, mafanikio hayo ni ishara tosha kwa Watanzania kwamba ahadi za Chama Cha Mapinduzi ndani ya kipindi cha miaka mitano (2015 hadi 2020) zinatekelezwa vyema na kwa mafanikio makubwa. Hivyo basi, katika Mwaka 2020/2021, Serikali pamoja na mambo mengine, itaweka mkazo katika masuala yafuatayo:

Mosi: Kuimarisha na kudumisha amani, utulivu, mshikamano na umoja wa kitaifa uliopo ili kuleta maendeleo endelevu hususan tunapoelekea kwenye Uchaguzi Mkuu mwezi Oktoba 2020;

Pili: Kulinda uhuru wa kujiamulia mambo yetu wenyewe bila kuingiliwa; mipaka ya Nchi; haki; kuimarisha ujirani mwema na kuunga mkono Sera ya Kutofungamana na Upande wowote kama dira na msimamo wetu katika mahusiano na Nchi nyingine katika Jumuiya ya Kimataifa;

Tatu: Kudhibiti upotevu wa mapato kwa kuimarisha matumizi ya mifumo ya kielektroniki ya ukusanyaji wa mapato na utoaji huduma hususan kwenye Mamlaka za Serikali za Mitaa kwa

lengo la kuondoa urasimu usio wa lazima pamoja na kuwahudumia wananchi wote kwa tija tena bila ubaguzi wa aina yoyote;

Nne: Kuendelea kuboresha zaidi mazingira ya biashara na uwekezaji;

Tano: Kuhimiza uwajibikaji wa watendaji wa Serikali katika ufuatiliaji wa miradi ya kielelezo hususan ujenzi wa miundombinu muhimu ya usafiri na usafirishaji, ikiwemo reli, bandari, ujenzi wa meli, vivuko, viwanja vya ndege, barabara na madaraja;

Sita: Kuwatumikia Watanzania wote kwa kuondoa kero mbalimbali zinazowakabili katika maeneo yao sambamba na kuimarisha upatikanaji wa huduma za jamii kwa kukamilisha na kuendelea na ujenzi wa miradi ya miundombinu ya maji, afya na elimu;

Saba: Kuimarisha uzalishaji na usambazaji wa nishati ya uhakika kwa kukamilisha Ujenzi wa Bwawa la Kufua Umeme wa MW 2,115 la Julius Nyerere na kuhakikisha vijiji vilivyobaki katika utekelezaji wa mradi wa REA III vinapatiwa umeme;

Nane: Kuongeza kasi ya upimaji wa ardhi, mashamba na maeneo ya makazi, uwekezaji na ujenzi wa viwanda ili kuongeza kasi ya ukuaji wa uchumi na kutengeneza ajira zaidi kwa watanzania;

Tisa: Kusimamia kikamilifu matumizi sahihi na yenye tija ya rasilimali zilizopo ili zitumike kwenye maeneo yanayochochea ukuaji uchumi na utoaji huduma bora kwa wananchi; na

Kumi: Kuhimiza Watanzania kufuata maelekezo ya Serikali kuhusu kujikinga, kudhibiti na kutosambaza virusi vya Corona ili kupunguza athari za kijamii na kiuchumi zinazoweza kujitokeza kutokana na maambukizi hayo. Serikali kwa upande wake inashirikiana kwa karibu na Jumuiya ya Kimataifa katika kukabiliana na kutokomeza maambukizi ya virusi hivyo vya Corona.

217. ***Mheshimiwa Spika***, natoa wito kwa kila mwananchi kuendelea kuunga mkono jitihada kubwa zinazofanywa na Serikali ya Chama Cha Mapinduzi chini ya uongozi mahiri na thabiti wa Mheshimiwa Dkt. John Pombe Joseph Magufuli, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, kwa kufanya kazi kwa bidii, weledi, uadilifu, tija na ufanisi, uaminifu na kupiga vita rushwa.

MAKADIRIO YA MAPATO NA MATUMIZI YA FEDHA ZA OFISI YA WAZIRI MKUU NA OFISI YA BUNGE KWA MWAKA 2020/2021

218. ***Mheshimiwa Spika***, kwa Mwaka 2020/2021, Ofisi ya Waziri Mkuu na Taasisi zilizo chini yake inaliomba Bunge lako Tukufu liidhinishe jumla ya **Shilingi bilioni mia tatu kumi na mbili, milioni mia nane na mbili na mia tano ishirini elfu (312,802,520,000)**; kati ya fedha hizo, **Shilingi bilioni themanini na nane, milioni mia nne ishirini na tisa na mia moja hamsini na sita elfu (88,429,156,000)** ni kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida na **Shilingi bilioni mia mbili ishirini na nne, milioni mia tatu sabini na tatu na mia tatu sitini na nne elfu (224,373,364,000)** ni kwa ajili ya Matumizi ya Maendeleo.

219. ***Mheshimiwa Spika***, Vilevile naliomba Bunge lako Tukufu liidhinishe jumla ya **Shilingi bilioni mia moja ishirini na moja, milioni mia saba themanini na sita na mia mbili hamsini na saba elfu (121,786,257,000)** kwa ajili ya Mfuko wa Bunge. Kati ya fedha hizo, **Shilingi bilioni mia moja kumi na tatu, milioni mia tano sitini na saba na mia sita arobaini na saba elfu (113,567,647,000)** ni kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida na **Shilingi bilioni nane, milioni mia mbili kumi na nane na mia sita na kumi elfu (8,218,610,000)** ni kwa ajili ya Matumizi ya ~~Maendeleo~~.

SPIKA: Mheshimiwa Waziri Mkuu, ahsante sana, hoja imetolewa na imeungwa mkono. Tunakushukuru sana, ~~ahsante sana~~ Mheshimiwa Waziri Mkuu kwa hatiha vako nzuri

mkubwa. (*Makof!*)

Waheshimiwa Wabunge wamekusikiliza kwa umakini na tutakuwa na muda sasa kama wa siku nne (4) kujadili hoja hii. Wale wote ambao wamejijandikisha natumaini watapata nafasi ya kuweza kujipanga na kuweza kujadili, tunaamini makabrasha husika yote muhimu tayari Waheshimiwa Wabunge mnayo kupitia *tablets* zenu na hotuba hii pia imo katika *tablets* zenu na pia kwa watanzania wote itakuwa inapatikana pamoja na tovuti za Serikali lakini katika tovuti ya Bunge ni hotuba ya Moshimiwa Waziri Mkului itakuwa

Kabla hatujaendelea, ngoja kwanza nikumbushe Waheshimiwa Wabunge na vilevile nirekebishe mambo hapa kidogo na *Sanitizer* hapa (*Kicheko*)

Nawakumbusha Waheshimiwa Wabunge katika mabegi yenu ni vizuri kubeba hivi vitu na kila baada ya dakika 15, 20, naona wengine wanazo aaaah! Afadhalii kabisa! Wanaume wenzangu hawajabeba, hii kitu haina cha nani wala nani. (*Kicheko*)

Kwa hiyo pamoja na kwamba tumeweka kwenye maeneo mbalimbali ya Bunge ni vizuri kuwa na hivi vitu isipite nusu saa bila kukumbuka kumbuka kidogo. (*Kicheko*)

Nawashukuruni sana Waheshimiwa Wabunge aaah! Afadhalii bwana, ahsante sana. Inaonesha Waheshimiwa Wabunge mnajali. (*Kicheko*)

Asanteni sana, kwa hiyo *Sanitizer* ni muhimu Watani zangu Wasukuma wanasesma sahani tisa, ni muhimu sana, ahsante sana. (*Kicheko*)

Basi sasa nimkaribishe Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Katiba na Sheria palepale ulipo uisome hotuba yako ila ongeza sauti tu halafu uzingatie dakika ishirini, ishirini kamili saa hizi angalia saa yako hapo twenty minutes umalize, karibu.

MHE. MOHAMED O. MCHENGERWA – MWENYEKITI WA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA KATIBA NA SHERIA: Awali ya yote nianze kwanza kumshukuru sana Mwenyezi Mungu mwiningi wa rehema aliyetuwezesha hewa ya kupumua, afya njema na akili timamu na kutufanikisha kuweza kukutana mbele ya Bunge lako hili Tukufu.

Mheshimiwa Spika, kwa mujibu wa Kanuni ya 99(9) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Januari 2016, naomba kuwasilisha Taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Katiba na Sheria kuhusu Utekelezaji wa Bajeti ya Ofisi ya Waziri Mkuu Bunge, Kazi, Ajira, Vijana na Wenye Ulemavu na Uwekezaji kwa Mwaka wa Fedha 2019/2020, pamoja na maoni ya Kamati kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi kwa Mafungu sita (6) yaliyo chini ya Ofisi hiyo kwa Mwaka wa Fedha 2020/2021.

Mheshimiwa Spika, Taarifa ya Utekelezaji wa Miradi ya Maendeleo iliyotengewa fedha kwa mwaka wa fedha kwa mwaka wa fedha 2019/2020. Katika kutekeleza Kanuni ya 98(1) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Kamati ya Katiba na Sheria ilipokea Taarifa ya Utekelezaji wa Mradi Na. 6581 wa Programu ya Kukuza Ujuzi nchini, ambao kwa mwaka wa fedha 2019/2020 ilitengewa kiasi cha shilingi 18,000,000,000. Kamati imeridhishwa na upatikanaji wa Fedha za kutekeleza mradi huo, kwani kwa kipindi cha Julai, 2019 hadi Februari, 2020 Ofisi ya Waziri Mkuu imepokea kiasi cha shilingi 12,000,000,000 sawa na asilimia 66.7 ya bajeti ya Mradi huo iliyoidhinishwa na Bunge kwa mwaka wa fedha 2019/2020.

Mheshimiwa Spika, Uchambuzi wa Taarifa ya Ofisi ya Waziri Mkuu kuhusu Utekelezaji wa Mpango wa Bajeti na Uzingatiaji wa Maoni ya Kamati kwa Mwaka wa Fedha 2019/2020. Uchambuzi wa Taarifa Kuhusu Ukusanyaji wa Maduhuli kwa Mwaka wa Fedha 2019/2020.

Mheshimiwa Spika, katika Mwaka wa Fedha 2019/2020 Bunge lako Tukufu liliidhinisha Makadirio ya Makusanyo ya Maduhuli yenye jumla ya shilingi 40,913,154,200.00 katika kipindi cha Julai, 2019 hadi Februari, 2020. Kiasi cha Maduhuli

kilichokusanya na Ofisi ya Waziri Mkuu na Taasisi zote zilizo chini yake ni shilingi 27,343,993,388.00. Kamati, inaipongeza Ofisi ya Waziri Mkuu kuwa mfano bora na wa kuigwa na Wizara pamoja na Taasisi zote za Serikali katika kuongeza ubunifu wa vyanzo vya mapato ya Serikali, hatua hiyo ambayo itasaidia kupunguza utegemezi kutoka nje ya nchi. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, Upatikanaji wa fedha za Matumizi ya Kawaida kutoka Hazina, Ofisi ya Waziri Mkuu pamoja na taasisi zake, katika mwaka wa fedha 2019/2020 ilitengewa shilingi 73,021,442,000.00 kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida. Kati ya fedha hizo 18,881,495,999.00 ziliikuwa ni mishahara, na 26,300,646,053.00 ziliikuwa ni Matumizi Mengineyo. Shilingi 27,839,299,948.00 ziliikuwa za Ruzuku kwa Taasisi na Vyama vya Siasa.

Mheshimiwa Spika, Katika kipindi cha Julai, 2019 hadi Februari, 2020, Mafungu hayo yalipokea jumla ya shilingi 46,858,108,638.6 sawa na asilimia 64.2 ya bajeti. Uchambuzi wa uwiano wa Bajeti iliyoidhinishwa na upatikanaji wa fedha ya Matumizi ya Kawaida hadi kufikia Februari 2020 umeainishwa katika Jedwali Namba 1 kama inavyoonekana kwenye taarifa hii. (*Makofii*)

SPIKA: Waheshimiwa alikuwa anaweka *Sanitizer* kidogo. (*Kicheko*)

MHE. MOHAMED O. MCHENGERWA – MWENYEKITI WA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA KATIBA NA SHERIA: Mheshimiwa Spika, uchambuzi huu unaonyesha kuwa kumekuwa na mwenendo mzuri kuhusu upatikanaji wa fedha kwa kila Fungu. Maoni ya Kamati ni kwamba hali ya upatikanaji wa fedha kwa wakati inatakiwa kuendelea na kuzingatiwa na Serikali kwa mwaka wa fedha 2020/2021, ili kurahisisha usimamizi na utekelezaji wa shughuli mbalimbali za Serikali kwa wakati na kwa ufanisi.

Mheshimiwa Spika, Uchambuzi wa Utekelezaji wa Bajeti ya Maendeleo kwa Mwaka wa Fedha 2019/2020. Katika

mwaka wa fedha 2019/2020 Ofisi ya Waziri Mkuu, ilitengewa jumla ya shilingi 56,637,565,737.00 kwa ajili ya Miradi Maendeleo. Katì ya fedha hizo shilingi 19,000,000,000.00 zilikuwa ni fedha za ndani na shilingi 37,639,033,834.00 zilikuwa ni fedha za nje. Hadi Februari, 2020, jumla ya shilingi 176, 449,818,037.00 zilikuwa zimepokelewa, ambazo ni sawa na asilimia 311.5 ya bajeti iliyoidhinishwa.

Mheshimiwa Spika, Uchambuzi wa Kamati ulibaini kuwa, mwenendo wa upatikanaji fedha ulifikia asilimia 311.5 kutokana na Ofisi ya Waziri Mkuu kupokea fedha za Kuboresha Daftari la Wapiga kura kutoka Hazina (Fungu 21 - Wizara ya Fedha na Mpango), kwa ajili ya Tume ya Uchaguzi, kiasi cha shilingi 139,450,389,534.00. Kamati inaipongeza sana Hazina kwa kutoa fedha za kuboresha Daftari la Wapiga kura kwa wakati, na imeridhishwa na jinsi Ofisi ya Waziri Mkuu inavyoratibu Uboreshaji wa Daftari hilo kupitia Tume ya Uchaguzi, hatua ambayo imeweza vijana wengi kujiandikisha na kupunguza kasoro nyingi zilizokuwepo hapo awali. Hivyo, hiyo ni dalili njema kuelekea Uchaguzi Mkuu, Uchaguzi utakaokuwa huru na haki ni wa mwaka 2020. (*Makofii*)

Uchambuzi wa Mpango na Makadirio ya Mapato na Matumizi kwa Mwaka wa Fedha 2020/2021. Uchambuzi wa Vipaumbele vya Bajeti ya Ofisi ya Waziri Mkuu. Mpango na Bajeti ya Ofisi ya Waziri Mkuu kwa mwaka wa fedha 2020/2021 umeainisha maeneo 19 ya vipaumbele kama vilivyooneshwa katika taarifa hii. Kamati iliridhishwa na vipaumbele vilivyowekwa na Ofisi ya Waziri Mkuu kwa sababu vinaendana na Mpango wa Taifa wa Mwaka 2020/2021. Aidha, Kamati imeridhika na vipaumbele hivi kwa sababu vinajumuisha maeneo yote ya msingi ambayo yapo katika Ofisi ya Waziri Mkuu Sera, Bunge, Kazi, Ajira, Vijana, Watu wenye Ulemavu na Uwekezaji.

Mheshimiwa Spika, Kamati inatoa rai kwa Ofisi ya Waziri Mkuu kuhakikisha kwamba utekelezaji wa vipaumbele vyake ulenge zaidi katika kuboresha na kuimarisha mazingira wezeshi ya uwekezaji kwa lengo la kuvutia wawekezaji wa

ndani na nje ya nchi, hatua ambayo itatengeneza ajira kwa wananchi wengi na kuongeza fursa mbalimbali za kibiashara na mapato kwa wananchi na Taifa kwa ujumla hivyo kupunguza utegemezi mkubwa kwa bajeti kutoka nje ya nchi.

Mheshimiwa Spika, Uchambuzi wa Makadirio ya Maduhuli kwa Mwaka wa Fedha 2020/2021. Katika mwaka wa fedha wa 2020/2021, Mafungu ya Ofisi ya Waziri Mkuu na Taasisi zake husika zinatarajia kukusanya maduhuli ya jumla ya shilingi 41,118,854,200.00. Kamati imebaini kuwa, Makadirio ya Makusanyo yanaongezeka kwa shilingi 205,700,000.00 ongezeko ambalo ni sawa na asilimia 0.5% ya Bajeti ya Maduhuli kwa Mwaka wa Fedha 2019/2020.

Mheshimiwa Spika, Kamati inakubaliana na mpango wa Ofisi ya Waziri Mkuu wa kuongeza makusanyo ya maduhuli kwa mwaka wa fedha 2020/2021 kwa kuwa ofisi hiyo imedhihirisha uwezo na ubunifu mkubwa katika ukusanyaji wa Maduhuli ya Serikali. Mchanganuo wa kiasi cha Maduhuli kinachotegemewa kukusanywa kwa kila Fungu ni kama ilivyoainishwa katika Jedwali Namba 2 ya taarifa yangu kama inavyoonekana kwenye taarifa hii.

Mheshimiwa Spika, Uchambuzi wa Makadirio ya Matumizi kwa Mwaka wa Fedha 2020/2021. Katika mwaka wa fedha 2020/2021 Ofisi ya Waziri Mkuu inaomba kuidhinishiwa jumla ya shilingi 76,607,103,000.00. Kati ya fedha hizo, shilingi 17,907,339,000.00 ni kwa ajili ya mishahara, shilingi 30,839,117,947.00 ni kwa ajili ya ruzuku kwa taasisi zilizo chini ya Ofisi ya Waziri Mkuu na Vyama vya Siasa, na shilingi 27,860,646,053.00 ni kwa ajili ya Matumizi Mengineyo. Uchambuzi wa Kamati umebaini kuwa Bajeti ya Matumizi ya Kawaida chini ya Ofisi ya Waziri Mkuu na Taasisi zake imeongezeka kwa kiasi cha Shilingi 3,585,661,000.00 sawa na asilimia 4.9 ya Bajeti ya Matumizi ya Kawaida iliyoidhinishwa na Bunge lako Tukufu kwa mwaka wa fedha 2019/2020.

Mheshimiwa Spika, Kamati imekubaliana na ongezeko hilo la kibajeti ili kuiwezesha Ofisi ya Waziri Mkuu kutekeleza majukumu yake kwa ufanisi mkubwa ikiwemo

kuimarisha uratibu wa masuala ya uwekezaji nchini pamoja na masuala ya vijana na watu wenyewe ulemavu. Hii inatokana na Ofisi hiyo kuiridhisha Kamati kuhusu utekelezaji wa mpango wa bajeti kwa mwaka wa fedha 2019/2020 kwa ufanisi mkubwa ndani ya robo tatu ya mwaka.

Mheshimiwa Spika, Mpango wa Maendeleo kwa Mwaka wa Fedha 2020/2021, katika Mwaka wa Fedha 2020/2021, Ofisi ya Waziri Mkuu na Taasisi zilizo chini yake zimeomba jumla ya Shilingi 219,472,625,000/= kwa ajili ya Mpango wa Maendeleo. Kati ya fedha hizo Shilingi 194,368,000,000/= ni fedha za ndani na Shilingi 25,104,625,000/= ni fedha za nje.

Mheshimiwa Spika, uchambuzi wa Kamati umebaini kuwa, Bajeti ya Maendeleo inayoombwaa imeongezeka kwa Shilingi 162,735,059,263/=. Ongezeko hilo ni sawa na asilimia 287.3% ya Bajeti ya Maendeleo iliyoidhinishwa na Bunge kwa Mwaka wa Fedha 2019/2020.

Mheshimiwa Spika, mabadiliko hayo katika Bajeti ya maendeleo pamoja na sababu nyingine muhimu, yanatokana na kuongezeka kwa Bajeti ya Fungu 61 (Tume ya Taifa ya Uchaguzi) kwa ajili ya kuiwezesha Menejimenti ya Uchaguzi ili iweze kutekeleza Majukumu yake yanayoikabili kwa Mwaka huu 2020 kwa ufanisi mkubwa zaidi unaotarajiwa.

Mheshimiwa Spika, Maoni na Ushauri wa Kamati, Fungu 37 Ofisi ya Waziri Mkuu, Kamati imeridhishwa kwa kiasi kikubwa na utekelezaji wa maoni na mapendekezo ya Kamati yaliyotolewa na Kamati kwa Ofisi ya Waziri Mkuu katika Mwaka wa Fedha 2019/2020. Aidha, Kamati imeridhishwa na uwezo wa Ofisi hii katika kuongeza makusanyo ya Maduhuli kwa lengo la kupunguza utegemezi. Hivyo, Serikali iendelee na jitihada hizo kwa Mwaka wa Fedha 2020/2021.

Mheshimiwa Spika, Kamati inaipongeza Serikali kwa kuboresha Miundombinu ya kazi katika Ofisi ya Mpiga Chapa Mkuu wa Serikali, ikiwa ni pamoja na kumpata Mpiga Chapa Mkuu wa Serikali ambaye ni pia ni Mwanamama, ambaye

amefanya mageuzi makubwa kwa kuboresha miundombinu na kuongeza Makusanyo ya Serikali kwa kiasi kikubwa na kwa muda mfupi. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, Kamati inaishauri Serikali kuendelea kuboresha Ofisi hiyo ikiwa ni pamoja na kuboresha mazingira ya kazi kwa Wafanyakazi wake. Hii ni pamoja na kuhakikisha kuwa fedha zote zinazoombwa na kuidhinishwa na Bunge kwa ajili ya Ofisi hii muhimu zinatolewa kwa wakati ili kuiwezesha kutekeleza majukumu yake kwa haraka na kwa ufanisi.

Mheshimiwa Spika, Kamati imeridhishwa na hatua ya utekelezaji wa Ushauri wa Kamati kuhusu kupunguza bajeti ya fedha za nje kwenye Miradi ya Maendeleo. Hivyo, Kamati inaendelea kuishauri Serikali kuhakikisha kuwa, fedha za ndani zinazotengwa zinapatikana kwa wakati kama zillivoombwa. Hatua hiyo inawezekana kama Serikali itaendelea kuongeza vyanzo vipyta vya Mapato, kuboresha mazingira ya Uwekezaji nchini kwa kuwavutia wawekezaji ndani na nje ya nchi kwa lengo la kuongeza kasi ya Ujenzi, Uendelezaji wa Viwanda nchini, hatua ambayo itaongeza fursa za kiuchumi na kuongeza pato la ndani.

Mheshimiwa Spika, Kamati inaendelea kuishauri Ofisi ya Waziri Mkuu kuwa, iendelee kuimarisha Usimamizi wa Masuala ya Uwekezaji nchini kwa lengo la kuongeza na kuchochaea ukuaji wa Uchumi kwa Viwanda nchini kuelekea Uchumi wa Kati ifikapo mwaka 2025.

Mheshimiwa Spika, Fungu 27 - Ofisi ya Msajili wa Vyama Vya Siasa, Kamati inaishauri Ofisi ya Msajili wa Vyama vya Siasa kuelekea Uchaguzi Mkuu, kuhakikisha inasimamia mwenendo wa Vyama vya Siasa kwa kuendelea kuchunguza na kufuatilia mienendo ya Vyama vya Siasa, ili vizingatieve Sheria, Kanuni, Taratibu na weledi kwa ustawi wa Taifa letu.

Mheshimiwa Spika, Kamati inaendelea kuishauri Ofisi ya Msajili wa Vyama vya Siasa kuimarisha usimamizi na udhibiti wa mienendo ya Vyama vya Siasa ikiwa ni pamoja na

kuchukua hatua stahiki kwa kila Chama kinachovunja Misingi ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania pamoja na Sheria zingine za nchi, kwa lengo la kulinda Umoja, Udugu, Amani, Ulinzi na Usalama wa nchi yetu, kabla na baada ya Uchaguzi mkuu ujao.

Mheshimiwa Spika, Mfuko wa Fidia kwa Wafanyakazi (*WCF*), pamoja na Kamati kuridhishwa na kazi nzuri inayofanywa chini ya Mfuko huu, Kamati inaendelea kushauri Mfuko uendelee kutoa Elimu ya kutosha kwa Waajiri na Wafanyakazi hususan Vyama vya Wafanyakazi kwa lengo la kuhakikisha kuwa Waajiri wote nchini wanazingatia matakwa ya Sheria katika kuhakikisha Wanajandikisha kwenye Mfuko, wanalipa Ada/Michango stahiki kwa wakati na kutoa taarifa sahihi.

Mheshimiwa Spika, Kamati inaendelea kushauri Mfuko kuweka na kuimarishe Mfumo mzuri wa kufanya tathmini za fidia kwa Wafanyakazi wanaopata ajali kazini na kuhakikisha kwamba malipo ya fidia yanafanywa kwa haraka kwa kila Mfanyakazi aliyetimiza vigezo.

Mheshimiwa Spika, Fungu 65 - Kazi na Ajira; pamoja na Kamati kuridhishwa na utendaji kazi wa Mamlaka ya Usalama na Afya Mahala pa Kazi (*OSHA*), Kamati inaendelea kushauri kuwa *OSHA* iendelee kubuni mikakati endelevu na kutekeleza kuhusu kusimamia afya na usalama wa wafanyakazi mahala pa kazi kwa kuzingatia ongezeko la uanzishwaji wa viwanda nchini kwa kulinda usalama wa wafanyakazi.

Mheshimiwa Spika, pamoja na Kamati kuridhishwa na hatua ya Serikali kuanzisha Kitengo cha Kuratibu Masuala ya Watu Wenye Ulemavu chini ikiwemo kuanzisha rasmi Baraza la Taifa la Kuratibu masuala kundi hilo la jumla. Kamati inaishauri kuwa Ofisi ya Waziri Mkuu ihakikishe inasimamia kitengo hicho na Baraza husika ili vyombo hivyo vitekeleze majukumu yake kwa uweledi mkubwa ikiwa ni pamoja na kuendeleza hatua zake za kutatua migogoro mbalimbali inayoendelea katika vyama vya watu wenye ulemavu nchini.

Mheshimiwa Spika, Kamati inaendelea kuishauri Ofisi ya Waziri Mkuu pia kuwa na kushirikiana Ofisi ya Rais, TAMISEMI wahakikishe wanaongeza udhibiti wa marejesho ya mikopo ya fedha za Mfuko wa Maendeleo wa Vijana ili Mfuko huo uwafikie vijana wengi zaidi. Hatua hiyo iende sambamba na utoaji wa elimu kuhusu matumizi bora ya fedha za Mfuko kwa maendeleo yaliyokusudiwa.

Mheshimiwa Spika, Tume ya Taifa ya Uchaguzi; Fungu 61 pamoja na Kamati kuridhishwa na utekelezaji wa ushauri wake kuhusu kuboresha daftari la wapiga kura; kwa uangalifu mkubwa Kamati inaendelea kuishauri Tume ya Taifa ya Uchaguzi kujitahidi kufanya kazi yake kwa weledi ili kuendelea kuaminika kwa wadau wake wa uchaguzi na hasa kipindi hiki kuelekea uchaguzi Mkuu wa mwaka 2020. Kamati inaendelea kushauri kwamba Tume ya Taifa ya Uchaguzi ihakikishe inafuatilia wasimamizi wake katika uchaguzi na kuwajibisha pale wanapofanya uzembe unaosababisha madhara ambayo yangeweza kudhibitiwa mapema na msimamizi aliye makini na aliyetambua kutelekeza wajibu wake kwa mujibu wa sheria.

Mheshimiwa Spika, pamoja na Kamati kuridhishwa na jinsi Hazina ilivyotoa kwa wakati fedha za kuiwezesha Tume ya Uchaguzi kuboresha daftari la wapiga kura, bado Kamati inaendelea kuishauri Serikali kuhakikisha inatoa fedha zillizoidhinishwa na Bunge lako Tukufu kwa wakati ili kuiwezesha Tume ya Taifa ya Uchaguzi kuratibu masuala mbalimbali ya uchaguzi kwa ufanisi mkubwa.

Mheshimiwa Spika, hitimisho. Napenda kukupongeza kwa kuendelea kuliongoza Bunge lako hili vyema kwa weledi na kwa umahiri wa hali ya juu nikishukuru kwa kunipa nafasi hii ya kuwasilisha maoni ya Kamati kwa niaba ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Katiba na Sheria. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, maelezo hayo pamoja na mengine ambayo sijayasoma naomba yaingie kwenye Kumbukumbu Rasmi za Bunge. Baada ya maelezo hayo, naliomba Bunge lako Tukufu sasa lijadili na kuidhinisha

makadirio ya mapato na matumizi ya Ofisi ya Waziri Mkuu, Sera, Kazi, Ajira, Vijana na Wenye Ulemavu na Uwekezaji kwa mwaka wa fedha 2020/2021 kama zilivowasilishwa na mtoa hoja.

Mheshimiwa Spika, naomba kuwasilisha na naunga mkono hoja. (*Makof*)

**TAARIFA YA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA KATIBA NA
SHERIA KUHUSU UTEKELEZAJI WA BAJETI YA OFISI YA WAZIRI
MKUU KWA MWAKA WA FEDHA 2019/2020; PAMOJA NA
MAONI YA KAMATI KUHUSU MAKADIRIO YA MAPATO NA
MATUMIZI YA OFISI HIYO KWA MWAKA WA FEDHA 2020/2021
KAMA ILIVYOWASILISHWA MEZANI**

UTANGULIZI

Mheshimiwa Spika, awali ya yote napenda kumshukuru Mwenyezi Mungu aliyetupa afya, uzima na nafasi nyingine ya kukutana hapa Dodoma katika Mkutano huu wa Kumi na Tisa wa Bunge la Kumi na Moja.

Mheshimiwa Spika, kwa mujibu wa Kanuni ya 99 (9) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Januari 2016, naomba kuwasilisha Taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Katiba na Sheria kuhusu Utekelezaji wa Bajeti ya Ofisi ya Waziri Mkuu kwa Mwaka wa Fedha 2019/2020, pamoja na maoni ya Kamati kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Ofisi hiyo kwa Mwaka wa Fedha 2020/2021.

Mheshimiwa Spika, Kifungu cha 6 (2)(a) cha Nyongeza ya Nane ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Januari 2016, kimeipa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Katiba na Sheria jukumu la kusimamia shughuli za Ofisi ya Waziri Mkuu - Sera, Bunge, Kazi, Vijana, Ajira, Watu wenye Ulemavu na Uwekezaji.

Aidha, Kanuni ya 7(1) (a) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Januari 2016 inatoa Mamlaka kwa Kamati zote za Kisikta kushughulikia bajeti za Wizara inazozisimamia. Jukumu hili la Uchambuzi wa Bajeti linaendana sambamba na jukumu la ukaguzi wa Miradi ya Maendeleo iliyoengewa fedha

katika Mwaka wa Fedha 2019/2020 kwa mujibu wa Kanuni ya 98(1) na (2) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Januari, 2016.

Mheshimiwa Spika, naomba kutoa taarifa kwamba Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Katiba na Sheria ilipokea na kujadili Taarifa ya Ofisi ya Waziri Mkuu kuhusu Utekelezaji wa Mradi wa kukuza ujuzi nchini (**Mradi Namba 6581, Fungu 65**) kwa Mwaka wa Fedha 2019/2020., uliotengewa **Shilingi Bilioni 18** na kupokea **kiasi cha Shilingi Bilioni 12** hadi Februari, 2020, ambacho ni sawa na **asilimia 66.7%** ya Fedha yote iliyoidhinishwa. Kamati pia ilifanya uchambuzi wa Bajeti ya Ofisi hiyo, kwa Mafungu yote Sita (6) yaliyo chini ya Ofisi hiyo, tarehe 25 Machi, 2020.

Mheshimiwa Spika, Mafungu Sita (6) ya Bajeti ya Ofisi ya Waziri Mkuu, Bunge, Kazi, Vijana, Ajira, Watu wenye Ulemavu na Uwekezaji ni kama ifuatavyo:-

- i) **Fungu 37** - Ofisi ya Waziri Mkuu,
- ii) **Fungu 25** - Ofisi Binafsi ya Waziri Mkuu,
- iii) **Fungu 65** – Kazi, Vijana, Ajira na Watu Wenye Ulemavu,
- iv) **Fungu 15** - Tume ya Usuluhishi na Uamuzi (CMA),
- v) **Fungu 61** - Tume ya Taifa ya Uchaguzi (NEC), na
- vi) **Fungu 27** - Ofisi ya Msajili wa Vyama vya Siasa Tanzania

Mheshimiwa Spika, Taarifa hii inatoa maelezo kuhusu maeneo Manne yafuatayo:-

- i) Taarifa ya Utekelezaji wa Miradi ya Maendeleo iliyotengewa fedha kwa mwaka wa Fedha unaoisha;
- ii) Mapitio ya Taarifa ya Utekelezaji wa Mpango na Bajeti kwa Mwaka wa Fedha 2019/2020;

iii) Uchambuzi wa Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Ofisi ya Waziri Mkuu kwa Mwaka wa Fedha 2020/2021 na;

iv) Maoni na Ushauri wa Kamati.

TAARIFA YA UTEKELEZAJI WA MIRADI YA MAENDELEO ILIYOTENGEWA FEDHA KWA MWAKA WA FEDHA 209/2020

Mheshimiwa Spika, katika kutekeleza Kanuni ya 98 (1) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Kamati ya Katiba na Sheria ilipokea taarifa ya utekelezaji wa **Mradi Na. 6581** wa Programu ya Kukuza Ujuzi nchini, ambao kwa Mwaka wa Fedha 209/2020 ilitengewa kiasi cha **Shilingi Bilioni Kumi na Nane (18,000,000,000/=)**.

Mheshimiwa Spika, *Kamati imeridhishwa na upatikanaji wa Fedha za kutekeleza Mradi huo, kwani kwa kipindi cha Julai, 2019 hadi Februari, 2020 Ofisi ya Waziri Mkuu imepokea kiasi cha Shilingi Bilioni Kumi na Mbili (12,000,000,000/=) sawa na asilimia 66.7% ya Bajeti ya Mradi huo iliyoidhinishwa na Bunge kwa Mwaka wa Fedha 2019/2020.*

UCHAMBUZI WA TAARIFA YA OFISI YA WAZIRI MKUU KUHUSU UTEKELEZAJI WA MPANGO WA BAJETI NA UZINGATIAJI WA MAONI YA KAMATI KWA MWAKA WA FEDHA 2019/2020

Mheshimiwa Spika, Kamati ilipokea na kuchambua Taarifa za Utekelezaji wa Bajeti kwa Mwaka wa Fedha 2019/2020 na uchambuzi wa Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Ofisi ya Waziri Mkuu pamoja na Taasisi zilizo chini yake kwa Mwaka wa fedha 2020/2021, kwa mujibu wa Kanuni ya 98 (2) ya Kanuni za Kudumu za Bunge Toleo la Januari 2016, tarehe 25 Machi, 2020. Naomba kulijulisha Bunge lako Tukufu kuhusu uchambuzi huo kama ifuatavyo:-

Uchambuzi wa Mapitio ya Utekelezaji wa Mpango na Bajeti kwa Mwaka wa Fedha 2019/2020

Mheshimiwa Spika, uchambuzi uliofanywa na Kamati katika Mapitio ya Utekelezaji wa Mpango na Bajeti ya Ofisi ya Waziri

Mkuu kwa Mwaka wa Fedha 2019/2020 ultazama mlinganisho wa kiasi cha fedha kilichoidhinishwa na Bunge Aprili 2019 na kiwango ambacho kimepokelewa kwa kipindi cha Julai, 2019 hadi Februari, 2020.

Aidha, uchambuzi huu ultazama kiasi cha fedha kilichoidhinishwa katika Mwaka wa Fedha 2019/2020 na kiasi cha Fedha kilichopokelewa katika Miradi ya Maendeleo hadi kufikia Mwezi Februari, 2020. Lengo la kufanya tathmini ya namna hii ni kufahamu Mwelekeo wa Mpango na Bajeti ya Mapato na Matumizi ya Serikali katika Mwaka wa Fedha 2020/2021 ili kujua vipaumbele vya kibajeti.

Mheshimiwa Spika, uchambuzi uliofanywa na Kamati ultazama pia eneo la ukusanyaji wa Maduhuli kwa kulinganisha kiasi kilichokusanywa katika kipindi cha Julai, 2019 hadi Februari, 2020 na ukamilishaji wa lengo la ukusanyaji liliowekwa wakati wa kupitisha bajeti Mwezi Aprili 2019. Lengo la uchambuzi wa namna hii ni kufahamu uwezo wa Serikali katika kukusanya Maduhuli. Kamati ilitumia njia mbalimbali katika uchambuzi wake kama kutazama hali halisi ya kila Taasisi, kujiridhisha na taarifa mbalimbali zilizowahi kuwasilishwa kwenye Kamati na mahojiano yaliyochangia upatikanaji wa taarifa muhimu kwenye Kamati.

Uchambuzi wa Taarifa Kuhusu Ukusanyaji wa Maduhuli kwa Mwaka wa Fedha 2019/2020

Mheshimiwa Spika, katika Mwaka wa Fedha 2019/2020 Bunge lako Tukufu liliidhinisha Makadirio ya Makusanyo ya Maduhuli yenye jumla ya **Shilingi Bilioni Arobaini, Milioni Mia Tisa Kumi na Tatu, Laki Moja Hamsini na Nne Elfu, Mia Mbili (40,913,154,200/=)**. Katika kipindi cha Julai, 2019 hadi Februari, 2020 kiasi cha Maduhuli kilichokusanywa na Ofisi ya Waziri Mkuu na Taasisi zilizo chini yake ni **Shilingi Bilioni Ishirini na Saba, Milioni Mia Tatu Arobaini na Tatu, Laki Tisa Tisini na Tatu Elfu, Mia Tatu Themanini na Nane (27,343,993,388/=)** sawa na asilimia **66.8**.

Kamati, inaipongeza Ofisi ya Waziri Mkuu kwa kuwa mfano **bora na wa kuigwa na Wizara pamoja na Taasisi zote za Serikali** katika kuongeza ubunifu wa vyanzo vya mapato ya Serikali, hatua ambayo itasaidia kupunguza utegemezi kutoka nje ya nchi.

Upatikanaji wa fedha za Matumizi ya Kawaida kutoka Hazina

Mheshimiwa Spika, Ofisi ya Waziri Mkuu pamoja na taasisi zake, katika Mwaka wa Fedha wa 2019/2020 ilitengewajumla ya **Shilingi Bilioni Sabini na Tatu na Milioni Ishirini na Moja, Laki Nne Elfu (73,021,442,000/=)** kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida. Kati ya fedha hizo, **Shilingi Bilioni Kumi na Nane, Milioni Mia Nane Themanini na Moja, Laki Nne Tisini na Tano Elfu, Mia Tisa Tisini na Tisa (18,881,495,999/=)** zilikuwa za Mishahara, na **Shilingi Bilioni Ishirini na Sita, Milioni Mia Tatu, Laki Sita Arobaini na Sita Elfu na Hamsini na Tatu (26,300,646,053/=)** zilikuwa za Matumizi Mengineyo na **Shilingi Bilioni Ishirini na Saba, Milioni Mia Nane Thelathini na Tisa, Laki Mbili Tisini na Tisa Elfu, Mia Tisa Arobaini na Nane (27,839,299,948/=)** zilikuwa za Ruzuku kwa Taasisi na Vyama vya Siasa.

Mheshimiwa Spika, Katika kipindi cha Julai, 2019 hadi Februari, 2020, Mafungu hayo yalipokea jumla ya **Shilingi Bilioni Arobaini na Sita, Milioni Mia Nane Hamsini na Nane, Laki Moja na Nane Elfu, Mia Sita Thelathini na Nane na Senti Sita (46,858,108, 638.6)** sawa na asilimia **64.2** ya bajeti. Uchambuzi wa uwiano wa Bajeti iliyoidhinishwa na upatikanaji wa fedha ya Matumizi ya Kawaida hadi kufikia Februari 2020 umeainishwa katika Jedwali Na. 1 .

JEDWALI NA. 1: Uchambuzi wa Uwiano wa Bajeti iliyoidhinishwa na Upatikanaji wa Fedha za Matumizi ya Kawaida hadi kufikia Februari, 2020

VA.	FUNGU	BAJETI ILIYOIDHINISHWA	FEDHA ILIYOPATIKANA	ASILIMIA
1.	37-Ofisi ya Waziri Mkuu	7,980,744,000	5,039,930,764	63.2
2	25 - Ofisi Binafsi ya Waziri Mkuu	3,741,512,000	2,213,594,814	59.2
3	65 – Kazi, Ajira ,Vijana na Wenye Ulemavu	23,671,461,000	16,852,477,550.35	71.2
4	27- Msajili wa Vyama vya Siasa	19,109,653,000	11,148,807,597	58.3
5	15-Tume ya Usuluhishi na Uamuzi	5,234,294,000	4,392,584,795.25	84
6	61- Tume ya Taifa ya Uchaguzi	13,283,778,000	7,210,713,118	54.3
JUMLA		73,021,442,000	46,858,108,6386	64.2

Chanzo: Taarifa ya WN-OWM, tarehe 25 Machi, 2020

Mheshimiwa Spika, uchambuzi huu unaonyesha kuwa kumekuwa na mwenendo mzuri kuhusu upatikanaji wa fedha kwa kila Fungu.

Mheshimiwa Spika, Maoni ya Kamati ni kwamba hali ya upatikanaji wa fedha kwa wakati inatakiwa kuendelea na kuzingatiwa na Serikali kwa Mwaka wa Fedha 2020/2021, ili kurahisisha usimamizi na Utekelezaji wa Shughuli mbalimbali za Serikali kwa wakati na kwa ufanisi.

Uchambuzi wa Utekelezaji wa Bajeti ya Maendeleo kwa Mwaka wa Fedha 2019/2020,

Mheshimiwa Spika, Katika Mwaka wa fedha 2019/2020 Ofisi ya Waziri Mkuu, ilitengewa jumla ya **Shilingi Bilioni Hamsini na Sita, Milioni Mia Sita Thelathini na Saba, Laki Tano Sitini na Tano Elfu, Mia Saba Thelathini na Saba (56,637,565,737/=)** kwa ajili ya Miradi Maendeleo. Kati ya fedha hizo **Shilingi Bilioni Kumi na Tisa Elfu (19,000,000,000/=)** zilikuwa ni fedha za ndani na **Shilingi Bilioni Thelathini na Saba, Milioni Mia Sita Thelathini na Tisa na Thelathini na Tatu Elfu, Mia Nane**

Thelathini na Nne (37,639,033,834/=) zilikuwa ni fedha za nje.

Mheshimiwa Spika, Hadi Februari, 2020, jumla ya **Shilingi Bilioni Mia Moja Sabini na Sita, Milioni Mia Nne Arobaini na Tisa, Laki Nane Kumi na Nane Elfu na Thelathini na Saba (176, 449,818,037/=)** zilikuwa zimepokelewa, ambazo ni sawa na asilimia 311.5 ya bajeti iliyoidhinishwa.

Mheshimiwa Spika, Uchambuzi wa Kamati ulibaini kuwa, mwenendo wa upatikanaji fedha ulifikia **asilimia 311.5** kutokana na Ofisi ya Waziri Mkuu kupokea fedha za Kuboresha Daftari la Wapiga kura kutoka Hazina (**Fungu 21 - Wizara ya Fedha na Mipango**), kwa ajili ya Tume ya Uchaguzi, kiasi cha **Shilingi Bilioni Mia Moja Thelathini na Tisa, Milioni Mia Nne Hamsini, Laki Tatu Themani na Tisa Elfu, Mia Tano Thelathini na Nane (139,450,389,538/=)**.

Mheshimiwa Spika, Kamati imeipongeza Hazina kwa kutoa fedha za kuboresha Daftari la Wapiga kura kwa wakati, na imeridhishwa na jinsi Ofisi ya Waziri Mkuu inavyoratibu Uboreshaji wa Daftari hilo kupitia Tume ya Uchaguzi, hatua ambayo imewezesha vijana wengi kujiandikisha na kupunguza kasoro nyingi zilizokuwepo hapo awali. Hivyo, hiyo ni dalili njema kuelekea Uchaguzi uliyo huru na haki kwa mwaka huu 2020.

Yatokanayo na Uchambuzi wa Taarifa ya Utekelezaji wa Miradi ya Maendeleo

Mheshimiwa Spika, uchambuzi wa Kamati umebaini kuwa upatikanaji wa Fedha za Mfuko wa Maendeleo ya Vijana kwa robo tatu ya Mwaka wa Fedha 2019/2020 siyo wa kuridhisha kwa kuwa, Mfuko huo haujapokea kiasi chochote cha Fedha zilizoidhinishwa na Bunge lako Tukufu.

Mheshimiwa Spika, Maoni ya Kamati ni kuwa, pamoja na Vijana kuendelea kunufaika na Mikopo mbalimbali kupitia Halmashauri nchini, pamoja na Mradi wa kuongeza ujuzi nchini, bado kuna kila sababu kwa Serikali kutoa fedha za

Mfuko wa Maendeleo ya Vijana kabla ya kuisha kwa Mwaka huu wa Bajeti 2019/2020.

UCHAMBUZI WA MPANGO NA MAKADIRIO YA MAPATO NA MATUMIZI KWA MWAKA WA FEDHA 2020/2021

Mheshimiwa Spika, Kamati ilipokea na kuchambua Mpango na Bajeti ya Ofisi ya Waziri Mkuu na Taasisi zilizo chini yake kwa Mwaka wa Fedha 2020/2021 tarehe 25 Machi 2020. Kamati imebaini kuwa, Mpango huu wa Bajeti na Makadirio ya Mapato na Matumizi kwa Mwaka wa Fedha 2020/2021 umeandaliwa kwa kuzingatia llani ya Uchaguzi ya Chama cha Mapinduzi ya Mwaka 2015 - 2020, Mwongozo wa Mpango wa Bajeti uliotolewa na Wizara ya Fedha na Mpango ambao umelenga utekelezaji wa Mpango wa Pili wa Maendeleo wa Miaka Mitano (2016/17-2020/2021).

Uchambuzi wa Vipaumbele vya Bajeti ya Ofisi ya Waziri Mkuu

Mheshimiwa Spika, Mpango na Bajeti ya Ofisi ya Waziri Mkuu kwa Mwaka wa Fedha 2020/2021 umeainisha maeneo 19 ya vipaumbele yakiwemo;

- i) Kuchapa Nyaraka mbalimbali za Uendeshaji wa Shughuli za Serikali Kuu, Bunge na Serikali za Mitaa,
- ii) Kujenga uwezo wa Serikali kukabiliana na Maafa;
- iii) Kuratibu na kusimamia Maendeleo ya Uwekezaji Nchini,
- iv) Kuratibu na kusimamia Shughuli za Baraza la Taifa la Biashara,
- v) Kuratibu Shughuli za Bunge na kushughulikia kero na malalamiko ya Wananchi;
- vi) Kusuluuhisha Migogoro sehemu za Kazi,
- vii) Kuratibu na kusimamia uwezeshaji wa Maendeleo ya Vijana,

viii) Kuratibu na Kusimamia Masuala ya Fidia kwa Wafanyakazi wanaoumia, kufariki au kupata madhara ya kiafya wakiwa kazini,

ix) Kuratibu Utekelezaji wa Sera, Sheria na Mikakati ya Kukuza Ajira nchini na kuongeza nafasi za Ajira za Watanzania nchi za nje,

x) Kusimamia, Kuratibu na kutoa huduma kwa Watu wenye Ulemavu, na

xi) Kusimamia Taasisiza Umma zilizo chini ya Ofisi ya Wazi ri Mkuu.

Mheshimiwa Spika, Kamati iliridhishwa na vipaumbele viliyowekwa na Ofisi ya Waziri Mkuu kwa sababu vinaendana na Mpango wa Taifa wa Mwaka 2020/2021. Aldha, Kamati imeridhika na vipaumbele hivi kwa sababu vinajumuisha maeneo yote ya msingi ambayo yapo katika Ofisi ya Waziri Mkuu - Sera, Bunge, Kazi, Ajira, Vijana, Watu wenye Ulemavu na Uwekezaji.

Mheshimiwa Spika, Kamati inatoa rai kwa Ofisi ya Waziri Mkuu kuhakikisha kwamba utekelezaji wa vipaumbele vyake ulenge zaidi katika kuboresha na kuimarisha mazingira wezeshi ya uwekezaji kwa lengo la kuvutia wawekezaji wa ndani na nje ya nchi, hatua ambayo itatengeneza Ajira kwa Wananchi wengi na kuongeza fursa mbalimbali za biashara na mapato kwa Wananchi na Taifa kwa ujumla hivyo, na kupunguza utegemezi mkubwa wa kibajeti kutoka nje ya Nchi.

Uchambuzi wa Makadirio ya Maduhuli kwa Mwaka wa Fedha 2020/2021

Mheshimiwa Spika, katika Mwaka wa Fedha wa 2020/2021, Mafungu ya Ofisi ya Waziri Mkuu (**Fungu 37**), Ofisi ya Msajili wa Vyama vya Siasa (**Fungu 27**), Tume ya Taifa ya Uchaguzi (**Fungu 61**) Ofisi ya Waziri Mkuu - Kazi, Vijana, Ajira na Watu Wenye Ulemavu (**Fungu 65**) zinatarajia kukusanya

maduhuli ya jumla ya **Shilingi Bilioni Arobaini na Moja, Milioni Mia Moja Kumi na Nane, Laki Nane Hamsini na Nne Elfu, Mia Mbili (41,118,854,200/=).**

Mheshimiwa Spika, Kamati imebaini kuwa, Makadirio ya Makusanyo yanaongezeka kwa **Shilingi Milioni Mia Mbili na Tano, Laki Saba Elfu (205, 700,000/=)** ongezeko ambalo ni **sawa na asilimia 0.5%** ya Bajeti ya Maduhuli kwa Mwaka wa Fedha 2019/2020.

Mheshimiwa Spika, Kamati inakubaliana na Mpango wa Ofisi ya Waziri Mkuu wa kuongeza Makusanyo ya Maduhuli kwa Mwaka wa Fedha 2020/2021, kwa kuwa Ofisi hiyo imedhihirisha uwezo na ubunifu mkubwa katika ukusanyaji wa Maduhuli ya Serikali.

Mheshimiwa Spika, mchanganuo wa kiasi cha Maduhuli kinachotegemewa kukusanya kwa kila Fungu ni kama ilivyoainishwa katika Jedwali **Na.2.**

Jedwali Na.2. Makisio ya Maduhuli kwa Mwaka wa Fedha 2020/2021, Ofisi ya Waziri Mkuu

FUNGU	TAASISI HUSIKA	MADUHULI YALIYOIDHINISHWA 2019/2020	MAKADIRIO YA MADUHULI 2020/2021
27	Msajili wa Vyama vya Slasa	10,300,000	36,000,000
37	Ofisi ya Waziri Mkuu	2,000,000,000	2,000,000,000
61	Tume ya Taifa ya Uchaguzi	20,000,000	200,000,000
65	Kazi, Vijana, Ajira na Watu Wenye Ulemavu	38,882,854,200	38,882,854,200
JUMLA		40,913,154,200	41,118,854,200

Chanzo: Taarifa ya WN-OWM, tarehe 25 Machi, 2020

Uchambuzi wa Makadirio ya Matumizi kwa Mwaka wa Fedha 2020/2021

Mheshimiwa Spika, katika Mwaka wa Fedha 2020/2021 Ofisi ya Waziri Mkuu inaomba kuidhinishiwa jumla ya **Shilingi Bilioni Sabini na Sita, Milioni Mia Sita na Saba, Laki Moja na Tatu Elfu (76,607,103,000/=)**. Kati ya fedha h i z o , Shilingi Bilioni Kumi na Saba, Milioni Mia Tisa na Saba, Laki Tatu Thelathini na Tisa Elfu (17,907,339,000/=) ni kwa ajili ya Mishahara, Shilingi Bilioni Thelathini, Milioni Mia Nane Thelathini na Tisa, Laki Moja Kumi na Saba Elfu, Mia Tisa Arobaini na Saba (30,839,117,947/=) ni kwa ajili ya ruzuku kwa Taasisi zilizo chini ya Ofisi ya Waziri Mkuu na Vyama vyta Siasa, na **Shilingi Bilioni Ishirini na Saba, Milioni Mia Nane Sitini, Laki Sita Arobaini na Sita Elfu na Hamsini na Tatu (27,860, 646, 053/=)** ni kwa ajili ya Matumizi Mengineyo.

Mheshimiwa Spika, uchambuzi wa Kamati umebaini kuwa Bajeti ya Matumizi ya Kawaida chini ya Ofisi ya Waziri Mkuu na Taasisi zake imeongezeka kwa kiasi cha **Shilingi Bilioni Tatu, Milioni Mia Tano Themanini na Tano, Laki Sita Sitini na Moja Elfu (3,585,661,000/=)** sawa na asilimia 4.9% ya Bajeti ya Matumizi ya Kawaida iliyoidhinishwa na Bunge lako Tukufu kwa Mwaka wa Fedha 2019/2020.

Mheshimiwa Spika, Kamati imekubaliana na ongezeko hilo la kibajeti ili kuiwezesha Ofisi ya Waziri Mkuu kutekeleza Majukumu yake kwa ufanisi mkubwa ikiwemo kuimarisha uratibu wa Masuala ya Uwekezaji nchini pamoja na Masuala ya Vijana na Watu wenyewe ulemavu. Hii inatokana na Ofisi hiyo kuiridhisha Kamati kuhusu ilivyotekeleza Mpango wa Bajeti wa Mwaka wa Fedha 2019/2020 kwa ufanisi mkubwa ndani ya Robo tatu ya Mwaka.

Mpango wa Maendeleo kwa Mwaka wa Fedha 2020/2021

Mheshimiwa Spika, katika Mwaka wa Fedha 2020/2021, Ofisi ya Waziri Mkuu na Taasisi zilizo chini yake zimeombewa **Shilingi Bilioni Mia Mbili Kumi na Tisa, Milioni Mia Nne Sabini na Mbili, Laki Sita Ishirini na Tano Elfu (219,472,625,000=)** kwa ajili ya Mpango wa Maendeleo. Kati ya fedha hizo **Shilingi Bilioni**

Mia Moja Tisini na Nne, Milioni Mia Tatu Sitini na Nane Elfu (194,368,000,000/=) ni fedha za ndani na Shilingi Bilioni Ishirini na Tano, Milioni Mia Moja na Nne, Laki Sita Ishirini na Tano Elfu (25,104,625,000/=) ni fedha za nje.

Mheshimiwa Spika, uchambuzi wa Kamati umebaini kuwa, Bajeti ya Maendeleo inayoombwaa imeongezeka kwa **Shilingi Bilioni Mia Moja Sitini na Mbili, Milioni Mia Saba Thelathini na Tano, na Hamsini na Tisa Elfu, Laki Mbili Sitini na Tatu (162, 735, 059, 263/=)**. Ongezeko hilo ni sawa na **asilimia 287.3%** ya Bajeti ya Maendeleo iliyoidhinishwa na Bunge kwa Mwaka wa Fedha 2019/2020.

Mheshimiwa Spika, mabadiliko hayo katika Bajeti ya maendeleo pamoja na sababu nydingine muhimu, yanatokana na kuongezeka kwa Bajeti ya **Fungu 61 (Tume ya Taifa ya Uchaguzi)** kwa ajili ya kuiwezesha Menejimenti ya Uchaguzi ili iweze kutekeleza Majukumu yake yanayoikabili Mwaka huu wa 2020 kwa ufanisi mkubwa zaidi unaotarajiwa.

Mheshimiwa Spika, Mpango wa Ofisi ya Waziri Mkuu katika Miradi ya Maendeleo katika Mwaka huu wa Fedha umelenga katika **maeneo Matano (5)** yakiwemo:-

- (i) Kuendeleza ujenzi wa Makazi ya Mhe. Waziri Mkuu Mlimwa Dodoma;
- (ii) Kuendeleza Mbegu za Mazao ya Kilimo na Uvubi (*Agricultural and Fisheries Development Program*);
- (iii) Kuratibu Utekelezaji wa Shughuli za Lishe (*Support Implementation of Nutritional Activities*);
- (iv) Ujenzi wa Jengo la Ofisi ya Msajili wa Vyama vyta Siasa Dodoma;
- (v) Kuendesha Uchaguzi Mkuu wa Mwaka 2020;
- (vi) Kuratibu na kukuza Kazi na Ajira za Staha Nchini;

(vii) Kutekeleza Programu ya Kukuza Ujuzi na Stadi za kazi ya nguvu kazi nchini kwa ajili ya uchumi wa viwanda katika sekta za kilimo-biashara, utalii, usafirishaji, TEHAMA, madini, mafuta na gesi; na

(viii) Kuwajengea uwezo wa Kiuchumi Vijana kuitia Mfuko wa Maendeleo ya Vijana.

MAONI NA USHAURI WA KAMATI

Mheshimiwa Spika, ninaomba sasa kutoa maoni na ushauri wa Kamati kuhusu masuala mbalimbali yaliyojitokeza katika uchambuzi wa Taarifa ya utekelezaji wa Bajeti kwa Mwaka wa Fedha 2019/2020 na Taarifa ya Makadirio ya Mapato na Matumizi kwa Mwaka wa Fedha 2020/2021 wa Ofisi ya Waziri Mkuu na Taasisi zake. Aidha, Maoni na Ushauri wa Kamati umezingatia pia Taarifa ya Utekelezaji wa Miradi ya Maendeleo iliyotengewa fedha katika Mwaka wa Fedha 2019/2020.

FUNGU 37- Ofisi ya Waziri Mkuu

i) **Mheshimiwa Spika**, Kamati imeridhishwa kwa kiasi kikubwa na utekelezaji wa maoni na mapendekezo ya Kamati yaliyotolewa na Kamati kwa Ofisi ya Waziri Mkuu katika Mwaka wa Fedha 2019/2020. Aidha, Kamati imeridhishwa na uwezo wa Ofisi hii katika kuongeza makusanyo ya Maduhuli kwa lengo la kupunguza utegemezi. Hivyo, Serikali iendelee na jitihada hizo kwa Mwaka wa Fedha 2020/2021.

ii) **Mheshimiwa Spika**, Kamati inaipongeza Serikali kwa kuboresha Miundombinu ya kazi katika Ofisi ya Mpiga Chapa Mkuu wa Serikali, ikiwa ni pamoja na kumpata Mpiga Chapa Mkuu wa Serikali ambaye ni Mwanamke, ambaye amefanya mageuzi makubwa kwa kuboresha miundombinu na kuongeza Makusanyo ya Serikali kwa kiasi kikubwa na kwa muda mfupi. Kamati inaishauri Serikali kuendelea kuboresha Ofisi hiyo ikiwa ni pamoja na kuboresha mazingira ya kazi kwa Wafanyakazi wake. Hii ni pamoja na kuhakikisha kuwa fedha zote zinazoombwa na kuidhinishwa na Bunge kwa ajili ya Ofisi

hii muhimu zinatolewa kwa wakati ili kuiwezesha kutekeleza majukumu yake kwa haraka na kwa ufanisi.

iii) **Mheshimiwa Spika**, Kamati imeridhishwa na hatua ya utekelezaji wa Ushauri wa Kamati kuhusu kupunguza bajeti ya fedha za nje kwenye Miradi ya Maendeleo. Hivyo, Kamati inaendeleo kuishauri Serikali kuhakikisha kuwa, fedha za ndani zilizotengwa zinapatikana kwa wakati kama zilivyoombwa. Hatua hiyo inawezekana kama Serikali itaendelea kuongeza vyanzo vipyta ya Mapato, kuboresha mazingira ya Uwekezaji nchini kwa kuwavutia wawekezaji wa ndani na nje ya nchi kwa lengo la kuongeza kasi ya Ujenzi na Uendelezaji wa Viwanda nchini, hatua ambayo itaongeza fursa za kiuchumi na kuongeza pato la ndani.

iv) **Mheshimiwa Spika**, Kamati inaendelea kuishauri Ofisi ya Waziri Mkuu kuwa, iendelee kuimarisha Usimamizi wa Masuala ya Uwekezaji nchini kwa lengo la kuongeza na kuchochaea ukuaji wa Uchumi wa Viwanda nchini kuelekea Uchumi wa Kati ifikapo mwaka 2025.

Fungu 27 - Ofisi ya Msajili wa Vyama Vya Siasa

i) **Mheshimiwa Spika**, Kamati inaishauri Ofisi ya Msajili wa Vyama vya Siasa kuelekea Uchaguzi Mkuu, kuhakikisha inasimamia mwenendo wa Vyama vya Siasa kwa kuendelea kuchunguza na kufuatilia mienendo ya Vyama vya Siasa, ili vizingatie Sheria, Kanuni, Taratibu na weledi kwa ustawi wa Taifa letu.

ii) **Mheshimiwa Spika**, Kamati inaendelea kuishauri Ofisi ya Msajili wa Vyama vya Siasa kuimarisha usimamizi na udhibiti wa mienendo ya Vyama vya Siasa ikiwemo kuchukua hatua stahiki kwa kila Chama kinachovunja Misingi ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania pamoja na Sheria zingine za nchi, kwa lengo la kulinda Umoja, Udugu, Amani, Ulinzi na Usalama wa nchi yetu, kabla na baada ya Chaguzi zijazo.

Mfuko wa Fidia kwa Wafanyakazi (WCF)

i) **Mheshimiwa Spika**, pamoja na Kamati kuridhishwa na kazi nzuri inayofanywa chini ya Mfuko huu, Kamati inaendelea

kushauri Mfuko uendelee kutoa Elimu ya kutosha kwa Waajili na Wafanyakazi hususan Vyama vya Wafanyakazi kwa lengo la kuhakikisha kuwa Waajili wote nchini wanazingatia matakwa ya Sheria katika kuhakikisha Wanajijandikisha kwenye Mfuko, wanalipa Ada/Michango stahiki kwa wakati na kutoa taarifa sahihi.

ii) **Mheshimiwa Spika**, Kamati inaendelea kushauri Mfuko kuweka na kuimarishe Mfumo mzuri wa kufanya tathmini za fidia kwa Wafanyakazi wanaopata ajali kazini na kuhakikisha kwamba malipo ya fidia yanafanyika kwa haraka kwa kila Mfanyakazi aliyetimiza vigezo vya fidia.

FUNGU 65 - Kazi na Ajira

i) **Mheshimiwa Spika**, pamoja na Kamati kuridhishwa na utendaji kazi wa Mamlaka ya Usalama na Afya Mahali pa Kazi (OSHA), Kamati inaendelea kushauri kuwa, OSHA iendelee kubuni mikakati endelevu na kuitekeleza kuhusu kusimamia Afya na Usalama wa Wafanyakazi Mahali Pa Kazi kwa kuzingatia ongezeko la uanzishwaji wa Viwanda nchini katika kulinda usalama wa Wafanyakazi.

ii) **Mheshimiwa Spika**, pamoja na Kamati kuridhishwa na hatua ya Serikali ya kuanzisha Kitengo cha kuratibu masuala ya Watu wenye Ulemavu nchini ikiwemo kuanzisha Rasmi Baraza la Taifa la kuratibu Masuala ya Kundi hilo kwa ujumla, Kamati inashauri kuwa, Ofisi ya Waziri Mkuu ihakikishe inasimamia kitengo hicho na Baraza husika ili vyombo hivyo vitekeleze majukumu yake kwa weledi mkubwa ikiwa ni pamoja na kuendeleza hatua zake za kutatua migogoro mbalimbali inayoendelea katika Vyama vya Watu wenye Ulemavu nchini.

iii) **Mheshimiwa Spika**, Kamati inaendelea kuishauri Ofisi ya Waziri Mkuu kuwa, kwa kushirikiana na Ofisi ya Rais-Tamisemi, wahakikishe wanaongeza udhibiti wa marejesho ya Mikopo ya Fedha za Mfuko wa Maendeleo ya Vijana ili Mfuko huo uwafikie Vijana wengi zaidi. Hatua hiyo iende sambamba na utoaji wa Elimu kuhusu matumizi bora ya fedha za Mfuko kwa maendeleo yaliyokusudiwa.

FUNGU 61-Tume ya Taifa ya Uchaguzi

- i) **Mheshimiwa Spika**, Pamoja na Kamati kuridhiswa na Utekelezaji wa ushauri wake kuhusu kuboresha Daftari la Wapiga Kura na kwa uangalifu mkubwa, Kamati inaendelea kuishauri Tume ya Taifa ya Uchaguzi kujitahidi kufanya kazi yake kwa Weledi ili kuendelea kuaminika kwa Wadau wake wa Uchaguzi, na hasa kipindi hiki kuelekea Uchaguzi Mkuu wa Mwaka 2020.
- ii) **Mheshimiwa Spika**, Kamati inaendelea kushauri kwamba, Tume ya Taifa ya Uchaguzi ihakikishe inafuatilia wasimamizi wake wa Uchaguzi na kuwawajibisha pale wanapofanya uzembe unaosababisha madhara ambayo yangeweza kudhibitiwa mapema na msimamizi aliye makini na anayetambua na kutekeleza wajibu wake kwa mujibu wa Sheria.
- iii) **Mheshimiwa Spika**, pamoja na Kamati kuridhishwa na jinsi Hazina ilivyotoa kwa wakati Fedha za kuiwezsha Tume ya Uchaguzi kuboresha Daftari la Wapiga kura, bado Kamati inaendelea kuishauri Serikali kuhakikisha inatoa Fedha zinazoidhinishwa na Bunge lako Tukufu kwa Wakati ili kuiwezesha Tume ya Taifa ya Uchaguzi kuratibu masuala mbalimbali ya Uchaguzi kwa ufanisi Mkubwa.

HITIMISHO

Mheshimiwa Spika, napenda kukupongeza kwa kuendelea kuliongoza Bunge hili vema na kwa weledi na umahiri wa hali ya juu. Nikushukuru kwa kunipa nafasi hii ya kuwasilisha Maoni ya Kamati kwa niaba ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Katiba na Sheria.

Mheshimiwa Spika, napenda kumpongeza Naibu Spika Mheshimiwa Tulia Ackson, Mb, kwa weledi na umahiri wake katika kukusaidia kuongoza Bunge. Niwapongeze pia Wenyeviti wa Bunge kwa kazi nzuri wanayoifanya ya kukushauri na kukusaidia kuendesha vikao vya Bunge la Kumi

na Moja. Wote kwa pamoja tunawaombea afya na uzima katika kutekeleza majukumu mliyopewa.

Mheshimiwa Spika, napenda kumpongeza na kumshukuru Waziri wa Nchi Ofisi ya Waziri Mkuu Sera, Bunge, Kazi, Ajira, Vijana, na Watu wenyе Ulemavu, Mhe. Jenista J. Mhagama, (Mb), Waziri wa Nchi (Uwekezaji), Mhe. Angella Kairuki, (Mb), Manaibu Waziri, Mhe. Antony Mavunde, (Mb), na Mhe. Stella Alex Ikupa, (Mb), Makatibu Wakuu na Wataalam wote wa Ofisi ya Waziri Mkuu kwa ushirikiano waliota kwa Kamati wakati wa uchambuzi wa Bajeti ya Ofisi ya Waziri Mkuu.

Mheshimiwa Spika, kwa namna ya pekee napenda kuwashukuru Wajumbe wa Kamati kwa ushirikiano na michango yao mizuri wakati wa kupitia na kuchambua Bajeti ya Ofisi ya Waziri Mkuu, Sera, Bunge, Kazi, Ajira, Vijana, Watu wenyе Ulemavu na Uwekezaji. **Naomba majina yao kama yalivyo katika Taarifa hii yaingie katika Taarifa Rasmi ya Bunge (Hansard):-**

1. Mhe. Mohamed Omary Mchengerwa, Mb - **Mwenyekiti**
2. Mhe. Najma Murtaza Giga, Mb – **Makamu /Mwenyekiti**
3. Mhe. Joseph Kizito Mhagama, Mb-Mjumbe;
4. Mhe. Makame Mashaka Foum, Mb - Mjumbe;
5. Mhe. Asha Abdallah Juma, Mb - Mjumbe;
6. Mhe. Amina Saleh Mollel, Mb - Mjumbe;
7. Mhe. Wanu Hafidh Amer, Mb - Mjumbe;
8. Mhe. Prof. Jumanne Abdallah Maghembe, Mb - Mjumbe;
9. Mhe. Dkt. Mathayo David Mathayo, Mb - Mjumbe;
10. Mhe. Nimrod Elirehemah Mkono, Mb - Mjumbe;
11. Mhe. Susan Peter Maselle, MB - Mjumbe;-
12. Mhe. Alfredina Apilinary Kahigi, Mb - Mjumbe;
13. Mhe. Latifah Hassan Chande,Mb - Mjumbe;
14. Mhe. Ally Abdulla Saleh, Mb - Mjumbe;
15. Mhe. Jacqueline Kandidus Ngonyani Msongozi,Mb-Mjumbe;
16. Mhe. Bupe Nelson Mwakang'ata, Mb - Mjumbe;
17. Mhe. Sixtus Raphael Mapunda, Mb - Mjumbe;
18. Mhe. Hassan Seleman Kaunje, Mb - Mjumbe;
19. Mhe. Yahaya Omary Massare, Mb - Mjumbe;
20. Mhe. Upendo Furaha Peneza, Mb – Mjumbe,

21. Mhe. Emmanuel A.Mwakasaka, Mb - Mjumbe;
22. Mhe. Dkt.Suzan Alphonse Kolimba, Mb - Mjumbe

Mheshimiwa Spika, mwisho, kabisa lakini si kwa umuhimu napenda kumshukuru Katibu wa Bunge, **Ndg. Stephen Kagaigai** kwa kuiwezesha Kamati kukamilisha kazi yake bila kukwama. Aidha, napenda kumshukuru Mkurugenzi wa Kamati za Bunge Ndg. Athuman Hussein, Wakurugenzi Wasaidizi Ndg. Michael Chikokoto na Ndg.Gerald S.Magili, Katibu wa Kamati hii, Ndg. Stanslaus Kagisa, na Msaidizi wa Kamati Ndg. Raheli Masima kwa kuihudumia vyema Kamati pamoja na kukamilisha taarifa hii kwa wakati. Napenda kuwashukuru Makatibu Muhtasi wa Idara ya Kamati za Bunge kwa kuchapa taarifa hii. Napenda pia kuwashukuru Watendaji wote wa Idara na Vitengo husika vya Ofisi ya Bunge, kwa kuhakikisha kwamba Taarifa hii inatoka kwa wakati na kwa ubora.

Mheshimiwa Spika, baada ya maelezo hayo naliomba Bunge lako Tukufu sasa lijadili na kuidhinisha Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Ofisi ya Waziri Mkuu, Sera, Kazi, Ajira, Vijana, Watu wenye Ulemavu na Uwekezaji, kwa Mwaka wa Fedha 2020/2021 kama yalivyowasilishwa na Mtoa Hoja.

Mheshimiwa Spika, naomba kuwasilisha na naunga mkono hoja hii.

Mohamed Omary Mchengerwa, Mb.

MWENYEKITI,

KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA KATIBA NA SHERIA

1 APRILI, 2020

SPIKA: Ahsante sana Mwenyekiti Mheshimiwa Mchengerwa tunakushukuru sana. Sasa moja kwa moja nimkaribishe Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Bajeti, sauti na dakika ni 20. (*Makof*)

MHE. MASHIMBA M. NDAKI- MWENYEKITI WA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA BAJETI: Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana kunipa nafasi ili niweze kutoa maoni ya Kamati kuhusu utekelezaji wa Bajeti ya Mfuko wa Bunge kwa mwaka wa fedha 2019/2020 pamoja na makadirio ya mapato na matumizi kwa mwaka wa fedha 2020/2021.

Mheshimiwa Spika, kwa mujibu wa Kanuni ya 99(9) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la 2016 naomba kuwasilisha taarifa ya kamati ya Kudumu ya Bajeti kuhusu utekelezaji wa Bajeti ya Mfuko wa Bunge kwa mwaka wa fedha 2019/2020 na makadirio ya mapato na matumizi kwa mwaka wa fedha 2020/2021.

Mheshimiwa Spika, kwa mujibu wa kifungu cha 71B cha Sheria ya Bajeti Na. 11 ya mwaka 2015 kamati ilikutana na Mheshimiwa Dkt. Phillip Isdori Mpango, Waziri wa Fedha na Mipango; Mheshimiwa Jenista Joakimu Mhagama, Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu Sera, Bunge, Kazi, Vijana na Wenye Ulemavu pamoja na Katibu wa Bunge ndugu Stephen Kagaigai na kupitia utekelezaji wa Bajeti ya Mfuko wa Bunge kwa mwaka wa fedha 2019/2020 pamoja na kufanya mashauriano kuhusu makadirio ya mapato na matumizi kwa mwaka wa fedha wa 2020/2021.

Mheshimiwa Spika, Taarifa hii inatoa mrejesho kwa Bunge lako tukufu kuhusu utekelezaji wa bajeti na majukumu ya Mfuko wa Bunge hadi kufikia tarehe 15 Machi 2020, pamoja na vipaumbele na masuala muhimu yanayopendekezwa katika mpango wa bajeti kwa mwaka wa fedha 2020/2021.

Mheshimiwa Spika, mapitio ya utekelezaji wa bajeti ya mwaka wa fedha 2019/2020. Katika mwaka wa fedha 2019/2020, Mfuko wa Bunge fungu namba 42 uliidhinishiwa jumla ya kiasi cha shilingi 124,537, 600 kati ya fedha hizo Sh.23,334,462 ni kwa ajili ya mishahara, shilingi 93,238,564 kwa ajili ya matumizi mengineyo na Sh.7,609,511,600 kwa ajili ya mpango wa maendeleo. Kati ya fedha za maendeleo Sh.5,000,000,000 ni fedha za ndani na Sh.2,609,511, 600 ni

fedha za nje. Vilevile Mfuko wa Bunge uliidhinishiwa kukusanya maduhuli ya kiasi cha Sh.54,777,000.

Mheshimiwa Spika, matumizi ya kawaida; hadi kufikia tarehe 15 Machi 2020 mfuko wa Bunge ulikuwa umepokea fedha za matumizi ya kawaida kiasi cha Sh.77,609,331,502 kati ya fedha hizo Sh.62,80,604,202 ni kwa ajili ya matumizi mengineyo sawa na asilimia 66.6 ya bajeti yote na Sh.15,121,576,780 kwa ajili ya mishahara sawa na asilimia 66.5. Kwa ujumla utolewaji wa fedha za matumizi ya kawaida mishahara na *OC* umekuwa mzuri na umewezesha Ofisi ya Bunge na Bunge lako Tukufu kutekeleza majukumu yake vizuri. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, matumizi ya fedha za maendeleo; hadi kufikia tarehe 15 Machi, 2020 kiasi cha Sh.5,233,746,339.35 sawa na asilimia 69 ya fedha zote za maendeleo zilitotengwa kwa mwaka wa 2019/2020 zilikuwa zimepokelewa kwa ajili ya kutekeleza shughuli zilizopangwa ambazo ni sawa na asilimia 68.8. Fedha hizo zilipangwa kutekeleza miradi minne ikiwa ni pamoja na Ukarabati wa Majengo ya Bunge, Ujenzi wa Miundombinu ya Bunge, Mradi wa Kuwajengea Uwezo Wabunge na Watumishi pamoja na Mradi wa Maboresho ya Usimamizi wa Fedha za Umma.

Mheshimiwa Spika, kuhusu maduhuli katika mwaka wa fedha 2019/2020, Mfuko wa Bunge ulidhiinishiwa kukusanya maduhuli ya Sh.54,777,000. Hadi kufikia tarehe 15 Machi 2020 kiasi cha Sh.49,404,550.78 sawa na asilimia 90.2 kilikuwa kimekusanywa. Makusanyo ya maduhuli haya yametokana na kodi ya pango, marejesho ya masurufu pamoja na kuza nyaraka za zabuni. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, sasa nijielekeze kwenye utekelezaji wa shughuli mbalimbali za Bunge. Napenda kuchukua fursa hii kuipongeza Ofisi ya Bunge kwa kutekeleza vyema malengo yake kwa mwaka uliotangulia ikiwa ni pamoja na mipango mizuri waliyojivekea kwa mwaka huu wa fedha. Katika kipindi cha Julai, 2019 hadi terehe 15 Machi, 2020, Mfuko wa Bunge yaani Fungu 42 umefanikisha kutekeleza shughuli mbalimbali

ikiwemo shughuli za kuratibu Bunge, lakini katika kutekeleza shughuli hizo mambo yafuatayo yamefanikiwa:-

Mheshimiwa Spika, Mfuko wa Bunge umeweza kufanikisha kutekeleza shughuli za Bunge kwa kutumia TEHAMA kwa kupitia mfumo wa Bunge Mtandao uliotengenezwa ka kusimamiwa na wataalam wa ndani wa Ofisi ya Bunge wakisaidiana na watalaam wa *eGovernment* kwa sasa Wizara, Idara na Taasisi za Serikali zinawasilisha taarifa na nyaraka mbalimbali Bungeni kwa kutumia nakala tete yaani *softcopy* badala ya nakala ngumu au *hardcopy* kama ilivyokuwa awali. Hatua hii imeweza kupunguza gharama za uendeshaji na hivyo kuokoa Sh.2,000,000,000 kwa upande wa Bunge kilichotarajiwa kutumika kuanzia mwezi Novemba, 2019 hadi Juni, 2020 katika uandaaji na uhifadhi wa nyaraka mbalimbali zinazoandaliwa kwa ajili ya utekelezaji wa shughuli za Bunge. Aidha, kupitia mfumo huu inakadiriwa kuwa kwa kipindi cha mwaka mzima Serikali inaweza kuokoa kiasi cha zaidi ya shilingi bilioni 100. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, kumekuwa pia na uzinduzi kwa Bunge *mobile application* unaowawezesha Waheshimiwa Wabunge pamoja na wadau mbalimbali kupata taarifa mbalimbali za shughuli za Bunge kupitia simu za mkononi kama vile orodha za shughuli za Bunge, (*Order Paper*), *Hansard* pamoja na Sheria na Miswada iliyopitishwa na Bunge; Kuboreshwa kwa mwonekano wa picha urushaji wa matangazo kwa kupitia Bunge Studio kwa kununua vifaa vipyta na vya kisasa vya studio hiyo; Kupandishwa vyeo kwa watumishi 45 na kuwabadilisha kada wengine nane; Kuimarisha ulinzi na usalama katika maeneo ya Bunge kwa Wabunge, watumishi na wageni mbalimbali wanaoingia kwenye maeneo ya Bunge ikiwa ni pamoja na kununua vifaa vipyta vya ulinzi na usalama.

Mheshimiwa Spika, pia Mfuko wa Bunge umekuwa ukipokea fedha kulingana na mpango kazi na maombi yanayowasilishwa Hazina na hivyo kuwezesha kutekeleza majukumu yake ipasavyo; Kushiriki kwenye michezo ya 10 ya Jumuiya ya Afrika Mashariki iliyo fanyika nchini Uganda mwezi

Desemba 2019; timu ya Bunge la Tanzania ilipata ushindi wa pili wa jumla na kupata medali za dhahau tano, medali za fedha 10 na medaliza shaba tatu kwa michezo yote iliyoshiriki. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, nипитie sasa Mfuko wa Bunge kwa Bajeti ya mwaka 2020/2021. Katika mwaka wa fedha 2020/2021, Mfuko wa Bunge unaomba kutengewa jumla ya Sh.121,276,257, kati ya kiasi hicho Sh.23,253,494,000 zimepangwa kwa ajili ya mishahara ya Wabunge na watumishi; Sh.90,314,153,000 zimepangwa kwa ajili ya matumizi mengineyo; na Sh.8,218,610,000 zinaombwa katika mpango wa maendeleo ambapo Sh.5,000,000,000 ni fedha za ndani na Sh. 3,218,610,000 ni fedha za nje. Aidha, hadi kufikia tarehe 30 Juni, 2021 Ofisi imepanga kukusanya maduhuli yenye jumla ya Sh.76,215,500. Maombi haya ya fedha kwa mwaka fedha 2020/2021 yamezingatia mahitaji ya msingi yakiwemo mahitaji ya shughuli za Bunge, Mikutano ya Bunge na Kamati za Bunge na uendeshaji wa Ofisi. Hivyo Mfuko wa Bunge umepanga kutekeleza shughuli za vipaumbele kama ambavyo zimeoneshwa katika taarifa yangu, sitaweza kuzisoma hapa lakini naomba ziingie katika Kumbukumbu zako za Bunge.

Mheshimiwa Spika, sasa niende kwenye maoni ya ushauri wa Kamati. Kuhusiana na Ofisi za Wabunge Majimboni, Kamati bado inaendelea kusisitiza juu ya suala la ujenzi wa Ofisi za Wabunge Majimboni na kuziwekea samani kwa utekelezaji wa majukumu yao kwa ufanisi pindi wanapokuwa Majimboni. Aidha, Kamati inaona kuwa suala la ujenzi wa Ofisi za Wabunge ufanywe kuitia Mfuko wa Bunge na sio suala hili kukasimiwa kwa TAMISEMI. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, la pili, kuhusiana na Bima ya Afya kwa Wabunge baada ya ukomo wa Bunge. Bima za Afya zinatolewa na NHF kwa Waheshimiwa Wabunge zinakoma tarehe 31 Juni, 2020 mara baada ya Bunge kuvunjwa. Hata hivyo kwa mujibu wa Katiba Ubunge hukoma pindi Mbunge mwingine anapoteuliwa, hivyo ni wazi kwamba lazima kuwa na utaratibu wa Waheshimiwa Wabunge kuwa na Bima

katika kipindi cha miezi minne kuanzia Juni hadi Oktoba 2020 pindi Wabunge wapya watakapoapishwa. Hivyo, Kamati inaomba suala hili muhimu lichukuliwe kwa uzito wake na kufanyiwa kazi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, kuhusiana na kuboresha mfumo wa Bunge Mtandao; Kamati inapenda kukupongeza wewe sana na watendaji wa Ofisi ya Bunge kwa kusimamia na kuhakikisha Bunge linaanza kutumia mfumo wa Bunge Mtandao kwa lengo la kuongeza ufanisi. Matunda ya matumizi ya mfumo huu yameanza kuonekana na yameweza kusaidia katika kuendesha shughuli mbalimbali za Bunge hasa kwa kipindi hiki cha mlipuko wa ugonjwa wa *Corona*. Kamati inaishauri Ofisi ya Bunge kuendelea kuboresha mfumo huu ili uweze kuongeza tija zaidi ikiwa ni pamoja na kuweza kutumika nje ya mipaka ya Bunge kwa kuzingatia usalama katika kupakia na kupakua nyaraka mbalimbali za Bunge na Serikali. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, nihitimishe kwa kukushukuru sana wewe, lakini pia Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kutuongoza vyema katika mashauriano kati ya Kamati ya Bajeti na Serikali. Pia naomba kumshukuru Mheshimiwa Dkt. Philip Mpango, Waziri wa Fedha na Mipango; na Mheshimiwa Dkt. Ashatu Kijaji, Naibu Waziri wa Fedha na Mipango kwa ushirikiano wao kwa Kamati. Aidha, kipekee nimshukuru Mheshimiwa Jenista Mhagama, Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu, Sera, Bunge, Kazi, Vijana, Ajira na Wenye Ulemavu kwa kushirikiana na Kamati wakati wa majadiliano kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, napenda kuwashukuru Wajumbe wa Kamati hii kwa umakini wao katika kujadili na kutoa maoni na mapendekezo mbalimbali kuhusu Bajeti ya Mfuko wa Bunge, naomba watambuliwe na *Hansard* kama ambavyo wameandikwa kwenye taarifa yangu hii.

Mheshimiwa Spika, napenda kuchukua fursa hii kumshukuru sana ndugu Stephen Kagaigai Katibu wa Bunge kwa kuiwezesha Kamati kutekeleza majukumu yake ipasavyo.

Aidha, napenda kuipongeza na kuishukuru Sekretarieti ya Kamati ikiongozwa na Mkurugenzi wa Idara ya Bajeti, ndugu Michael Kadebe kwa uratibu na kutoa ushauri wa kitaalam ambaao umesaidia Kamati katika kukamilisha taarifa hii. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, baada ya maelezo hayo naliomba Bunge lako Tukufu sasa lijadili na kuidhinisha makadirio ya mapato na matumizi ya Mfuko wa Bunge - Fungu 42 kwa mwaka wa fedha 2020/2021, kama yalivyowasilishwa na Mheshimiwa Waziri Mkuu. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja na naomba kuwasilisha. (*Makofii*)

**MAONI YA KAMATI KUHUSU UTEKELEZAJI WA BAJETI YA
MFUKO WA BUNGE KWA MWAKA WA FEDHA 2019/20
PAMOJA NA MAKADIRIO YA MAPATO NA MATUMIZI KWA
MWAKA WA FEDHA 2020/21 KAMA YALIVYOWASILISHWA
MEZANI**

1.0. UTANGULIZI

Mheshimiwa Spika, kwa mujibu wa kanuni ya 99(9) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la 2016, naomba kuwasilisha Taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bajeti, kuhusu utekelezaji wa Bajeti ya Mfuko wa Bunge kwa Mwaka wa Fedha 2019/20 na Makadirio ya Mapato na Matumizi kwa Mwaka wa Fedha wa 2020/21.

Mheshimiwa Spika, kwa mujibu wa kifungu cha 71 (b) cha Sheria ya Bajeti Na. 11 ya Mwaka 2015, kamati iilikutana na Mheshimiwa Dkt. Philip Isidor Mpango, Waziri wa Fedha na Mipango, Mhe. Jenista Joackim Mhagama, Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu (Sera, Bunge, kazi, Vijana, Ajira na Wale mavu) pamoja na Katibu wa Bunge Ndg. Stephen Kagaigai na kupitia utekelezaji wa Bajeti ya Mfuko wa Bunge kwa Mwaka wa Fedha 2019/20 pamoja na kufanya mashauriano kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi kwa Mwaka wa Fedha wa 2020/21.

Mheshimiwa Spika, taarifa hii inatoa mrejesho kwa Bunge lako Tukufu kuhusu utekelezaji wa bajeti na majukumu ya Mfuko wa Bunge hadi kufikia tarehe 15 Machi, 2020, pamoja na vipaumbele na masuala muhimu yanayopendekezwa katika Mpango wa Bajeti kwa Mwaka wa fedha 2020/2021.

2.0. MAPITIO YA UTEKELEZAJI WA BAJETI YA MWAKA WA FEDHA 2018/2019

Mheshimiwa Spika, katika kuwezesha Ofisi ya Bunge kutekeleza majukumu yake, Kifungu cha 32 cha Sheria ya Uendeshaji wa Bunge kama iliyofanyiwa rejea mwaka 2015 kilianzisha Mfuko wa Bunge. Hivyo, Mfuko wa Bunge hutengewa fedha kwa ajili ya kugharamia mahitaji mbalimbali, ambapo **asilimia 85** ya mahitaji hayo ya fedha hutumika kugharamia Mikutano ya Bunge, Kamati za Bunge, posho ya Jimbo na usafiri kwa Wabunge, matibabu kwa Wabunge na sehemu iliyobaki **asilimia 15** hutumika kutekeleza shughuli za utawala na uendeshaji.

Mheshimiwa Spika, Ofisi ya Bunge inatekeleza Bajeti yake kwa kuzingatia Sheria ya Bajeti, Sheria ya Usimamizi wa Fedha za Umma pamoja na Mpango Mkakati wa Ofisi ya Bunge (*Strategic Plan 2016-2021*) na Mpango wa Muda wa Kat (Medium Term Expenditure Framework). Utekelezaji wa Bajeti umezingitia malengo yaliyotarajiwa kutekelezwa katika vipindi husika na makisio ya Bajeti yamezingatia kuboresha na kutoa huduma mbali mbali kulingana na mahitaji halisi.

Bajeti ya Mfuko wa Bunge iliyoidhinishwa kwa mwaka 2019/20

Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa fedha 2019/20 Mfuko wa Bunge – Fungu 42 uliidhinishiwa jumla ya kiasi cha **Sh.124,182,537,600.00**. Kat i ya fedha hizo **Sh.23,334,462,000.00** ni kwa ajili ya Mishahara (PE), **Sh.93,238,564,000.00** kwa ajili ya Matumizi Mengineyo (OC) na **Sh.7,609,511,600.00** kwa ajili ya Mpango wa Maendeleo. Kat i ya fedha za Maendeleo **Sh.5,000,000,000.00** ni fedha za ndani na **Sh.2,609,511,600.00** ni fedha za Nje. Vilevile, Mfuko wa Bunge uliidhinishiwa kukusanya maduhuli ya kiasi cha **Sh.54, 777,000. 00**.

Matumizi ya Kawaida

Mheshimiwa Spika, hadi kufikia 15 Machi, 2020 Mfuko wa Bunge ulikuwa umepokea fedha za matumizi ya kawaida kiasi cha **Sh.77,609,331,502**. Kati ya fedha hizo **Sh. Sh.62,080,604,202** ni kwa ajili ya matumizi mengineyo (OC) sawa na **asilimia 66.6** ya bajeti yote na **Sh. 15,121,576,780** kwa ajili ya mishahara (PE) sawa na **asilimia 66.5**.

Mheshimiwa Spika, kwa ujumla utolewaji wa fedha za matumizi ya kawaida (mishahara na OC) umekuwa mzuri na umewezesha Ofisi ya Bunge na Bunge lako Tukufu kutekeleza majukumu yake vizuri.

Matumizi ya Fedha za Maendeleo

Mheshimiwa Spika, hadi kufikia tarehe 15 Machi, 2020 kiasi cha **Sh. 5,233,746,339.35** sawa na **asilimia 69** ya fedha zote za maendeleo zilizotengwa kwa mwaka 2019/2020 zilikuwa zimepokelewa kwa ajili ya kutekeleza shughuli zilizopangwa ambazo ni sawa na **asilimia 68.8**. fedha hizo zilipangwa kutekeleza miradi minne ikiwa ni pamoja na ukarabati wa Majengo ya Bunge, Ujenzi wa Miundombinu ya Bunge, Mradi wa kujengea uwezo Wabunge na Watumishi (LSP) pamoja na Mradi wa Maboresho ya Usimamizi wa Fedha za Umma (PFMRP).

Maduhuli

Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa fedha 2019/20 Mfuko wa Bunge uliidihiishiwa kukusanya maduhuli ya **Sh. 54,777,000. 00**, hadi kufikia tarehe 15 Machi, 2020 kiasi cha **Sh.49,404,550.78** sawa na **asilimia 90.2** kimekusanywa. Makusanyo ya maduhuli haya yametokana na kodi ya pango, marejesho ya masurufu pamoja na kuuza nyaraka za zabuni.

UTEKELEZAJI WA MAJUKUMU YA MFUKO WA BUNGE KWA MWAKA WA FEDHA 2019/20.

Utekelezaji wa shughuli mbalimbali za Bunge

Mheshimiwa Spika, napenda kuchukua fursa hii kuipongeza Ofisi ya Bunge kwa kutekeleza vyema malengo yake kwa

mwaka uliotangulia ikiwa ni pamoja na mipango mizuri waliyojiwekea kwa mwaka huu wa Fedha.

Mheshimiwa Spika, katika kipindi cha Julai, 2019 hadi tarehe 15 Machi, 2020 Mfuko wa Bunge (Fungu – 42) umefanikisha kutekeleza shughuli mbalimbali ukiwemo uratibu wa shughuli za Bunge kama ifuatavyo:-

- i) Kuimarisha utendaji wa Bunge kwa kutumia mfumo wa Bunge Mtandao (*e-Parliament*) na hivyo kuongeza ufanisi wa Bunge katika kusimamia utekelezaji wa shughuli za Serikali;
- ii) Kuratibu na kusimamia shughuli za Mikutano Mitatu ya Bunge (16,17 na 18) na Mikutano Mitatu ya Kamati;
- iii) Kutoa ushauri wa Kisheria kwa Wabunge na uchambuzi wa Miswada;
- iv) Kuratibu, kuchapisha na kutunza Taarifa Rasmi za Bunge (Hansard) pamoja na nyaraka mbalimbali za Bunge na Serikali;
- v) Kugharamia malipo ya stahili za Wabunge (Posho ya Jimbo na usafiri) pamoja na matibabu ya Wabunge na familia zao;
- vi) Kuratibu shughuli za Ofisi za Viongozi, Tume ya Utumishi wa Bunge na Utawala;
- vii) Kutoa huduma mbalimbali za Utafiti kwa Wabunge zinazohusiana na masuala ya kiuchumi, kisiasa na kijamii;
- viii) Kutolewa kwa mafunzo mbalimbali kwa Wabunge na Watumishi;
- ix) Kuratibu stahili za Watumishi;
- x) Kuwezesha ushiriki wa Bunge katika Mikutano ya Kimataifa ambayo Bunge ni mwanachama ambayo ni SADC PF, PAP, CPA, Great Lakes, IPU, ACP-EU;

- xi) Kuwezesha Wabunge kushiriki mashindano ya michezo kwa Mabunge ya Jumuiya ya Afrika mashariki;
- xii) Kuratibu kazi ya utoaji wa habari kwa wananchi kuhusu shughuli za Kamati na Bunge pamoja na kutoa elimu kwa umma kwa wadau na wageni walitembelea Bunge;
- xiii) Kuandaa vipindi vyta Televisheni na kurusha matangazo ya Bunge;
- xiv) Ukarabati wa Majengo ya Ofisi pamoja na Ujenzi wa Makazi ya Viongozi ambapo hadi kufikia tarehe 15 Machi 2020, Mfuko wa Bunge (Fungu – 42) umeweza kusimamia na kuratibu kazi zifuatazo:-
 - Uboreshaji wa Majengo ya Ofisi.
 - Uboreshaji wa Ukumbi wa Bunge.
 - Ujenzi wa Nyumba za Viongozi.
- xv) Usimamizi wa matumizi ya fedha zilizokasimiwa kwenye Mfuko wa Bunge ulifanyika kwa kuzingatia Sheria ya Bajeti, Sheria ya Fedha za Umma na Sheria ya Manunuvi ya Umma; na

Mafanikio ya Utekelezaji

Mheshimiwa Spika, Mfuko wa Bunge umeweza kufanikisha yafuatayo:-

- a) Kutekeleza shughuli za Bunge kwa kutumia TEHAMA kuitia mfumo wa Bunge Mtando (e-Parliament) uliotengenezwa na kusimamiwa na wataalamu wa ndani wa Ofisi ya Bunge wakisaidiana na Wataalamu wa e-Government (e-Ga). Kwa, sasa Wizara, Idara na Taasisi za Serikali zinawasilisha taarifa na nyaraka mbalimbali Bungeni kwa kutumia nakala tete (*Softcopy*) badala ya nakala ngumu (*Hard copy*) kama ilivyokuwa awali. Hatua hii imeweza kupunguza gharama za uendeshaji na hivyo kuokoa shilingi bilioni 2 kwa upande wa

Bunge kilichotarajiwa kutumika kuanzia Mwezi Novemba 2019 hadi Juni 2020 katika uandaaji na uhifadhi wa nyaraka mbalimbali zinazoandaliwa kwa ajili ya utekelezaji wa shughuli za Bunge. Aidha, kupitia mfumo huu inakadirisha kuwa, kwa kipindi cha Mwaka mzima, Serikali inaweza kuokoa kiasi cha zaidi shilingi bilioni 100.

- b) Kuzinduliwa kwa „Bunge Mobile Application’ unaowezesha Waheshimiwa Wabunge pamoja na wadau mbalimbali kupata taarifa mbalimbali za shughuli za Bunge kupitia simu za mkononi kama vile orodha ya shughuli za Bunge (order paper), *hansard* pamoja na sheria na miswada iliyopitishwa na Bunge;
- c) Kuboresha kwa muonekano wa picha na urushaji wa matangazo kupitia Bunge studio kwa kununua vifaa vipyta na vya kisasa vya studio hiyo;
- d) Kupandishwa vyeo kwa watumishi arobaini na tano (45) na kuwabadilisha kada watumishi nane (8);
- e) Kuimarisha ulinzi na usalama katika maeneo ya Bunge, kwa Wabunge, watumishi na wageni mbalimbali wanaoingia kwenye maeneo ya Bunge ikiwa ni pamoja na kununua vifaa vipyta vya ulinzi na usalama;
- f) Mfuko wa Bunge umekuwa ukipokea fedha kulingana na Mpango Kazi na maombi yanayowasilishwa Hazina na hivyo kuweza kutekeleza majukumu yake ipasavyo.
- g) Kushiriki kwenye Michezo ya Kumi (10) ya Jumuiya ya Afrika Mashariki iliyofanyika nchini Uganda Mwezi Disemba 2019. Timu ya Bunge la Tanzania ilipata ushindi wa pili wa Jumla na kupata Medali za Dhahabu Tano (5), Medali za Fedha Kumi (10) na Medali za Shaba Tatu (3) kwa michezo yote iliyoshiriki.

MAKADIRIO YA MAPATO NA MATUMIZI YA MFUKO WA BUNGE KWA MWAKA WA FEDHA 2020/21

Bajeti ya Mfuko wa Bunge kwa Mwaka wa Fedha 2020/21

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka wa fedha 2020/21 Mfuko wa Bunge unaomba kutengewa jumla ya **Sh. 121,786,257,000**. Kati ya kiasi hicho, **Sh. 23,253,494,000.00** zimepangwa kwa ajili ya Mishahara ya Wabunge na Watumishi, **Sh. 90,314,153,000.00** zimepangwa kwa ajili ya matumizi mengineyo na **Sh. 8,218,610,000.00** zinaombwa katika Mpango wa Maendeleo ambapo **Sh. 5,000,000,000.00** ni fedha za ndani na **Sh. 3,218,610,000.00** ni fedha za nje. Aidha, hadi kufikia Juni 30, 2021 Ofisi imepanga kukusanya maduhuli yenye jumla ya **Sh. 76,215,500**.

Mheshimiwa Spika, maombi haya ya fedha kwa mwaka wa fedha 2020/21 yamezingatia mahitaji ya msingi yakiwemo mahitaji ya shughuli za Bunge (Mikutano ya Bunge na Kamati za Bunge) na uendeshaji wa Ofisi. Hivyo, Mfuko wa Bunge umepanga kutekeleza shughuli za vipaumbele kama ifuatavyo: -

- a) Kuratibu na kusimamia shughuli za Mikutano wa Bajeti (1) na Mikutano Midogo Miwili (2) ya Bunge;
- b) Kuratibu na kusimamia shughuli za Mikutano mitatu (3) ya Kamati za Kudumu za Bunge ambayo ni Mikutano Mmoja wa Kamati kuhusu uchambuzi wa bajeti na Mikutano Midogo Miwili (2);
- c) Kuwezesha shughuli za Wabunge katika majimbo na maeneo yao ya uwakilishi;
- d) Kuratibu na kuchapisha Taarifa Rasmi za Bunge (*Hansard*) pamoja na nyaraka mbalimbali za Bunge na Serikali;
- e) Kutoa ushauri wa kisheria kwa Wabunge na uchambuzi wa miswada;

- f) Kutoa huduma za Utafiti kwa Wabunge ("Information Research") pamoja na kukamilisha mfumo wa kidijitali wa Maktaba;
- g) Kuratibu na kusimamia kazi na majukumu ya Tume ya Utumishi wa Bunge.
- h) Kuwezesha Wabunge kushiriki kwenye baadhi ya Mikutano ya Kimataifa kama vile Mikutano ya Bunge la Afrika (PAP), Umoja wa Wabunge wa Jumuiya ya Madola (CPA) Kanda ya Afrika, CPA- International, Africa Caribbean Pacific and European Union (ACP/EU) na Jukwaa la Kibunge la Jumuiya ya Nchi za Kusini mwa Afrika (\$ADC- PF), Bunge la Afrika Mashariki na Umoja wa Mabunge Duniani (IPU);
- i) Kuandaa vipindi vyta televisheni na kurusha matangazo ya Bunge;
- j) Kuratibu utoaji wa habari kwa wananchi kuhusu shughuli za Bunge na Kamati;
- k) Kuratibu ushiriki wa Wabunge kwenye vikao vyta Kamati na Bunge kwa kuwawezesha malipo ya posho na stahiki zao (Posho ya Jimbo, vikao, kujikimu na usafiri);
- l) Kuratibu shughuli mbalimbali za kiutawala (huduma kwa Wabunge, ununuzi wa vifaa vyta Ofisi, malipo ya maji, umeme na simu, usafi na ulinzi);
- m) Kuwezesha matibabu ya Waheshimiwa Wabunge ndani na nje ya nchi;
- n) Kuwezesha Watumishi kushiriki mafunzo ya muda mfupi na mrefu ndani na nje ya nchi;
- o) Kuwajengea Wabunge uwezo ili waweze kutekeleza majukumu yao kikatiba;
- p) Kusimamia uendeshaji wa Ukumbi wa Bunge, mitambo na mashine;

q) Kuratibu kazi ya kukarabati Jengo la ukumbi wa Bunge na majengo ya Ofisi ya Bunge pamoja na ujenzi wa nyumba ya Makazi ya Viongozi; na

r) Kugharamia maandalizi ya Bunge la Kumi na mbili (12).

MAONI NA USHAURI WA KAMATI

Ofisi za Wabunge Majimboni

Mheshimiwa Spika, kamati bado inaendelea kusisitizia juu ya suala la ujenzi wa Ofisi za Wabunge majimboni na kuziwekea samani kwa utekelezaji wa majukumu yao kwa ufanisi pindi wanapokuwa majimboni. Aidha, Kamati inaona kuwa suala la ujenzi wa Ofisi za Wabunge ufanywe kupitia Mfuko wa Bunge na sio suala hili kukasimiwa kwa TAMISEMI;

Bima ya Afya kwa Wabunge baada ya ukomo wa Bunge.

Mheshimiwa Spika, bima za afya zinazotolewa na NHIF kwa Waheshimiwa wabunge zinakoma tarehe 31 Juni, 2020 mara baada ya Bunge kuvunjwa. Hata hivyo, kwa Mujibu wa Katiba Ubunge hukoma pindi mbunge mwingine anapoteuliwa. Hivyo ni wazi kwamba lazima kuwe na utaratibu wa waheshimiwa wabunge kuwa na bima katika kipindi cha miezi minne kuanzia Juni hadi Oktoba 2020 pindi wabunge wapya watakapoapishwa. Hivyo, Kamati inaomba suala hili muhimu lichukuliwe kwa uzito wake na kufanyiwa kazi.

Kuboresha mfumo wa Bunge Mtandao (*e-Parliament*).

Mheshimiwa Spika, Kamati inapenda kukupongeza wewe binafsi na watendaji wa Ofisi ya Bunge kwa kusimamia na kuhakikisha Bunge linaanza kutumia mfumo wa Bunge Mtandao kwa lengo la kuongeza ufanisi. Matunda ya matumizi ya Mfumo huu yameanza kuonekana na yameweza kusaidia katika kuendesha shughuli mbalimbali za Bunge hasa kwa kipindi hiki cha mripuko wa ugonjwa wa Corona. Aidha, Kamati inashauri Ofisi ya Bunge kuendelea

kuboresha mfumo huu ili uweze kuongeza tija zaidi ikiwa pamoja na kuweza kutumika nje ya mipaka ya Bunge kwa kuzingatia usalama katika kupakia na kupakua nyaraka mbalimbali za Bunge na Serikali.

HITIMISHO

Mheshimiwa Spika, naomba nihitimishe kwa kukushukuru wewe Mheshimiwa Spika na Naibu Spika kwa kuongoza vema mashauriano kati ya Kamati ya Bajeti na Serikali. Pia naomba kumshukuru Mheshimiwa Dkt. Philip Mpango (Mb), Waziri wa Fedha na Mipango na Mheshimiwa Dkt. Ashatu Kijaji, Naibu Waziri wa Fedha na Mipango kwa ushirikiano wao kwa Kamati. Aidha, kipekee nimshukuru Mheshimiwa Jenista Mhagama, Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu (Sera, Bunge, Kazi, Vijana, Ajira na Watu wenye Ulemavu) kwa kushirikiana na Kamati wakati wa majadiliano kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu.

Mheshimiwa Spika, napenda kuwashukuru wajumbe wa Kamati hii kwa umakini wao katika kujadili na kutoa maoni na mapendekezo mbalimbali kuhusu Bajeti ya Mfuko wa Bunge. Naomba kuwatambua wajumbe hao kama ifuatavyo;

- 1) Mhe. Mashimba Mashauri Ndaki, Mb – M/Mwenyekiti
- 2) Mhe. David Ernest Silinde, Mb
- 3) Mhe. Mbaraka Kitwana Dau, Mb
- 4) Mhe. Mendorad Lutengano Kigola, Mb
- 5) Mhe. Maria Ndilla Kangoye, Mb
- 6) Mhe. Dkt. Immaculate Swale Semesi, Mb
- 7) Mhe. Ali Hassan Omar, Mb
- 8) Mhe. Freeman Aikael Mbowe, Mb
- 9) Mhe. Martha Jachi Umbulla, Mb
- 10) Mhe. Makame Kassim Makame, Mb
- 11)Mhe. Dkt. Dalaly Peter Kafumu, Mb
- 12) Mhe. Albert Obama Ntabaliba, Mb
- 13) Mhe. Oran Manase Njeza, Mb
- 14)Mhe. Riziki Said Lulida, Mb
- 15) Mhe. Hasna Sadi Katunda Mwilima, Mb

- 16) Mhe. Balozi Adadi Mohamed Rajabu, Mb
- 17) Mhe. Abdallah Majurah Bulembo, Mb
- 18) Mhe. Prof. Anna Kajumulo Tibaijuka, Mb
- 19) Mhe. Stephen Julius Masele, Mb
- 20) Mhe. Marwa Ryoba Chacha, Mb
- 21) Mhe. Balozi Diodorus Buberwa Kamala, Mb
- 22) Mhe. Joseph George Kakunda, Mb
- 23) Mhe. John Kibera Kishimba, Mb
- 24) Mhe. Andrew John Chenge, Mb
- 25) Mhe. Shally Josepha Raymond, Mb
- 26) Mhe. Suleiman Ahmed Saddiq, Mb
- 27) Mhe. Dkt. Raphael Masunga Chegeni, Mb

Mheshimiwa Spika, napenda kuchukua fursa hii, kumshukuru Ndg. Stephen Kagaigai, Katibu wa Bunge kwa kuiwezesha Kamati kutekeleza majukumu yake ipasavyo. Aidha, napenda kuipongeza na kuishukuru Sekretarieti ya Kamati ikiongozwa na Mkurugenzi wa Idara ya Bajeti Ndugu Michael Kadebe kwa kuratibu na kutoa ushauri wa kitaalamu ambao umesaidia Kamati katika kukamilisha taarifa hii.

Mheshimiwa Spika, baada ya maelezo hayo naliomba Bunge lako tukufu sasa lijadili na kuidhinisha Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Mfuko wa Bunge – Fungu 42, kwa Mwaka wa Fedha 2020/21 kama yalivyowasilishwa na Mheshimiwa Waziri Mkuu.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja na naomba kuwasilisha.

Mashimba M. Ndaki, Mb
M/MWENYEKITI
KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA BAJETI

01 APRILI, 2020

SPIKA: Ahsante sana Mwenyekiti wa Kamati ya Bajeti, tunakushukuru sana na tunaendelea kuipongeza Kamati yetu

ya Bajeti na kuipa moyo kwa sababu ndio mwanzo wa kazi sasa, kazi yenu ni kubwa sana mpaka kipindi hiki kiishe mtakuwa mmetufanya kazi nzuri. Kwa hiyo tunawashukuru sana. Sasa nimuite Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Masuala ya UKIMWI, 20 minutes (*Makofi*)

MHE. OSCAR R. MUKASA – MWENYEKITI WA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA MASUALA YA UKIMWI: Mheshimiwa Spika, ahaa *sorry*.

SPIKA: Mheshimiwa Mwenyekiti, karibu sana, Mheshimiwa Mukasa.

MHE. OSCAR R. MUKASA – MWENYEKITI WA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA MASUALA YA UKIMWI: Mheshimiwa Spika, ahsante sana kwa mujibu wa Kanuni za Bunge zinazohusika, naomba kuwasisha taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Masuala ya UKIMWI kuhusu utekelezaji wa Bajeti ya Mamlaka ya Kudhibiti Na Kupambana Na Dawa Za Kulevyta - Fungu 91 na Tume ya Kudhibiti UKIMWI (*Tanzania TACA/DS*) - Fungu 92 kwa mwaka wa fedha 2019/2020 pamoja na maoni ya Kamati kuhusu makadirio ya mapato na matumizi ya mafungi hayo kwa mwaka wa fedha 2020/2021.

Mheshimiwa Spika, awali ya yote napenda kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutupa nafasi ya kukutana hapa leo na kuendelea kutulinda na dhoruba inayoendelea kote duniani. Pia napenda kuwashukuru Ndugu Happiness Ndalua na Ndugu Asia Msangi, Makatibu wa Kamati kwa kuratibu vyema kazi za Kamati na kuhakikisha taarifa hii inakamilika kwa wakati. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, pia napenda kuwashukuru watumishi wa Bunge wakiongozwa na Ndugu Stephen Kagaigai, Katibu wa Bunge; Ndugu Michael Chikokoto. Mkurugenzi wa Idara za Kamati za Huduma; na ndugu Gerald Magiri, Mkurugenzi Msaidizi; Wajumbe wa Kamati ya Masuala ya UKIMWI nawashukuru sana kwa sababu wamefanya kazi kubwa sana kwa kipindi chote na kwa uaminifu; Mheshimiwa Tisekwa, Makamu Mwenyekiti wa Kamati; lakini napenda

kuwashukuru Dkt. Maboko na Dkt. James Kaji ambao ni Viongozi wa hizi Tume za TACAIDS na Mamlaka ya Madawa ya Kulevyia kwa kazi nzuri. Kwa namna ya pekee Mawaziri husika wa shughuli yetu a mbaao ni Mheshimiwa Jenista akisaidiwa na Mheshimiwa Mavunde na Mheshimiwa Ikupa; Mheshimiwa Ummy, Waziri wa Afya na Mheshimiwa Ndugulile, Naibu Waziri, Makatibu Wakuu Dkt. Chaula na Ndugu Tickson tunawashukuru sana kwa kazi nzuri iliyotukuka kwa kukusaidia wewe kufanya kazi ya kutuongoza vizuri. Hata hivyo, kwa namna ya pekee namshukuru Mheshimiwa Spika kwa ulezi wa Kamati yetu kama unavyofanya kwa kamati nytingine. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, kwa namna ya pekee, niwashukuru Mawaziri wahusika wa shughuli yetu ambaao ni Mheshimiwa Jenista akisaidiwa na Mheshimiwa Mavunde na Mheshimiwa Ikupa; Mheshimiwa Ummy, Waziri wa Afya na Mheshimiwa Ndugulile, Naibu Waziri; Makatibu Wakuu, Dkt. Chaula na Ndugu Tixon. Tunawashukuru sana kwa nzuri iliyotukuka.

Mheshimiwa Spika, nakushukuru wewe kwa kutuongoza vizuri. Kwa namna ya pekee nakushukuru kwa ulezi wa Kamati yetu kama anavyofanya kwa Kamati nytingine. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, kwa sababu nitasoma muhtasari tu wa ripoti yetu, naomba ridhaa yako, taarifa hii iingie kwenye Taarifa Rasmi za Bunge yaani *Hansard* kwa ujumla wake kama ilivyowasilishwa hapo awali.

Mheshimiwa Spika, nachukua nafasi hii pia kuliomba Bunge lako Tukufu likubali kuidhinisha Makadirio ya Matumizi ya Tume ya Kudhibiti UKIMWI Tanzania, Fungu 92 jumla ya shilingi bilioni 7.6 na Fungu 91 ambaloni Mamlaka ya Kudhibiti Madawa ya Kulevyia, jumla ya shilingi bilioni 9.03. Tunaomba makadirio haya yaidhinishwe kwa sababu kiujumla tunaridhika na kazi nzuri iliyofanywa na tunapongeza mapendekezo yaliyowekwa kwa mwaka unaofuata ingawa

kuna maeneo ya kurekebisha ambayo tutayataja wakati tunatoa maoni yetu. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, naomba kuwasilisha maoni, ushauri na mapendekezo ya Kamati baada ya kuzingatia shughuli zote, kufanya uchambuzi na kuona ni maeneo gani yanahitaji kuboreshwa na maeneo gani Serikali inastahili kupon gezwa.

Mheshimiwa Spika, eneo la kwanza ni upatikanaji wa fedha za ndani kwa ajili ya afua za UKIMWI. Mpaka sasa kwa kiwango kikubwa bajeti ya kutekeleza Miradi ya Maendeleo kwa *TACAIDS* inategemea fedha za wahisani. Kwa mfano kwa mwaka 2019/2020, Serikali ilitenga jumla ya shilingi bilioni 2 lakini mpaka sasa fungu hilo halijaweza kupatiwa fedha yoyote.

Mheshimiwa Spika, fedha za wahisani zinaendelea kupungua na muelekeo tunaonaa. Kwa mfano, kwa mwaka 2019/2020 wenzetu wa Serikali ya Marekani ambao walikuwa wanashughulika kwa kiwango kikubwa na muitikio wa UKIMWI kwa sababu za kutofautiana mambo fulani kisera, walipunguza kiasi cha asilimia 23 ya bajeti ambayo wanaleta kwenye muitikio huo ambapo ni takribani shilingi bilioni 282. Hiki ni kiashiria kwamba ni wakati sasa sisi kuanza kujipanga. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, Mfuko wa ATF. Kwa mujibu wa sharia, Mfuko huu ulianzishwa na Bunge mwaka 2015. Tunaipongeza Serikali kwa kazi hiyo lakini mpaka sasa haujawa na chanzo mahsusni na endelevu ambacho kinaweza kuufanya uweze kusimama wenyewe ili na sisi kama Watanzania tuanze kupunguza utegemezi wa muitikio wa UKIMWI kutoka kwa wahisani.

Mheshimiwa Spika, kuna umuhimu mkubwa wa kuimarisha ukusanyaji, uhifadhi na matumizi ya takwimu mbalimbali kwenye shughuli zote za mwitikio wa UKIMWI. Utekelezaji wa afua mbalimbali za UKIMWI unategemea sana ubora wa takwimu zinazopatikana kutoka katika vyanzo

mbalimbali. Kwa mujibu wa shughuli tulizozifanya za ukaguzi na uchambuzi, kuna upungufu mkubwa sana katika ukusanyaji, uhifadhi na matumizi ya takwimu mbalimbali zinazohusiana na mapambano dhidi ya UKIMWI. Kamati inashauri Serikali kupitia *TACA/IDS*, Wizara ya Afya, TAMISEMI na Mamlaka watafute namna ya kufanya kujenga uwezo wa Halmashauri zetu na vituo vya afya katika eneo hilo la matumizi ya takwimu kwa ajili ya kuongoza shughuli zetu za mapambano dhidi ya UKIMWI.

Mheshimiwa Spika, ipo mifano kuna Halmashauri moja tulishuhudia, ripoti inatolewa kabisa inasema maambukizi ya UKIMWI mionganoni mwa wanawake ni asilimia 63 jambo ambalo ukisikia tu dunia nzima inaweza kuja hapa Tanzania kuangalia nini kinaendelea. Hata hivyo, hali halisi siyo hivyo ni kwa sababu tu kuna upungufu wa namna gani wa kuelewa na kuandaa takwimu kwa ajili ya mapambano dhidi ya UKIMWI. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, Kamati pia ilipata hoja mahsusini ambayo inaiona kwamba ni kubwa ni msongamano wa wafungwa kwenye Magereza ambapo una mahusiano makubwa na maambukizi ya kifua kikuu. Magereza mengi nchini yana msongamano mkubwa sana na hivyo kuwa na uwezekano mkubwa wa maambukizi ya kifua kikuu.

Mheshimiwa Spika, katika uchambuzi wa Kamati, moja ya sababu ya uwepo wa msongamano mkubwa ni Jeshi la Magereza kupewa majukumu ambayo yapo nje zaidi ya mamlaka yake kisheria. Sehemu kubwa ya watu walio kwenye Magereza ni mahabusu kuliko wafungwa ambao ndiyo kisheria ni wajibu wa Jeshi la Magereza. Kwa mujibu wa uchambuzi inaonekana kwamba kazi hii ya kutunza mahabusu ikipelekwa kwa Polisi wenyewe kutakuwa na ongezeko la uangalifu wa Jeshi la Polisi la kuchuja ni watu wapi hasa wanastahili kuingia mahabusu kuliko ambavyo sasa wengine baadhi wanafika kule bila sababu za msingi sana. Kama wakiona jukumu la kubeba mahabusu ni la kwao basi watafanya kazi ya kuchuja na kupeleka wale tu ambao kwa kweli wanahitaji kuwa kwenye mahabusu. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, yapo mambo mtambuka mawili ambayo Kamati inapenda kuyasemea ambayo tuliyaona kwenye Jeshi la Magereza la Mkoani Kilimanjaro. Moja, Kamati inadhani matumizi ya rasilimali zinazozalishwa kwenye Magereza yetu kwa namna fulani zinahitaji kuboreshwa. Kwa mfano, Gereza la Kisonga-Arusha linazalisha mahindi, linamuuzia mfanyabiashara gunia moja Sh.100,000 lakini kwa sababu ya mchakato wa zabuni, mfanyabiashara huyo huyo anakuja kuliuzia gereza hilo mzigo ule uliouzwa kwake kwa Sh.100,000 kwa Sh.200,000 yaani mara mbili. Kwa hiyo, ni mchezo fulani unaoendelea, sawa tunafuata utaratibu lakini hautupatii tija.

Mheshimiwa Spika, kuna tatizo tunalitoa kama mfano la Hospitali ya Mkoa ya Mawenzi haina Mganga Bingwa wa Watoto lakini kwenye Mkoa huo huo kuna Kituo cha Afya kuna Mganga Bingwa wa Watoto. Kwa hiyo, Mganga Bingwa yuko Kituo cha Afya anatoa rufaa kutoka Kituo cha Afya kwenda Hospitali ya Mkoa ambayo haina Mganga Bingwa lakini ni Mkoa uleule ambapo Wizara na mamlaka husika wanaweza kuzungumza wakarekebisha jambo hilo.

Mheshimiwa Spika...

SPIKA: Hebu Mwenyekiti rudia hapo.

MHE. OSCAR R. MUKASA – MWENYEKITI WA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA MASUALA YA UKIMWI: Mheshimiwa Spika, Mawenzi Hospitali ni Hospitali ya Mkoa na ya Rufaa kwa ngazi ya Mkoa, haina Daktari Bingwa wa Magonjwa ya Watoto lakini kwenye Mkoa huo huo wa Kilimanjaro, Wilaya ya Hai kuna Daktari Bingwa wa Magonjwa ya Watoto yuko kwenye Kituo cha Afya kwenye Wilaya ya Hai. Sasa watoto wanaopewa rufaa kutoka kokote kule kwenda Mkoani hawapati huduma za kibingwa Mkoani lakini bingwa huyo naye aliyeko kwenye Kituo cha Afya naye anashiriki kupeleka rufaa Mkoani ambako hakuna bingwa. (*Kicheko*)

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, ni kazi tu ya mamlaka husika kushauriana pale na kuweka vizuri mambo yakaisha

na hakuna rasilimali pesa inayohitajika kwenda pale. Kwa hiyo, ni mifano michache tumeiweka mambo ambayo Serikali inapaswa kuyaangalia kwa namna ambayo wala hatuhitaji kutumia rasilimali fedha ni kujipanga tu lakini mambo yanakaa vizuri.

Mheshimiwa Spika, Mamlaka ya Kudhibiti na Kupambana na Dawa za Kulevy haitengewi bajeti ya miradi ya maendeleo kwa muda mrefu sana. Ni maoni ya Kamati kwamba kuweka pesa za shughuli za kila siku kwenye Mamlaka bila kuweka fedha za maendeleo itakuwa haileti tija kwenye fedha hizo tunazozitumia kwenye shughuli za kila siku. Maana yake tutakuwa tunafanya shughuli za zimamoto lakini shughuli za uendelevu wa kudhibiti mambo ya *harm reduction, demand reduction* na *supply reduction* kimkakati haitafikia mwisho kwa sababu tunashughulika na mambo ya kuzima moto badala ya kushughulika na mambo ya kuzuia mambo hayo kimkakati.

Mheshimiwa Spika, moja ya mfano kwa nini Mamlaka ile inaathirika kwa kutopewa fedha ya maendeleo ni kukosa maabara yake kwa ajili ya uchunguzi. Inategemea Maabara ya Mkemia Mkuu ambayo sawa nayo ni ya Serikali hakuna shida lakini Maabara ile imezidiwa na kazi nyininge nydingi tofauti na kazi za Mamlaka ambazo zinahitaji umahsusii fulani na uharaka wa kushughulikiwa. Kwa hiyo, ni mapendekezo ya Kamati kwamba Mamlaka hii ya Kupambana na Madawa ya Kulevy ianze kuwekewa fedha za maendeleo ili jambo hili tupambane nalo kimkakati zaidi kuliko kushughulika na jambo moja moja kwa wakati mchache mchache.

Mheshimiwa Spika, kuna umuhimu wa kuongeza mkakati wa ushirikishwaji wa asasi za kiraia katika mapambano dhidi ya dawa za kulevy. Tunaipongeza sana Serikali, imefanya mtandao mzuri sana wa asasi za kiraia za kuwaibua waraibu majumbani mwao na wao kuwa ndiyo daraja la kuwaleta kwenye vyombo husika kwa ajili ya kushughulika na *harm reduction* lakini mtandao huo ni mdogo, hautoshi. Ni maoni ya Kamati kwamba mtandao huo

ukiongezeka na ukawekewa mfumo wa kufanya kazi vizuri tija kubwa itaonekana zaidi.

Mheshimiwa Spika, Kamati inaipongeza Serikali kwa hatua ya kuanzisha *Methadone Centers na Sobber Houses* na kuratibu zile ambazo ziko kwenye sekta binafsi. Kamati inaipongeza Serikali kwa kuwa na mpango wa kuongeza *Sobber Houses* kwenye Mikoa ya Tanga, Pwani, Morogoro, Dodoma, Arusha na Kilimanjaro. Hata hivyo, Kamati inasisitiza umuhimu wa Serikali kutekeleza mpango huo kwa wakati. Jambo hili lina tija sana kwa sababu kwa mujibu wa wataalam, mraibu ambaye amekaa muda wa kutosha kwenye matumizi ya madawa ya kulevyaa aina ya *heroin* analazimika kutumia dawa ya aina hiyo yenye thamani ya Sh. 21,000 kwa siku. Kwa sababu mpaka sasa kwenye *Sobber Houses* zetu tuna waraibu 7,300 na kitu, jumla ya mzunguko wa billioni 55 kama hutahudumia hawa waraibu wakaondoka kwenye matumizi ya dawa zitazunguka kwenye matumizi ya dawa hiyo na huu ni uchumi mkubwa ambao unakwenda kwenye mzunguko wa mambo yasiyo na tija kwa Taifa badala ya kuzifanya zizunguke sehemu yenye tija.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, tunaipongeza Serikali kwa kuwa na mpango wa kuanzisha vituo hivyo lakini tunasisitiza ifanyike kwa wakati muafaka ili kuokoa fedha hizi ambazo zinazunguka kwenye mambo yasiyo na tija ili zikazunguke kwenye uchumi wenyewe faida kwa Taifa hili.

Mheshimiwa Spika, kuna umuhimu wa suala ya madawa ya kulevyaa kuwa ajenda ya Kamati ya UKIMWI katika ngazi ya Halmashauri na Manispaa. Jambo hili limeleta tija sana upande wa UKIMWI kuna namna ambavyo mwitikio wa UKIMWI unaratibiwa vizuri kwenye ngazi ya Halmashauri lakini mapambano dhidi ya madawa ya kulevyaa kwa nyanja zake zote tatu bado yako ngazi ya Kitaifa zaidi na hakuna mfumo unaokwenda chini kule kwenda kushirikisha umma kwa ngazi ya Halmashauri ili mwitikio mzuri tunaouona upande wa UKIMWI ufanane na upande wa madawa ya kulevyaa kwenye ngazi za Halmashauri na jamii. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, naomba kuwasilisha na naunga mkono hoja. (*Makofi*)

**MAONI YA KAMATI KUHUSU UTEKELEZAJI WA BAJETI YA OFISI
YA WAZIRI MKUU TUME YA KUDHIBITI UKIMWI TANZANIA NA
MAMLAKA YA KUDHIBITI NA KUPAMBANA NA DAWA ZA
KULEVYA KWA MWAKA WA FEDHA 2019/2020 NA MAKADIRIO
YA MATUMIZI KWA MWAKA WA FEDHA 2020/2021 KAMA
YALIVYOWASILISHWA MEZANI**

SEHEMU YA KWANZA

1.0 UTANGULIZI

Mheshimiwa Spika, kwa mujibu wa Kanuni ya 99(9) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Januari 2016, naomba kuwasilisha Taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Masuala ya UKIMWI kuhusu Utekelezaji wa Bajeti ya Mamlaka ya Kudhibiti na Kupambana na Dawa za Kulevya – **Fungu 91** na Tume ya Kudhibiti UKIMWI Tanzania (*TACAIDS*) – **Fungu 92** kwa Mwaka wa Fedha 2019/2020 pamoja na Maoni ya Kamati kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi ya mafungu hayo kwa Mwaka wa Fedha 2020/2021.

Mheshimiwa Spika, Kwa mujibu Kanuni ya 10 (d) ya Nyongeza ya Nane ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Januari, 2016, Kamati ya Masuala ya UKIMWI imepewa jukumu la kushughulikia Bajeti za Tume ya Kudhibiti UKIMWI Tanzania na Mamlaka ya Kudhibiti na Kupambana na Dawa za Kulevya. Hivyo, msingi wa maoni yatakayotolewa katika Taarifa hii ni kutoka katika Kanuni za Kudumu za Bunge.

Mheshimiwa Spika, mnamo tarehe Tarehe 28 - 29 Machi, 2020, Kamati ilipokea na kujadili Taarifa ya Utekelezaji wa Bajeti ya Mwaka wa Fedha wa 2019/2020 na kufanya uchambuzi wa Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Mwaka wa Fedha 2020/2021, **Fungu 92** – Tume ya Kudhibiti UKIMWI Tanzania (*TACAIDS*) na **Fungu 91** – Mamlaka ya Kudhibiti na Kupambana na Dawa za Kulevya.

Mheshimiwa Spika, Baada ya Uchambuzi wa kina wa Taarifa za (**Fungu 92 & 91**), naomba kutoa taarifa ya Kamati inayofanua masuala makubwa matano (5) yafuatayo: -

1.1 Utekelezaji wa Mpango wa Bajeti ya Tume ya Kudhibiti UKIMWI Tanzania (TACAIDS) kwa Mwaka wa Fedha 2019/2020;

1.2 Utekelezaji wa Mpango wa Bajeti ya Mamlaka ya Kudhibiti na Kupambana na Dawa za Kulevyaa kwa Mwaka wa Fedha 2019/2020;

1.3 Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Tume ya Kudhibiti UKIMWI Tanzania (TACAIDS) kwa Mwaka wa Fedha 2020/2021;

1.4 Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Mamlaka ya Kupambana na Kudhibiti Dawa za Kulevyaa Tanzania kwa Mwaka wa Fedha wa 2020/2021; na

1.5 Maoni, Ushauri na Mapendekezo ya Kamati kwa Fungu 92 na Fungu 91

SEHEMU YA PILI

2.0 UCHAMBUZI WA KAMATI

2.1 *Utekelezaji wa Ushauri wa Kamati – TACAIDS*

Mheshimiwa Spika, katika kufanya uchambuzi wa taarifa ya utekelezaji wa Bajeti ya Mwaka wa Fedha wa 2019/2020, kwa Fungu 92, Kamati ilifanya mapitio ya Utekelezaji wa Maoni na Mapendekezo yaliyotolewa wakati wa kupitisha Bajeti ya Tume hii kwa mwaka wa 2019/2020. Jumla ya Mapendekezo manne (4) yaliyotolewa na Kamati na Mapendekezo yote Serikali imeyachukua na imeahidi kuendelea kuyafanyia kazi. Kamati inaipongeza Serikali Kwa kushirikiana na Kamati ya Masuala ya UKIMWI na hivyo kuweza kupata fedha kupitia Mfuko wa Dunia (*Global Fund*) kwa ajili ya kuanzisha mchakato wa kutunisha Mfuko wa UKIMWI (*ATF*) kupitia ***Endowment Fund***. Aidha, Kamati inaishauri Serikali kuendelea kuwashirikisha Sekta Binafsi katika mpambano dhidi ya UKIMWI ikiwa ni pamoja na mpango huo wa ***Endowment Fund***.

Hata hivyo, kuna baadhi ya maoni na mapendekezo yaliyotolewa na Kamati hapo awali ambayo utekelezaji wake umekuwa na kasi ndogo ikiwa ni pamoja na pendelezo la kuwa na vyanzo vya uhakika na endelevu vya fedha kwa ajili ya Mfuko wa Taifa wa UKIMWI (*AIDS Trust Fund*) ili angalau 75% ya Bajeti ya Tume ya Kudhibiti UKIMWI Tanzania, fedha za mwitikio wa UKIMWI ziwe fedha za ndani na 25% tu itokane na wafadhili wa nje. Kamati inaishauri Serikali kuongeza kasi ya utekelezaji wa mapendekezo ambayo hayajakamilishwa ili yaweze kutoa matokeo chanya kwa ajili ya kuendeleza juhudzi za Udhibiti wa UKIMWI hapa nchini.

2.2 Utekelezaji wa Ushauri wa Kamati-Mamlaka ya Kudhibiti na Kupambana na Dawa za Kulevy

Mheshimiwa Spika, Kamati ilifanya mapitio ya Utekelezaji wa Maoni na Mapendekezo ya Fungu 91 na kutoa Jumla ya Mapendekezo manne (4). Mapendekezo hayo yalihu kutenga bajeti ya miradi ya maendeleo kwa ajili ya Mamlaka, kuongeza kasi ya kukamilisha zoezi la utambuzi na uratibu wa Asasi zote zinazojishughulisha na dawa za kulevy, kusimamia nidhamu kikamilifu kwa wagonjwa wanaopata dawa za *methadone* na kukamilisha mwongozo wa Hadidu za Rejea za namna ya Kamati za UKIMWI katika Mamlaka za Serikali za Mitaa zinavyoweza kutekeleza majukumu ya kudhibiti na kupambana na dawa za kulevy. Kwa kiasi kikubwa mapendekezo haya yametekeliza na mengine yapo katika hatua tofauti za utekelezaji.

Mheshimiwa Spika, Kamati imeendelea kubaini kwamba, Mamlaka ya Kudhibiti ya Kupambana na Dawa za Kulevy haikutengewa fedha za Miradi ya Maendeleo kama ilivyokuwa kwa Mwaka wa Fedha 2019/2020. Kuacha kuitengea fedha za maendeleo ni kudunisha juhudzi za kupambana na dawa za kulevy nchini kwani shughuli za uchunguzi na ujenzi wa maabara kwa ajili ya Mamlaka zinazidi kukwama. Kwa mfano, hadi sasa tunategemea maabara moja ya Mkemia Mkuu wa Serikali, hali ambayo inasababisha kuwa na mrundikano mkubwa wa kesi kwa kuwa ina vipaumbele vyake inavyotakiwa kuvishughulikia

Mheshimiwa Spika, Serikali imeendelea kuwaunganisha waraibu walioachana na dawa za kulevyta na Mpango wa Taifa wa Kuwajengea Uwezo Vijana (*Skills Development*) kutoka Fungu 65 chini ya Ofisi ya Waziri Mkuu. Hata hivyo, Kamati hajjaridhika na suala la kuahirisha utekelzaji wa pendekezo hili kwani kwa Mwaka 2020/2021 bado hakuna fedha za Miradi ya Maendeleo iliyotengwa kwa Fungu 91. Aidha, Kamati inaipongeza Serikali kupitia Mamlaka na Ofisi ya Waziri Mkuu – Kazi, Vijana, Ajira na Watu wenyewe Ulemavu, kutumia fursa ya *skills development levy* ili kuviwezesha vikundi vyta waraibu wa dawa za kulevyta walio katika tiba na hivyo kuwawezesha kufanya shughuli za kuwaongeza kipato.

Mheshimiwa Spika, Kamati inaipongeza Serikali kwa kuufanya kazi ushauri wa kuzitambua Asasi za Kiraia zinazojihuisha na shughuli za uelimishaji kuhusu madhara ya dawa za kulevyta kwani hadi kufikia Februari, 2020 jumla ya Asasi 53 nchi nzima zinazojishughulisha na dawa za kulevyta zilitambuliwa. Asasi 30, ambazo ni sawa na asilimia 57, zilitkeleza shughuli zake kwa kufuata miongozo na taratibu zilizowekwa na Serikali na Mamlaka kuanzisha mfumo rasmi wa utoaji taarifa za utekelezaji wa shughuli za kila Asasi hizo kwa kila mwaka. Aidha, ni maoni ya Kamati kuwa umuhimu wa kuwa na miradi itakayowezesha waathirika wa dawa za kulevyta kuongeza kipato ndio njia rahisi ya kuwaepusha kurudi katika matumizi ya dawa hizo.

SEHEMU YA TATU

- 3.0 UCHAMBUZI WA TAARIFA YA UTEKELEZAJI WA MPANGO
WA BAJETI NA UZINGATIAJI WA MAONI YA KAMATI KWA
MWAKA WA FEDHA WA 2020/2021**
- 3.1 Uchambuzi wa Mapitio ya Utekelezaji wa Mpango wa
Bajeti kwa Mwaka wa Fedha 2019/2020 (Fungu 92 &
91**

3.1.1 Makusanyo ya Maduhuli

Katika Mwaka wa Fedha wa 2019/2020 Tume ya Kudhibiti UKIMWI (Fungu 92) na Mamlaka ya Kudhibiti na Kupambana

na Dawa za Kulevyaa (Fungu 91) hakukuwa na Makadirio ya makusanyo ya maduhuli yaliyoidhinishwa na Bunge.

3.1.2 Upatikanaji wa Fedha Tume ya Kudhibiti UKIMWI Tanzania (TACAIDS)- Fungu 92

Mheshimiwa Spika, Kamati ilifanya uchambuzi wa Bajeti (Fungu 92) ambayo ilitengewa Tume kwa ajili ya kutekeleza shughuli zake kwa Mwaka wa Fedha 2019/2020 kama ambavyo ziliidhinishwa na Bunge lako Tukufu ili kuona matumizi yake. Katika Mwaka wa Fedha 2019/2020 Tume illidhinishiwa bajeti ya jumla ya shilling **8,769,193,747,00**. Kati ya fedha hizo shilling **2,812,559,000.00** ni kwa ajili ya matumizi ya kawaida na shilingi **5,956,634,747.00** ni kwa ajili ya miradi ya maendeleo, ambapo fedha za ndani ni shilingi **2,000,000,000** na fedha za nje ni shilingi **3,956,634,747,00**.

Mheshimiwa Spika, Uchambuzi wa taarifa ya Utekelezaji wa Fungu 92, hadi kufikia mwezi Februari, 2020 kiasi cha fedha kilichokuwa kimepokelewa kwa ajili ya matumizi ya kawaida na maendeleo ni kiasi cha shilingi **8,513,647,055.00**, sawa na asilimia **79** ya fedha yote zilizopangwa. Kati ya fedha zilizopokelewa, fedha za matumizi ya kawaida ni **1,816,844,167** ni sawa na asilimia **65** (zikijumuisha sh. **792,548,000** kwa matumizi mengineyo- OC aidi. **1,024,296,167** kwa matumizi ya mishahara). Fedha za maendeleo zilizopokelewa ni **Sh. 6,696,802,886**, sawa na **asilimia 68** ya fedha za maendeleo zilizopangwa. Hata hivyo fedha za maendeleo zinaonekana kuwa kubwa mpaka kiwango cha asilimia **68** kutokana na Tume kupata fedha za DoD na GGM ambazo hazikuwa kwenye bajeti iliyopangwa.

Uchambuzi wa Kamati unaonesha kwamba fedha iliyopokelewa, kwa kiasi kikubwa ni fedha za Miradi ya Maendeleo, ambazo zilitolewa kwa kiwango cha asilimia **68**, ikilinganishwa na fedha za matumizi mengine ambazo zilitolewa kwa kiwango cha asilimia **65**. Aidha kiasi kikubwa cha fedha za maendeleo zilizopokelewa ni fedha za nje, kiasi cha **Sh 825,193,812** sawa na **asilimia 201**, ikilinganishwa na fedha za ndani ambazo ni Sh **28,208,453** (**Michango ya wadau mbalimbali**) siyo fedha za kutoka Hazina .

Mheshimiwa Spika, Kamati inaona kwamba utekelezaji wa shughuli za Tume kwa kiasi kikubwa unategemea sana fedha kutoka kwa wafadhilli; Kutokana na hali hiyo ni dhahiri kuwa endapo ufadhilli huu utakoma basi Tume itashindwa kutekeleza majukumu yake ipasavyo.

Mheshimiwa Spika, Kamati inaiomba Bunge kuihimiza Serikali kukamilisha upelekaji wa fedha hasa za ndani kwa Tume ili iweze kukamilisha utekelezaji wa shughuli zake kama zilivyopangwa kabla aidia wa fedha wa 2019/2020 haujamalizika. **Rejea Jedwali Na. 1**

Jedwali Na. 1: **Ulingenifu wa Bajeti iliyoidhinishwa na kiasi cha Fedha zilizopatikana hadi Mwezi Februari, 2020 (FNGU 92)**

BAJETI ILIYOIDHINISHWA		UPATIKANAJI WA FEDHA	
Mgawanyo	Kiasi Kilichoidhinishwa	Kiasi kilichopokelewa hadi Feb 2020	Asilimia %
MATUMIZI YA KAWAIDA (FEDHA ZA NDANI)			
Mshahara	1,599,813,000.00	1,024,296,167.00	64
Kawaida (OC)	1,212,746,000.00	792,548,000.00	65
Mfuko wa UKIMM (ATF)	2,000,000,000	28,208,453 (Mchango mbalimbali) siyo fedha za kutoka Hazina	
JUMLA ANDOGO (PE & OC)	4,772,559,000.00	1,816,844,167	65
MAENDELEO (MFUKO WA UKIMM) – ATF			
ATF	2,000,000,000.00	28,208,453 (Mchango mbalimbali) siyo fedha za kutoka Hazina	
MAENDELEO (FEDHA ZA NNE)			
DoD	0 (Ne ya bajeti)	1,063,664,404	NA
GGM Kill Challenge	0(Ne ya bajeti)	100,757,792	NA
UNDAP	383,875,000.00	825,193,812.00	201
GLOBAL FUND	3,572,759,747.00	2,158,631,016	60
JUMLA ANDOGO (MAENDELEO)	3,956,634,747	4,048,247,024	102

Chanzo. Taarifa ya Tume (TACAIDS) ya Makadirio ya Matumizi ya Mwaka 2020/2021

3.1.3 *Upatikanaji wa Fedha Mamlaka ya ya Kudhibiti na Kupambana na Dawa za Kulevyia (DCEA)- Fungu 91*

Mheshimiwa Spika, Mamlaka ya Kudhibiti na Kupambana na Dawa za Kulevyia (Fungu 91), iliidhinishiwa kiasi cha shilingi **7,592,818,000.00** kwa ajili ya utekelezaji wa shughuli zake. Kati ya fedha hizo, kiasi cha shilingi **shilingi 2,644,266,000.00** sawa na **asilimia 34.8** zilitengwa kwa ajili ya mishahara (*PE*) na shilingi **4,948,552,000.00** sawa na **asilimia 65.2** zilitengwa kwa ajili ya matumizi mengineyo (*OC*). Na kwamba Mamlaka haikutengewa fedha yoyote kwa ajili ya maendeleo kwa mwaka 2019/2020.

Uchambuzi wa Taarifa iliyowasilishwa mbele ya Kamati umebaini kuwa, hadi kufikia mwezi Februari, 2020, Mamlaka ilikuwa imepokea jumla ya shilingi **4,219,523,000.00**, sawa na **asilimia 55.6** ya fedha yote iliyoidhinishwa na Bunge kwa ajili ya matumizi ya Mwaka wa Fedha wa 2018/2019. Kati ya fedha hizo, shilingi **920,491,000.00** sawa na **asilimia 34.8** ni kwa ajili ya mishahara ya watumishi na shilingi **3,299,032,000.00**, sawa na **asilimia 66.7** ni kwa ajili ya matumizi mengineyo. **Rejea Jedwali Na. 2**

Jedwali Na. 2: **Ulingenifu wa Bajeti iliyoidhinishwa na kiasi cha Fedha zilizopatikana 2019/2020 (FNGU 91) hadi kufikia Mwezi Februari, 2020.**

BAJETI ILIYOIDHNISHWA		UPATIKANAJI WA FEDHA	
Mgawanyo	Kiasi Kilichaidhinishwa	Kiasi kilichopokelewa hadi Feb 2020	Asilimia
MATUMIZI YA KAWAIDA (FEDHA ZA NDANI)			
Mshahara	2,644,266,000.00	920,491,000.00	34.8
Kawaida (OC)	4,948,552,000.00	3,299,032,000.00	66.7
Mraidi ya Maendeleo	0	0	0
JUMLA	7,592,818,000.00	4,219,523,000.	55.6

Chanzo: Taarifa ya Mamlaka Kuhusu Utekelezaji wa Bajeti ya Mwaka 2020/2021

3.1.4 Fedha za Miradi ya Maendeleo kwa Mwaka 2019/2020, Fungu 92 & 91

Mheshimiwa Spika, katika Mwaka wa Fedha 2019/2020 Tume ya Kudhibiti UKIMWI ilitengewa jumla ya shilingi **5,956,634,747** kwa ajili ya kutekeleza Miradi ya Maendeleo. Kati ya fedha hizo, shilingi **2,000,000,000** ni fedha za ndani na **shilingi 3,956,634,747** ni fedha za wahisani. Hata hivyo, hadi kufikia wakati Kamati inapokea taarifa Machi 2020, jumla ya fedha za nje zilizopokelewa kwa ajili ya maendeleo ni kiasi cha shilingi **4,048,247,024**, kiasi ambacho ni zaidi kwa **asilimia 102** ya kilichotengwa na kuidhinishwa na Bunge kwa Bajeti ya **Fungu 92** kwa Mwaka wa Fedha 2019/2020.

Mheshimiwa Spika, kwa upande wa fedha za maendeleo za ndani, uchambuzi wa Kamati umebaini kwamba, Tume ya Kudhibiti UKIMWI Tanzania imepokea kiasi cha **shilingi 28,208,453.00 (fedha za michango ya wadau mbalimbali siyo kutoka Hazina)**. Hakuna kiasi cha fedha za ndani zilizotolewa na kilichoidhinishwa na Bunge. Hali hii imepelekea Tume kuendelea kutekeleza Miradi yake ya Maendeleo kwa utegemezi wa fedha kutoka kwa wafadhili kwa **asilimia 99**. Hii ni kutokana na ukweli Kwamba, jumla ya matumizi ya maendeleo yaliyokwishafanywa na Tume mpaka Februari ni kiasi cha shilingi, **6,696,802,886**. Hivyo, kiasi cha fedha za ndani ni **asilimia 67.5** pekee. Ni maoni ya Kamati kuwa, mwenendo huu wa utegemezi wa fedha za Miradi ya Maendeleo siyo jambo sahihi endapo nia ya dhati ya Serikali ni kwamba, Taifa liweze kudhibiti UKIMWI kwa mujibu wa mipango iliyopo. Kamati imeendelea kusikitishwa na kuhuzunishwa sana na hali hii ya kutokutolewa kwa fedha za ndani kutoka Hazina kwa ajili ya Miradi ya Maendeleo katika Tume, hadi sasa suala la UKIMWI linashughulikiwa na Tume hii peke hapa nchini.

Mheshimiwa Spika, kwa upande wa Mamlaka ya Kudhibiti na Kupambana na Dawa za Kulevyta, haikutengewa kabisa fedha za Miradi ya Maendeleo. Kamati bado inasisitiza kwamba, ajenda ya kupambana na dawa za kulevyta ni kubwa na pana kuliko inavyotafsiriwa kwa kuzingatia hali ya maambukizi ya juu sana ya ugonjwa wa homa ya ini miongoni

mwa waraibu wa dawa za kulevyia ni hatarishi kwa jamii nzima. Kamati inaishauri Serikali kuliangalia suala hili kwa uzito unaostahili. Ni maoni ya Kamati kuwa, miradi ya maendeleo inayoweza kunufaika na fedha za maendeleo ni pamoja na kuwawezesha waraibu kiuchumi kwa kuwaunganisha na kuwapatia mitaji ambayo itawasaidia kuwainua na kufanya shughuli mbalimbali kama mikopo nafuu ya stadi za maisha mfano kilimo cha bustani, ufundi wa magari, kufyatua matofali na kazi nyinginezo.

Mheshimiwa Spika, Kamati iliona upo umuhimu wa Serikali kuweka mikakati ya programu ya kusaidia kuwaunganisha waraibu kwenye jamii yao tena na shughuli za kiuchumi. Hata hivyo Kamati inaitaka Serikali kuja na msimamo mmoja wa kisera kati ya kuwa na miradi ya uzalishaji mali kama vile karakana ndani ya vituo vya tiba au kutumia karakana zilizo kwenye mfumo wa kawaida wa mafunzo na uzalishaji mali kama vile VETA na kadhalika.

3.1.5 Ukaguzi wa Miradi ya Maendeleo na Utekelezaji wa Afua za UKIMWI.

Mheshimiwa Spika, kwa kuzingatia masharti ya Kanuni 10 (b), Nyongeza ya Nane ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Aprili, 2016 10(b), inayoitaka Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Masuala ya UKIMWI kufuatilia utekelezaji wa Sera na Mipango ya Serikali kuhusu UKIMWI na Udhibiti wa Madawa ya Kulevyia, Kamati ilifanya ziara kati ya tarehe 2– 7 Machi 2020, kutembelea na kukagua utekelezaji Afua na shughuli zinazotekelizwa na Wizara, Taasisi na Mamlaka za Serikali katika mwitikio dhidi ya mapambano ya UKIMWI, Kifua Kikuu na biashara na matumizi ya Madawa ya Kulevyia katika Mikoa ya Dodoma , Arusha na Kilimanjaro.

3.1.5.1 Maeneo na Afua zilizokaguliwa na Kamati

Kwa ujumla, ziara na ufuatiliaji ulifanywa katika maeneo yafuatayo: -

- a) Kituo cha kuwahudumia waathirika wa Dawa za Kulevyia Itega - Mkoani Dodoma;

- b) Halmashauri ya Mji wa Kondoa, Kituo cha Huduma na Tiba - CTC Hospitali ya Mji wa Kondoa na Shule ya Sekondari Masawi;
- c) Gereza la Kisongo - Mkoani Arusha;
- d) Halmashauri ya Mkoa wa Arusha, Kliniki ya CTC – Hospitali ya Mount Meru;
- e) Hospitali ya Magonjwa Ambukizi Kibong'oto;
- f) Halmashauri ya Mkoa wa Kilimanjaro Kliniki ya - CTC-Hospitali ya Mkoa wa Kilimanjaro - Mawenzi;

3.1.5.2 Malengo ya Ziara katika maeneo yaliyotembelewa Mheshimiwa Spika, wakati wa kutekeleza ratiba ya ziara, Kamati ilipokea na kujadili taarifa za maeneo/vituo ilivyovitembelea, pamoja na kushuhudia utoaji wa huduma mbalimbali za masuala ya UKIMWI, Kifua Kikuu na Madawa ya Kulevya.

Kwa ujumla taarifa zilizowasilishwa na kujadiliwa na ukaguzi uliofanywa ulilenga kubaini mambo makubwa yafuatayo: -

- a) Mwitikio wa UKIMWI kwa ujumla kwenye Halmashauri za Wilaya;
- b) Hali ya maambukizi ya VVU na upatikanaji wa dawa za kufubaza makali ya VVU pamoja na tiba ya magonjwa nyemelezi kwa muktagha wa malengo ya 90-90-90;
- c) Utekelezaji wa afua za UKIMWI mahala pa kazi miongoni mwa Watumishi; mafanikio na changamoto;
- d) Udhibiti wa biashara na matumizi ya dawa za kulevya pamoja na huduma ya utoaji *Methadone* kwa watumiaji wa dawa za kulevya, mafanikio na changamoto; na
- e) Ukusanyaji, usimamizi na matumizi ya takwimu za Masuala ya UKIMWI katika ngazi mbalimbali za utoaji huduma za afya.

3.1.5.3 Uchambuzi wa mambo yaliyobainishwa na Kamati wakati wa ziara

Mheshimiwa Spika, uchambuzi wa Kamati katika maeneo tajwa ultiweza kubaini, mambo ya msingi kuhusu mafanikio na changamoto zilizopo pamoja na hatua zinazochukuliwa. Aidha, Kamati ililibua hoja pamoja na kutoa ushauri na mapendekezo ya hatua za kuchukua ili kuimarisha mapambano dhidi ya UKIMWI na dawa ya Kulevya. Baadhi ya mambo ya msingi ambayo Kamati ilibaini ni pamoja na yafuatayo: -

(a) Katika ngazi mbalimbali, hususan baadhi ya Halmashauri na vituo vya afya, hakuna ufahamu wa kutosha juu ya utekelezaji wa shughuli za mwitikio wa UKIMWI na Kifua Klkuu katika muktadha wa 90-90-90. Jambo hili linapunguza uwezo wa Serikali na wadau kufanya tathmini ya matokeo ya hatua zinazochukuliwa. Kutokuwepo na takwimu za makadirio ya wanaokusudiwa kupimwa maambukizi ya VVU ni mojawapo ya upungufu uliobainika katika Halmashauri na Manispaa zote zilizotembelewa na Kamati. Jambo hili lina uzito mkubwa kwani ndio msingi wa takwimu zote za mkakati wa 90-90-90;

(b) Kuwepo kwa changamoto ya umbali wa vituo vya kutolea dawa, gharama za usafiri na ukizingatia wateja wengi wanatoka nje ya Halmashauri zao, kumechangia kwa kiasi kikubwa utoro wa dawa. Aidha, wateja wengi kutoa taarifa zisizo sahihi kuhusu makazi na namba za simu na uchache wa watoa huduma ngazi ya jamii, pia kuendelea kuwepo kwa unyanyapaa na hivyo mteja kulazimika kwenda kuchukua dawa katika vituo vya mbali na maeneo anayoishi.

(c) Kuwepo kwa changamoto ya kukithiri unyanyapaa mionganoni mwa watumishi wa Jeshi la Gereza la Kisongo, ambapo umepelekea idadi ndogo sana ya watumishi kuweza kujitokeza na kufahamu hali ya afya zao sambamba na kuweka wazi hali zao kama njia ya kuweza kuwapatia huduma stahiki. Kamati inataka kufahamu ni hatua gani mahsusizi zinachukuliwa kukabiliana na unyanyapaa mionganoni mwa Askari amgeerza nchini katika kuimarisha afua za

upimaji kwa hiari, matumizi ya dawa za kufubaza makali ya VVU. Pamoja na mafanikio yanayoolezwa katika kudhibiti Ugonjwa wa Kifua Kikuu katika Gereza la Kisongo, Kamati inashauri Jeshi la Magereza kushirikiana na Kitengo cha Taifa cha kudhibiti Kifua Kikuu na Ukoma (NTLP) ili kufanya ukaguzi na tathmini ya pamoja katika Magereza yote nchini kujua hali halisi ya Kifua Kikuu katika Magereza Tanzania kwa sasa. Aidha, Jeshi la Magereza lishirikiane na wadau mbalimbali katika kuwafuatilia wafungwa/mahabusu wenyewe VVU wanaotoka gerezani kwa lengo la kuwaunganisha na huduma zilizopo kwenye jamii kwa urahisi wa ufuatiliaji, kama waratibu wa kifua Kikuu na waratibu wa UKIMWI.

(d) Afua za masuala za UKIMWI na madawa ya kulevyu mashuleneni.

Mheshimiwa Spika, Kamati imebaini udhaifu mkubwa wa kutokuwepo kwa afua za masuala ya UKIMWI mashuleneni baada ya kushuhudia ushuhuda uliotolewa na wanafunzi katika Shule ya Sekondari iliyotembelewa. Aidha, Kamati imebaini kutokuwepo mkakati wa uratibu na usimamizi wa mapambano dhidi ya UKIMWI na matumizi ya madawa ya kulevyu mashuleneni. Kwa mfano, katika Shule zilizotembelewa na Kamati, wanafunzi waliiarifu Kamati kwamba, hawajawahi kusikia kuhusu muktadha wa 90-90-90 kama mkakati wa mwitikio wa UKIMWI nchini na pia waratibu wa elimu ya afya mashuleneni waliitaarifu Kamati kuwa hawajawahi kufika katika shule hiyo. Kwa maana hiyo, hakuna hatua madhubuti zinazoonekana kutekelezwa kulingana na miongozo iliyopo. Aidha, suala la kutekeleza afua kudhibiti dawa za kulevyu na UKIMWI limebaki kuwa ni suala la ziada, bila msukumo, mipango, bajeti na bila rasilimali fedha. Ni ushauri wa Kamati kuwa, Serikali ianzishe afua mahsusini za mapambano dhidi ya UKIMWI mashuleneni kwa ajili ya kufanya mwitikio wa maambukizi mapya mionganoni mwa vijana wa umri wa miaka 15 - 24 .

(e) Uelewa mdogo kuhusu Malengo ya Kimataifa ya Kupambana na UKIMWI ya 90 90-90

Mheshimiwa Spika, kumekuwepo na uelewa mdogo katika muktadha wa Malengo na Mkakati wa Kimataifa wa

Kupambana na UKIMWI wa 90-90-90- ifikapo Mwaka 2020. Hii ni kutokana na kwamba, pamoja na takwimu nyingi zilizowasilishwa zililenga kuonyesha mafanikio katika kudhibiti maambukizi ya VVU/UKIMWI, mafanikio yanayoelezwa hayapimiki kutokana na takwimu kutoonyesha malengo yaliyowekwa na ambayo yanahitaji kufikiwa. Kwa mfano, taarifa nyingi hazonyeshi makadirio ya wanaokadiriwa kuwa na maambukizi ya VVU, haioneshi wanapimwa wangapi kati ya waliokadiriwa, badala yake inaonyesha waliopatikana na maambukizi. Adha, takwimu pia hazoneshi idadi ya WAVIU wanaotumia dawa na waliofanikiwa kufubaza makali ya VVU. Hali hii, inaathiri kwa kiasi kikubwa maamuzi mbalimbali yanayohusu hatua za kuchukua katika kuimaraisha mapambano dhidi ya UKIMWI. Kamati ina maoni kuwa, ili kukidhi haja na kutekeleza Mpango wa Taifa wa Kudhibiti na Kupambana na UKIMWI wa 90-90-90 ifikapo mwaka 2020, Serikali kupitia TACAIDS, Wizara ya Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto na Mamlaka ya Kudhibiti na Kupambana na Dawa za Kulevyaa iimarishe mafunzo ya kujengewa uwezo wa uwasilishaji takwimu kwa Watendaji wa Afya na halmashauri kwa ujumla pamoja na kusisitiza usimamizi shirikishi katika ukusanyaji takwimu za VVU/UKIMWI na magonjwa nyemelezi;

Kamati ya UKIMWI ya Halmashauri ya Kondoa haina ushirikiano na Waratibu wa Masuala ya UKIMWI katika Halmashauri hiyo. Hali hii inachangia kwa kiasi kikubwa kukwamisha shughuli za utekelezaji wa mwitikio wa UKIMWI kwenye Halmashauri husika.

(f) Kukosekana hatua mahsusini na za makusudi za kudhibiti maabukizi ya UKIMWI zinazoendana na kasi ya kukua miji

Mheshimiwa Spika, pamoja na Halmashauri ya Mji wa Kondoa, inakadiriwa kuwa na idadi ya watu 74,718 ambao wanajishughulisha na shughuli nyingi za uchumi, likiwa na maeneo mengi yenye vichocheo ambavyo vinasababisha viashiria vya ongezeko la maambukizi VVU katika jamii ikiwemo, mila na desturi potofu (ukeketaji), kuwa na wapenzi wengi kwa wakati mmoja, ulevi na usiri. Aidha, pamoja na

viashiria hivyo, hakuna hatua madhubuti za kudhibiti hali hii, kwani idadi ya waliopima ni 21,083 na maambukizi kwa Halmashauri ya Mji Kondoa ni sawa na asilimia 1.7. Aidha, takwimu zilizowasilishwa kuhusu hali ya mambukizi ya VVU/UKIMWI hazijazingatia makundi maalum, rika, jinsia, na umri. Hivyo, kuzifanya kutoweza kutumika ipasavyo kufanya maamuzi madhubuti ya hatua za kuchukua katika kupambana na VVU/UKIMWI.

(g) Mahusianisho ya madawa ya kulevyta na maambukizi ya VVU, Homa ya Ini na

Mheshimiwa Spika, takwimu zinaonyesha kuwa maambukizi ya VVU kwa watumia dawa za kulevyta yapo juu ya kiwago cha wastani wa maambukizi Kitaifa. Aidha, kumekuwepo na ongezeko la maambukizi ya ugonjwa wa Kifua Kikuu na Homa ya Ini B na C kwa waraibu wanaotumia dawa za kulevyta wanaoishi na VVU. Aidha, Kamati ilipotembelea Kituo cha Kutolea Methadone kilichopo Itega, Mkoani Dodoma, ilibaini hali ya maambukizi ya juu sana ya ugonjwa wa homa ya ini mionganoni mwa waraibu wa madawa ya kulevyta. Hali hii ni hatarishi kwa jamii nzima. Katika taarifa hiyo ilieleza kuwa Waraibu wanne (4) waligundulika kuwa na Ugonjwa wa Kifua Kikuu, wagonjwa 176 walipimwa homa ya ini ambapo 64 sawa na asilimia 36 waligundulika kuwa na maambukizi ya ugonjwa huo aina ya B na C. Wagonjwa 51 sawa na asilimia 29 waligundulika na homa ya Ini C. Hivyo, Kamati inasisitiza kuwa, pamoja na huduma za methadone kwa waraibu ni muhimu kuimarisha utoaji huduma za Kifua Kikuu na Homa ya Ini na kuliangalia suala hili kwa uzito unaostahili.

(h) Waraibu wa madawa ya kulevyta kukosa namna ya kumudu maisha hata baada ya kukamilisha matibabu

Waraibu wengi wa madawa ya kulevyta hawana ujuzi wa kuweza kujajiri, hali ambayo inawaweka katika hatari kubwa ya kurudia kuyatumia tena madawa hayo baada ya matibabu kutohana na kukosa makazi maalum, kukosa kitu cha kufanya na kumudu maisha.

(i) Juhudi za kutoa huduma na mapambano dhidi ya maambukizi ya VVU na UKIMWI

Mheshimiwa Spika, Kamati inaipongeza Hospitali ya Mkoa wa Arusha – Mount Meru kwa juhudini zinazofanywa za kutoa huduma na mapambano dhidi ya maambukizi ya VVU na UKIMWI. Pia Kamati inaipongeza Hospitali ya Mount Meru kwa kuonesha ufanisi katika matumizi ya takwimu ikilinganishwa na maeneo mengi ambayo Kamati imewahi kuyatembelea. Aidha, ni maoni ya Kamati kuwa wakati umefika sasa wa Serikali kuwa na utaratibu utakatoa mwongozo wa uwasilishaji wa takwimu ili kuondoa vikwazo wanavyokutana navyo watumiaji wa takwimu katika maamuzi na usimamizi. Aidha, hali ya usafi kwenye Kitengo cha CTC kwanyo Hospitali ya Mount Meru ni nzuri sana. Kamati inaipongeza Wizara kwa jambo hilo na kutoa wito kwamba, itakuwa ni jambo zuri endapo Serikali itaweka juhudini ya kuhakikisha kuwa hali kama hiyo inaonekana kwenye hospitali nyingine zote hapa nchini.

SEHEMU YA NNE

4.0 UCHAMBUZI WA MPANGO WA MAKADIRIO YA MATUMIZI KWA MWAKA WA FEDHA WA 2020/2021

4.1 *Uchambuzi wa Vipaumbele vya ikilinganishwa na Makadirio ya Mapato kwa Mwaka wa Fedha wa 2020/2021*

4.1.1 *Vipaumbele vya Tume ya Kudhibiti UKIMWI*

Mheshimiwa Spika, Tume ya Kudhibiti UKIMWI Tanzania kwa Mwaka wa Fedha 2020/2021 imepanga kujikita katika kuongeza juhudini za utoaji uongozi wa kimkakati wa mwitikio wa Taifa wa UKIMWI. Tume imeainishaa maeneo ambayo itaweka mkazo kwa Mwaka wa Fedha wa 2020/2021. Maeneo hayo ni pamoja na;

i. Kutafuta rasilimali za UKIMWI kutoka vyanzo vya ndani na nje ya nchi ;

ii. Kufuatilia watekelezaji wa shughuli za UKIMWI katika ngazi zote ikiwemo uimarishaji wa upatikanaji wa taarifa zenye ubora kwa wakati na kuzisambaza kwa wadau;

- iii. Kutayarisha na kusambaza miongozo ya UKIMWI kwenye sekta na mikoa ya kipaumbele;
- iv. Kuimarisha uratibu wa wadau wanaofanya afua za UKIMWI kwa vijana na uhamasishaji wa kampeni za kinga, mfano AGYW na DREAMS;
- v. Kuimarisha majadiliano ya kisekta na wadau wa UKIMWI;
- vi. Kuendelea kusambaza matokeo ya tafiti za UKIMWI kwa wadau;
- vii. Kuimarisha uraghibishi wa kudhibiti UKIMWI kwa watunga sera na wenyewe maamuzi ya Kitaifa; na
- viii. Kuongeza jitihada za kupeleka huduma za UKIMWI kwenye Mikoa 14 ya vipaumbele ukiwemo Mkao wa Iringa, Mwanza, Njombe, Kagera, Katavi, Mbeya, Pwani, Ruvuma, Shinyanga, Tabora, Dodoma, Geita na Songwe.

Aidha, Tume ilianisha maeneo matatu (3) na kuyawekea mkazo katika utekelezaji wake katika kipindi cha kati yafuatayo:-

- i. Kuimarisha Uratibu wa afua na wadau kupitia mipango ya pamoja, ufuatiliaji na tathimini;
- ii. Kutoa Uongozi wa kimkakati wa Mwitikio wa Taifa dhidi ya Virusi vya UKIMWI(VVU) na UKIMWI; na
- iii. Ufuatiliaji na Usimamizi wa rasilimali na uelimishaji umma katika utekelezaji wa Mkakati wa Nne wa Taifa wa Kudhibiti UKIMWI wa Mwaka 2018/2019 – 2022/23 .

Mheshimiwa Spika, Kamati ilipitia maeneo ambayo Tume ilianisha na kuyaridhia kwa kuwa yalioneka kuwa na tija katika suala zima la uboreshaji wa mapambano dhidi ya VVU/ UKIMWI. Maeneo hayo yanashabihiana na Mipango na Mikakati mbalimbali yakiwemo makubaliano ya kitaifa na kimataifa yenye lengo la kupambana na maambukizi ya UKIMWI.

Mheshimiwa Spika, Kamati ilijiridhisha kwamba, Tume imepanga kutekekeleza malengo ambayo yameainishwa katika miongozo mbalimbali ikiwemo Dira ya Taifa ya Maendeleo (2025), Mpango wa Maendeleo ya Muda wa Kati (2018/2019 - 2020/2021), Malengo ya Maendelao endelevu (*Sustainable Development Goals 2030*). Aidha, utekelezaji wa shughuli hizo zote unalenga katika kuhakikiasha tisini tatu (90-90-90) zinapatikana ikiwemo kutokuwepo mtu au watu wenye maambukizi wanaofariki kutokana na UKIMWI. Kwa kutekeleza haya yote kutapelekea kuwa na jamii yenye afya bora na ustawi wa jamii ambao utachangia jamii isiyo na maambukizi ya VVU.

Hata hivyo, kwa mujibu wa *Tanzania HIV Impact Survey (THIS 2017)*, ambapo asilimia 40 ya maambukizi mapya ya UKIMWI yapo kwenye umri wa kuanzia miaka 15-24 na asilimia 80 ya maambukizi hayo ni mlongoni mwa wasichana, Kamati inashauri Serikali kulipa umuhimu mkubwa katika suala hili.

4.1.2 *Vipaumbele vya Mamlaka ya Kudhibiti na Kupambana na Dawa za Kulevyta*

Mheshimiwa Spika, Mamlaka ya Kudhibiti na Kupambana na Dawa za Kulevyta kwa Mwaka wa Fedha 2020/2021 imejipangia madhumuni ya kudhibiti matumizi ya dawa za kulevyta, kudhibiti upatikanaji wa dawa za kulevyta pamoja na utekelezaji wa masuala ya kinga na tiba kwa watu wanaotumia dawa za kulevyta. Mamlaka imepanga kufikia madhumuni hayo kwa kuweka mikakati mitatu (4) ifuatayo:-

- i. Kupunguza upatikanaji wa dawa za kulevyta katika nchi yetu (*Supply Reduction*);
- ii. Kupunguza uhitaji wa dawa za kulevyta (*Demand Reduction*);
- iii. Kupunguza madhara yanayosababishwa na utumiaji wa dawa za kulevyta (*Harm Reduction*); na
- iv. Kuboresha ushirikiano wa kikanda na kimataifa (*Regional and International Cooperation*)

Mheshimiwa Spika, Kamati ilijadili mikakati hii na kuona kwamba, ina tija kwa taifa zima endapo mikakati hii itatekelezwa kwa wakati. Hata hivyo, kwa kuwa utekelezaji wake unategemeana na upatikanaji wa fedha, ni muhimu Serikali ikafanya juhudhi kubwa zaidi katika kutenga na kutoa fedha kwa wakati. Aidha, Kamati inasisisitiza upatikanaji fedha za maendeleo kwa ajili ya Miradi ya Maendeleo kupewa msukumo wa kipekee kutokana na umuhimu wake.

4.2 *Uchambuzi wa Makadirio ya Matumizi*

4.2.1 *Tume ya Kudhibiti UKIMWI*

Mheshimiwa Spika, katika Mwaka wa Fedha wa 2019/2020 Tume ya Kudhibiti UKIMWI Tanzania kupitia **Fungu 92** linatarajia kukusanya maduhuli ya jumla ya shilingi **5,000,000.00**.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa Fedha wa 2020/2021 Tume ya Kudhibiti UKIMWI Tanzania kupitia **Fungu 92** inaomba jumla ya kiasi cha shilingi **7,689,447.000** kwa ajili ya kutekeleza majukumu yake. Kati ya fedha hizo, kiasi cha **shilingi 4,900,739,000**. sawa na **asilimia 64** kwa ajili ya Miradi ya Maendeleo na shilingi **1,212,746,000** sawa na **asilimia 16** ni kwa ajili ya mengineyo, ikijumuisha matumizi ya kawaida (OC) **shilingi 2,788,708,000.00** sawa na **asilimia 36** na mishahara ya watumishi (PE) ni **shilingi 1,575,962,000.00**

Mheshimiwa Spika, makadirio haya ya matumizi ya mwaka 2020/2021 ni pungufu kwa takribani shilingi **1,079,746,747** sawa na asilimia **12** ikilinganishwa na bajeti ya matumizi ya Tume kwa mwaka wa Fedha wa 2019/2020. Aidha, kwa upande wa Bajeti ya maendeleo ni pungufu kwa takribani ni shilingi **1,055,895,747** sawa na asilimia **18** ya kiasi kilichotengwa mwaka unaoisha. Kamati inasisisitiza wasiwasi wake kuwa, upungufu wa fedha za kwa ajili ya shughuli za Tume kwa wastani wa asilimia **12** ni mkubwa sana. Aidha upungufu wa fedha za miradi ya maendeleo kwa asilimia **18** ni jambo la kutazamwa upya, kwani bado mapambano dhidi ya UKIMWI yanahitaji fedha za kutosha ili kuweza kuendelea kupata matokeo chanya. Kwani kwa mujibu wa taarifa mbalimbali utekelezaji, afua nyingi za UKIMWI hazijakamilika na

uendelevu wake bado unahitaji fedha za kutosha na zitakazo patikana kwa wakati.

4.2.2 *Mamlaka ya Kudhibiti na Kupambana na Dawa za Kulevy-a-Fungu 91*

Mheshimiwa Spika, Mamlaka ya Kudhibiti na Kupambana na Dawa za Kulevy-a, kwa Mwaka wa Fedha 2020/2021 imekadiria kufanya matumizi ya kiasi cha **Shilingi 9,033,345,000** kwa ajili ya kutekeleza majukumu yake. Kati ya fedha hizo, **Shilingi 6,167,415,000** sawa na **asilimia 68 ya** fedha yote inayoombwa ni kwa ajili ya Matumizi mengineyo na Shilingi **2, 865,930,000**, sawa na **asilimia 32** kwa ajili ya Mishahara. Makadirio haya yameongezeka kwa kiasi cha shilingi **1, 440,527,000**, sawa na **asilimia 16** ikilinganishwa na makadirio ya matumizi kwa Mwaka wa Fedha wa 2019/2020.

Mheshimiwa Spika, uchambuzi wa Kamati, ulibaini kwamba Mamlaka haijatenga fedha kwa ajili ya utekelezaji wa miradi ya maendeleo kwa mwaka wa Fedha wa 2020/2021 kama ambavyo ilijitokeza kwa mwaka wa fedha wa 2019/2020 na 2018/2019. Mwenendo huu wa kutotenga fedha za maendeleo unaashiria kutolitazama suala la madawa ya kulevy-a kataika mapana yake. Aidha, endapo hatua hazitachukuliwa mapema, linaweza kusababisha hasara kwa kutopata matokeo mazuri ya fedha zinazotengwa na kutumika kwa ajili ya kukabiliana na dawa za kulevy-a nchini.

Mheshimiwa Spika, Kamati inasisitiza kuwa ni muhimu kwa Mamlaka ya Kudhibiti na Kupambana na Dawa za Kulevy-a kuanza kutenga fedha kwenye Bajeti yake kwa ajili ya Miradi ya Maendeleo. Kwa kufanya hivyo, kutasaidia kujenga mfumo bora wa kudhibiti na kupambana na dawa za kulevy-a nchini kwa upana wake ikiwa ni pamoja na kujenga jamii ya Watanzania isiyotumia dawa za kulevy-a na kutoshiriki katika biashara na matumizi ya dawa za kulevy-a.

SEHEMU YA TANO

5.0 MAONI, USHAURI NA MAPENDEKEZO YA KAMATI

Mheshimiwa Spika, baada ya uchambuzi wa Utekelezaji wa Bajeti kwa Mwaka wa Fedha wa 2019/2020 na Makadirio ya matumzi kwa Mwaka wa Fedha wa 2020/2021 kwa Tume ya Kudhibiti UKIMWI Tanzania (TACAIDS) na Mamlaka ya Kupambana na kudhibiti Dawa za kukevya, Kamati ina Maoni, Mapendekezo na Ushauri katika maeneo mbalimbali kama ifuatavyo;

5.1 *Tume Ya Kudhibiti UKIMWI Tanzania*

5.1.1 *Upatikanaji wa fedha za ndani kwa ajili ya Afua za UKIMWI*

Mheshimiwa Spika, wakati wa kupitia Bajeti Kamati imebaini kuwa, mpaka sasa asilimia kubwa Bajeti ya kutekeleza Miradi ya Maendeleo ya Tume ya Kudhibiti UKIMWI Tanzania bado imekuwa ikitegemea fedha za wahisani. Katika Mwaka wa Fedha wa 2019 /2020, Serikali ilitenga kiasi cha shillingi **Bilioni 2** tu sawa na **asilimia 1.4** ya fedha yote iliyotengwa kwa ajili ya Miradi ya Maendeleo ya Tume. Kiasi kilichotolewa ni shillingi **28,208,453**, ambazo hazikutoka hazina bali ni fedha za wadau mbalimbali wa masuala ya UKIMWI .

Kamati inasisitiza kuwa, kuendelea kutegemea wafadhili wa nje hakutoi uhakika wa mwitikio endelevu wa mapambano dhidi ya UKIMWI ikizingatiwa kwamba, baadhi ya wafadhili wameanza kupunguza kiwango cha ufadhili wa fedha za UKIMWI kwa Tanzania. Kwa mfano, PEPFAR wamepunguza **asilimia 23** ya fedha zilizokuwa zitolewe kwa Tanzania kwa mwaka 2019/2020 kiasi cha **USD 119Mil**, sawa na shillingi **282,854,000,000**. Kupunguzwa kwa kiasi hiki cha fedha kunaathari mipango iliyokuwa itekelezwa katika kupambana na UKIMWI nchini.

Kamati inashauri Serikali ione umuhimu wa kutenga fedha zake za ndani kwa ajili ya udhibiti wa UKIMWI kwa wananchi

wake. Aidha, Serikali iweke mpango mkakati wa kupata vyanzo vingine vya mapato vitakavyosaidia kutenga fedha zaidi kwa ajili ya Miradi ya Maendeleo. Itakuwa jambo jema endapo bajeti ya UKIMWI angalau asilimia 75 ya fedha ya maendeleo ya Tume iwe ni fedha za ndani na asilimia 25 tu itokane na wafadhili wa nje.

5.1.2 Kuanzisha Tozo kwa Mfuko wa UKIMWI wa Taifa (AIDS Trust Fund - ATF)

Mheshimiwa Spika, Kamati imebaini kuwa, pamoja na nia nzuri ya Serikali ya kutenga fedha katika bajeti kuu, changamoto kubwa imekuwa ni kutoa fedha zinazotengwa kwa ajili ya kugharamia shughuli za UKIMWI. Mfuko wa UKIMWI (*Aids Trust Fund - ATF*) lengo lake ni kuhakikisha Serikali inatenga fedha zake za ndani kwa ajili ya kupambana na janga hili.

Mheshimiwa Spika, Bajeti ya Mfuko wa Udhagini wa UKIMWI kwa Mwaka wa Fedha 2020/2021 unaonesha kuwa, shilingi milioni 2,000 zilitengwa kwa ajili ya ATF. Kamati imebaini kuwa, pamoja na nia nzuri ya Serikali ya kutenga fedha katika bajeti kuu, bado Serikali inatakiwa kufanya uchambuzi wa vyanzo mbalimbali vya mapato kwa ajili ya kutunisha Mfuko huu. Ni maoni ya Kamati kuwa, Serikali ibuni uwekezaji kwa kushirikiana na Sekta Binafsi ili kuwekeza katika miradi ambayo sehemu ya faida itakuwa chanzo cha mapato kwa ajili ya Mfuko.

5.1.3 Kuimarisha ukusanyaji, hifadhi na matumizi ya takwimu mbalimbali za UKIMWI

Mheshimiwa Spika, utekelezaji wa afua mbalimbali za UKIMWI unategemea sana na ubora wa takwimu zinazopatikana kutoka katika vyanzo mbalimbali. Kuna upungufu mkubwa katika ukusanyaji, uhifadhi na matumizi ya takwimu mbalimbali zinazohusiana na mapambano dhidi ya maambukizi ya VVU na UKIMWI. Kamati inashauri Serikali kuititia Tume ya Kudhibiti UKIMWI Tanzania (*TACA/IDS*), Wizara

ya Afya, Maendelo ya Jamii, Jinsia Wazee na Watoto na TAMISEMI kuimarisha ujengaji wa uwezo, usimamizi na ufuatiliji katika maeneo ya ukusanyaji, utunzaji na matumizi ya takwimu kwa ngazi za Hlmashauri na Vituo nya Afya. Jambo hili ni muhimu ili Taifa liweze kuongeza kasi ya kutekeleza Mpango Mkakati wa Kimataifa wa kudhibiti na Kupambana na UKIMWI wa 90-90-90.

5.1.4 Msongamano wa Wafungwa Gerezani na Maambukizi ya Kifua Kikuu.

Mheshimiwa Spika, *Magereza mengi nchini yana msongamano wa wafungwa na mahabusu ambapo, mazingira halisi ya magereza vyumba vyake havina mzunguko wa kutosha wa hewa, hali inayoweza kuchochaea maambukizi ya Ugonjwa wa Kifua Kikuu kwa haraka, pamoja na hatua za awali za upimaji na kuanzishiva dawa kwa wanakuwa na Kifua Kikuu, Kamati inataka kufahamu ni hatua gani mahsususi zinachukuliwa kwa waliopo magerezani kiasi cha kuyafanya magereza yasiwe na wagonjwa wa Kifua Kikuu. Aidha, yapo masuala ya jumla kwenye Jeshi la Magereza yanayohitaji kuangaliwa kwa haraka na kwa makini kama ifuatavyo:-*

a. Mfumo wa matumizi ya mapato yanayotokana na shughuli za uchumi za Jeshi la Magereza uangaliwe upya. Kwa mfano, ni jambo la ajabu kwamba Jeshi la Magereza linanunua chakula kwa mzabuni kwa bei ya juu kuliko bei ambayo Jeshi hilo lilimuuzia mzabuni huyo huyo.

b. Msongamano wa mahabusu ni mkubwa sana magerezani kuliko hata idadi ya wafungwa ambao ndio hasa wanatakiwa kutunzwa na Jeshi la Magereza kwa mujibu wa sheria. Hali hii ni hatarishi kwa maambukizi ya kifua kikuu na hata upatikanaji wa huduma zinazohusu masuala ya UKIMWI. Serikali iangalie uwezekano wa kutenganisha mahabusu na wafungwa ili mahabusu wahifadhiwe na Jeshi la Polisi na wafungwa wahifadhiwe na Jeshi la Magereza kwa mujibu wa sheria. Utaratibu huo utasaidia pia kupunguza idadi ya mahabusu waliohifadhiwa kwa hali ya uonevu au kukosekana

kwa uangalifu katika utendaji wa Jeshi la Polisi. Endapo Jeshi la Polisi litarudishiwa wajibu wake wa kutunza mhaabusu, kuna uwezekano mkubwa wa kuongezeka kwa uangalifu katika kutambua ni watuhumiwa wepi wapelekwe mahabusu na ni wepi masuala yao yatatuliwe bila kuwekwa mahabusu. Katika hali ya sasa, yako malalamiko kwamba, Jeshi la Polisi wanakosa umakini katika kuchuja wahusika wasioepukika wa mahabusu na wale ambao masuala yao yanaweza kumalizwa bila kufika mahabusu kwani wahusika wa Jeshi hilo hawajui machungu ya msongamano wa watu kwenye magereza.

5.2 Mamlaka ya Kudhibiti na Kupambana na Dawa za Kulevy

5.2.1 Athari za kutotenga Bajeti ya Miradi ya Maendeleo kwa Mamlaka ya Kudhibiti na Kupambana na Dawa za Kulevy

Mheshimiwa Spika, uchambuzi wa Kamati umebaini kuwa kwa miaka kadhaa Tume ya Kudhibiti na Kupambana na Dawa za Kulevy imekua haitengewi Bajeti kwa ajili ya Maendeleo. Mojawapo ya athari za kutotenga fedha za maendeleo ni kukosekana kwa maabara ya Mamlaka ya Kupambana na Dawa za Kulevy kwa ajili ya uchunguzi.

Mheshimiwa Spika, maabara inayotumika mpaka sasa ni ya Mkemia Mkuu wa Serikali ambayo ina vipaumbele katika utekelezaji shughulia zake. Siyo lazima vipaumbele vya Mamlaka ya Kupambana na Dawa za Kulevy viwiane. Pamoja na kwamba ipo ahadi ya Wafadhili ya kujenga maabara kwa ajili ya Mamlaka, lakini utekelezaji wa ahadi hiyo umekuwa ukiahirishwa kila mwaka. Vilevile ukosefu wa fedha za maendeleo umepelekea kasindogo au kukosekana kwa mfumo maalumu kwa ngazi ya jamii kwa ajili ya kuwatambua waraibu wa madawa ya kulevy na hivyo kuweza kuwashirikisha na kuwasaidia kumudu maisha na kuachana na biashara na matumizi ya madawa hayo.

Mheshimiwa Spika, Kamati inasisitiza kwamba, ajenda ya kupambana na Dawa za kulevy ni kubwa na pana kuliko

inavyotafsiriwa. Kamati inaanmini kuwa, Miradi ya Maendeleo inayoweza kutekelezwa na fedha za maendeleo ni pamoja na kuwawezesha waraibu klichumi kwa kuwaunganisha, kuwapa mbinu za ujasiriamali, mikopo nafuu ya biashara, stadi za maisha, uongezaji wa vituo vya kupata nafuu kwa waathirika wa dawa za kulevyta, kufanya uraghibishi kwa jamii wa namna ya kupambana na kudhibiti dawa za kulevyta na hata kuikinga jamii ili isishiriki katika njia yoyote ya matumizi ya dawa za kulevyta.

Mheshimiwa Spika, kwa maana hiyo ni maoni ya Kamati kwamba, utoaji na utumiaji wa fedha kwa ajili ya matumizi ya kawaida bila kuambatana na mifumo na mipango endelevu utumiaji usiokuwa wa kimkakati. Kwa mfano, bila miradi ya kimkakati kunakosekana mzunguko wa kupunguza idadi ya watumiaji wa madawa za kulevyta na wakati huo huo kutoa fursa ya kuwarudisha waraibu kwenye tatizo hilo kwa kasi ile ile au zaidi ya awali. Kwa hiyo, siyo rahisi kwa afua zilizopo kuweza kuleta matokeo yanayotarajijiwa. Kwa sababu hiyo ni maoni ya Kamati kwamba fedha za maendeleo zinaweza kutoa fursa kwa Mamlaka kuanza kujenga mifumo itakayo jumuisha jamii nzima kimkakati katika kuwapokea, kuwatambua, kuwashirikisha na kuwasaidia watu waliowahi kutumia madawa ya kulevyta na hivyo kuiwezesha Mamlaka kupata matokeo yenye manufaa ya muda mfupi, muda wa kati na muda mrefu.

5.2.2 Ushirikishwaji wa Asasi za Kiraia katika Mapambano dhidi ya Dawa za Kulevyta

(a) **Mheshimiwa Spika**, mpango wa kushirikisha asasi za kiraia katika kuwafikia waraibu wengi zaidi unaonesha kuleta matumaini. Hata hivyo, asasi hizo bado ni chache sana ukilinganisha na mahitaji na asasi hizo chache zilizopo hazifanyi kazi kama mtandao. Badala yake kila asasi inafanya jitihada zake peke yake. Kamati inaishauri Serikali kushirikiana na Asasi zisizo za kiserikali kubuni namna sahihi ya kutengeneza mtandao wa kitaifa kwa ajili ya kazi hii. Kwa kupitia mtandao huo itakuwa rahisi kuwafikia watu walioathirika na dawa za kulevyta ili kuwatambua, kuwashirikisha na kuwasaidia katika muktadha mpana wa

mwitikio wa kitaifa wa janga hili. Aidha, njia hii inaweza kusaidia kufuatilia kwa ukaribu mienendo yao ili kuacha matumizi ya dawa hizo, kupunguza unyanyapaa mionganini wa jamii, kuwawezesha kufanya shughuli nyingine za kiuchumi pamoja na kupata takwimu sahihi ya waraibu. Kwa njia ya mtandao wa asasi hizi jithada zinaweza kufanywa chini ya uratibu wa Viongozi wa Halmashauri husika kama ambavyo imefanikiwa kwa upande wa UKIMWI.

5.2.3 *Kuimariisha huduma kwa waathirika wa madawa ya kulevyaa wanaopata dawa za Metahadone katika Sobber Houses.*

Mheshimiwa Spika, uwepo wa huduma za Sobber Houses zinazotolewa na sekta binafsi ambapo wagonjwa hulipia kulingana na makubaliano ya mgonjwa na watoa huduma kulingana na muda ambaao mgonjwa ataishi katika nyumba au usitiri wa mihadarati. Aidha, huduma hizi za Sobber Houses hutolewa kulingana na miongozo ya kitaifa. Kamati inapongeza Serikali kwa hatua ya mpango wa Serikali wa kuongeza nyumba za tiba katika Mikoa ya Tanga, Pwani, Morogoro, Dodoma, Arusha na Kilimanjaro. Hata hivyo, Kamati inasisitiza umuhimu wa Serikali kutekeleza mpango huu kwa wakati uliopangwa. Aidha, wakati umefika wa sasa wa kuanzisha Sobber Houses za Serikali. Aidha, Serikali indelee kuongeza rasilimali fedha pamoja na jithada katika afua hizi za kuwatambua waraibu wa madawa ya kulevyaa na kuwajumuisha kwenye afua zilizopo. Hatua hii ni muhimu kwa sababu tiba ya *methadone* ina mchango mkubwa kwa taifa kijamii na kiuchumi pia. Kwa mfano, kwa sasa matumizi yao ya heroine kwa siku moja na kwa mraibu mmoja ni wastani wa kete 3 zenyе thamani ya shilingi 7,000 kila moja. Hivyo basi, jumla ya TZS 21,000 ndio wastani wa matumizi ya mraibu mmoja kwa siku, sawasawa na shilingi 7,665,000 kwa mwaka; na kwa kuwa kuna jumla ya waraibu 7,300 nchini nzima (bila kuhesabu waraibu ambaao wamejitokeza kwenye nyumba za huduma) hivyo basi Kiasi cha walau shilingi **55,881,500,000** zinaondolewa kwenye mzunguko wa pesa kwa kupitia njia inayoleta madhara ya kiafya na kijamii. Kiasi hiki cha fedha ni kikubwa sana endapo kitaingia kwenye mzunguko wa fedha katika njia yenye tija kiuchumi.

5.2.4 Suala la madawa ya kulevyaa kuwa ajenda ya Kamati za UKIMWI katika Halmashauri na Manispaa.

Mheshimiwa Spika, Kamati za UKIMWI katika Halmashauri na Manispaa Nchini zimekuwa zikiratibu masuala yanayohusu UKIMWI katika Halmashauri na Manispaa kwa ufanisi wa kutosha. Uchambuzi wa Kamati katika ufuutilaji wa shughuli za mapambano dhidi ya madawa ya kulevyaa katika ngazi za Halmashari na Manispaa umeonesha kutokuwepo utaratibu au mfumo rasmi wa namna ya kushughulika na suala la madawa ya kulevyaa. Aidha, kwa kuzingatia mahusiano ya karibu yaliyopo mionganii mwa waathirika wa madawa ya kulevyaa na waathirika wa maambukizi ya UKIMWI, hatua na afua za pamoja katika kudhibiti na kupambana na UKIMWI na Madawa ya kulevyaa ni muhimu.

SEHEMU YA SITA

6.0 HITIMISHO

Mheshimiwa Spika, nakushukuru wewe binafsi kwa kuipa Kamati ushirikiano na ulezi uliotukuka na pia kwa kunipa muda wa kuwasilisha Taarifa hii mbele ya Bunge lako Tukufu. Pia napenda kumshukuru Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu - Sera, Bunge, Kazi Ajira, Vijana na Watu wenyewe Ulemavu, Mhe. Jenista Mhagama (Mb) pamoja na Manaibu Waziri; Mheshimiwa Antonny Peter Mavunde (Mb) na Mheshimiwa Stella Alex Ikupa (Mb), vilevile namshukuru Waziri wa Afya na Ustawi wa Jamii, Mhe. Ummy Ally Mwalimu na Naibu Waziri Mhe. Dkt Faustine Ndugulile, kwa ushirikiano wao mkubwa wanaondelea kuutoa kwa Kamati wakati wote wa shughuli za Kamati. Vilevile napenda kuwashukuru Makatibu Wakuu, Ofisi ya Waziri Mkuu wa Sera na Uratibu na Uwekezaji na Katibu Mkuu, Ofisi ya Waziri Mkuu wanaohusika na Bunge Ndg. Tixon Tuyangine Nzunda pamoja na Maafisa Waandamizi wa Ofisi ya Waziri Mkuu.

Mheshimiwa Spika, aidha, napenda kumshukuru Mkurugenzi Mtendaji wa Tume ya Kudhibiti UKIMWI Tanzania, Dkt. Leonard Maboko na Kaimu Kamishna Jenerali wa Mamlaka ya Kudhibiti na Kupambana na Dawa za Kulevyaa, Ndg. James

Kaji na Watendaji wote, kwa ushirikiano walioutoa kwa Kamati hii ili kutekeleza majukumu yake.

Mheshimiwa Spika, kwa nafasi ya kipekee kabisa naomba niwashukuru Wajumbe wa Kamati ya Bunge ya Masuala ya UKIMWI , kwa kazi nzuri waliyoifanya ya kujadili na kuchambua Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Tume ya Kudhibiti UKIMWI Tanzania na Mamlaka ya Kudhibiti na Kupambana na Dawa za Kulevyia kwa Mwaka wa Fedha 2020/2021. Pamoja na ufinyu wa muda, Wajumbe hawa walikuwa tayari kutekeleza jukumu hili kubwa na kwa wakati. Kwa heshima kubwa, nomba kuwatambua kwa majina Waheshimiwa wafuatao:-

- | | | |
|--|---|--------------|
| 1. Mhe. Oscar Rwegasira Mukasa | - | Mwenyekiti |
| 2. Mhe. Dkt. Jasmine Tiisekwa Bunga, Mb | - | M/Mwenyekiti |
| 3. Mhe. Rose Cyprian Tweve, Mb | - | Mjumbe |
| 4. Mhe. Asha Abdallah Juma, Mb | - | Mjumbe |
| 5. Mhe. Dkt. Haji Hussein Mponda, Mb | - | Mjumbe |
| 6. Mhe. Salma Rashid Kikwete, Mb | - | Mjumbe |
| 7. Mhe. Edward Franz Mwalongo, Mb | - | Mjumbe |
| 8. Mhe. Gibson Blasius Meiseyeki, Mb | - | Mjumbe |
| 9. Mhe. Prof. Norman Adamson S. King, Mb | - | Mjumbe |
| 10. Mhe. Kemirembe Julius Lwota, Mb | - | Mjumbe |
| 11. Mhe. Albert Obama Ntabaliba, Mb | - | Mjumbe |
| 12. Mhe. Mattar Ali Salum, Mb | - | Mjumbe |
| 13. Mhe. Masoud Abdallah Salim, Mb | - | Mjumbe |
| 14. Mhe. Oliver Daniel Semuguruka, Mb | - | Mjumbe |
| 15. Mhe. Susan Anselim Lyimo, Mb | - | Mjumbe |
| 16. Mhe. Zainab Matitu Vullu, Mb | - | Mjumbe |
| 17. Mhe. Omary Ahmed Badwel, Mb | - | Mjumbe |
| 18. Makame Mashaka Foum, Mb | - | Mjumbe |
| 19. Munde Tambwe Abdallah, Mb | - | Mjumbe |
| 20. Mhe Amina Nassor Makilagi, Mb | - | Mjumbe |
| 21. Mhe. Yussufu Haji Khamisi, Mb | - | Mjumbe |
| 22. Mhe. Amina Saleh Mollel, Mb | - | Mjumbe |
| 23. Mhe. Ester Nicholas Matiko, Mb | - | Mjumbe |
| 24. Mhe. Fratei Gregory Massey, Mb | - | Mjumbe |
| 25. Mhe. Godfrey W. Mgimwa | - | Mjumbe |
| 26. Mhe. Mwigulu L. Nchomba, Mb | - | Mjumbe |

Mheshimiwa Spika, napenda kuwashukuru kwa dhati Watumishi wa Ofisi ya Bunge, wakiiongozwa na Ndugu Stephen Kagaigai - Katibu wa Bunge, Ndg. Michael Chikokoto, Kaimu Mkurugenzi wa Idara ya Kamati za Bunge na Ndg. Gerald Magili, Mkurugenzi Msaidizi kwa kuisaidia na kuiwezesha Kamati hii kutekeleza majukumu yake kwa weledi mkubwa. Kipekee, nawashukuru Makatibu wa Kamati Ndg. Happiness Ndalu na Ndg. Asia Msangi, kwa kuratibu vyema kazi za Kamati na kuhakikisha Taarifa hii inakamilika kwa wakati.

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema haya, sasa naliomba Bunge lako Tukufu likubali kuidhinisha Makadirio ya Matumizi ya Tume ya Kudhibiti UKIMWI Tanzania - **Fungu 92** jumla ya shillingi **7,689,447,000.00** na Mamlaka ya Kudhibiti na Kupambana na Dawa za Kulevyta - **Fungu 91** jumla ya shillingi **9,033,345,000.00**

Mheshimiwa Spika, naomba kuwasilisha na ninaunga mkono hoja.

Mhe. Oscar R. Mukassa, (Mb)

MWENYEKITI

KAMATI YA BUNGE YA MASUALA YA UKIMWI

1 Aprili, 2020

SPIKA: Ahsante sana Mheshimiwa Mukasa kwa uwasilishaji mzuri sana. Niipongeza sana Kamati ya Masuala ya UKIMWI tulianza kwa tabu sana lakini tumemaliza vizuri mno. (*Makofii*)

Nawapongeza sana *and I am really proud of you* Kamati ya Masuala ya UKIMWI, mmejitahidi sana. Mmepambana kweli kwa kishirikiana na Serikali kuyaweka masuala haya kwenye ajenda mpaka mmeweza kutuitia Viongozi wote Wakuu wa madhehebu mbalimbali ya dini ya nchi yetu na tumekubaliana nao mambo mbalimbali. Kwa kweli mmeweza msukumo mkubwa katika maeneo mengi,

mmeefanya ziara, mmeishauri Serikali, tunawapongezeni sana.
(Makofii)

Naamini wakati Wizara ya Afya itakapokuwa inawasilisha bajeti yake pamoja na mambo mengine tutapenda kujua hili la Kilimanjaro labda lina sababu na maelezo yake, la kumweka Daktari Bingwa kwenye Kituo cha Afya labda ni Kituo cha Adhabu au nini watatuambia, *there has to be a reason* kwa sababu haiwezi kuwa ni error. *It has to be a very big reason*, watatufahamisha wakati huo nini kinachoendelea.

Waheshimiwa Wabunge, hotuba inayofuata inapaswa kuwa ya Msemaji Mkuu wa Kambi Rasmi ya Upinzani kuhusu Ofisi ya Waziri Mkuu. Nilitaarifu Bunge kwamba Mheshimiwa Halima Mdee ndiyo anakaimu nafasi ya Kiongozi wa Upinzani kwa sababu Mheshimiwa Kiongozi wa Upinzani hayupo kwa sababu ambazo alishaziainisha na sisi Wabunge wenzake tunazifahamu. Kwa hiyo, kwa mambo yote Mheshimiwa Halima ndiyo anakaimu nafasi hiyo.

Sasa nimeipata hotuba hii mapema na nimeipitia kama nilivyopitia hotuba nydingine ikanipa tabu sana. Mtaona hoja iliyotolewa ni hoja ya Mheshimiwa Waziri Mkuu mahsus kabisa iliungwa mkono kuhusu utekelezaji wa Wizara hiyo lakini ni maombi ya Mapato na Matumizi kwa Mwaka wa Fedha unaokuja. Imeanza Kamati ya Katiba na Sheria imejikita na kujielekeza kwenye jambo hilo, ikaja Kamati ya Bajeti nayo imejikita na kujielekeza na kuchambua kwenye jambo hilo, imekuja Kamati ya Masuala ya UKIMWI nayo imefanya hivyo hivyo. Zinapokuja hotuba za Upinzani zinakuwa kama vile hotuba ambazo hazikuandikwa na Wabunge wenyewe, kama vile hotuba ambazo zimeandikwa na mtu ambaye hajakuwepo, hajashiriki, haelewi kinachoendelea.

Tunafikia hatua hii baada ya Waheshimiwa Wabunge kupitia Kamati zinazohusika kuwa tumefanya ziara. Mwaka huu ilikuwa fupi zaidi lakini tumefanya ziara za ufuatiliaji kwenye Wizara mbalimbali. Pia tunafikia hatua hii baada ya

kupata taarifa za utekelezaji za Wizara mbalimbali hadi Februari mwaka huu lakini tunakuwa tumepewa na kuitia *forecast* za Wizara kwa maana ya bajeti ya mwaka 2020/2021 kila watu mahali pao. Kwa hiyo, tunapofikia hatua hii tayari tuna *insight* kubwa ya nini kimefanyika na nini kinapangwa kufanyika.

Sasa zinapokuja hotuba za Upinzani na hii kwa sababu ni ya kwanza niiseme mapema zina shida. Kwa mfano, hii ya leo ina mambo mengi nayoweza kuyaita ya kubuni, ya kubahatisha, mambo ambayo kiuandishi hayajawa *substantiated* na ama *source* ya hiyo *information* ama *evidence*. Ni *sentence* zinapigwa tu juu kwa juu kama mtu yuko kwenye mkutano wa hadhara kule Kongwa, kwenye Bunge haiwezi kuwa hivyo. Lazima twende na viwango, huu ni mwaka wa tano wa Bunge hili, kwa hiyo, hatuwezi kuruhusu mambo ya mwaka wa kwanza, wa pili yakaendelea kujitokeza, naamini tume-*advance*, tumekua.

Sasa hotuba hii ina mambo mengi mno sina muda wa kuitia yote lakini kubwa zaidi kuna *a lot of spelling mistakes printing errors* nyingi sana. Ukiitoa hii kwenye mitandao inakwenda duniani, inatoa picha ya watu ambao *they are not serious. A lot of spelling mistakes, every page ina several spelling mistakes* kwa nakala niliyopewa mimi lakini pia lugha ambazo zina shida.

Kubwa zaidi inausema vibaya mhimili wa Mahakama kwa kuzungumzia baadhi ya maamuzi ya Mahakama na ikiwepo baadhi ya mambo ambayo yako huko Mahakamani. Kama suala la Wakurugenzi kusimamia/kutosimamia uchaguzi yamejaa humu, masuala ya *CAG* aliyepita wao wenyewe baadhi wana marufaa yao yako huko huko sioni kuyaleta hapa yana sababu gani mkijua kwamba wenyewe mmeenda huko Mahakamani kulituhumu Bunge kwa mambo hayo hayo ambayo tulifanya maamuzi na wengine mkapata adhabu humu humu, mnarudisha mambo yale yale ambayo mimi nilidhani tumeshavuka Yordan. Kuna matumizi mabaya sana ya jina la Mheshimiwa Rais na mwenendo wa

Mheshimiwa Rais jambo ambalo Kanuni zinakataza hasa ile Kanuni ya 64(1)(d) na (e).

Wamelihukumu sana Bunge la 11 naita kizushi kwa sababu hoja nydingi sana zina maelezo yake, zinahitaji mjadala nje ya hapa muwe mmesimama hapo na sisi tumesimama hapa halafu mlete hiso hoja muone jinsi tunavyokwenda. Sasa huu siyo wakati wa kufanya hayo.

Wengine ambao wameendelea na kiburi hicho mnaona na huko mtaani matokeo yake ni hayo hayo tu ya mipambano isiyokuwa na sababu. Ndiyo sisi ni Wabunge na mimi ni Mbunge pia lakini lazima tutambue yako maeneo ni *restricted areas*. Mojawapo ya maeneo ambayo ni *restricted areas* ni maeneo ya Majeshi mbalimbali. Sasa Mbunge ukienda kwenye eneo la Jeshi mojawapo na bahati nzuri ukapata faida ya kuambiwa hebu toka hapo kwa unayaelewa utatoka mbio kabisa kwa sababu *it is a restricted area*, utaingia kwa ruhusa ya wahusika. Sasa yakikupata yaliyokupata kwa kweli sijui Spika akutetee nini sasa katika mazingira hayo. Kwa hiyo, hata ukija hapa usome hotuba, useme yaani sijui tunatafuta nini, unashindwa kuelewa kimsingi. (*Makofii*)

Kwa ujumla wake nadhani hotuba za Upinzani zinakosa ile, kama wangeandika pamoja wasingeefika hapa lazima hotuba zao zingekuwa na *improvementfulani inayojifocus* kwenye Ofisi ya Mheshimiwa Waziri Mkuu kama ni kuikosoa, ikosoa mwanzo mwisho na idara zao, mimi siko hapa kutetea chochote na kadhalika lakini kwa mwendo mnaokwenda msipojirekebisha kwa kweli hotuba zenu nydingi itakuwa kama...

Tulijitahidi siku za nyuma kuwa tunajaribu kuwaambia hili liko Mahakamani liruke, hili liko hivi liruke, kazi hiyo safari hii sifanyi. Ukiweka jambo lolote sijui la Mahakamani, la nini ambalo linaendelea huko hiyo hotuba nzima mimi basi haitasomwa hapa. Mkifanya hayo mambo yenu basi, tuko mwisho hapa sasa siyo mahali pa kufundishana tena. Ni

mahali pa kufanyakazi ambayo inatakiwa kwa sababu hakuna tena mwanafunzi tunaendelea.

Tuhuma ambazo hazina kichwa wala mguu, hazina sababu. Ooh, Tundu Lissu hajalipwa sijui mishahara yake na posho. Tundu Lissu hadai hata shilingi moja, wala mshahara hata mmoja. Mwulizeni aseme tena. Mpaka alipositishiwa Ubunge wake, hakuna Mbunge anayedai wala nani anayedai. Vitu vya kuzusha zusha kila siku, tuwe tunabishana mambo ambayo wala hayana mbele wala nyuma yana faida gani? Haina faida. Ni vizuri tukaenda tu vizuri.

Kiongozi wa upinzani Bungeni ananyanyaswa sana, huduma hapati. Gari lipo na hatujapata magari mapya Bungeni, tutayapata kupitia bajeti hii ya sasa kwa ajili ya lile Bunge la Kumi na Mbili. Gari liliopo amekuwa akilitumia yeye kwa muda mrefu, lipo. Sasa hiyo ni kazi ya Katibu na Kiongozi wa Upinzani kujua shida nini? Labda kama ni modeli ama nini, hayo ni mambo ambayo siyo ya kuyaleta Bungeni *as such*.

Nyumba hana. Imeandikwa huku. Nyumba ipo, ambayo inahudumiwa na Bunge na ni ile nyumba ambayo aliikataa tangu mwanzo. Badala ya yeye kukaa, akawa anakaa Mheshimiwa Tundu Lissu. Ile nyumba aliyokuwa anakaa Mheshimiwa Tundu Lissu siyo nyumba ya *Cheaf Whip; Cheaf Whip* hatumpi nyumba katika *provisions* za kibunge, anayepewa huduma ya nyumba ni kiongozi wa Upinzani Bungeni. Yeye aliikataa, nadhani iko *site three*, akaenda kukaa *site two* kwenye nyumba aliyo-prefer yeye mwenywewe.

Pamoja na hayo, zile huduma ambazo zilitakiwa zitolewe kwenye nyumba hiyo rasmi ambayo yeye ameikataa, anakaa kwenye nyumba yake mwenywewe, zile huduma zinatolewa, zikiwemo kuwepo mhudumu wa kufanya mapishi na usafi, ikiwemo ulinzi na mambo mengine kama umeme, maji, Bunge linalipia. Kama halifanyi hivyo, Katibu hebu fanya hayo mambo kwenye nyumba hiyo aliyeichaguwa yeye mwenywewe.

Sasa kuliandika humu; na tukumbuke, Kiongozi wa Upinzani Bungeni ni Mjumbe wa Tume ambaye anasimamia mambo hayo. Sasa kama hawezি kujisemea mwenyewe kwenye Tume, unapolileta humu jambo ambalo ni *a litter bit personal* sijui kama ni mahali pake sana.

Hana wasaidizi. Wasaidizi ambao tuliwakataa hapa Bungeni ni wa vyama vyote *including* CCM, ambapo CCM imekuwa inaleta watu wake kutoka huko wanakuja wanaka kwenye maofisi hapa; CHADEMA walikuwa wanaleta watu wake, wanakuja kukaa kwenye maofisi yetu hapa. Tukasema hapana, kwa ajili ya usalama wa Wabunge wakati huu na sasa sababu zimezidi za *Corona* na na kadhalika, wageni wote marufuku. Kwa hiyo, kuliandika hili sidhani kama ni sawa sawa.

Kwa hiyo, kujenga hoja kwamba hana wasaidizi siyo kweli kwa sababu anao wasaidizi wanne, ana ofisi na ana bajeti. Wasaidizi hao wanne kwa kumbukumbu zangu kwanza ni *Principle Officer* wa Bunge, anakuwa *attached pale* kwa ajili ya *ku-manage* mambo yote *including finances* na kadhalika. Anakuwepo *Secretary*, anakuwepo Mhudumu na Dereva. Wote hao wanne anastahili na ninaamini anao *unless* nipaye taarifa. Ni mambo ya *admiration* tu kama kuna shida yoyote katika haya.

Kwa hiyo, nashauri sana, hebu tujielekeze kwenye *subject matter*, tupinge tukosoe, tufanyeje *there is no problem*, lakini kulifanya Bunge kuwa ni mahali pa uzushi uzushi, maneno yasiyokuwa na mbele na nyuma haifai. Kwa hiyo basi, kwa mamlaka nilyonayo, sitaruhusu hotuba hii kusomwa humu Bungeni kwa sababu inavunja kanuni kadhaa. Pia zinazokuja huko mbele, zikiwa za aina hii itakuwa hivyo tena. (*Makof!*)

Hizo dakika 20 mtakuwa mmezipoteza, lakini mimi kama Spika nakupeni Dakika 10 za uchangiaji za ziada. Mchangiaji wenu ni mmoja, lakini nitawapeni dakika 10 za ziada, mkitaka hata Halima mwenyewe ambaye ndio Kiongozi, sasa utachangia kama wewe hizo dakika 10. Ukitaka

I give you that opportunity. Vile vile, tunaendelea na uchangiaji.

Sasa katika uchangiaji, wa kwanza ni Mheshimiwa Allan Kiula, atafuatiwa na Mheshimiwa Rashid Shangazi. Mheshimiwa Allan Kiula, dakika kumi kumi. (*Makofi*)

MHE. ALLAN J. KIULA: Mheshimiwa Spika nashukuru kwa kunipa nafasi nami niweze kuchangia hotuba hii ya Waziri Mkuu. Nashukuru sana kwa sababu nakuwa mchangiaji wa kwanza na hili Bunge ni muhimu kwa sababu sasa tunamaliza miaka mitano.

Mheshimiwa Spika, cha pili, nampongeza Mheshimiwa Rais, Dkt. John Pombe Magufuli kwa kazi kubwa iliyofanywa na Serikali ya Awamu ya Tano; na Waziri Mkuu alipokuwa anatupitisha kwenye hotuba yake, alikuwa anatembea kwenye kazi ambazo zimefanyika. Ni kazi ambazo unaweza ukaziona kwa macho, ukazigusa na ukapapasa. Kwa hiyo, hayo siyo maneno matupu ila kazi zilizofanyika. (*Kicheko*)

Mheshimiwa Spika, napongeza Viongozi Wakuu wa Serikali akiwepo Makamu wa Rais. Vile vile siyo kwa umuhimu, lakini nikupongeze wewe Mheshimiwa Spika kwa kutuongoza kwa miaka mitano. Mambo mengi mazuri yamefanyika na mambo makubwa yamefanyika. Hili linalozungumzwa "Bunge Mtandao" watu waliona haliwezekani, lakini leo hii hata sisi tulikuwa tunafikiri Bunge baada ya *Corona* tutaendanalo vipi? Sasa jinsi uliviyolipima na kuliratibu Spika, basi umekuwa Spika mahiri sana. Nakupongeza sana. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, pamoja na pongezi hizi, naanza kwa kuunga mkono hoja iliyowekwa mbele yetu. Yako mambo ambayo ningependa kuyazungumza kidogo, kutokana na mazingira tuliyonayo sasa hivi na angalizo langu liko kwenye suala la mapato; tuna sehemu ya matumizi na mapato. Leo hii wakati hotuba hii imesomwa, tuna

changamoto ya ugonjwa huu, janga la *Corona* ambalo janga hili limefanya sekta nyingi zisimame au zisifanye kazi.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, pamoja na kwamba tunapitisha bajeti hii, nashauri sana Ofisi ya Waziri Mkuu na Wizara zinazofuata, pesa tutakazopelekewa wazitumie kwenye maeneo muhimu kwa sababu hatuna uhakika kama *flowya* hizo pesa itaendelea hivi, kwa sababu mchango wa sekta mbalimbali za kiuchumi ikiwepo utalii, madini na sehemu nyingine tunaona kwamba zinaathirika na hili janga. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, baada ya angalizo hilo nampongeza Mheshimiwa Rais kwa hatua alizochukua za suala nzima la kuangalia namna ya kudhibiti janga hili la *Corona*. Jambo la muhimu hapa ni usimamizi; tunasimamia vipi hizo hatua ambazo tumejiwekea sisi wenyewe? Hilo ni jambo muhimu sana, maana hii *social distancing* inatupa shida kidogo, lakini ni utamaduni ambao tunatakiwa tuuchukue.

Mheshimiwa Spika, tukifuatilia hotuba ya Ofisi ya Waziri Mkuu, yako mambo mengi yamezungumzwa, kazi nyingi zimefanyika, zile nguzo kuu za uchumi ambayo ndiyo mafanikio ya Serikali ya Awamu ya Tano zimeelezwu kikamilifu na hatua ambazo tumefikia. Sasa pamoja na mafanikio tuliyoyapata, tukienda kwenye suala la miundombinu; ujenzi wa reli ya mwendo kasi na maeneo mengine, kwa sababu Ofisi ya Waziri Mkuu inaratibu, basi zile rasilimali inatakiwa zisimamiwe kikamilifu ili miradi hiyo isiweze kuathirika na hali inavyoendelea sasa hivi. Nazungumza hali ya kiuchumi inavyoendelea.

Mheshimiwa Spika, Sekta mbalimbali zimegusiwa katika hotuba hii. Nikigusa Sekta ya Kilimo, Sekta ya Kilimo ni sekta muhimu sana. Kwa hiyo, tunamba Ofisi ya Waziri Mkuu ikaratibu Sekta ya Kilimo lakini imtambue mkulima mdogo, pia twende mpaka chini tumwangalie mkulima mdogo tuone tunamsaidia vipi? Kwa sababu tunapozungumza viwanda, malighafi zinatoka huko chini kwa wakulima wadogo

wadogo ambao ni wengi. Kwa hiyo, ni jambo muhimu sana. Tunashauri jicho la karibu liweze kutupiwa huko.

Mheshimiwa Spika, tukienda kwenye Sekta ya Elimu, mambo makubwa yamefanyika na mafanikio makubwa yameweza kufanyika. Yapo mambo kadhaa ambayo inabidi yaangaliwe kwa karibu. Elimu bila ada imekwenda vizuri sana isipokuwa tumekuwa na changamoto ya miundombinu kwa maana ya madarasa, nyumba za walimu na walimu wenyewe. Kwa hiyo, ni eneo ambalo linatakiwa liangaliwe kwa karibu sana kwa maana ya uratibu. Wizara husika inafanya kazi vizuri, lakini eneo hilo linatakiwa liangaliwe vizuri likiwepo suala nzima la uratibu wa mikopo ya elimu ya juu. Hilo ni jambo muhimu pia.

Mheshimiwa Spika, Sekta ya Maji na yenyewe inahitaji kuangaliwa kwa karibu sana. Takwimu zimetolewa hapa zinaonyesha tunapiga hatua nzuri na tunaipongeza Serikali kwa hatua inazochukua na kwa uwekezaji mkubwa unaofanyika kwenye Sekta ya Maji, isipokuwa bado uko umuhimu wa kuhakikisha kwamba rasilimali kwenye Sekta ya Maji zinaongezeka hili tatizo hili liweze kutatuliwa. Tumeona kwamba maji vijijini sasa hivi ni asilimia 64, kwa hiyo, tunatarajia kwamba asilimia hiyo iweze kuongezeka kuititia huo Mfuko wa Maji.

Mheshimiwa Spika, miundombinu imezungumziwa. Atakuja Waziri mhusika kuzungumza habari ya miundombinu hapa, ninachokiona, mwaka huu tumepata mvua nyingi. Mvua hizo zimeharibu sana miundombinu kama barabara na madaraja. Kwa hiyo, chochote ambacho tutakuwa tumekipanga hapa kitakwenda kwenye miundombinu, lakini hakitakwenda kwenye kutengeneza miundombinu mipya, itakwenda kwenye kukarabati miundombinu hii. Kwa mfano, daraja la Kiyegeya halikuwepo kwenye mpango, lakini sas limeshatumia rasilimali kubwa. Kwa hiyo, suala hilo na lenyewe inabidi liangaliwe kwa ukaribu tuweze kuona tunasonga mbele vipi. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, nimesema suala nzima la ukusanywaji wa mapato, sasa ni muda muafaka kabisa kupanua wigo lakini na Halmashauri zetu kuziwezesha. Siku za nyuma katika bajeti zilizopita, Halmashauri ziliombwa ziandike miradi ya mikakati; jambo hilo lilikwenda baadaye likasimama kidogo, lakini tunaiomba Ofisi ya Waziri Mkuu iweze kusimamia hilo jambo hili Halmashauri ziwe na hiyo miradi ya kimkakati ili ziweze kuzalisha mapato zaidi.

Mheshimiwa Spika, tukienda Sekta ya Afya, kazi kubwa imefanyika na takwimu kwenye hotuba ya Waziri Mkuu zimeonyeshwa dhahiri. Nami namshukuru Waziri Mkuu alifika hata Jimboni kwangu kule, alikagua hiyo Sekta ya Afya na alifanya kazi kubwa sana. Sasa hizo hospitali zilizojengwa zinahitaji vifaa na zinahitajika zianze kufanya kazi. Kwa nguvu kubwa iliyowekwa na ofisi zote kuanzia Mheshimiwa Rais, Ofisi ya Waziri Mkuu, sasa inatakiwa ionekane kule kwa wananchi kwamba hizo hospitali, zahanati na vituo vya afya, vinafanya kazi kwa kupelekewa vifaa.

Mheshimiwa Spika, fursa za uwekezaji zimezungumzwa kwenye hotuba ya Waziri Mkuu. Tumeweke nguvu sana na msukumo mkubwa kupata wawekezaji, mimi niseme wawekezaji wa nje. Sasa ni muhimu tukangalia namna ya kuwawezesha wawekezaji wa ndani, kuwawekea mazingira mazuri waweze kupata mikopo kwenye mabenki au kwenye taasisi nyingine za fedha lakini pia hata kuwasaidia kuona maeneo ambayo wanaweza...

(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)

SPIKA: Ahsante sana Mheshimiwa Allan.

MHE. ALLAN J. KIULA: Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja.

SPIKA: Ahsante Sana kwa kutufungulia kipindi cha uchangiaji kwa Bunge hili la bajeti la mwisho.

Mheshimiwa Rashid Shangazi nilishakutaja, atafuatiwa na Mheshimiwa Raphael Michael, Mbunge wa Moshi Mjini.

MHE. RASHID A. SHANGAZI: Mheshimiwa Spika, ahsante sana kwa nafasi hii ya kuwa mchangiaji katika bajeti hii ya Waziri Mkuu. Binafsi nianze na pongozi kwa Serikali yetu ya Awamu ya Tano chini ya Mheshimiwa Rais Dkt. John Pombe Magufuli kwa kazi kubwa ambayo inafanyika na inaendelea kufanyika na pia wasaidizi wake wa karibu, Mheshimiwa Makamu wa Rais, Mama Samia Suluhu Hassan, Kiranja mkuu wa shughuli za Serikali, Mheshimiwa Kassim Majaliwa Majaliwa anafanya kazi kubwa sana ambayo kila mwenye macho anaona na asiye na macho anaweza akapapasa hatua kubwa za maendeleo ambazo zimefikiwa katika awamu hii. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, kipekee pia nakupongeza wewe mwenyewe kwa namna ambavyo unaendesha Bunge letu Tukufu. Mara nyingi sana binadamu mpaka asiwepo ndiyo sifa zake zinaelezwa kedekede, lakini ni vizuri zaidi tukazieleza sifa hizi wakati wewe mwenyewe ukiwa unashuhudia. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, katika awamu hii ambayo tumekuwa na Bunge mtandao, kwa kweli nilikuwa nataniana na ndugu yangu Musukuma hapa, alikuwa anasema, hivi huyu mtani wako naye ana utabiri kidogo? Maana alituletea falsafa hii ya Bunge mtandao, halafu mwaka huu tukakutana na changamoto ya *Corona*. Sasa unaweza ukapata wateja safari hii kuhusu utabiri wa uchaguzi unaokuja, kwa sababu umeonekana katika eneo hilo ni mahiri. (*Makofi/Kicheko*)

Mheshimiwa Spika, nianze kuchangia bajeti iliyoko mbele yetu katika eneo la fungu 37 - Ofisi ya Waziri Mkuu haswa suala la linalohusu Mfuko wa Maafa.

SPIKA: Eh, Nilikuwa namsikiliza vizuri sana Mheshimiwa Shangazi alipokuwa hasa anatamka neno *Corona*, kwa sababu wao kule wanasesma *Coona*. Mheshimiwa endelea. (*Kicheko*)

MHE. RASHID A. SHANGAZI: Mheshimiwa Spika, ni kweli kabisa. Kule tunazo *Coona* za kuchakata mkonge.

Mheshimiwa Spika, Fungu Na. 37 - Ofisi ya Waziri Mkuu linahusu maafa, lakini kwa muda mrefu sasa hatuoni ukiwekewa fedha kiasi kwamba limekuwa ni tatizo kubwa sana. Mwaka huu tumejapata neema ya mvua nyingi katika nchi yetu na hasa mikoa ya kaskazini na mashariki. Kwa kweli watumishi wa Serikali wamekuwa wakipata shida sana katika eneo hili la maafa kwa sababu hakuna hata zile pesa za mwanzo za kufanya *intervention*. Hata Mwenyekiti wa Kamati ya Katiba na Sheria Mheshimiwa Mchengerwa, tumeona wiki mbili hizi akiwa amepanda kwenye boti anazunguka katika maeneo mbalimbali huko Rufiji, lakini unamwona yeze kama Mbunge, hata huwezi kumwona DC wala watu wengine. Kwa hiyo, unaona kabisa ni tatizo la kutokuwa na fedha katika Mfuko huu wa Maafa. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, naomba sana Mheshimiwa Waziri eneo hili tulitafutie mwarobaini wa kudumu. Tutafute vyanzo vya uhakika vya kuweza kuweka pesa katika Mfuko huu wa Maafa. Tena ikiwezekana zipatikane hata kwa asilimia, kwa sababu majanga ni mengi yanayotokea nchi hii. Tumeona tu kwa mfano kwa mwaka huu wa fedha ambao tunaenda kuukamilisha, tulianza na tatizo la nzige; kulikuwa na tishio la nzige, lakini Mwenyezi Mungu ameepushia mbali, hawakuingia katika nchi yetu. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, sasa tumekutana na changamoto ya mvua, hali ya barabara zetu siyo nzuri huko vijijini, kiasi kwamba kwa ile asilimia 30 TARURA wanaipata naamini katika eneo hili mwaka huu haiwezi ikatosha, hivyo inaweza ikaadhiri hata namna ya usafirishaji wa vifaa mbalimbali wakati wa uchaguzi. Kwa hiyo, tunaomba eneo hili tulitizame kwa kina sana.

Mheshimiwa Spika, eneo lingine ningetaka nilizungumze ni eneo la kuhusu anuani za utambulisho wa makazi (*post code*). Hili ni eneo ambalo limeanza Dar es

Salaam kama *pilot study*, lakini eneo hili nalo limefika mwisho na waliokuwa wanasi mamia mradi huo ambao ulikuwa ni *pilot* ni *TCRA* kuititia Wizara ya Mawasiliano na Uchukuzi.

Mheshimiwa Spika, sasa tungeweza kuoanisha Mfumo wa Utambuzi wa Makazi pamoja na Vitambulisho vya Taifa, ingekuwa na maana sana; kwa maana kwamba mtu anakuwa anatambulika kwa anuani ya makazi lakini pia na kitambulisho cha Taifa, kiasi kwamba hata kuzuia uhalifu inakuwa rahisi kwamba unafahamu kwa kuititia kitambulisho hiki, huyu mtu anaishi maeneo gani na mambo mengine hata katika mifumo ya kibashara na mambo mengineyo.

Mheshimiwa Spika, pia katika eneo hili tumeona kabisa kwamba kwa mfano kwa Mkoa wa Dar es Salaam, wenzetu wale wenye utaratibu wa *taxizile* za *UBA* unasa idia sana kiasi kwamba mtu popote alipo kwa sababu kwa Dar es Salaam wameshaingiza kwenye mtandao na ipo mpaka kwenye *google* unapata, inasa idia hata kurahisisha biashara.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, tunatamani sana kwamba hili eneo la utambuzi wa makazi liwe eneo la nchi nzima ikiwezekana, eneo hili liendelee lakini pia liunganishwe na mfumo wa vitambulisho ili hata mtu anapohama eneo moja kwenda lingine, inaweza kuwa ni rahisi kufuatilia vitambulisho vya Taifa na pia kuititia anuani za makazi.

Mheshimiwa Spika, eneo lingine ambalo ningetaka kuzungumza ni hili la *NIDA*, katika eneo la watumishi. *NIDA* wana watumishi wachache sana nitatoa mfano kwa Wilaya ya Lushoto ambayo ina takribani watu 600,000 inao watumishi watatu tu wa *NIDA* katika wilaya nzima. Sasa utaona kwamba wale wazee walioko vijijini watu wenye shida mbalimbali zikiwemo za ulemavu hawawezi kufika Lushoto au wengine inabidi watumie gharama kubwa kwenda kufatilia vitambulisho hivi sasa tungependa kuona kwamba angalau hili liangaliwe ikiwezekana waongeze idadi ya watumishi lakini pia wapatikane hata watumishi wa kuwasaidia wasaidizi maana tumezungumza hili eneo la wasaidizi na wenyewe wanajitetea kwamba hawana mafungu. Kwa hiyo, ni vizuri

wakawekewa mafungu ya kutosha ili na eneo hili nalo waweze kutusaidia vizuri.

Mheshimiwa Spika, eneo lingine ambalo ningependa kushauri ni katika uanzishwaji wa mfuko wa ugharamiaji elimu kwa maana ya *student loan fund* tunatumia pesa nyngi sana kila mwaka ambazo ni lazima zitengwe kutoka hazina lakini kama tutaanzisha mfuko mahususi wa kugharamia elimu maana yake Serikali pamoja na wadau mbalimbali katika taasisi za kifedha kama mabenki lakini pia ni mifuko ya hifadhi wanaweza wakatengeneza mpango wa ku-*capitalize* pesa katika mfuko hata kwa muda fulani na baadaye sasa mfuko huu ukawa unakopesha wanafunzi kwa ngazi hata ya diploma na *degree* lakini pia hata wa digrii ya pili na hata wa udaktari. Ili sasa tuondokane na hii hali ya kuweka pesa kila mwaka shilingi bilioni 500 nakadhalika nadhani tukiweza kutengeneza eneo hilo tukalltengenezea mpango mahususi hata kwa kutumia mikopo nafuu kutoka vyanzo vingine vya kimataifa mikopo ya muda mrefu inaweza likawa ni eneo ambalo tunaweza tukaondoka na hii adha ambayo kila mwaka lazima tutenge bilioni 500 kwa ajili ya kusaidia wanafunzi katika eneo hili.

Mheshimiwa Spika, lakini katika nukta hiyo ningependa sana kupongeza Benki ya Dunia kwa kutuachia ule mkopo wa milioni 500 *US Dollar* ambaao kwa kweli ni kazi kubwa sana imefanywa na Mheshimiwa Waziri mwenye dhamana Mambo ya Nje tunakupongeza sana pia watanzania kwa pamoja tunashukuru sana kwa mkopo huu kwa sababu hapo mwanzo ulikuwa na figisu nyngi za baadhi ya watu kukosa uzalendo lakini kwa nukta hii tunashukuru sana kwa msaada huu tunaamini kwamba msaada huu utaenda kuongeza tija katika utoaji wa elimu yetu hapa nchini.

Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana ahsante sana kwa nafasi hii. (*Makofii*)

SPIKA: Ahsante sana Mheshimiwa Rashid Shangazi na hasa hapo ulipomalizia ndio penywewe kabisa. Kama Spika

tunamsubiri rafiki yetu aje atuambie hela tume pata sasa jimboni kwako isijengwe Sekondari si ndio uliv yotaka aje atujibu hapa au Kigoma kama mko a zisiende ahsante sana nishamtaja Mheshimiwa Raphael Michael atafatiwa na Mheshimiwa John Kadutu, na Mheshimiwa Masoud jiandae.

MHE. RAPHAEL J. MICHAEL: Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi hii ya uchangiaji katika hotuba hii ya Mheshimiwa Waziri Mkuu. Nilikuwa nataka nijikite kwenye baadhi ya mambo machache lakini jambo moja kubwa la kwanza ni janga la ugonjwa huu wa Corona ambalo limekumba dunia Tanzania ikiwa ni mojawapo. Nilikuwa na ushauri kidogo kwa Serikali kwamba ni lazima tuongeze bidii katika zile hatua ambazo zilishachukuliwa lakini lazima tuongeze bidii ya kusukuma hatua zingine zaidi ili tujitahidi kuzuia janga hili lisije likaingia nchini kwa kiwango ambacho limeshaingia katika mataifa mengine nadhani kwa uwezo wa uchumi wetu hatutakuwa na uwezo wa kukabiliana nalo.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo nilikuwa nashauri jambo la kwanza ni lazima tuone namna ya kupata fedha kwa namna yoyote kupitia njia zozote zile za kibajeti na zile ambazo sio za kibajeti labda za kutumia wadau mbalimbali tupate fedha kwa ajili ya kuweza kununua vifaa vya upimaji angalu watu wengin kadri iwezekanavyo waweze kufikiwa na vipimo ili tujuu kiwango cha watu walivyoathirika katika Taifa hili.

Mheshimiwa Spika, mpaka sasa tunaweza tukaamini kwamba tuna watu wachache sana amba o ni wagonjwa lakini hatuna uhakika kulingana na vipimo bali kuto kana na hali ya kuibuka kwa wagonjwa ambako inawezekana bado wagonjwa wengi wamejificha ndani. Kwa hiyo, ni vizuri tukajua kiwango ambacho tuna maambukizi ili tuweze kukabiliana nayo kwa haraka kadri iwezekanavyo kabla ya kuruhusu hii jambo likawa kubwa katika jamii yetu.

Mheshimiwa Spika, jambo la pili ni kuona namna ambavyo hata vifaa hivi vya kunawia mikono vinavyoweza

kupatikana katika maeneo mbalimbali mpaka sasa hivi hivi vifaa vinapatikana kwa watu wenyewe uwezo fulani, kwa kundi fulani. Lakini walio wengi bado hawajaweza kufikiwa na hivi vifaa.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, watu sasa hivi wanachukua sabuni wanajitahidi kunawa lakini je hizi *defectant* ambazo zinatakiwa zitumike kwa kiwango gani zimefika kwa jamii yetu ni suala la Serikali kusukuma hili ili tuone namna ambavyo tunatumia Serikali zetu za mitaa, wakurugenzi wetu, watendaji wetu wa kata tuone jinsi ambavyo tunaweza tukasaidiana ku-*mobilize* watu hata wadau mbalimbali wachangie kuhakikisha kwamba hata watu wa chini wanafikiwa na huduma hii ili tupunguze uwezekano wa haya maambukizi. Pia elimu iende kwa upana zaidi kuliko inavyoenda sasa kuna jitihada zipo lakini tuongeze jitihada zaidi katika elimu.

Mheshimiwa Spika, jambo lingine ni kuangalia athari zake kiuchumi, janga hili kwa sura yoyote ya kawaida lazima litakuwa na athari za uchumi katika Taifa. Tunavyozungumza sasa nina hakika kabisa kwamba sekta ya utalii itakuwa imeathirika sana na wafanyabiashara wengi wa utalii kwa vyovyyote vile watakuwa tena hawapokei watalii. Shirika kama la ndege litakuwa limeathirika sana na watu wanaopeleka bidhaa nje watakuwa wameathirika, watu wanaoingiza bidhaa kutoka nje watakuwa wameathirika. Kwa maana hiyo hata wafanyabiashara wa ndani ya nchi watakuwa wameathirika kwa kiwango fulani sasa tunapimaje hiyo adha na hiyo hali manake *slogan* yetu kubwa kama Serikali ni kukusanya kodi lakini tunatakiwa tukusanye kodi kwa watu wenyewe uwezo wa kulipa kodi, tunasaidiaje hao watu ili angalau wapungukiwe na huo mzigo unaotokana na adhari wanayopata kiuchumi.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, ni vizuri Serikali ingekuwa inakaa na wataalam wake kupima adhari za kiuchumi za tatizo hili na kuona jinsi ambavyo wanaweza kuchukua hatua za kusaidia watu wetu katika athari hizi za kiuchumi, kwa sababu wenzetu wa Rwanda wameshafanya, wenzetu wa

Kenya wameshafanya baadhi ya hatua kiuchumi tumefanana nao kwa kiwango fulani. Kwa hiyo, nadhani tunaweza tukachukua baadhi ya hatua tukiangali wenzetu wanavyofanya na zile ambazo tunaweza tukachukua ndani yetu sisi wenyewe. Kwa hiyo, nilidhani kwamba tunapaswa kulipima hili janga kwa uzito unaostahili ili watu wetu wasumie, wafanyabiashara wetu wasumie na wananchi wetu wa kawaida pia wasumie.

Mheshimiwa Spika, nilitaka nizungumze suala la uchaguzi mkuu, tunaenda kwenye uchaguzi kulingana na hotuba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu kwamba tunaenda kwenye uchaguzi mkuu mwaka huu Octoba. Ni vizuri tukajitambua kwamba hapa ndani sote ni watanzania na kujitambua kwamba wote tuna haki ya kufurahia matunda ya uhuru wa Tanzania. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, ni jambo bay a sana kama watanzania kutakuwa na kundi linaloamini kwamba lenyewe ni bora zaidi kuliko kundi lingine katika nchi moja. Kwa hiyo, ni vizuri kwanza *sense* yetu wote mawazo yetu tubaki pale ambapo mwasisi wa Taifa hili alituweka miaka yote kwamba sisi wote ni watanzania. Mifumo hii ya vyama vya siasa isiwe sababu ya kutubagua na kutugawanya, mifumo ya vyama vya kisiasa iwe ni sababu ya kutuunganisha na kuweka mawazo mbadala kusukuma Taifa hili mbele. Sasa kama tutatafsiri vinginevyo mifumo hii ya vyama vya kisiasa ikatubagua ikaonekana kuna watu bora kuliko wengine katika Taifa moja maana yake tunalipeleka Taifa hili mahali ambapo sipo mahali ambapo si salama kabisa. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, tuna amani ambayo tumejenga kwa miaka mingi sana amani hii haikuangauka imejengwa kwa nguvu za watu na kwa jitihada za watu ni lazima amani hii ilindwe kwa nguvu zote. Mara nyingi chaguzi zimekuwa ndio sababu ya kuvunja amani ya Taifa, amani za nchi, kuvunja umoja wa watu. Kwa hiyo, ni lazima tukubaliane kama kuna watu wanaonung'unika wanaoamini kwamba kuna mambo ambayo hayaendi sawasawa ndani ya Taifa letu tusijadili kwamba wanaonung'unika ni akina nani

tusiwaangalie kwa itikadi ya vyama vyao vya kisiasa kwa dini zao wala makabila yao tuwaangalie kama watanzania na tuwasikilize. (*Makof!*)

Mheshimiwa Spika, kilio kikubwa cha watanzania hao wanaoonekana wanapenda kulalamika ni Tume huru ya uchaguzi lazima tuijulize tume hii maana yake tukijadili hapo mara nydingi majibu ya Serikali ni kwamba mbona na nyie mlishinda na nyie mko huku ndani. Ni kweli tulishinda lakini tukishinda kwa ngarambe hatukushinda kirahisi. (*Makof!*)

Pili, angalau hata mazingira yale ya kipindi yalikuwa yana nafuu sio mazingira ya sasa ambapo msimamizi wa uchaguzi anaweza akaondoka kwenye ofisi yake asipokee fomu za mgombea. Anaweza akakataa fomu za mgombea, polisi anaweza akaingia mahala akafanya vurugu yoyote kusumbua mawakala sio hali hiyo illiyokuwa huko nyuma, kulikuwa kuna shida lakini zilitakuwa sio kwa kiwango hiki. Sasa sisi tunachokiomba ni kwamba uchaguzi huu uwe huru na uwe huru kweli, ili kila mmoja aridhike.

Mheshimiwa Spika, tunaamini kuna mambo ambayo yamefanyika ambayo siku zote tunasema ni mazuri yamefanywa na awamu hii sasa kwa maana hiyo twendeni kwenye uchaguzi ulio haki na uhuru. Kwa hiyo nilidhani kwa machache hayo nikushukuru kwa nafasi hii ahsante sana.

SPIKA: Ahsante sana Mheshimiwa Raphael Michael Mbunge wa Moshi Mjini, Mheshimiwa John Kadutu nilikutaja, Mheshimiwa Masoud Abdallah Salim jiandae.

MHE. JOHN P. KADUTU: Mheshimiwa Spika, nikushukuru kwa nafasi lakini nianze kukupongeza wewe mwenyewe kwa miaka mitano hii umetuvumilia sehemu kubwa ni kipindi chetu cha kwanza yawezekana mara moja mara mbili labda tulikosea hata kanuni umeendelea kutuvumilia, kwa kweli nafikiria namna ya kuja kukusaidia kampeni kule Kongwa. Pia nimpongeze Mheshimiwa Waziri Mkuu kwa kuiongoza Serikali hapa Bungeni lakini kwa kuja kututembelea Ulyankulu.

Wewe kule ni kwako na tuendelee kukuomba ukipata nafasi uje, bado watu wanakukumbuka sana. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, baada ya pongezi hizo nianze na Tume ya Uchaguzi na jambo hili nitaendelea kulisema hata nje ya Bunge mpaka pale tutakapopata ufumbuzi. Mwaka 2015 wakati wa uchaguzi kundi kubwa la watu wetu kule Ulyankulu hawakupiga kura za madiwani na kwa kweli ililetu sintofahamu sana mpaka leo hawajapiga kura kisingizio ni raia wapya lakini kule Katumba na Mishamo ni raia wapya lakini waliweza kupiga kura. Tumefatilia jambo hili kila wakati hatupati majibu na kila wakati nasema hapa na inawezekana Waheshimiwa Wabunge wakawa wanashangaa Kadutu alishang'ang'ania hiyo hoja hapana karibu asilimia 70 ya wapiga kura wa Ulyakulu wanatoka kwenye eneo hili ambalo halikuruhusiwa kupiga kura ya madiwani.

Mheshimiwa Spika, lakini mwaka huu watu hawa hawakuruhusiwa kupiga kura ya Serikali za Mitaa kwa maana ya mwaka jana Novemba hata kuandikishwa na sasa haijajulikana kama watapiga kura au wataendelea tu kukaa kimya au wataendelea kutupigia kura Wabunge na Mheshimiwa Rais.

Mheshimiwa Spika, nilikuwa nadhani jambo hili lifikie mwisho Kamati yetu ya Bunge ya Mambo ya Nje na Usalama imekuwa inajadili TAMISEMI inajadili na bahati nzuri Mheshimiwa Waziri Mkuu unalifahamu jambo hili hebu huko Serikalini limalizeni ili na wengine tupate hoja zingine kwa sababu kila ukifika kule swalii ni hilo, Mheshimiwa Kadutu tutapiga kura au hatupigi kura hawana maswali mengine, je tutaendelea kuishi hapa au tutahamishwa, je wale ambao hawataki uraia wa Tanzania na hawataki kurudi Burundi wataondoka lini? Je, kambi ya wakimbizi na hizo zingine zitafungwa lini? Ni jambo ambalo linawapa shida sana ndugu zangu hawa. Lakini ni lazima tufikirie kama tumewapa narudia tena tuliwapa uraia kwa roho safi basi tuwaruhusu na kama kuna uamuzi tofauti wa Serikali uje badala ya watu kukaa hawajui kinachoendelea hawajengi hawafanyi shughuli

kubwa za kiuchumi na mnajua wenzetu wale na sisi wenyewe ni wazalishaji wazuri wa mazao. Tunalisha Kahama, Shinyanga, Mwanza kama mtu anabisha asimame hapa.

Mheshimiwa Spika, nzungumzie habari ya kilimo, kwenye kilimo nimshukuru tena Waziri Mkuu kwa kushughulikia kero za mazao na hasa tumbaku. Waziri Mkuu alijikita sana kuhakikisha tumbaku inasimama inakaa vizuri, vyama vyaa ushirika vinakaa vizuri lakini yawezekana Serikalini hamfahamu wiki iliyopita nilikuwepo jimboni nashuhudia kwa macho tumbaku inanunuliwa shilingi 100 mpaka 300 kutoka maalfu ya pesa sasa tumbaku inanunuliwa kwa dharau ile ni dharau. Huwezi kununua tumbaku kwa shilingi 100 kwa shilingi 300 na kama hutaki watu wanasema toa tumbaku ichomwe moto. Hivi kweli mtu msimu mzima masika yote ameshughulika na zao leo anakuja kuwaambiwa shilingi 100 au anaambiwa 300. 300 mtu ana kilo 1000 hakuna kitu pale nilombe sana Serikali isimame iongee nao hawa wenyewe makampuni wasifanye dharau na ni dhuluma, hii ni dhuluma. Mtu anachukua tumbaku kwa shilingi 300 kwa kweli ni dhuluma.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, Mheshimiwa Waziri Mkuu mimi nikucombe urejee tena uangalie namna ya kuwasaidia wakulima wa tumbaku vinginevyo kilimo cha tumbaku kitakufa na watu wataangalia tena habari ya mazao mengine. Lakini huko nyumba tumbaku ndio ilikuwa zao linalongoza kwa kuingiza pesa nydingi za kigeni. Leo hii sio kama ilivyokuwa zamani.

Mheshimiwa Spika, linalofanana nalo liko suala la mawakala wa mbolea limechukua muda mrefu toka tumeingia hapa Bungeni mawakala wa Mbolea wamejikusanya wanakuja Dodoma hawajapatiwa majibu. Yaliwahi kutoka majibu kwamba baadhi yao walifanya udanganyifu tukasema sawa lakini wapeni majibu wajue kwamba jambo hili liko mwisho na nani amekosema atolewe ambaa hawana makosa wafanye kazi hizo. Kero kama alivyosema mtani wangu mgosi Shangazi suala la *NIDA*, *NIDA* hasa vijijini ni tatizo hata huo usajili wa laini za simu umesumbua. Hebu Serikali ihakikishe ifanye tathmini watu

wameandikisha na wapya hawajaandikisha waandikishwe lakini Serikali itengeneze mpango mtoto anazaliwa apate usajili wa moja kwa moja tuepukane na jambo hili.

Mheshimiwa Spika, mwisho kabisa kwa sababu mengine tutakutana nayo kwenye Wizara wapo watu wanashangilia ligi ya mpira wetu kusimama. Niwaambie wenzenetu wale watoto wa mama mdogo, ligi hata ikisimama bingwa ni Simba.

Mheshimiwa Spika, nakushukuru. (*Makofi*)

SPIKA: Ahsante sana Mheshimiwa Kadutu na hasa ulivyomalizia! Nilishakutaja Mheshimiwa Masoud Abdallah Salim atafatiwa na Mheshimiwa Joseph Mhagama.

MHE. MASOUD ABDALLAH SALIM: Mheshimiwa Spika, nichukue fursa hii kwanza kumshukuru Mwenyezi Mungu Subhana Wataala aliyetulia uzima na afya nje ilikuwa bado siku 25 kufika mwezi mtukufu wa Ramadhan tumwombe Mwenyezi Mungu atufikishe salama wasalumini, tumwombe Mwenyezi Mungu atuepushe na janga la *Corona* ambalo linatukabili na sisi ni rai kwa watu wote duniani na watanzania rai yangu tuachaneni na dhambi ambazo zinamchukiza Mwenyezi Mungu tupunguzeni madhambi. Rai yangu kwa watanzania wote kwa imani na dini zote tuacheni dhambi dunia imebadilika, dunia imesimama.

Mheshimiwa Spika, baada ya hayo, machache sasa nianze kuchangia. Niendelee na mwenzangu alipomalizia kuhusu *Corona*. Ni vyema mkakati ukaongezwa zaidi kupambana na *Corona* na inaonekana vitakasa mikono (*sanitizers*), bei zake sasa zimekuwa zikiongezeka siku hadi siku. Ile ambayo ilikuwa inauzwa 1,500 kabla ya *Corona* sasa inauzwa 3,000 hadi 2,500 na ile ya 2,500 sasa ni 4,500 hadi 5,000. Ni ushauri wangu kwa Mheshimiwa Waziri Mkuu kwamba jambo hili ni jambo kubwa, Serikali haziko vijijini, elimu hakuna vijijini, viziba midomo navyo bei zimepanda. Niombi Serikali iingilie kati suala hili tuone kwamba tunafanyaje.

Mheshimiwa Spika, namwomba Mheshimiwa Waziri Mkuu, bajeti yake mimi sina pingamizi nayo sana. Katika bilioni zake ambazo zimetajwa tumpitishie ila kwa sababu yeye ana Mafungu tisa, sina pingamizi na Fungu 15 lakini pingamizi yangu iko na Fungu 27; *Registrar of Political Parties* (Msajili wa Vyama vya Siasa). Shida yangu iko kwenye Fungu 61 - Tume ya Taifa ya Uchaguzi, Fungu 41, Fungu 42 sina wasiwasi nalo, Mafungu 91, 92, 65, Mafungu yote tisa ambayo Waziri Mkuu anasimamia sina mapingamizi nayo, lakini Fungu 27 - *Registrar of Political Parties*; na Fungu 61 - Tume ya Taifa ya Uchaguzi, ni shida. Nasema hayo kwa sababu zifuatazo:-

Mheshimiwa Spika, Msajili wa Vyama vya Siasa yeye ni mlezi. Ningependa kuona kwamba Msajili huyu anakwenda vizuri na kuona kwamba vyama vyote ni sawasawa na sote ni Watanzania, lakini akitokea kiongozi yejote akianza kutoa matamshi ya uchochezi akisema kwamba tutashika dola mwaka huu kwa kutumia dola, tafsiri si nzuri. Hata vyovyote ambavyo yeye amekusudia lakini haijengi taswira nzuri ya ulinzi na usalama, si jambo jema sana.

Mheshimiwa Spika, si muda mrefu umesema hapana, mambo haya si mazuri, hotuba hii si nzuri, hii si nzuri, lakini mtu anasema tutashika dola kwa kutumia dola na nchi ambayo haikutumia dola kama vile *KANU* ikaondoka, hatufanyi kosa hilo; *why? Mambo gani hayo?* (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, kiongozi mkuu yeye haipaswi, mimi ningetarajia Msajili amuite amtake atoe maelezo kwa sababu vyama vingine vya Upinzani viongozi wakisema maneno mengine wanaitwa wanahojiwa wamekusudia nini, lakini sisi wapinzani tunaonekana kama vile sijui watu gani tumetoka nchi gani. Ushauri wangu kwa Mheshimiwa Waziri Mkuu, ushauri wangu viongozi kama hawa muanze kuwafanyia utafiti; ni kweli? Stori ni za kweli? Maana yake wana uchungu kweli na nchi hii? Ni shida.

Mheshimiwa Spika, Tume ya Taifa ya Uchaguzi; Mheshimiwa Waziri Mkuu wakati anatoa hotuba yake ambayo ni nzuri sana na alisema kwamba tunakwenda

kwenye Uchaguzi Mkuu na utakuwa huru na haki, lakini jambo la kwanza kabisa uchaguzi huru na wa haki ni Tume huru ya Uchaguzi. Tume huru ya Uchaguzi ni muhimu sana, kuanzia uandikishaji, tunakwenda kwenye kampeni, kwenye kupiga kura, kwenye kutangaza matokeo, lazima Tume ya Taifa ya Uchaguzi ifanye kazi yake kwa uadilifu mkubwa sana, vinginevyo kama hatutakuwa na Tume huru ya Uchaguzi uchaguzi hauwezi kuwa huru na wa haki tunaweza tukapelekana tena mahali ambapo sio pazuri sana.

Mheshimiwa Spika, nimwombe Mheshimiwa Waziri Mkuu awe makini sana na uchaguzi wa mwaka 2020. Kenya wana kitu kinaitwa *IEBC* (*Independent Electoral and Boundaries Commission*), uchaguzi wa Kenya huo. Kuna hofu gani kuwekwa kwa Tume Huru ya Uchaguzi? Tuige nchi jirani tu Kenya mipaka hii hapa.

Mheshimiwa Spika, nasema hivyo kwa uzoefu. Mimi nilikuwa mmoja wa Wasimamizi wa Uchaguzi wa Kenya, mimi nilikuwa Busia na Bungoma katika kaunti hizo, majimbo 16. Sasa kuna jambo gani? Nasema kwamba tubadilike tuone kwamba tunakwenda vizuri tuone kwamba kwa vyovoyote iwavyo tunapata utambuzi zaidi.

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Waziri Mkuu, lakini kwenye suala la *Corona* kuna jambo moja; mgonjwa kuthibitika kama ana *Corona* uthibitisho wake uko eneo moja tu la Hospitali ya Muhimbili peke yake. Mikoa yote hakuna kipimo hicho mpaka sampuli ipelekwe Muhimbili iende ikachunguzwe baada ya hapo ndipo inakuwa imethibitika kama mgonjwa huyo tayari ana maradhi ya *Corona*. Ushauri wangu; tuandae mazingira sasa angalau kila mkoa; tuna mikoa 32, sampuli ichukuliwe Kagera ipelekwe Dar es Salaam, kwa Wapemba wenzangu huko Dar es Salaam. Nimwombe sana Mheshimiwa Waziri Mkuu, hili liangaliwe. Nijambo kubwa kwelikweli, kujua afya zetu wakati huu ni muhimu sana. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, naomba niendelee, jambo lingine ambalo napenda niendelee ni suala zima la msongamano

wa wafungwa. Amesema Mheshimiwa Mbunge mmoja hapa; suala la msongamano wa wafungwa linachangiwa na mambo mengi lakini mpaka sasa Bunge letu limeshindwa kuweka ukomo wa upelezi. Msongamano wa wafungwa na mahabusu, mahabusu hadi sasa wanafika 17,000, wafungwa 15,000 jumla 32,000. Mahitaji ya magereza ni nusu tu lakini mpaka sasa sheria bado haijaweka wazi ukomo wa upelelezi. Kuna watu wako magerezani miaka mitatu, wako miaka mine, wako miaka mitano, wako miaka sita, wako miaka saba. Ukomo wa upelelezi uko wapi? Na huyo akithibitishwa kwamba hana kosa tayari alikuwa ameshafungwa.

Mheshimiwa Spika, Bunge hili sasa, naishauri Serikali, Mheshimiwa Waziri Mkuu sina pingamizi naye sana mimi maeneo yangu ni mawili makubwa, lakini lazima Bunge hili tutoke na jambo moja kubwa; kuwepo na ukomo wa upelelezi, watu magerezani wanateseka na ni kesi za kubambikiza, kesi zingine ni za kubambikiza, watu wanateseka, watu wanaumia, watu wamepoteza imani na Serikali kwa sababu gani, muda umekuwa ni mkubwa kesi zinaendelea unaambiwa upelelezi bado haujakamilika; kwa nini?

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Rais mwenyewe alipita magerezani huko akasema hawa fyekela mbali. Sisi Bunge tunashindwaje kuandaa mazingira ya kuweka ukomo wa upelelezi? Tutaendelea kuweka msongamano mkubwa, wanaendelea kula, wakati huu wa *Corona* sisi tuna *sanitizers*, wao amba wanalala kama pipi hivi? Sisi huku tunaambiwa tukae mbalimbali Wabunge, wewe kaa kule, wewe kaa kule, wewe kaa kule; wale kule magerezani mmekwenda mkaona? *Corona* hii, mmekwenda mkaona? Niishauri Serikali, lazima kuwepo na ukomo wa upelelezi kwenye shughuli hizi.

Mheshimiwa Spika, baada ya maneno hayo, nashukuru sana.

SPIKA: Ahsante Mheshimiwa Masoud Abdallah Salim. Tunakushukuru sana, umezungumzia mambo ya magereza lakini wewe huna uzoefu kule. Wenye uzoefu wa huko wala

hawajasema hayo unayosema. Nakushukuru sana Mheshimiwa Masoud huwa tunataniana kidogo. (*Kicheko*)

Umeisifia Tume ya Uchaguzi ya nchi jirani lakini wao wenyewe karibu wamalizane shingo kule mpaka mahakama yao ikasema huu uchaguzi, wakati mwingine mtu anaitwa tu *independent electoral* kumbe ni jina. Ndiyo maana sasa hivi wana kitu kinaitwa *Building Bridges Initiative* ili pamoja na mengine kurekebisha mambo ya namna hiyo. Hata hivyo, sio mbaya baadhi yenu wakipata nafasi, hata sio lazima iwe leo, hata siku nydingine yoyote, kueleza tume huru ya uchaguzi hiyo mnayoizungumza inafanananje kuliko mkitaja tu, hata akisimamishwa mtu yejote hapa harakaharaka anaweza akashindwa kuelewa huru ndiyo ipi na kadhalika. (*Makofii*)

Nilimtaja Mheshimiwa Joseph Mhagama. Kaimu kiongozi wa Upinzani bado hujanipa *indication* kama dakika kumi utazichukua au? Kama utakuwa tayari *just give me a nod.*

MHE. JOSEPH K. MHAGAMA: Mheshimiwa Spika, ahsante kwa kunipa nafasi ya kuchangia hotuba ya Waziri Mkuu. Kwanza nitumile nafasi hii kuipongeza sana Serikali ya Awamu ya Tano inayoongozwa na Jemedari Dkt. John Pombe Magufuli na wasaidizi wake akiwemo Mheshimiwa Waziri Mkuu kwa kufanya kazi iliyotukuka kwa Watanzania kwa miaka hii mitano. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, kwenye hotuba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu jambo kubwa ambalo limejitokeza ni dhana ya uchumi jumuishi (*inclusive economy*). Mfumo huu wa uchumi jumuishi ni uchumi ambaou unatoa fursa kwa Watanzania wote, kwa wananchi wote kuweza kunufaika nao. Dhana hii inatofautiana na dhana ya uchumi ambaou sio jumuishi (*extractive economy*) ambayo inawanyima fursa watu walio wengi kuweza kushiriki kwenye uchumi au kunufaika na uchumi. Unawakumbatia mabeberu wachache na mabepari, hautoi fursa kwa watu wengi na watu wa kawaida.

Mheshimiwa Spika, Serikali yetu kwa miaka hii mitano imekuwa inatekeleza dhana ya uchumi jumuishi na imekuwa inafanya hivyo kwanza kwa kujenga mazingira na miundombinu wezeshi inayomfanya kila Mtanzania aweze kushiriki na kunufaika na uchumi wa Taifa lake. Imefanya hivyo kwa kujenga miundombinu ya reli, sasa programu kubwa ya ujenzi wa reli za kisasa imeanza na hii ya *SGR* inayoendelea sasa ni hatua ya kwanza na naamini tutaendelea kujenga reli. Pia programu kubwa ya umeme. leo Serikali imefikia vijiji 9,001 kutoka vijiji 2,118; ni *achievement* kubwa sana. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, katika kutafsiri hii dhana ya uchumi shirikishi, Serikali imewekeza kwenye usafiri wa anga ili Watanzania waweze kujenga uchumi wao kwa kusafiri kwa haraka na kufanya mambo mengine ikiwemo uchumi wa utalii, lakini pia dhana hii tunaitafsiri kwenye namna ambavyo Watanzania wananaufaika na ukuaji wa uchumi. Tunaona uchumi wetu unakua kwa asilimia 6.9. Kwenye maisha ya Mtanzania ananufaika nao vipi? Serikali imefanya kazi za kutukuka kwenye eneo hili. Leo tuna huduma za afya kwa kupitia vituo vya zahanati zaidi ya 1,198, Watanzania kwa maelfu wanapata huduma huko. Lakini tuna vituo vya afya, hospitali 69 mpya na hospitali za rufaa kumi, hiyo ni sehemu tu ya tafsiri ya ukuaji wa uchumi ambao umejengwa na Awamu hii ya Tano.

Mheshimiwa Spika, hata hivyo nina ushauri wa mambo ya nyongeza kwa Serikali; kazi iliyofanyika ni kubwa sana, tumeona uchumi unakuwa na miundombinu inakuwa na mazingira wezeshi ya kiuchumi yanajengwa na Watanzania wananaufaika na uchumi wao. Hata hivyo kuna mambo ambayo Serikali inapaswa kwenda kuyatifikari.

Mheshimiwa Spika, ukiangalia takwimu za ukuaji wa uchumi ambao tumesema unakuwa kwa asilimia 9.9, sekta zilizochangia ukuaji huo zinatofautiana kwa umuhimu lakini Sekta ya Kilimo, Mifugo na Uvuvi ambayo inaa jiri asilimia 64 ya Watanzania ukuaji wake ni asilimia 3.6 wakati sekta zingine ambazo zimechangia kwenye ukuaji wa uchumi wa Taifa letu

kama ujenzi unakua kwa asilimia 14.8, mchango wake kwenye ajira ni asilimia 2.42.

Mheshimiwa Spika, ukiangalia uchukuzi, unakua kwa asilimia 8.8 lakini mchango wake kwenye ajira za Watanzania ni asilimia 2.94; ukiangalia huduma za usambazaji maji vijijini mchango wake kwenye ajira ni 0.05. Tafsiri yake ni nini; tafsiri yake eneo ambalo linawagusa Watanzania wengi ambaao ni asilimia 64 mchango wake wa ukuaji ni mdogo sana ambaao ni asilimia 3.6. Niiombe sana Serikali; dhana ya uchumi shirikishi ni kuwafikia hawa Watanzania walio wengi ambaao sehemu kubwa ya maisha yao wanategemea kilimo. Nikiri, Serikali imefanya kazi kubwa kwenye kilimo, lakini kazi bado haijawkisha. Niiombe Serikali tunavyoendelea na mchakato huu wa bajeti ifikirie sasa kwenda kuwekeza zaidi kwenye kilimo.

Mheshimiwa Spika, pili, Watanzania wengi, asilimia 60 mpaka 70 wanaishi vijijini. Dhana ya uchumi shirikishi au uchumi jumuishi ni kuwawezesha Watanzania hawa kuweza kushiriki kwenye uchumi. Watashiriki vipi kama barabara zao hazipitiki? Leo maeneo mengi ya vijijini bado yana changamoto na mafuriko ya mwaka huu yatufumbue macho tuone kwamba yapo maeneo ambayo tunahitaji kwenda kuwekeza nguvu zaidi.

Mheshimiwa Spika, Watanzania wengi wapo maeneo ya vijijini. Kule Madaba kuna Vijiji nya Ifinga, kilometra 48 hazipitiki msimu mzima wa mvua, lakini huko ndiko kwenye Mbuga ya Selous na huko ndiko kwenye Watanzania ambaao wanahitaji kushiriki kwenye uchumi. Niiombe Serikali yangu Tukufu inayoongozwa na Mheshimiwa Dkt. John Pombe Magufuli kuwekeza pia kwenye miundombinu ya barabara, miundombinu ya uchumi vijijini ili Watanzania walio wengi wanaoishi katika maeneo hayo waweze kunufaika zaidi na uchumi.

Mheshimiwa Spika, ahsante sana na naunga mkono hoja. (*Makofii*)

SPIKA: Ahsante sana Mheshimiwa Joseph Mhagama.

Mheshimiwa Godfrey Mgimwa, Mbunge wa Kalenga, atafuatiwa na Mheshimiwa Mchungaji Peter Msigwa.

MHE. GODFREY W. MGIMWA: Mheshimiwa Spika, ahsante kwa nafasi uliyonipa kuweza kuchangia hotuba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu. Awali nianze kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu lakini pia nimshukuru sana Mheshimiwa Rais kwa kazi nzuri anayoifanya, lakini pia nimshukuru Makamu wa Rais, Waziri Mkuu na nikushukuru wewe binafsi kwa kazi nzuri ambayo unaendelea kuifanya hapa Bungeni. Vilevile niendelee kuwashukuru na kuwapongeza Mawaziri; Mheshimiwa Jenista Mhagama, Naibu Waziri Mheshimiwa Mavunde lakini vilevile na Mheshimiwa Ikupa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, hotuba ya Waziri Mkuu lazima niseme kwamba imesheheni mambo makubwa na ya msingi sana na nasema hivi kwa sababu kuna baadhi ya mambo ambayo yameelezwala kwenye hotuba hii ambayo nitaenda kuyagusa, naamini kabisa kwa upana wake tunaweza tukabadilisha mtazamo wa nchi lakini vilevile kama tutajikita vizuri katika hotuba hii tunaweza tukapata majibu mazuri kwa changamoto mbalimbali ambazo ziko mbele.

Mheshimiwa Spika, labda nianze tu kwa kusema kwamba nitaanza kwa masuala mtambuka hasa kwenye hotuba ambayo kidogo imegusa kwenye masuala ya UKIMWI. Tatizo tunalolipata katika Taifa letu ni maeneo mbalimbali ambayo yanaguswa kwa kiasi kikubwa na maambukizi ya UKIMWI lakini vipaumbele vinapelekwa katika maeneo mengine.

Mheshimiwa Spika, nasema hivi nikiwa na takwimu za mikoa kadhaa. Kwa mfano kwa Mikoa ya Iringa, Njombe, Mbeya na hasa sasa hivi Mkoa wa Dodoma ambapo tunaona maambukizi ya Ugonjwa wa UKIMWI yanazidi kuongezeka kwa kiasi kikubwa. Miaka mitano iliopita Mkoa wa Dodoma ulikuwa kwenye asilimia 3.5, leo hii Dodoma tunazungumza asilimia 5.8, haya ni maambukizi ambayo

yanakwenda kwa kiasi kikubwa na hivyo basi napenda kuishauri Wizara husika kwamba, tunavyoangalia tatizo hili la UKIMWI linavyoendelea kukua katika mikoa mbalimbali basi tupeleke nguvu pale ambapo kuna tatizo kubwa.

Mheshimiwa Spika, sasa unakuta Asasi nyingi za Kijamii na za Kiraia zinaenda kupeleka misaada mbalimbali kwenye maeneo ambayo takwimu zinaonesha kwamba maambukizi ya ugonjwa huu yapo chini. Sasa kwenye maeneo kwa mfano Mkao wa Iringa ambapo kwa kweli tatizo ni kubwa, lishe duni na mambo ambayo yanaendana na hayo, naomba sana Nyanda za Juu Kusini iweze kutazamwa vizuri kwa sababu kule ndiko kwenye matatizo makubwa sana. Naamini kabisa Mheshimiwa Jenista tumekuwa naye kwenye Kamati mara kwa mara, ni msikivu na ataendelea kufanya kazi vile ambavyo fedha zitaendelea kupatikana. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, lakini niseme tu kwamba kuna tatizo kubwa kwenye Mfuko wetu wa *ATF*. Ukiangalia mwaka jana unakuta Serikali ilitenga fedha za kwenye Mfuko wa *ATF* shilingi milioni 804 lakini ilitoa shilingi milioni 705. Sasa maeneo mengi ambapo Mfuko wa *ATF* ulitakiwa uimarishe labda hauimarishe kwa sababu maeneo yenye matatizo haya ni mengi na ni makubwa.

Mheshimiwa Spika, niseme tu kwamba fedha ambazo zimetolewa na wadau au ambazo zinaendelea kutolewa na wadau, kama alivyosema Mwenyekiti wa Kamati kwamba wadau wanaanza kujitoa. Sijui kama nchi tunajipanga vipi kuhakikisha kwamba Mfuko huu wa *ATF* ambaa ulikuwa mahsusii kabisa kwa ajili ya kuboresha suala hili la UKIMWI tunafanyaje kuhakikisha tunaongeza fedha kwa kiasi kikubwa ili tuweze kujimudu wenywewe kama nchi. Naomba sana eneo hili tuweze kuliwekea mkazo ili fedha ziweze kupatikana na Serikali ya Tanzania tuweze kuona namna gani sasa tunaweza kujiiamarisha wenywewe bila kutegemea wageni. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, niseme tu kwambabajeti ya Mheshimiwa Waziri Mkuu ni endelevu. Nilikuwa nikitizama bajeti ya mwaka jana 2018/2019 nikililinganisha na hii, nasema

endelevu kwa sababu gani? Bajeti ya mwaka jana ilikuwa inaonesha kwamba vijiji ambavyo tunavyo Tanzania ni 12,268. Kwenye upande wa REA peke yake mwaka huo kulikuwa kuna vijiji 5,746 ambavyo vilikuwa vimeunganishwa na umeme lakini kwa upande wa asilimia tulikuwa tuna asilimia 47. Mwaka jana 2019/2020 vijiji vimeongezeka kutoka 5,746 mpaka 9,001, hii ni sawasawa na asilimia 73. Kwangu mimi naona lazima tuipongeze Serikali kwa juhudhi kubwa ambazo inazifanya kuhakikisha kwamba umeme unapelekwa vijiji na wananchi wetu wanapata umeme. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, vilevile kwenye maji, maji pia kulikuwa kuna miradi 65 sasa hivi 2020 tuna miradi 94 ambayo ukiangalia kwa ujumla wake ni asilimia 64. Kwa hiyo, tunaona ambavyo Serikali imejikita moja kwa moja kwa wananchi kuhakikisha kwamba inaondoa tatizo la maji na umeme. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, vilevile kuna baadhi ya maeneo kwenye maliasili tunaona kwamba miradi mbalimbali imeongezeka lakini mapori mengi yameongezwa na yamepandishwa hadhi kwa mfano Burigi, Ibanda na Rumanyika. Nilipata nafasi ya kwenda kule Rumanyika na Ibanda kwa kweli, ukiangalia unaona Serikali imejikita kuhakikisha kwamba inaongeza mapato yake kwa kiasi kikubwa kuititia maliasili na utalii. Kwa hiyo, tuendelee kui-support Serikali ili tuweze kupata fedha za kigeni za kutosha. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, vilevile kwa upande wa vijana, mwaka 2018/2019 mikopo ilitolewa kwa jumla ya shilingi bilioni 4.2 lakini mwaka uliofuata mikopo ilishuka kwa vijana ikatoka kutoka shilingi bilioni 4.2 ikaenda shilingi bilioni 3.2. Nashauri Serikali iangalie eneo hili la vijana ambao ndio Taifa la leo na kesho kuhakikisha wanapata ajira za kutosha na wanajisimamia wenyewe. Vilevile kuhakikisha kwamba ujasiriamali ambao wao binafsi wameamua kujiwekeza basi tunawaongeza nguvu na tunawapa namna ya kuhakikisha kwamba wanaweza kujikimu na kuendelea kufanya kazi kwa ajili ya ujenzi wa Taifa letu.

Mheshimiwa Spika, jambo la mwisho ni suala la ugonjwa wa *Corona*. Kwa kweli, ugonjwa huu ni janga kubwa kwa sababu ukiangalia Marekani, Uingereza, Italia, Hispania, ni mataifa makubwa ambayo yana uchumi mkubwa lakini kwa namna moja yameshindwa kuzuia ugonjwa huu. Tatizo nalolipata mimi ni kwamba, je, Serikali yetu ya Tanzania tunafanyaje kuhakikisha kwamba wananchi wanapata elimu ya kutosha ili kufahamu ukubwa wa tatizo hili? (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, ukiangalia katika maeneo mbalimbali ya starehe, vijana sasa hivi unakuta kuanzia saa moja, saa mbili mpaka usiku wa manane wako katika maeneo ya starehe. Sasa maeneo kama yale tukishindwa kuyazuia sijui tukipata tatizo hili tutakuwa katika hali gani? (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, lazima tuangalie uchumi ambao tunao katika nchi yetu. Lazima tuwe na dawa na lazima tuweze kuwapeleka waathirika wa ugonjwa huu katika maeneo ambayo yatakuwa yametengwa. Sasa tunawawezeshaje watu hawa kielimu kuhakikisha kwamba wanaweza kuepukana na tatizo hili?

Mheshimiwa Spika, nakushukuru na naunga mkono hoja. (*Makofi*)

SPIKA: Ahsante sana Mheshimiwa Godfrey Mgimwa. Nakushukuru sana kwa mchango wako.

Nilishakutaja Mheshimiwa Mchungaji Peter Msigwa na atafuatiwa na Mheshimiwa Senator George Malima Lubeleje.

MHE. MCH. PETER S. MSIGWA: Mheshimiwa Spika, nikushukuru. Nami nianze kuzungumzia ambapo ameishia Mbunge mwenzangu wa Iringa kuhusiana na ugonjwa wa *CORONA*.

Mheshimiwa Spika, kiukweli mimi pamoja na mambo mengine mazuri ambayo Waziri Mkuu ameyasema lakini katika hotuba yake sijaridhika kabisa na jinsi ambavyo

amelizungumzia suala la huu ugonjwa wa *Corona*, amelizungumza kwa kifupi sana. Jana wakati ulitupa nafasi ya kujadiliana hapa tulisema kwamba tuko vitani na tunapokuwa vitani lazima tuijandae kwa kiwango kikubwa sana. Tukiwa wa kweli kama Watanzania na kama Wabunge suala la kunawa mikono ambalo Serikali inajua imechukua hatua, suala la *hygiene*, masuala ya kunawa mikono wenzetu Ulaya, Marekani, ni kitu cha kawaida kabisa. Sipingani kabisa na hatua zilizochukuliwa na Serikali za kunawa mikono, lakini kama tunataka tudanganyane hapa tu kwa kunawa mikono na visabuni vile tumeweka kwenye maduka kwamba tunapambana na *Corona* wenzetu Ulaya suala la kunawa mikono sio swalii. Ndiyo maana unawakuta wanakula bila kunawa wakati mwingine lakini suala la kunawa mikono haliko kwenye akili kwa sababu wakati wote wananaawa mikono. Kwa hiyo, mimi nadhani...

SPIKA: Katika watu ambao hawanawi mikono Wazungu namba moja.

MHE. MCH. PETER S. MSIGWA: Mheshimiwa Spika, hapana, sio kweli. Sio kweli, tabia ya kunawa mikono Wazungu ni ya kawaida kabisa, ni maisha yao.

MBUNGE FULANI: Hamna!

(Hapa baadhi ya Waheshimiwa Wabunge waliongea bila utaratibu)

MHE. MCH. PETER S. MSIGWA: Mheshimiwa Spika, mimi naomba nipewe nafasi nizungumze. (*Kicheko*)

SPIKA: Waheshimiwa namlinda Mheshimiwa.

MHE. MCH. PETER S. MSIGWA: Mheshimiwa Spika, naomba unilinde, inategemeana, mimi nimekaa na Wazungu sana, nimeishinao.

(Hapa baadhi ya Wabunge walizungumza bila kufuata utaratibu)

MHE. MCH. PETER S. MSIGWA: Kwa hiyo, huwezi kunidanganya, suala la kunawa mikono sio suala la kufundishana.

SPIKA: Mchungaji, Wazungu hawanawi wala hawaogi. (*Kicheko*)

MHE. MCH. PETER S. MSIGWA: Mheshimiwa Spika, wananaawa.

SPIKA: Mzungu anaoga mara moja kwa wiki. (*Kicheko*)

MHE. MCH. PETER S. MSIGWA: Mheshimiwa Spika, kwa hilo nitawapinga.

SPIKA: Namlinda, namlinda jamani, endelea.

MHE. MCH. PETER S. MSIGWA: Mheshimiwa Spika, nachoweza kusema kama tunadhani kukabiliana na *CORONA* ni kunawa mikono tu peke yake tutakuwa tunajidanganya, kuna hatua za zaidi kama nchi tunatakiwa tuzichukue. Huu ndiyo wajibu wetu sisi kama Wabunge kuitask Serikali kwamba ni mipango gani ya dharura ambayo Serikali imeifanya.

Mheshimiwa Spika, takwimu nilizonazo mimi Tanzania nzima pamoja na kuwa na watu millioni 58 tuna *ICU* 38 *in case* tukipata matatizo, haya ni masuala ya kujadiliana hapa tupewe ripoti. Kama nchi nzima tuna *ICU* 38 ...

MBUNGE FULANI: Vitanda.

MHE. MCH. PETER S. MSIGWA: Mheshimiwa Spika, vitanda 38, kama ugonjwa huo...

(Hapa baadhi ya Wabunge walizungumza bila kufuata utaratibu)

NAIBU WAZIRI WA AFYA, MAENDELEO YA JAMII, JINSIA, WAZEE NA WATOTO: Mheshimiwa Spika, taarifa.

SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri Afya nimekuona.

TAARIFA

NAIBU WAZIRI WA AFYA, MAENDELEO YA JAMII, JINSIA, WAZEE NA WATOTO: Mheshimiwa Spika, nalazimika kusimama kwa sababu mchangiaji ambaye anachangia sasa hivi anapotosha sana na nataka nimpatie taarifa za kitaalam tu kabisa. *Corona Virus* ambaye ni *COVID19* ukuta wake umetengenezwa na mafuta na sababu ni silaha ya kutosha ya kuki-*destroy* kirusi hiki. Hatutoi hizi taarifa kwa ajili tu ya kuudanganya umma, sabuni na maji tiririka ni silaha ya kutosha kabisa kukiwa kirusi cha *Corona*. (*Makof!*)

Mheshimiwa Spika, lakini la pili, muongeaji ambaye ametoka kuongea sasa hivi anasema Tanzania tuna vitanda 38 vya *ICU*. Hospitali ya Muhimbili peke yake ina vitanda zaidi ya 40, hizo taarifa anazitoa wapi? (*Makof!*)

SPIKA: Ni taarifa tu hiyo Mchungaji kukuweka sawa.

MHE. MCH. PETER S. MSIGWA: Mheshimiwa Spika, nadhani tunajaribu kukimbia hoja ya msingi tunayojenga hapa. Nimesema sipingani na masuala ya kunawa na sabuni zillizowekwa barabarani na kwenye maeneo mengi. Nimesema kama tunadhani tutaondoa *Corona* kwa sabuni tunazonawa tunajidanganya. Hoja ya *Corona* ni zaidi ya tunavyodhani na ndiyo maana nchi za wenzetu zimeamua kuwatoa watu wake Barani Afrika. Jana nilikuwa nasikiliza *Al-Jazeera* wanasesma ndani ya wiki tatu ugonjwa huu tutaanza kuyaona matokeo yake katika Bara la Afrika kwa sababu *measures* tunazochukuahaziendani na tatizo tulillonalo, hili ni tatizo kubwa. Bunge saa hizi hapa tunajadili bajeti *as if* hakuna chochote kitakachotokea.

Mheshimiwa Spika, Spain na Italy walipuuza kwa sababu waliona hilo suala halitawafikia, lakini mtu ye yeyote mwenye busara anajiaandaa kabla ya vita. Tunachozungumza hapa ni kutaka kufahamu ni kwa kiwango gani tumejipanga. Wakilipuka wagonjwa laki moja hapa

tutawalaza wapi? Hayo mambo tunatakiwa Serikali ituambie. Haya masuala ya kusema kuna vitanda 40, nyumba za *ICU* ziko 38, huwezi kukataa hiyo hatuna *ICU* za kutosha hapa. Mimi ndiyo nasema Serikali ituambie *incase* wakizuka wagonjwa laki moja tutawaweka wapi kama nchi? Serikali muwe na majibu hapa, hamna majibu. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, lakini la pili, *consequences* za ugonjwa huu zina athari za kiuchumi. Wewe ni shahidi, sekta ya utalii kuna *direct employment* zaidi ya milioni moja na laki tatu au laki nne ambao sasa hivi hawana kazi na wengine wanaathirika, sekta ya utalii karibu watu milioni mbili hawako kazini kwa sababu hamna kazi. Hoteli zimefungwa, Zanzibar kule zaidi ya hoteli za kitalii 250 zimefungwa, Bara zaidi ya hoteli 250 zimefungwa, *these are the issues* tunatakiwa tu-discuss hapa, *revenues* mtakusanya kutoka wapi? Utalii unaingiza 25% ya *forex*, hiyo *forexinatoka* wapi? 25% ya *forex* katika nchi siyo kitu kidogo, haya ndiyo mambo tunatakiwa tuyajadili hapa, sio *stories*. Serikali ituambie ina mpango gani tuweze kuishauri. Hili ndiyo Bunge tushauriane hapa.

(Hapa baadhi ya Wabunge walizungumza bila kufuata utaratibu)

MBUNGE FULANI: Anza wewe kutoa ushauri.

MHE. MCH. PETER S. MSIGWA: Mheshimiwa Spika, kuna watu katika *industry* hiyo wamekopa...

TAARIFA

WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU, SERA, BUNGE, KAZI, VIJANA, AJIRA NA WENYE ULEMAVU: Mheshimiwa Spika, taarifa.

MHE. MCH. PETER S. MSIGWA: Serikali hajatuambia *ime-negotiate* vipi na mabenki...

SPIKA: Mheshimiwa Mchungaji, namwona Mheshimiwa Waziri wa Nchi amesimama.

WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU, SERA, BUNGE, KAZI, VIJANA, AJIRA NA WENYE ULEMAVU: Mheshimiwa Spika, naomba tu kumpa taarifa Mheshimiwa Msigwa kwamba, kwanza anapoona hali hii ya mwenendo wa *Corona* tunavyokwenda nayo inaonesha dhahiri shahiri ni kwa namna gani Serikali imejitahidi na iko kazini. Naomba tu nimwambie Mheshimiwa Msigwa ili tuweze kuwa pamoja, huu ndiyo muda muafaka nadhani badala ya kuendelea kulaumu ilikuwa ni fursa kwake...

(Hapa baadhi ya Wabunge walizungumza bila kufuata utaratibu)

WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU, SERA, BUNGE, KAZI, VIJANA, AJIRA NA WENYE ULEMAVU: Mheshimiwa Spika, ilikuwa ni fursa kwake na ye ye kutushauri kwa sababu tumeshapokea maagizo yako kwamba hata sisi tutakuja kama Serikali na umetuambia tutoe taarifa mbili; taarifa ya mwenendo mzima wa tatizo la *Corona* na tatizo la mafuriko nchini. Sasa anaposimama ajue sio kwamba Serikali imekaa tu ila tungefurahi sana Mbunge atushauri kuliko kulaumu. *(Makof)*

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, naomba tu nimpe taarifa kwamba tunajiandaa, hili ni tatizo la dunia. Hata huko anakosema Ulaya hata *ICU* za Ulaya hazitosh na wao wana shida hiyohiyo. Kwa hiyo, kila mtu anapambana na *Corona* kwa mazingira aliyonayo na kwa namna anavyoweza kukabiliana nayo. *(Makof)*

SPIKA: Mheshimiwa Msigwa unapokea taarifa hiyo?

MHE. MCH. PETER S. MSIGWA: Mheshimiwa Spika, mimi hapa silaumu. Serikali yoyote duniani ipo kwa ajili ya kulinda uhai wa raia wake, *that is a paramount*, hicho ni kitu cha kwanza. Wao hapa waje na mpango kwamba jamani wakilipuka wagonjwa elfu hamsini tumepanga hivi, Wabunge mnatushauri nini? Waje na *plan*, tuko vitani hapa. Waje na *plan* Wabunge tuwashauri, wamekaa kimya muda unaenda,

tunavyoviona tu ni visabuni huko barabarani, ndiyo hicho nachozungumza.

Mheshimiwa Spika, tunazungumzia uchumi hapa, kuna wafanyabiashara wamekopa benki, Serikali haijatuambia...

(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)

TAARIFA

MHE. GOODLUCK A. MLINGA: Mheshimiwa Spika, taarifa.

SPIKA: Ahsante Mheshimiwa Msigwa, muda wako umeisha. Tunaendelea na Mheshimiwa Lubeleje atafuatiwa na Mheshimiwa Jacqueline Msongozi.

MHE. GEORGE M. LUBELEJE: Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi ili na mimi niweze kuchangia bajeti ya Mheshimiwa Waziri Mkuu.

Mheshimiwa Spika, kwanza nimpongeze Mheshimiwa Waziri Mkuu kwa kazi nzuri anayowafanya Watanzania. Hongera sana Mheshimiwa, tuko pamoja nawe, hatuna wasiwasi kabisa kwamba kazi inafanyika vizuri. (*Makofî*)

Mheshimiwa Spika, suala la kwanza ni ujenzi wa barabara ya Mpwapwa - Kongwa kwa kiwango cha lami. Kwanza nishukuru sana Serikali kwamba bajeti iliyopita ambayo tunamalizia mwezi Juni ilitenga fedha kidogo kwa ajili ya kuanza kutengeneza barabara ya lami kutoka Mpwapwa - Kongwa lakini barabara hiyo mpaka sasa haijaanza kutengenezwa. Nina wasiwasi hata fedha haijatolewa, sasa naomba maelezo kwa nini fedha haijatolewa. Mheshimiwa Waziri Mkuu mwaka huu nina hakika atatenga fedha za kutosha kwa ajili ya utengenezaji wa barabara ya lami Mpwapwa - Kongwa.

Mheshimiwa Spika, Iakini barabara ya Mpwapwa inaanzia Mbande kwenda Kongwa, kuna barabara inatengenezwa kuanzia Mbande kwenda Kongwa na ilianza kutengenezwa mwaka 2012 mpaka leo hii hajakamilika. Tatizo Mheshimiwa Waziri Mkuu wakandarasi hawalipwi. Kwa hiyo, naomba wakandarasi walipwe na hii barabara inayokwenda kwa Mheshimiwa Spika kutoka Mbande kwenda Kongwa iweze kukamilika na barabara ya kutokwa *Kongwa junction* mpaka Mpwapwa nayo itengenezwe kwa kiwango cha lami. (*Makofî*)

Mheshimiwa Spika, Iakini suala la pili ni fedha kuchelewa kufika katika mikoa yetu pamoja na Halmashauri za Wilaya. Suala hili linatuathiri sana katika Halmashauri, miradi mingi sana imelala. Ujenzi wa madarasa, vituo vyâ afya na zahanati umekwamba. Kwa sababu fedha zimechelewa kupelekwa mikoani na wilayani kuna viporo vingi sana katika Jimbo la Mpwapwa, Jimbo la Kongwa, pamoja na Jimbo la Kibakwe. Kwa hiyo, naomba fedha zitolewe mapema kwenye mikoa na Halmashauri za Wilaya ili ile miradi iweze kutekelezwa.

Mheshimiwa Spika, suala la tatu ni kuhusu mapato ya Halmashauri pamoja na madeni ya Madiwani. Mwezi Februari, Waziri wa TAMISEMI aligawa mashine za kukusanya mapato katika Halmashauri lakini jambo la kushangaza bado Halmashauri nyingi mapato ya ndani (*own source*) ni kidogo sana na *own source* ndio uhai wa kila Halmashauri. Ni kweli Serikali inatenga fedha kwa ajili ya Halmashauri lakini fedha zinachelewa kufika na zinazofika ni kidogo sana. Kwa hiyo, mapato ya ndani yakikusanywa vizuri nina uhakika kabisa miradi ya maendeleo katika Halmashauri itatekelezwa vizuri.

Mheshimiwa Spika, suala la nne, Halmashauri ya Wilaya ya Mpwapwa ina madaraja matatu, Daraja la Godegode ambapo namshukuru sana Waziri wa Ujenzi ametenga fedha kwa ajili kujenga daraja lile, nakushukuru sana Mheshimiwa Waziri na Daraja la Nghambi la Kinyasungwi nalo vilevile limebomoka.

Mheshimiwa Spika, wiki iliyopita Daraja la Mpwapwa Mjini limebomoka. Kwa hiyo, kutoka Posta kwenda Mpwapwa Mjini hakuna daraja, magari hayawezি kupita. Jana kuna daraja lingine tena la kutoka Hospitali kwenda Godegode nalo limechukuliwa na maji. Sasa sina madaraja, magari yatapita wapi?

Mheshimiwa Spika, naomba msaada wa Serikali na kama inawezekana Waziri wa Ujenzi kesho au keshokutwa au Jumamosi atume Naibu Waziri atembelee Daraja lile la pale *TANESCO* kuona kama kuna uwezekano liweze kufanyiwa angalau matengenezo. Niliomba angalau *Barry Bridge* ili magari yaweze kupita kwa muda. Kwa sasa hivi mvua bado zinanyesha lakini mkituwekea *Barry Bridge* katika daraja lile la kutoka Posta kwenda Mjini pamoja na Daraja la Godegode ili magari yaweze kupita. Ni tatizo kubwa sana kwa wananchi wa Mpwapwa, naomba msaada wa Serikali.

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo nakushukuru sana kwa kunipa nafasi na naunga mkono hoja kwa asilimia 100 bajeti ya Mheshimiwa Waziri Mkuu. (*Makofii*)

SPIKA: Ahsante sana Mheshimiwa Lubeleje, Mbunge wa Mpwapwa na yeye pia ni Mbunge Kivuli wa Kibakwe na Kongwa. (*Makofii*)

Nilikutaja Mheshimiwa Jacqueline Msongozi utuchangamshe kidogo na Mheshimiwa Joseph Kasheku Musukuma atamalizia shughuli ya jioni ya leo. (*Makofii*)

MHE. JACQUELINE N. MSONGOZI: Mheshimiwa Spika, naomba nichukue nafasi hii kukushukuru kwa kunipa nafasi ili nami niweze kuchangia hotuba ya Waziri Mkuu.

Mheshimiwa Spika, naanza kwanza kwa kukupongeza wewe uliyenipa nafasi hii ya kuchangia. Wewe ni Spika wa kiwango cha hali ya juu, lakini pia mwenye weledi, mwadilifu, mwenye busara na ni mchapakazi. Nakupongeza kwa dhati hasa kwa sababu ya utendaji wako mzuri wa kazi, lakini pia kwa ajili ya Bunge mtandao.

Mheshimiwa Spika, mimi binafsi imenisaidia sana. Kwanza imenisaidia kuongeza uelewa, lakini pia imenisaidia kuondoa mabegi na viroba vya vitabu ambavyo vilikuwa vinajazana nyumbani kwangu. Ahsante sana. Sasa hivi nyumba imekuwa na nafasi ya kutosha. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, lazima nimpongeze sana Mheshimiwa Rais wangu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mheshimiwa Dkt. John Joseph Pombe Magufuli, Rais anayetokana na Chama cha Mapinduzi, Chama ambacho kina sera nzuri, chama imara, kinakubalika na sera zake zinatekelezeka. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, pia nawapongeza wasaidizi wake, Makamu wa Rais pamoja na Waziri Mkuu. Waziri mkuu amekuwa akifanya kazi nzuri sana. Tumemwona kila maeneo ya nchi yetu. Kama kuna jambo lolote linajitokeza, basi mara moja anatokea na kuweza kufanya suluhisho la jambo hilo ambalo liejitokeza. Hongera sana Mheshimiwa Waziri Mkuu, Mungu akujaalie kila la kheri, akupe uzima na afya njema na Bunge lijalo urudi ukapate kura za kishindo, ikiwezekana upite bila kupingwa Ruangwa. Hongera sana. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, nina kila sababu ya kuendelea kupongeza Ofisi ya Waziri Mkuu ambayo anasaidiwa na wanawake wawili mahiri sana; Mheshimiwa Jenista Joachim Mhagama na Waziri Angellah Kairuki. Hawa akina mama wanafanya kazi vizuri sana.

Mimi ni Mjumbe wa Kamati ya Katiba na Sheria ambaye ninafanya kazi sana na Ofisi ya Waziri Mkuu. Tunaona namna ambavyo wamekuwa wakijibu hoja zetu Waheshimiwa Wabunge ambao ni Wanakamati na pia tumeona umahiri wa utendaji wao wa kazi. Hongereni sana, wanawake, tunaweza. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, kwa misingi hiyo ndiyo maana wameweza kukidhi maono ya Mheshimiwa Rais; kwanza kwa uratibu mzuri ambao wamekuwa wakiufanya na usimamizi mzuri. Hongereni sana. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, progaramu ya kukuza ujuzi kwa vijana ambayo iko chini ya Ofisi ya Waziri Mkuu, imetekelezwa vizuri sana. Kutokana na ufinyu wa ajira, lakini Wizara hii imekwenda mbali zaidi, vijana wengi wameweza kupelekwa kwenye mafunzo ya Vyuo vya Ufundı Stadi ikiwepo *VETA* na vyuo vingine kama Don Bosco. Vijana wamepata mafunzo mazuri sana.

Mheshimiwa Spika, hata hivyo, tunapozungumzia suala la ajira kwa vijana huwezi kuacha kuzungumzia suala la vitalu nyumba ambayo inaitwa *greenhouse*, ambapo kwa mapana na marefu sana sisi tumekwenda tumekagua miradi mbalimbali ya vijana kwenye kila Halmashauri, miradi hii imewekwa. Niseme tu baada ya muda mfupi, inawezekana kabisa tukawa tumefikia uchumi wa katı tunaoutarajia kuitia hawa vijana. Vijana hawa pia wamejikita katika shughuli za viwanda vidogo vidogo vya utengenezaji wa chaki, pamoja na kutengeneza mafuta na mambo mengine mengi. Kwa kweli Ofisi hii iko makini sana.

Mheshimiwa Spika, miradi mikubwa ambayo inaendeshwa katika nchi yetu inayotekelzwa kwa sasa ikiwemo miradi ya barabara za lami lakini pia reli ya umeme, *standard gauge*, *Stiegler's Gorge*, bomba la mafuta, umeme wa *REA* na usafiri wa anga, kwa kweli imeleta tija sana katika nchi yetu. Miradi hii imefungamanisha maendeleo ya watu, uchumi wa nchi pamoja na kipato cha kila mmoja. Miradi hii imeongeza ajira. Uchumi wa sekta binafsi kwa kutoa huduma umekua.

Mheshimiwa Spika, miradi hii pia imesababisha wananchi kupata kipato kuitia katika shughuli mbalimbali, mfano; kwenye suala la ujenzi, wananchi waweza kupeleka kokoto, wameweza kuuza *cement*, kukusanya mchanga na kupeleka maeneo ya ujenzi. Kwa hiyo, hii imesaidia sana kukuza kipato kutokana na miradi hiyo mikubwa.

Mheshimiwa Spika, nachelea kusema miradi hii ina tija na niseme tu kwamba Ofisi ya Waziri Mkuu iendelee kutoa

mafunzo mbalimbali ili hawa vijana waweze kuendelea kuwekeza na kupata tija zaidi katiak maisha yao.

Mheshimiwa Spika, naipongeza sana Tume ya Uchaguzi kwa sababu imetekeleza takwa la kikatiba na kisheria kwa kuboresha daftari la kudumu. Hata sasa tunavyozungumza wananchi wapya zaidi ya milioni saba wameweza kujiandikisha katika daftari la kudumu. Sasa niseme tu, kwa wale wenzetu wenyewe tabia ya kuchukua mpira na kuweka kwapani, safari hii tunaomba sana msichukue mpira kuweka kwapani na kukimbia uwanjani. Twendeni uwanjani, uchaguzi upo, twende tukapambane uwanjani. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, kwa dhati kabisa, naomba nichukue nafasi hii kumpongeza sana Kamishna Mkuu wa *TRA*, Dkt. Mhede, kwa kazi nzuri sana ambayo analifanya ya ukusanyaji wa mapato. Amekuwa mbunifu na tumeshuhudia mwezi Desemba amekusanya mapato na kufikia shilingi trilioni 1.9, haijapata kutokea. Pongezi nyngi sana kwake. Namwomba tu Rais wangu kipenzi, Mheshimiwa Dkt. John Joseph Pombe Magufuli, ikibidi huyu Dkt. Mhede ampe zawadi nono.

Mheshimiwa Spika, tunapozungumzia suala la kukua kwa maendeleo, ni muhimu sana tukazungumzia pia barabara ambazo ziko pembezoni kwenye mikoa ya pembezoni ili kuweza kufungua mawasiliano ya kiuchumi na uchumi wetu uweze kukua kwa pamoja, usiende kukua kwa upande upande. Kwa mfano hapa, nitazungumzia barabara ambayo ina urefu wa kilometra 124, inayotoka Songea Mjini kwenda Mkenda. (*Makof*)

(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)

SPIKA: Ahsante sana Mheshimiwa Jacqueline.

MHE. JACQUELINE N. MSONGOZI: Mheshimiwa Spika, ahsante. Naunga mkono hoja.

SPIKA: Ahsante sana. Mheshimiwa Joseph Musukuma.

MHE. JOSEPH K. MUSUKUMA: Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi nami niweze kuchangia kwenye hotuba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu.

Mheshimiwa Spika, nianze kwa kukupongeza sana wewe. Nakumbuka wakati tumekuchagua, ulipokuwa unaeleza vipaumbele vyako, moja ya kipaumbele ulichotueleza ni kwamba baadaye sisi Wabunge hatutahangaika tena na makaratasi, utaleta Bunge mtandao. Tunakushukuru sana. Hata mimi mwenyewe sasa hivi sibebi karatasi, nami pia nimekuwa wa kisasa. Mungu akubariki sana. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, nilikuwa nakaangalia ka Msigwa sijui kameenda wapi, kwa sababu unajua mimi huwa najuliza, yaani haya maneno yanazungumzwa na mtu anaitwa Mchungaji,...

MHE. MCH. PETER S. MSIGWA: Mheshimiwa Spika, taarifa.

MHE. JOSEPH K. MUSUKUMA: ...anatuaminisha tuache kufuata maelekezo ya Madaktari, watu walioumiza vichwa, wakasoma wanajua kinga ya *Corona*, anatuaminisha kama Mganga wa Kienyeji, halafu kenyewe kanatoka kanaenda kunawa pale. (*Kicheko*)

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, hawa watu ni watu wa hatari sana na tusikae kimya Waheshimiwa Wabunge. Sisi tunaelekeza kusikiliza maelekezo ya Madaktari, watu wanaojua; na tutanawa. Tunaiomba Serikali ongezeni hata ndoo barabarani tuendelee kunawa. Hawa watu kama akina Msigwa hawa, anapiga porojo humu anakaa kwenye *you tube*, kenyewe kamepita mlangoni pale kamenawa maji kameondoka.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, naomba sana watu kama hawa tusiwafumbie macho, lazima tupate muda wa

kuwaambia, hili siyo suala la mizaha. Kuna watu wetu kule vijijini walishaamini kabisa na tunanawa mara tatu au nne, anakuja kutueleza Wazungu wananaawa maji. Wazungu wa wapi aliowaona wananaawa kila dakika? Hata ukiingia kwenye *washroom* zao kuna makaratasi, halafu mtu anakuja kutuambia mambo ya kihunihuni. Naomba sana watu kama hawa tuweze kuwakemea. (*Makofi/Kicheko*)

Mheshimiwa Spika, niwapongeze sana watu wa Mkoa wa Dar es Salaam. Tunaona na kweli Watanzania wameelewa. Jana nilikuwa naangalia kwenye *TV*, ule mlundikano wa kwenye daladala umeisha *automatically*. Kwa hiyo, tunaomba na Wakuu wa Mikoa wengine waige mfano kama ule wa Dar es Salaam. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, nataka nikupe mfano mmoja; mimi na mwenzangu Mheshimiwa Tizeba na Mheshimiwa Ngeleja hapa; ili wapiga kura wetu Mwanza, pale kuna pantoni. Ukiondoa ile *pantoni* ya Serikali kuna *ferry* za mizigo kule *Kamanga Ferry*. Hizi *ferry* zinabeba watu zaidi ya 1,500 wakati uwezo wake wa kubeba labda ni watu 300 au 400. Malori humo humo, mafuta humo humo. Kwa hiyo, naomba Serikali iangalie namna kwa watu wetu ambaao wanatumia hicho kivuko. Ikiwezekana Mheshimiwa *Engineer Kamwelwe* kama yuko hapa aweke watu wasimamie, zile *ferry* zinatakiwa zibebi watu 300, haiwezekani ukalundika watu 1,000. Tusije tukasababisha mambo mengine kwa wapiga kura wetu.

Mheshimiwa Spika, lingine, kwanza tunaishukuru sana Serikali. Tumepata taarifa kwamba mmepeata mkono ule ambaao watu walisafiri kwenda kuupinga. Kitu ambacho nitawashangaa, kama watu walitumia mamilioni kwenda kuharibu tusipewe hela, halafu sasa hivi zimekuja hela, umpelekee mgao wa hizi hela, nitawashangaa Mawaziri. Ninaomba kabisa sisi ambaao tulikaa kimya na kuomba kila siku kwa Mungu tupate huo mkopo, mtuangalie, sisi tuna shida na shule zetu. Hao watu ambaao walienda kuponda, achaneni nao msiwape.

Mheshimiwa Spika, lingine, tunaishukuru sana Serikali ya Awamu ya Tano, tumepeata Halmashauri kwenye vijiji vyetu. Ni kweli Serikali ina wazo zuri kabisa, imepeleka huduma kwa wananchi, lakini naomba kama kuna uwezekano, Serikali ione dharura yoyote, kule tulikohamia hakukuwa na maandalizi na hatukuwa na bajeti. Kwa hiyo, ni vizuri Serikali ikaona dharura sasa, zile Halmashauri ambazo zimegawanywa ziweze kupelekewa hela ili waweze kuandaa makazi na ofisi za kufanya kazi.

Mheshimiwa Spika, lingine nilijaribu kuingia siku moja kwenye Kamati ya TAMISEMI, nikawa nasikiliza, kwa mfano Mkoa wa Dar es Salaam; tunapiga kelele kila siku hapa tipeleke hela kwa vijana, watu wenyewe mahitaji maalum na akina mama, lakini ukisikiliza mpango mzima, tunatengeneza Taifa la watu wajinga tu. Hakuna mtu anapewaga hela ya bure. Zile hela za Halmashauri ni kama tunazitupa tu bila kuwa na mkakati wowote wa kuhakikisha fedha inarejeshwa.

Mheshimiwa Spika, hata kule Bungeni nilikuwa nawasikiliza Wajumbe mle hakuna aliyesema zimelipwa ngapi? Tunang'ang'ana kulundika tu. Mkao mmoja wa Dar es Salaam peke yake umetoa kama shilingi bilioni nne, hamna mtu anayezifua tilia hizo hela. Mnawaza tu tena na mwakani kulundika. Tutakuwa tunatengeneza watu wajinga tu baadaye hawana akili ya kutafuta.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, naomba kama kuna utaratibu, basi tuangalie baadhi ya mikoa yenyeye uwezo tuweze kuzilinda hizi hela, tufungue hata taasisi ambaao tutaweka watu wenyewe kazi hiyo hiyo kwa ajili ya kushughulika na masuala ya kukopesha na kudai kuliko kuwa tunachukua hela, tunalundika, watu wanaenda kuolea. Hii naona kama hajakaa vizuri.

Mheshimiwa Spika, suala la afya. Serikali imefanya vizuri sana kwenye afya. Tumepeata Vituo vya Afya na Hospitali za Wilaya. Naomba sana, mimi kwangu kule ninakotokea, hospitali nzima ya Wilaya nina Madaktari watatu kwenye *population* ya watu 600,000. Hicho kitu hakiwezekani. Kwa

hiyo, naiomba Serikali, yale mazingira ambayo tumepewa hospitali mpya, basi waangalie kwenye huo mgao hao madaktari walioajiriwa watupatie Madaktari kwa sababu unakuta ikama inataka labda watu 20, una Madaktari watatu utafanyaje?

Mheshimiwa Spika, tumepewa *x-ray* na vitu vyote kama *echo machine* na kadhalika halafu hakuna mtumishi. Mpaka leo unakuta labda zina miaka miwili yamelundikwa tu ndani lakini hakuna mtaalam wa kuzitumia. Kwa hiyo, naiomba Serikali tunapokuwa tunanunua vitu, tuandae na mpango mzima wa kuweza kusimamia zile hela.

Mheshimiwa Spika, la mwisho, limezungumzwa suala la Ofisi za Wabunge, kwa kweli ni shida. Waheshimiwa Wabunge wengi hapa ukiwaangalia hapa, Ofisi zao ni magari na wananyanyasika kweli kwa Wakurugenzi. Mkurugenzi mwenyewe hana Ofisi, iwe wewe Mbunge! Kwa hiyo, naomba kama alivyoeleza Mwenyekiti wa Bajeti, ni vizuri suala hili likasimamiwa na Bunge, tuache kupeleka TAMISEMI, hatutapata Ofisi. Unakuta mtu ameniga tai halafu Ofisi iko kwenye gari. Kwa hiyo, ni vizuri walivyopendekeza Kamati, basi mrudishe kwenye Bunge, halafu Bunge lenyewe ndiyo lisimamie kutengeneza Ofisi za Waheshimiwa Wabunge. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana, ahsante sana. Naunga mkono hoja. (*Makofi*)

SPIKA: Ahsante sana Waheshimiwa Wabunge. Mjadala wetu umeenda vizuri. Kama kawaida, baada ya dakika fulani fulani kupita, basi lazima tena *sanitizerna* wale mlio nazo pia msisahau mkaondoka mkarudi nyumbani bila ku-*sanitize* kidogo. Niwahakikishie kwamba ukumbi huu tunapoondoka tu wanaingia vijana kuufanya usafi unaotakiana kabisa.

Pia kumbi ambazo tumeandaa na wenzetu wako huko na zenyewe zinafanyiwa usafi *thorough* kabisa. Mara mbili kwa wiki nyakati za usiku, *compound* nzima ya Bunge

inafanyiwa usafi na kupulizwa kinachohitajika kwa ajili ya kuhakikisha kwamba tunapambana na janga hili la *Corona* katika maeneo yetu na tunawalindeni Waheshimiwa Wabunge ninyi na familia zenu. Tunajitahidi. Kama kuna pendekezo lolote la juhudhi gani zaidi tufanye, kwa kweli tunalipokea hilo pendekezo, msisite kutushirikisha. Tutafanya kila tunaloweza kuona kwamba tunakuwa salama. (*Makofii*)

Kwa hiyo, mnapotoka hapa kwenda majumbani, hatuna namna ya kumzuia anayetaka kwenda *disco* kumwambia bwana huko usiende, unahatarisha maisha yako, lakini na ya wenzako. Kwa hiyo, nitoe wito wa jumla wa kujizuia kwenda katika maeneo yenye watu wengi, tujizue sana. Fanya kile kitu ambacho jana tulikuwa tunaambiana kinaitwa *social distancing*. Kwa kipindi hiki ambacho tumeshauriwa na Serikali tuwe na utulivu, wakati huo utakaporuhusiwa mambo yamekuwa mazuri, basi tutajirusha tena kwa kulipiza na zile siku ambazo tulizikosakosa kidogo.

Vinginevyo mjadala wetu umeanza vizuri, tutaendelea tena kesho kwa utaratibu ule ule. Mwendelee kuijandaa Waheshimiwa Wabunge, mnayo makabrasha yote yanayohusiana na bajeti hii ya Mheshimiwa Waziri Mkuu, mnayo hotuba ya Waziri Mkuu, mnazo hotuba za Kamati zote za bajeti nyingine ambazo zimechambua mambo haya. Bahati nzuri kwa Waziri Mkuu unaweza ukachangia Wizara yoyote ile, ndiyo maana Waheshimiwa Mawaziri wanajitahidi kuwepo na kama katika bajeti hii Waziri kwa sababu moja au nyingine anakuwa hayupo, basi Naibu wake anakuwepo au wote wawili wanakuwepo ili kuchukua mambo ambayo ni muhimu, wewe kama mwakilishi wa wananchi ungependa yaifikie Serikali.

Pia tukumbuke pia ushauri unaoandikwa kuititia *tablets* zetu, uje Ofisi ya Bunge nasi tutauwasilisha Ofisi ya Waziri Mkuu *promptly*. Kama kuna shida katika haya mawasiliano pia, tupeane taarifa mapema labda *tabletyako* ina shida fulani na kadhalika tuhakikishe kwamba hilo tatizo linatatuliwa.

NAKALA MTANDAO(ONLINE DOCUMENT)

Basi kwa vile shughuli zote zilizopangwa kwa ajili ya siku ya leo zimekamilika na saa 12.00 ndiyo hii, basi sasa naomba niahirishe shughuli za Bunge hadi kesho saa 8.00 mchana.

*(Saa 11.59 jioni Bunge lilahirishwa hadi siku ya Alhamisi,
Tarehe 2 Aprili, 2020 Saa 8.00 Mchana)*